

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TANO

Kikao cha Tisa – Tarehe 18 Novemba, 2011

(Mkutano Ulianaza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

MHE. ENG. RAMO M. MAKANI - MWENYEKITI WA KAMATI TEULE YA BUNGE:

Taarifa ya Kamati Teule ya Bunge.

MHE. JANUARY Y. MAKAMBA - MWENYEKITI WA KAMATI YA NISHATI NA MADINI:

Taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini juu ya Uendeshaji wa Sekta Ndogo ya Gesi Nchini.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 109

Mikopo ya Wajasiriamali iliyotolewa na Mheshimiwa Rais

MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE (K.n.y. MHE. JAMES D. LEMBELI) aliuliza:-

(a) Je, ni wananchi wangapi wa Wilaya ya Kahama walionufaika na fedha za mikopo ya wajasiriamali, maarufu kama mamilioni ya Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete?

(b) Je, ni wananchi wa makundi gani kutoka maeneo gani ya Wilaya walinufaika na mamilioni hayo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE alijibu:-

Mshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda kujibu swali la Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mbunge wa Kahama lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, wananchi wa Wilaya ya Kahama walionufaika na fedha za mikopo ya wajasiriamali maarufu kama Mabilioni ya Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrishi Kikwete, hadi kufikia Disemba, 2010 ni 1,357. Wananchi hawa kwa ujumla waliokopeshwa shilingi 753,840,000 kupitia Benki ya NMB.

(b)Mheshimiwa Spika, wananchi walionufaika na mikopo kwa kuzingatia wingi ni vijana na wanawake kutoka maeneo ya mijini na vijiji.

MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa jibu zuri ambalo Waziri amejibu, lakini naomba niulize swali la nyongeza;

Kwa kuwa, mikopo hii iliwanufaisha zaidi wananchi wanaokaa mijini na vijijiini kwa sehemu kubwa walikosa, Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba hawa wananchi wanaokaa vijijiini hasa wajasiriamali nao wanapata?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, fedha hizi zilianza kutumika mwaka 2007 na kuishia Oktoba, 2009 awamu ya kwanza na kwa ujumla Benki ya *NMB* ilitoa shilingi bilioni 16.3 na *CRDB* ilitoa shilingi bilioni 29.94. Kwa hiyo, jumla ya fedha zote zilizotumika katika awamu ya kwanza ni bilioni 37.17.

Awamu ya pili ilianza ilianza mwaka 2007 na kuna fedha zilizotenga bilioni 11.3 na awamu hii inakamilika mwezi Machi. Baada ya hapo kutafanywa tathmini kwa maagizo ya Rais ili tuone watu gani wamenufaika zaidi katika mpango huu ili awamu inayofuata sasa tuelekeze kwa watu hawa ambao watakuwa hawajanufaika zaidi wakiwemo hawa wa vijijiini.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza;

Mheshimiwa Spika, suala la kunufaika ni moja na suala la impact ya kila pesa zinapotolewa, Je katika kipindi chote hiki kabla ya kutolewa kwa awamu ya pili, ile awamu ya kwanza impact yake ya 37 bilioni ilikuwa ni nini na hatimaye Serikali ikaridhika kuendelea na kutoa mikopo hiyo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, kwa takwimu inaonesha kwamba mikopo hii imeleta impact kubwa sana. kwanza kutokana na riba yake kuwa tofauti na riba ya kawaida ya mabenki, lakini pili urasimu wake kuwa mfupi na tatu fedha hizi zimeweza kuwafikia wananchi wengi sana kwa muda mfupi sana.

Kwa hiyo impact yake ni kubwa lakini hasa impact imejionesha kwa akina mama kwa sababu asilimia zaidi ya hamsini wamekopeshwa akina mama na ulipaji wao ambao umeonesha faida kutokana na miradi yao inazidi asilimia themanini.

Na. 110

Wananchi Kuchimbiwa Visima Virefu vya Maji

MHE. SELEMANI J. ZED aliuliza:-

Katika Kata za Semembela, Karitu, Igusule na Sigili katika Jimbo la Bukene kuna matatizo makubwa ya upatikanaji wa maji kwa matumizi ya binadamu na mifugo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuzipatia Kata hizo visima virefu vya maji ili wananchi wapate huduma kwa mwaka mzima?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mbunge wa Bukene kama ifuatavyo:-

Mhehsimiwa Spika, Wilaya ya Nzega ina jumla ya visima virefu 197, visima 315 na miradi ya maji ya bomba minne (4) inayofanya kazi ambapo jumla ya wakazi 195,934 wanaopata huduma ya maji safi na salama sawa na asilimia 37 ya wakazi wote. Kati ya visima virefu 197 na vifupi 315, visima virefu 71 na visima vifupi 211 vipo katika Jimbo la Bukene.

Mheshimiwa Spika, katika programu ya maendeleo ya sekta ya maji, miradi mbalimbali imetekelezwa katika Jimbo la Bukene ikiwemo miradi ya *quick wins*, programu ya maji na usafi wa mazingira vijiji na mradi wa maji vijiji unaotekelawa kwa pamoja kati ya Serikali za Tanzania na Japan kupitia Shirika lake la Maendeleo la JICA kama ifuatavyo:-

(i) Miradi ya *Quick wins*

(a) Uchimbaji wa visima 20 na kufungwa pampu za mkono kwenye kata za Karitu, Isaganhe, Mogwa na Kahama ya Nhalanga. Gharama iliyotumika ni shilingi 90,654,000 mwaka 2008/2009. (*Makofii*)

(b) Uchimbaji wa visima virefu viwili katika Kata ya Bukene ambao umegharimu kiasi cha shilingi 34,930,000 mwaka 2008/2009 ambapo kisima 1 kinatumika kama chanzo cha maji ya bomba.

(c) Ukarabati wa miradi miwili ya maji ya bomba katika Kata za Bukene na Igusule. Mradi wa Kata ya Bukene uligharimu shilingi 24,300,000 mwaka 2008/2009 na ule wa Igusule uligharimu shilingi 80,753,000 mwaka 2009/2010. Upatikanaji wa maji katika mradi wa Bukene ni kidogo kutokana na eneo la chanzo cha maji kutumika kwa shughuli za kilimo zinazofanywa na mwananchi mmoja ambaye ni mmiliki wa eneo hilo.

(ii) Program ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijiji.

Kupitia programu ya maji na usafi wa mazingira Vijiji visima virefu 10 vimechimbwa katika Kata za Itobo, Sigili, Ikindwa na Mwamala ambapo kati ya visima 10 vilivyo chimbwa visima 6 vimepata maji na visima 4 havikupata maji.

Katika visima 6 vilivyopata maji visima 5 vinategemewa kutumika kama vyanzo vya miradi ya maji ya bomba. Hii inatokana na kisima kimoja katika Kata ya Sigili kutokuwa na maji ya kutosha hivyo kilipendekezwa kufungwa pampu ya mkono. Gharama iliyotumika katika mradi huu ni shilingi 269,270,000 kwa mwaka 2010. Katika mwaka 2011 /2012 Halmashauri ya Wilaya Nzega imeidhinisha shilingi billioni 1.5 kwa ajili ya mradi wa maji.

(iii) Miradi ya maji unaohisaniwa na JICA.

Ipo miradi ya maji inayohisaniwa kati ya Serikali za Tanzania na Japan kupitia Shirika lake la Maendeleo la JICA. Mradi huu umesaidia kukarabati visima 11 katika Jimbo la Bukene kati ya visima 23 vilivyokarabatiwa katika Wilaya ya Nzega. Mradi uliokarabati una jumla ya visima 45 Mkoa wa Tabora kwa gharama ya dola za kimarekani 35,000 mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali ni kuvipatia vijiji vyote huduma ya maji safi na salama karibu na maeneo yao. Aidha, kutokana na ufinyu wa bajeti Serikali itatekeleza miradi hii kwa awamu.

MHE. SELEMAN J. ZEDI: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Waziri nina swali la nyongeza:-

Tofauti na visima vifupi, visima virefu vinapaswa kutoa maji mwaka mzima, lakini visima vingi kati ya visima hivi vinavyotajwa kuwa ni virefu sehemu kubwa ya mwaka havina maji, kwa mfano kisima cha Bukene ambacho kimetajwa kwamba ni kisima kirefu, wiki tatu zilizopita nilikuwa Bukene, maji yapo chini na pampu iko juu haiwezi kuyavuta.

Je, Serikali iko tayari kuteua Tume ya Watalaam waende katika Jimbo la Bukene na Wilaya ya Nzega kwa ujumla wavikague hivi visima vinavyoitwa virefu na kujua sababu ni kwanini visima vinachimbwa kama virefu lakini sehemu kubwa ya mwaka havina maji na wananchi wanapata matumaini kwamba wana visima virefu. Lakini bado wanapata kero ile ile kwa sehemu kubwa ya mwaka kutokuwa na maji.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nikubaliane naye kwamba kwa Mkoa wa Tabora kwa sehemu kubwa maji chini ya ardhi ni tatizo na visima vingi tumejaribu kuchimba na maji yanapatikana kwa asilimia labda hamsini. Sasa ndio tunatafuta njia kwamba tunafanyaje mahali ambapo tumechimba visima na maji hakuna.

Mheshimiwa Spika, tunatafuta vyanzo vingine kama mabwawa au kuyachukua maji kama ambavyo sasa hivi tunataka kuchukua maji ya Ziwa Victoria kwa mradi wa kutoka Kahama, Nzega, Tabora na Igunga, hili litasaidia vijiji vingi vilivyopo kandokando ya lile bomba kupata maji.

Hiyo ni njia moja ambayo nafikiri ni ya uhakika zaidi. Lakini kwa hili la visima, kwa kweli kwa sehemu kubwa kwa Mkoa wa Tabora ni tatizo, watalaaam wameshakwenda na taarifa tulizo nazo ndio hizo. (*Makofii*)

Na. 111

Mnada wa Wafanya Biashara Ndogondogo Msalato

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA aliuliza:-

(a) Je, mnada wa wafanyabiashara ndogo wa Msalato, ambao hufanyika kila siku ya Jumamosi ni wa kudumu au ni wa muda?

(b) Kama ni wa kudumu. Je, ni kwa nini mazingira ya biashara hususani vibanda yasiboreshw na kufanywa ya kudumu?

(c) Je, ni kiasi gani cha ushuru hukusanya kila siku ya mnada na fedha hizo zinatumikaje?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a),(b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, soko la wafanyabiashara ndogo ndogo Msalato ni Gulio ambalo kwa tafsiri sahihi ni mahali ambapo watu wanakutana kwa shughuli za kibiashara kwa juma au mwezi mara moja. Gulio hili ilianzishwa mwaka 2005 kwa lengo la kusogea karibu huduma za soko kwa wananchi wa Kata ya Msalato na Kata jirani kupata bidhaa katika gulio hilo. Gulio la Msalato kwa sasa ni la kudumu na linafanyika kila siku ya Jumamosi.

(b)Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma imekuwa ikiboresha soko hili ili kuwawezesha wananchi wanaokwenda katika soko hili kupata huduma zote muhimu kama kuwepo kwa maji na vyoo. Aidha, mpango uliopo ni kuliboresha gulio hilo ambapo katika Bajeti ya mwaka 2011/2012 zimetengwa shilingi milioni 40 kwa ajili ya kujenga sehemu ya machinjio, uvutaji wa maji safi na salama, ujenzi wa maji takaa, kuongeza huduma za vyoo na kujenga uzio wa machinjio.

(c) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma imeingia mkataba na Wakala aitwae *Olele Enterprises* kwa ajili ya kukusanya ushuru katika gulio hilo. Kwa wastani kiasi cha shilingi 140,000/- hukusanya kila siku ya gulio kama ushuru ambazo ni sawa na shilingi 560,000 kwa majuma yote manne kwa mwezi. Asilimia 20 ya mapato yanayopatikana hupelekwa katika Kijiji cha Msalato kutokana na soko hilo kuwa katika Kijiji hicho na asilimia 80 ya makusanyo hutumika kwa ajili ya miradi ya Maendeleo iliyopangwa kutekelezwa ndani ya Halmashauri.

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Spika ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kabla sijaauliza maswlai yangu naomba ku-*declare interest* kwamba katika kipindi kirefu Wabunge huwa tunakaa hapa Dodoma. Kwa hiyo, mimi ni mmoja wa wadau wa nyama choma katika mnada ule wa msalato.

(a) Mheshimiwa Spika, kuwawezesha wananchi kiuchumi pamoja na kuwapatia mikopo ya kufanya biashara, pomoja na mambo mengine lakini inahusisha pia kuwapa uhakika wa mazingira ya kufanya biashara zao. Katika kipindi cha mvua ukienda pale mnadani utashuhudia heka heka za kutisha inaponyesha mvua ya ghafla. Wateja pamoja na wajasiriamali wanakimbia huku na kuel kwa ajili ya kujikinga mvua. Ni adha kubwa sana, sasa wajasiriamali wanadai kwamba hawajengi miundombinu ya kudumu kwa sababu lile ni soko la muda. Ninachotaka kujua ni kwamba kwanini wajasiriamali hawa wasiruhusiwe kujenga miundombinu ya kudumu? Kwa sababu ukiangalia utaona kwamba Serikali yenye inataka kujenga machinjo kitu ambacho ni cha kudumu vile vile. (*Makofi*)

(b) Kwanini sasa hizi pesa zinazokusanywa zisitumike kujenga angalau basi jengo dogo tu kwa ajili ya kujikinga na mvua wakati wa kipindi cha mvua?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwamba ye ye ameondoka kwenye Majimbo amekuwa *National figure* na amesema kabisa kwamba ye ye ni mpenda nyama choma.

Mheshimiwa Wambura anatusaidia sana hapa kwa sababu ukienda katika eneo hili siku ya Jumamosi unakuta pale pamejaa magari mengi sana yanakwenda pale na hivi ninavyozungumza na wewe nimewita Nicholas Bureta, ambaye ni Kaimu Mkurugenzi nikamwambia nataka uniambaie tunafanya nini kuhakikisha kwamba tuna-*improve* hali iliyopo pale na ndio maana nimesema hapa kwamba zimetengwa shilingi milioni 40 ambazo zitafanyakazi hiyo kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunaboresha. Kwa kuanza tumesema tutaanza kwanza na vyoo, tutaanza na mahali pa kukaa, tutahakikisha kwamba maji safi na salama yanapita kule na kuhakikisha kwamba tunapatengeneza pale.

Mheshimiwa Spika, nimewuliza swalii hili analoniuliza Mheshimiwa Wambura. Je, hapa ni mahali pa muda au ni kwa kudumu na ye ye huko aliko ananisikia ametuambia ni mahali pa kudumu. Ni mahali pa kudumu, siyo maana yake kwamba kila siku watakuwa wanakwenda pale. Maana ya gulio ni mahali ambapo unakwenda mara moja kwa mwezi au kwa wiki na sisi huwa tunakwenda pale siku ya Jumamosi. Kwa hiyo, awe na uhakika kabisa kwamba tutafanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, anauliza swalii la pili anasema kwamba hela zinazopatikana pale kwa nini zisichukuliwe zote zikapelekwa pale kwa ajili ya kuendeleza sasa miundombinu, kupanga ni kuchagua, sisi hapa tunalipokea. Kinachotokea ni kwamba asilimia 20 zinapelekwa katika kijiji cha Msalato na asilimia 80 zinakwenda kwenye Halmashauri. Mimi nitakaa na Halmashauri wapo hapa hapa Dodoma, nitawaambia kwamba kuna mawazo kwamba hizi hela zote tupeleke pale ili tu-*improve* pale kwa sababu sasa hivi hela zinapatikana pale na kijiji cha Msalato kinataka kupokea shilingi mia tano kwa kila gari litakalopaki pale.

Mheshimiwa Spika, Mbunge huyu anatusaidia hapa hili ni jambo zuri kufanya hivi ni mtindo wa kisasa wa kuishi. Kwa hiyo, sisi tunakubali kwamba mawazo yake haya tutayapeleka kwenye Halmashauri na Halmashauri ndio yenye *mandate* ya kufanya maamuzi hayo, hakuna tatizo katika jambo hili. (*Makofi/Kicheko*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri haujasema kama ni mahali pa kudumu kwamba walishafanya mchoro wa eneo hilo au kuweka vibanda vibanda tu, Waziri wa nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayehusika na *CDA*.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, mimi ni mdau kwa sababu ndiye nilyewapa mamlaka liwe soko la kudumu nikiwa Mkuu wa Mkoa wa hapa Dodoma na kwa sasa ni Mwenyekiti wa Mamlaka ya Ustawishaji, Makao Makuu

Dodoma (CDA) ambaye ndiye anapanga matumizi ya ardhi hii. Nasema kama Manispaa wanasumbuliwa na CDA kwa tafsiri tulioitoa waje wanione na nathibitisha leo kwamba lile eneo liwe la kudumu. (*Makofii*)

Na. 112

Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM)

MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC (K.n.y. MHE. SAID AMOUR ARFI) aliuliza:-

Kuwepo kwa Mpango wa Maendeleo ya Afya ni pamoja na kuhakikisha kuwepo kwa Zahanati na vituo vya Afya kila kijiji na Kata.

Je, ni lini zahanati ya Mwamkulu itakamilishwa na ni sababu zipi zilizofanya isikamilishwe?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa katika sera ya afya ya mwaka 2007 inayotekelze chini ya mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) msisitizo ni kujenga zahanati kila kijiji na Kituo cha Afya kila Kata.

Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda inatekeleza Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi kwa kujenga Zahanati katika Kijiji cha Mwamkulu kilichohamishiwa katika Halmashauri ya Mji wa Mpanda ingawa ujenzi bado unasimamiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda. Mkataba wa ujenzi wa Zahanati ya Mwamkulu ulisainiwa tarehe 21 Februari, 2010 kwa gharama ya shilingi 19,991,368 na kazi ilitakiwa imalizike tarehe 21 Januari, 2011.

Mheshimiwa Spika, sababu za kuchelewa kwa ujenzi wa zahanati hii ni mwamko mdogo wa wananchi kuchangia vifaa visivyo vya viwandani (*non Industrial Building Materials*) kama mchanga, matofali, mawe na kokoto. Aidha, baada ya wananchi kuhamasishwa wamekusanya vifaa hivyo na ujenzi unaendelea. Mradi utakamilika mwezi Februari, 2012.

MHE. ANNAMARYSTELLA JOHN MALLAC: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, lakini nina swalii la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali imejitahidi kujenga zahanati kila kijiji lakini zahanati hizo zimekuwa hazina madawa ya kutosha, hazina huduma za maji kwa maana ya visima, hazina huduma za mawasiliano kwa maana habari, madaktari/wauguzi wanapata shida sana kwenda mbali, labda umbali wa kilomita 3 kufuata milima kwenda kupiga simu wanapopatwa na dharura ya wagonjwa.

Je, Serikali inatoa kauli gani kwa suala hilo? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Annamarystella John Mallac, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hili la Zahanati tunaamua sisi wenyewe kama Serikali kwamba kila kijiji kiwe na zahanati na kwamba katika Kata inabidi tuwe na Kituo cha Afya na katika Halmashauri kwenye *level* ya Wilaya kuwe na Hospitali ya Wilaya. Anachokisema hapa ni jambo ambalo lipo ni tazizo hakuna maji, hakuna dawa.

Lakini Wizara ya Afya na akisimama Waziri wa Afya hapa huwa anazungumzia kitu kinachoitwa *Integrated Logistic System* ambayo ndio tumeanzisha kwa kuhamisha sasa *MSD* kutoka Dar es Salaam tumepeleka katika Kata. Ukienda Kilimanjaro pale, Arusha wanakwenda pale Kilimanjaro. Ukienda Arusha hivyo hivyo. Mpango huu umekusudiwa kuona kwamba twende tukachukue takwimu halisi za aina ya magonjwa yanayojitekeza katika zahanati na aina za magonjwa zinazotokeza katika vituo vya afya na hospitali za Wilaya.

Matumaini yetu ni kwamba baada ya kuwa sasa hatuendi tena Dar es Salaam kwenda kuchukua dawa kule Dar es Salaam tunazichukulia huko huko na tunajua kwamba mahitaji pale katika kijiji ni ya namna gani tatizo hili analolizungumza Mheshimiwa Mbunge litakuwa limepungua.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nataka tu nimsaidie hapa sasa hili la mawasiliano la kwamba wanapanda kwenye milima/mti Mheshimiwa Nundu yupo hapa anasikia yeye ni Serikali mimi siwezi kumjibia lakini mimi nitashirikiana na Mheshimiwa kuwasiliana na Serikali kuomba ili tuhakikishe kwamba wanapata mawasiliano mazuri. Lakini *in the meantime* kwa huu utaratibu wa kutumia simu za upepo, tutawasiliana na zahanati kama kuna mgonjwa waweze kupeleka *ambulance* na vitu vingine. Lakini tutashirikiana na Mheshimiwa Mbunge kuhakuhakikisha kwamba mawasiliano yanaimarishwa katika maeneo hayo.

Suala la maji hilo tutamalizana nalo kwa sababu tuna mpango ambao Mheshimiwa Lwenje kila siku anazungumza hapa katika Makao Makuu ya Wilaya na Mikoa tumesema tuna *program* ya maji inayokuja kuhakikisha kwamba tunaondoka na tatizo la maji. Matumaini yangu ni kwamba na hizi zahanati nazo zitakuwa zimenufaika na mpango huu.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba nimwulize Waziri, Serikali katika huu mpango wa kujenga zahanati katika kila vijiji je, imejipangaje hizo zahanati wananchi wanakishirikiana na Serikali wakikamilisha watalaam madaktari na manesi na wakunga wamejipangaje kwamba wawepo ili baadaye lisitokee tatizo kama inavyotokea katika sekta ya elimu?

WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Soni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali katika mpango wa MMAM ina mkakati wa kuongeza idadi ya watumishi katika sekta ya afya tumejipanga kwamba tutakachoanza nacho ni kuongeza udahili wa wanafunzi ambao wanachukua mafunzo ya sekta ya afya wakiwemo madaktari, manesi, wafamasia na watalaam wengine. Pili, baada udahili huo wakimaliza vyuoni wote watapata ajira.

Mheshimiwa Spika, mojawapo ya Wizara ambazo zinaajiri moja kwa moja na zimepewa fursa hiyo ni Wizara ya Elimu, Wizara ya Afya na Wizara ya Kilimo hii yote ni kuongeza idadi ya watumishi hao ili iende sambamba na ongezeko ambalo tumelenga la kuongeza idadi ya vituo ambavyo vinatoa huduma za tiba ikiwemo zahanati, kituo cha afya na hospitali ya Wilaya.

Lakini vile vile pamoja na kuongeza idadi yao bado tuna mikakati ya kuweza kuwaweka pale kuwa-*retain* katika sehemu ambazo tumewapangia hiyo ikiwa ni pamoja na kutoa vivutio ikiwa nyumba na posho ili kwamba pale wanapopangiwa hawa watumishi waweze kubaki watoe huduma kwa wananchi. (*Makof*)

Na. 113

Vijana Kukosa Nafasi ya Kujunga na Vyuo vya Ualimu

MHE. JENISTA J. MHAGAMA aliuliza:-

Vijana wengi wanaomaliza Elimu ya Sekondari na kupata sifa za kujunga na mafunzo ya Ualimu kwa ngazi ya cheti na stashahada wakati mwingine hukosa nafasi hizo kwa miaka miwili mfululizo.

- (a) Je, Serikali inalitambua tatizo hilo?
- (b) Je, ni vijana wangapi wenyе sifa wamekumbwa na tatizo hilo na kusaidiwa?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Peramiko, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua tatizo la vijana wengi wanaomaliza elimu ya sekondari na wenyе sifa kukosa nafasi za kujunga na mafunzo ya ualimu. Uchaguzi wa waombaji ulifanyika kwa kuzingatia sifa na vigezo vinavyotakiwa kwa kila aina ya mafunzo. Kwa ngazi ya cheti kipaumbele kimetolewa kwa waliofaulu masomo ya Hisabati, Sayansi na *English* kwa kiwango cha ufaulu cha daraja la kwanza mpaka la nne (alama 28).

Kwa upande wa stashahada kipaumbele kimetolewa kwa wenyе ufaulu wa kidato cha sita daraja la III (*Principal Pass moja na Subsidiary moja*) katika masomo yanayofundishwa katika shule za sekondari (*core subjects*). Aidha, idadi ya waliochaguliwa kujunga na mafunzo ya ualimu inazingatia nafasi zilizopo na bajeti illyotolewa na Serikali kuendesha mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba vijana wengi wanaomaliza kidato cha nne na kuomba nafasi za mafunzo ya ualimu ngazi ya cheti wanakosa nafasi katika Vyuo vya Ualimu vya Serikali. Kwa mfano, mwaka huu wa masomo 2011/2012 waombaji wenyе sifa walikuwa 41,787 na waliochaguliwa walikuwa 17,722 kati yao 7,138 wamekwenda vyuo vya Serikali na wanafunzi 10,594 wamekwenda vyuo vya binafsi.

Aidha, waombaji wa mafunzo ya ualimu ngazi ya stashahada walikuwa na sifa walikuwa 10,345 na kati yao waliochaguliwa walikuwa 8,876 sawa na asilimia (85.79). Kwa wale wanaokosa kujunga na Vyuo vya Ualimu vya Serikali, Wizara yangu huwa inawasaidia kwa kuwapa ushauri wa kuomba nafasi za mafunzo katika Vyuo vya Ualimu visivyo vya Serikali.

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa jamii kutumia fursa nyininge zilizopo nje ya ualimu kuendeleza vijana. Fursa hizo ni pamoja na mafunzo ya ufundi, kilimo, biashara, uvuvi, nyuki, uuguzi, jeshi na ukutubi na sehemu zingine.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kabisa kwamba idadi ya waliochukuliwa ni asilimia ndogo sana na ninao uhakika na ushahidi ya wengi wa vijana hawa ambao hawajachukuliwa ni wale ambao wanatoka maeneo ya vijiji na nina ushahidi wa wanafunzi hao na wamekuwa wakiachwa kila mwaka kwa mfululizo wa miaka miwili/mitatu. Tatizo la walimu katika nchi yetu ni kubwa na hasa walimu wa kwenda kufundisha katika shule za vijiji.

(a)Je, Mheshimiwa Waziri haoni sasa ni wakati muafaka wa kuwachukua wanafunzi wote wanaoomba kujunga na mafunzo ya ualimu kwa kuwashauri Serikali kuwa na mpango maalum wa kuwachukua na kuwafundisha wanafunzi hao ili kuondo tatizo la walimu na kuacha hiyo tabia ya kuwachukua wachache na kuondo kigezo cha kuwaacha katika miaka kama inavyokwenda na inavyoeleka?

(b)Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, hapa ameniambia anatoa wito kwa jamii kutumia fursa nyininge zilizopo kuwashauri na kuwasaidia hawa wanafunzi. Hivi wajibu wa kuwasaidia vijana wa nchi hii ya Tanzania kabla hatujashirikiana na jamii haoni uko katika mikono ya Serikali kutafuta nafasi ya kufungua mafunzo mengine kwa hali yoyote iwezekanayo kuondo tatizo la ajira kwa vijana nchini? (*Makof*)

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, ningependa kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jenista Mhagama kama ifuatavyo:-

Kwanza kuhusu uchaguzi wa wanafunzi hao kuingia masomo ya ualimu kwamba tumebadilisha utaratibu wa uchaguzi wa wanafunzi hawa katika mwaka huu wa masomo ili kuhakikisha kwamba kila Mkoa unachangia kutoa wanafunzi amba wanakwenda kwenye masomo ya ualimu badala ya kuchagua tu Mkururo kwa orodha ya waombaji kwa Tanzania nzima, tunahakikisha kwamba tunaangalia kila Mkoa.

Kwa hiyo, ugawaji wa nafasi hizi zilienda kila Mkoa ili Watanzania wote washiriki katika sehemu hii ya mafunzo. Kwa hiyo, hakuna wanafunzi wale amba walipendeleta kutoka mijini tu ndio wakachaguliwa kwenda kwenye ualimu ni kutoka Mijini na vijiji kimko na ndio wamekwenda kule.

Kazi kubwa tuliyokuwa nayo ni kwamba tumeongeza vyuo vya ualimu mpaka sasa vya Serikali tunavyo 34 jumla vyuo vyote pamoja na vyuo vya binafsi 103 lakini bado nafasi zinatakiwa zaidi. Kwa hiyo, tutaendelea na juhudili tuweze kupata walimu wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira jukumu la Serikali tunaendelea hivyo na tunahakikisha tunafungua fursa zingine kama mpango wa kujenga vyuo vya ufundi nchi nzima ili vijana wetu wawe na fursa zaidi za kupata *skills* za kazi na mpango huo amba Chama cha Mapinduzi kimewahidi ya kujenga Chuo cha Ufundu kila Wilaya unaanza kutekelezwa kuanzia mwaka huu wa fedha na pia kuvitumia vyuo vya mafunzo vya wananchi ama *FDCs* kuwa ni sehemu ya kutoa mafunzo ya elimu ya ufundi nchi kwetu. (*Makof*)

Na. 114

Kuharibika kwa Boti ya Ngunguri – Kituo cha Polisi Bandarini

MHE. JUMA SURURU JUMA aliuliza:-

Boti maalum ya ulinzi wa doria hasa nyakati za usiku ya Ngunguri iliyokabidhiwa katika Kituo cha Polisi cha Bandari Zanzibar mwaka 2005, imeharibika karibu miaka mitatu sasa:-

- (a) Je, Serikali ina taarifa juu ya kuharibika kwa boti hiyo?
- (b) Kama inajua. Je, Serikali ina mpango gani wa kuitengeneza boti hiyo?
- (c) Je, Serikali ina mpango gani wa kupata boti nyingine ya doria katika Kituo cha Polisi cha Bandarini Zanzibar?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mbunge wa Bububu, lenye sehemu (a),(b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inayo taarifa kwamba boti aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge iliharibika ikiwa inafanya kazi katika Kituo chake cha Zanzibar na kuletw Dar es Salaam kwa ajili ya kufanyiwa matengenezo.

Mheshimiwa Spika, tathimini iliyofanywa imebainisha kwamba injini za boti hiyo zimeharibika sana na gharama ya kuitengeneza tena ni kubwa mno takribani Tshs. Bilioni 1.75.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukosefu wa rasilimali fedha, katika mwaka 2011/2012 Jeshi la Polisi halikutengewa pesa kwa ajili ya ununuvi wa vyombo vya moto vipyta.

MHE. JUMA SURURU JUMA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri inaonekana kwamba chombo hiki hakirudi kwa kipindi hiki.

(a) Je, Serikali kuititia Wizara hiyo ina mpango gani wa kuweka boti mbadala kwa ajili ya kazi za doria hasa ukichukulia kwamba sasa hivi kuna vikundi viovu vinajingiza kikiwemo cha Al-shabab?

(b) Kuendelea kutopeleka vifaa hivyo haoni kudhoofisha kazi za doria katika Visiwa vya Zanzibar? (*Makof*)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge Juma Sururu Juma, kama ifuatavyo:-

Nimwambie tu kwamba kwa sasa hivi hatuna mpango mahususi wa kuweka chombo mbadala kwa kuzingatia hali halisi tulikuwa nayo na ufinyu wa fedha/bajeti ambayo tuliyokuwa nayo. (*Makof*)

Kuhusu suala la kudhoofisha hali ya usalama Zanzibar mimi niseme kwamba kwa kweli tunafanya kila jitihada ya kujipanga na mahali ambapo tunashindwa kwa kweli kutumia vifaa vyetu tunaweza kutumia vifaa vya Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwa kuzingatia kwamba usalama wa nchi yetu ni jambo ambalo linapewa umuhimu mkubwa. (*Makof*)

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa pamoja na sababu zilizosababisha kuharibika boti hii pia ziko sababu za watu/mabaharia wa boti ambao walipata elimu DMI lakini hawakupangwa katika boti na wakapelekwa watu wengine. Je, Wizara yako ina mpango gani ya *job allocation* kuaweka watu wanaohusika hasa na boti ile na kuendeleza kwa masomo ambayo watu hao wamekaa sasa hivi zaidi ya miaka mitano hakuna juhudu yoyote ya kuendeleza masomo yao ambayo ndio watu wangeweza kufaa katika kuendeleza boti hii?

SPIKA: Kwanza ilikuwa boti kutengenezwa sasa sijui imetengenezwa?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mnyaa kama ifuatavyo:-

Asemavyo ni sahihi lakini chombo hakipo kwa sasa hivi. Kwa hiyo, kwa kuwa chombo hakipo hatuna uhakika wa kusema kwamba ajira ya hawa watu itakuwa namna gani. Lakini nataka nimhakikishie kwamba tunafanya kila jitihada kuhakikisha kwamba mazoezi ambayo wanastahili kupata ili kuhakikisha kwamba ule uzoefu na *training* yao haipotei hiyo inaendelea. Sasa wapi watakwenda hii inategemeana na hali ya kifedha kama nilivyosema katika jibu langu la msingi tutakapopata chombo kingine nina uhakika ajira yao itakuwa ya uhakika.

Na. 115

Kupungua Kodi ya Uchimbaji wa Chumvi

MHE. FATUMA ABDALLAH MIKIDADI aliuliza:-

Mikoa inayochimba chumvi hupata adha ya kutozwa tozo nyingi kama vile kodi ya Madini (50,000), ushuru wa mikoko (80,000), mrahaba (3% ya Bei ya Chumvi), ushuru kwa kila pakiti ya kilo 50 (50,000/=) madini joto (30,000/= kwa kilo) na usajili wa shamba kwa mwaka (200,000).

- (a) Je, Serikali haioni kuwa kodi za chumvi ni nyingi ukizingatia kuwa chumvi haina soko?
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza kodi hizi?

(c) Je, madini ya chumvi yapo chini ya Wizara gani?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kuna malalamiko kutoka kwa baadhi ya wazalishaji chumvi kuhusiana na malipo makubwa yanayotozwa na Halmashauri za Wilaya au Taasisi za Serikali kwa chumvi wanayozalisha. Naibu Waziri wa Nishati na Madini alipofanya ziara ya Mikoa ya Pwani, Lindi na Mtwara mwezi Januari, 2011 alipata fursa ya kukagua maeneo yote ya uzalishaji na kuongeza na wazalishaji kwa maana ya Jumuiya yao, *TASPAC* kuhusiana na masuala yote.

Kwa sasa Wizara inafanya mawasiliano na Halmashauri za Wilaya na taasisi ambazo zinalalamikiwa kwa kutozwa malipo makubwa ya ushuru bila ya kuzingatia sheria ya madini, ili kupata ufumbuzi na kuondoa malalamiko hayo.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali kuitia Wizara yangu italifanyia kazi suala hili kwa kushirikisha wadau wengine kama Wizara ya Fedha na Uchumi, TAMISEMI na Halmashauri husika ili kuweka mazingira mazuri kwa wazalishaji chumvi. Aidha, mkakati huu unaendana na hatua za Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine, za kuboresha viwango vya uzalishaji wa chumvi hiyo kwa ajili ya masoko.

(c) Mheshimiwa Spika, madini ya chumvi yapo chini ya Wizara ya Nishati na Madini.

MHE. FATUMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Spika, nashukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika miaka 1980 Wizara ya Afya na *UNICEF* walifanya utafiti katika miili ya binadamu ikagundua kwamba haina madini joto. Kwa hiyo, ikachukuliwa madini joto ikawekwa kwenye chumvi ili iwapate wananchi wengi.

(a) Sasa madini hayo je, Serikali haiwezi kutoa kama ruzuku kwa wakulima wa chumvi kwa sababu inatumika kama mradi wa *UNICEF* na Wizara ya Afya kama Serikali?

(b) Chumvi haina kwa sababu aliyekuwa ananunua chumvi Kiwanda cha Mgololo ananunua chumvi za nchi za nje. Na kwamba chumvi mpaka sasa tangu miaka ya 1940 kilo 50 ni shilingi 1500.

Je, Serikali ina kauli gani kuhusu hili? (*Makofu*)

SPIKA: Bei haipandi?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu maswali la Mheshimiwa Fatuma Mikidadi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hili la iodine kwenye chumvi ni kweli maana haya yalifanywa kwenye miaka ya 1980 lakini yalifanywa kwa sura mbili, moja yalifanywa kwa sababu ya vigezo vya afya kwamba chumvi inavyokosa *iodine* na kwa sababu chumvi inatumika *almost everyday* kwa mwili wa binadamu ina athari kubwa kwenye matatu, ina athari kwenye magonjwa ya goita, kwenye mtindio wa ubongo lakini pia kwenye mimba za akina mama.

Kwa hiyo, ikaonekana hii *iodine* iingie kwenye chumvi na *standard format* kwa chumvi ambavyo inauzwa duniani kote. Tulipokuwa Lindi na Mtwara tumezangumza na wazalishaji tunatafuta formula ya kuangalia kwa sababu hii *iodine* pia inachangia kwenye uboreshaji kwenye zao lenyewe la madini. Kwa hiyo, tunaangalia kama Wizara ya Fedha itakubali kwamba nusu ya gharama za *iodine* ziende kama ruzuku na nusu walipie wenyewe wazalishaji kwa sababu ni

jambo linaloendana pia na kuboresha zao lenyewe kwa soko. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge hili tunalifanya kazi na tulikubaliana na Wizara hiyo nadhani tutafikia majibu haraka.

Mheshimiwa Spika, hili la pili la kwamba chumvi halina chumvi hili ni tatizo, chumvi nyingi ya Tanzania ilikuwa inakwenda Mgololo kwa upande wa chumvi iliyokuwa inazalishwa Kusini na Congo na wapi kwa chumvi iliyokuwa inazalishwa Bagamoyo na Uvinza.

Kwa hiyo, hili linafanyiwa kazi, tunajaribu kwanza kabisa chumvi yetu ilingane na chumvi zinazotoka sehemu zingine. Hiyo chumvi tunaitoa nje kwa mfano Afrika Kusini lakini tunalifanya kazi juzi juzi Wizarani walikuja watu kutoka Afrika Kusini wanataka chumvi ya Tanzania. Kwa hiyo, tutaangalia namna ya kufanya ili chumvi yetu iendane na viwango vinavyotakiwa kimataifa.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Spika, nilikuwa na swali dogo tu la nyongeza kwa Mheshimiwa Waziri.

Kwanza nisahihishe kauli yake ya kusema kwamba baadhi ya wazalishaji chumvi ndio wanaolalamika. Wanaolalamika ni wazalishaji wote wa chumvi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Serikali siku zote imekuwa ikiweka utaratibu kwenye uagizaji wa sukari hamuoni sasa upo umuhimu wa kusimamia uagizaji wa chumvi kutoka nje kwa sababu chumvi tunayozalisha ndani ya nchi inatosheleza kabisa soko na inabaki chumvi nyingi sana? (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Murtaza Mangungu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kwanza nirekebishe labda kwenye matumizi ya baadhi, lakini ni kweli kwamba wazalishaji walio wengi wanalamikia hali iliyokuwepo sasa hivi ikiwa ni wazalishaji wa jimbo langu la Mkuranga na Bagamoyo na kadhalika. Kwa hiyo, hili suala ni gumu lakini tukubaliane tu kwamba kwa sasa hivi tuna tatizo kiwango cha chumvi tunayozalisha. Bado tuna matatizo. Tulipokwenda pale tumezungumza na wazalishaji na tumewaomba kwamba wajaribu kuangalia chumvi inayozalishwa nje ambayo inakuja na sisi wenye kujibu swali na standards hizo.

Kwa hiyo, tulichofanya tumekubaliana kwamba tutaongea na watu wa TBS wajaribu kutusaidia ili kile kiwango cha iodine na usafi wa chumvi yenye kujibu swali na kadhalika vijaribu kuboreshwa zaidi ili chumvi yetu iendane na chumvi inayotoka nje. Sasa tukishafika hapo naamini kwamba tunaweza tukaweka vigezo vya kuzuia chumvi inayotoka nje kwa sababu chumvi yetu ya ndani itakidhi viwango.

Na. 116

Matokeo ya utafiti wa Maji ya Mto Pinyinyi

MHE. KAIKA S. TELELE aliuliza:-

Maji ya Mto Pinyinyi yalifanyiwa upembuzi yakinifu miaka 3 – 4 iliyopita kwa ajili ya kuzalisha umeme.

- (a) Je, ni nini matokeo ya utafiti huo?
- (b) Je, utafiti huo unaweza kufanya katika maporomoko ya maji ya Engaresero katika eneo la Ziwa Natron?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kaika S. Telele Mbunge wa Ngorongoro lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli chanzo nya kuzalisha umeme kwa kutumia nguvu za maji cha mto Pinyinyi kilifanyiwa upembezi yakinifu na wahandisi washauri *DECON – SWECO Inter Consult* na kutoa matokeo ya awali katika taarifa yao ya Desemba, 2005. Katika ripoti hiyo ilipendekezwa ifanyike tena marejeo ya upembuzi yakinifu wa mwisho marejeo ambayo yangetoa maamuzi ni lini utekelezaji wa mradi huo uanze na kwa kiwango gani cha uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2010 Mhandisi Mshauri *NORPLAN* katika mpango wa Norway wa kuwezesha utekelezaji wa miradi midogo midogo ya kuzalisha umeme kwa nguvu za maji alipewa kazi ya kuangalia mradi upi wenyewe gharama nafuu wa kuweza kulipatia umeme eneo la Kaskazini la Ngorongoro. Chanzo cha kuzalisha umeme kwa kutumia nguvu za maji cha Mto Pinyinyi kiliangaliwa tena.

Aidha, katika ripoti yao ya Machi, 2010 walipendekeza kufanyike tena upembuzi yakinifu wa makini zaidi ukihusisha upimaji wa maji katika Mtoto Pinyinyi ili kuona kama uzalishaji wake utakidhi MW 3 hasa wakati wa kiangazi ili kiasi cha maji cha chini kabisa cha kuzalisha umeme kijulikane. REA wanaendelea kuwasiliana na *NORAD* ili kufadhili upembuzi yakinifu kama ilivyoshauriwa na tathimini mbalimbali zilizofanyika. Iwapo *NORAD* hawatakuwa tayari kufadhili kufanyika kwa upembuzi yakinifu taratibu za kilitangaza kwa tenda eneo hilo zitafanya.

(b) Mheshimiwa Spika, utafiti huo unaweza kufanyika katika maporomoko ya maji ya Mto Engaresero. Ugumu wake ni kwamba eneo hilo linatumika kama kivutio cha watalii na eneo ni nyeti kimazingira kwa kuwa ni mojawapo ya mazalio ya ndege aina ya Flamingo.

MHE. KAIKA S. TELELE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa nishati ya umeme ni muhimu sana kwa maendeleo ya wananchi Mijini na Vijijini na kwa kuwa eneo la ziwa Natron na Mlima Lingai ni maarufu sana kwa biashara ya utalii.

Je, Serikali itafufua kiwanda cha magadi kilichokuwa chini ya shirika la umma *STAMIC State Mining Corporation* katika Kijiji Engaresero ikiwa nishati ya umeme itapatikana kutoka Mto Pinyinyi?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Telele kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa sasa ugomvi uliokuwepo pale wa kuendeleza madini ya magadi yanayotoka pale kwenye Ziwa Natron linahusiana na masuala ya mazingira. Kwa bahati nzuri watalaan wamebaini kwamba badala ya kufanya *vertical drilling* unaweza kufanya *horizontal drilling*.

Kwa hiyo, kwa maana ya kwamba kama madini yenyewe yako mbali kidogo zaidi unaweza kuingia ardhini kama kilomita 30 au 40 kutoka eneo lenyewe na bado uka-access magadi na kwa sababu magadi yanajizalisha yenyewe athari kwa mazingira yale ya mazalio ya Flamingo yanaweza ikawa siyo kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninachosema ni kwamba ukipatikana umeme pale kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge naomba nikubaliane naye itatoa fursa zaidi kwa *industrial development* ambayo itawezesha utaalam huu kutumika na mimi naamini kwamba tutaweza kuafikiana na watu wa mazingira ili tuweze ku-access madini haya badala ya kutoka Kenya kwa wenzenetu.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Spika, mto Nzovwe ulioko Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga ulishafanyiwa utafiti katika maporomoko yake kwamba unaweza ukatoa umeme zaidi ya MW 8 na kuendelea. Ukizingatia kwamba umeme huo unaweza kutosheleza kutawanya umeme Mji wa Sumbawanga, Wilaya Sumbawanga Vijijini, Nkasi hata Mpanda

Mashariki kwenye jimbo la Mheshimiwa Waziri Mkuu. Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa fedha kuanza kujenga mradi huo?

SPIKA: Swali jipya sana.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu la Mheshimiwa Malocha kama ifuatavyo:-

Katika miradi ambayo iko katika tathimini ya min hydra kupitia kupitia wakala wa nishati vijiji REA moja ni hili la Nzovwe na lingine liko Namtumbo kwa Mheshimiwa Vita Kawawa na iko miradi mingine Mbanga pia naamini kwa Mheshimiwa Jenista na Njombe. Iko miradi hii ambayo iko chini ya MW 10 ambayo iko chini ya tathimini za min hydra na REA inaifanya kazi na moja katika hizo ni Nzovwe.

Sasa naomba nimfahamishe kwamba Mheshimiwa Mbunge kwamba wa Norway walionesha tamaa ya kuendeleza mradi huu wa MW 8 mpaka MW 10 ni kweli na mafanikio yake tukiutekeleza ni makubwa kwa sababu utapunguza (dependency) utegemezi wa umeme kwa sasa hivi unaotoka Mbala Zambia.

Kwa hiyo, naomba niseme tu kwamba hili linafanyiwa kazi kwa karibu na jana tu Mheshimiwa Aeshi na Mheshimiwa Keissy walikuwa wameomba kwamba Wizara iende kule watalaan wa TANESCO na REA ili kuweza kuliangalia hili eneo kulifanya tathimini lakini pia kulitangaza kwa wawekezaji wengine watakaopenda kuliendeleza. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Malocha kwamba tunalifanya kazi kwa karibu kwa sababu una umuhimu wa pekee mradi huu.

Na 117

Madhara Yatokanayo na Kupasuka Kwa Bomba la Tazama

MHE. HAMOUD ABUU JUMAA aliuliza:-

Hivi karibuni Bomba la mafuta mazito linalotoka Dar es Salaam kwenda Zambia TAZAMA lilipasuka katika maeneo ya Jimbo la Kibaha Vijiji Kata ya Janga na kuharibu mazingira kama vile mimea ya asili, mazao, mifugo na afya zetu.

Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kufanya tathmini ya madhara ya ajali hiyo na kuwalipa fidia wananchi walioathirika?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa naiaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamoud Abuu Jumaa, Mbunge wa Kibaha Vijiji kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tarehe 23 Septemba katika ameneo ya Tanga Kata ya Mlandizi Wilaya ya Kibaha, bomba la kusafirisha mafuta la TAZAMA lilipata hitilafu na mafuta kumwagika. Taarifa ilipokelewa majira ya saa sita mchana na mara moja hatua ya kusimamisha usukumaji wa mafuta kutokea Kituo cha Kigamboni zilichukuliwa. Aidha, TAZAMA walipelekea mafundi kwenye eneo kwa ajili ya kufanya tathmini ya hali yenye halisi.

Mheshimiwa Spika, maamuzi yaliyofikiwa na mafundi ni kufunga funguo za bomba *line valves* kwenye eneo la tukio na kuweka tuta au kizuizi Ridge ili kuzuia mafuta hayo kusambaa zaidi. Askari wa Jeshi la Polisi walifika kwenye eneo ili kudhibiti uwezekano wa watu kujaribu kuchota mafuta yaliyomwagika. Tarehe 24 Septemba kile kipande cha bomba kwa maana ya kesho yake kile kipande cha bomba kilichopasuka kilibadilishwa na kipande kingine na hivyo ule umwagiliaji wa mafuta kwenye bomba ukadhibitiwa.

Mheshimiwa Spika, mafuta yaliyomwagika kwenye eneo hilo yalipakiwa kwenye malori ya mafuta na kusafishwa kwenda kwenye eneo maalum la kuhifadhi Kigamboni. Kazi ya kusafisha eneo ilianza na tathmini ya awali ilifanywa na wataalam wa TAZAMA. Mimea aina ya *Reeds* ambayo ni mimea ambayo hujiotea kwenye sehemu zenye maji, iliathirika kutokana na kumwagika kwa mafuta hayo na kuathiri eneo la mita 3000 za mraba. Eneo hili halina mashamba wala mimea ya kilimo. Aidha, ulinzi uliowekwa ulizua mifugo kunya maji yaliuchafuliwa kwa mafuta. Hadi hivi sasa hakuna athari ya moja kwa moja iliyobainika kwa wakazi wanaoishi kwenye eneo hili, au maeneo ya jirani.

Mheshimiwa Spika, naomba kumshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wake wa karibu wa suala hilo. Aidha, naomba awasiliane na uongozi wa Wizara yangu moja kwa moja ili kushughulikia masuala yote yanayohusiana na fidia pale ambapo uharibifu kwa binaadamu, wanyama au mimea unathibitika.

MHE. HAMOUD ABUU JUMAA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nilikuwa na maswali mawili ya nyongeza.

(a)Mheshimiwa Waziri anasema walifanya tathimini, sasa nilitaka kujua tathimini hiyo waliyofanya pale walishirkisha wananchi na Halmashauri? (*Makof*)

(b)Je, atakuwa tayari kutuma watu wake ili tathimini ile ifanywe upya? Ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Hamoud Abuu Jumaa Mbunge wa Kibaha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa dhamana ya kudhibiti uharibifu ule ni ya mwenye bomba kwa maana TAZAMA hiyo ndiyo ya kisheria. Kwa hiyo, ilipotokea ni kwamba baada ya kutokea tukio lile TAZAMA wenye walipeleka mafundi wao na kugharamia hatua zote za kudhibiti uhalibifu wowote utakaokuwa uliotokea. Sasa mpaka dakika hii tuliyokuwa nayo TAZAMA wanaendelea na hatua za kusafisha lile eneo. Katika tathimini iliyofanya kuna bwana mmoja anaitwa bwana Bongo Lingoma ndio ameonekana amedai fidia ya uchafuzi.

Sasa ndio maana nikasema kwa sababu kuna mita za mraba kama 3000 mpaka kufikia eneo la *Ridge* lile tuta lilloluia mafuta kwenda walichofanya ni kwamba wanapangua udongo wote ule na wanafidia udongo mwengine.

Zoezi hili iote likimalizika la *ku-control environmental damage* iliyotokea tumekubaliana kwamba by 29/11/2011 Uongozi wa Wizara ya Nishati na Madini, Idara ya Mazingira Nishati na Madini, watu wa Wizara ya Mazingira Makamu wa Rais na kadhalika wote tutakwenda kuangalia uhalibifu uliotokea pale. Naomba nimthibitishie kwamba zoezi hilo litamshirkisha yeye Mheshimiwa Mbunge na Viongozi wa Halmashauri yake. (*Makof*)

Na. 118

Mikopo ya wanafunzi wa Law School

MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI aliuliza:-

Sheria ya Bodi ya Mikopo hairuhusu wanafunzi wanaosoma *Law School* kupata mikopo licha ya Sheria ya mwaka 2007 iliyanzisha *Law School* kuwataka kupata mafunzo hayo kwanza kabla ya kufanya kazi kwenye sekta za umma.

Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu wahitimu wengi waliopo mitaani kwa kukosa udhamini wa kupata mafunzo hayo huku ikilalamika kuwa kuna upungufu wa Mahakimu na Mawakili?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swalii la Mheshimiwa Christina Lissu Mughwai, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama inavyofahamika, kwa mujibu wa Sera ya Elimu ya Juu wanafunzi pamoja na wazazi/walezi wao ndio wenye wajibu wa kwanza wa kulipa gharama mbalimbali za elimu au mafunzo yao hapa nchini.

Kwa kutambua kuwa sio wanafunzi/wazazi wpti wanaoweza kumudu gharama za elimu ya juu nchini, Serikali ilianzisha Bodi ya Mikopo kwa wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu (*Higher Education Students' Loans Board*) kwa Sheria Na. 9 ya Bunge ya mwaka 2004 ili iweze kuratibu na kutoa mikopo kwa wanafunzi wahitaji (*needy students*). Kwa mujibu wa Sheria hiyo, wanafunzi wa Taasisi hii si miongoni mwa wanafunzi wanaostahili kunufaika na mikopo hiyo, japo kwa wengi wao walinufaika na mikopo kwenye mafunzo yao ya Shahada ya Kwanza ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Serikali mekuwa ikitoa fedha kupitia Wizara yangu kwa ajili ya kuwakopesha wanafunzi wa Taasisi hii. Mikopo hii inasimamiwa na Bodi ya Uendeshaji ya Taasisi yenye we. Hadi sasa wanafunzi 1,396 wa Taasisi hii wamekwishapewa mikopo yenye jumla ya thamani ya shilingi bilioni tatu milioni mia nne themanini na tano, laki nane na thelathini na saba elfu (3,831,485,837.00). Serikali inaendelea kutafakari utaratibu wa kudumu wa utoaji mikopo kwa wanafunzi wahitaji wa taasisi hii.

MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Waziri katika jibu lake amesema ni idadi ya wanafunzi 1396 tu ndio waliopata mikopo tangu utaratibu wa *Law School*/uanzishwe.

Je, Serikali inapata kigugumizi gani kuwaingiza wanafunzi wa *Law School* katika utaratibu wa Bodi ya Mikopo ambapo ukiangalia utaratibu wa sasa ambapo wanapata mikopo kutoka taasisi husika na utaratibu ambao hautoshelezi mikopo na badala yake wanafunzi hao wako mitaani kwa kukosa ajira na wengine wakilazimika kufanya kazi ambayo hawakusomea?

Swali la pili, kwa kuwa utaratibu huu wa *Law School* haujaonyesha ufanisi katika udahili na umekuwa ukilalamikiwa sana. Je, Serikali haioni kwamba utaratibu huu sasa uweze kufutwa na badala yake masomo ya *Law School* yaongezwe katika Shahada ya Kwanza ili wanafunzi waweze kunufaika na mikopo wakiwa vyuoni?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA) (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA): Mheshimiwa Spika, kwa nini wanafunzi hawa wasipewe mikopo na *Loans Board*? Hili ni swali la kisheria, *Loans Board* Sheria yake hairuhusu wanafunzi wanaosoma hapo *Law School* kupewa mikopo. Tunachowea kufanya kama Bunge hili litaona ni jambo la muhimu sana basi suala la kuleta Muswada ikabadilishwa sheria wakaingizwa katika taratibu za mikopo. Lakini kwa sasa sheria halwatambui kama wanafunzi wanaostahili kulipwa mikopo.

Pili, *Law School* ni suala la mazoezi. Masomo yale ni masomo ya mazoezi, ni *practical* wanajifunza jinsi ya Mawakili wanavyofanya kazi. Sasa imetokea Mahakama kama *Authority* wameamua kwamba wao hawahitaji wafanyakazi wao wapitimia *Law School* kwa sababu wakishaingia Mahakama wanafundishwa kuwa Mahakimu. Kwa hiyo utakuta wengi wanaokwenda kufanya kazi ya uhakimu hawana haja na wala hawapitii *Law School*. Vivyo hivyo Ma-Lawyers Wanasheria ambao wanakwenda kufanya kazi kwenye Halmashauri zetu kwa mfano, kazi tu za ukarani, au kwenye mashirika mengine ambayo hawahitaji kuingia Mahakamani si lazima waende *Law School*.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Asante sana Mheshimiwa Spika kwa kuniona. Kwa katika nchi yetu tumekuwa na wanasheria wazuri ambao hawakupitia *Law School* kwa mfano akina Shivji, akina Marando, akina Tundu Lissu. Huoni kama ni wakati muafaka sasa wakutokuwalazimisha hawa vijana wapitimia *Law School* kwa sababu *ime-prove* kwamba hata bila kupitia *Law School* tumekuwa na ma-Lawyer wazuri? (*Makof!*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA) (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA):
Mheshimiwa Spika, uamuvi wa kuanzisha *Law School* ulifikiwa baada ya mapendekezo ya Tume ya Mheshimiwa Jaji Bomani ambavyo wallona uko umuhimu wa kuzalisha ma-Advocate sasa wengi ili tuweze kuingia katika somo la ushindani la Afrika Mashariki na sisi tuwe na Mawakili wengi wa kutosha. Tukaamua iundwe hiyo *Law School* na Bunge hili lako tukufu ndiyo ilipitisha Sheria ile na sasa kama Mheshimiwa Msigwa na Wabunge wote wanaona ni muhimu hakuna haja ya kuwa na *Law School* ni suala la kisheria tu.

Lakini kimsingi bado tunaamini ni jambo zuri sana na kwa sasa tumekwishatoa wanafunzi wengi sana kutoka *Law School* ambao wamekuwa Mawakili. Sasa suala la uzuri wa Wanasheria ama kutokuwa wazuri mimi naomba nisilisemee kwa sasa hasa kwa hao aliowataja. (*Kicheko/Makofi*)

Na. 119

**Athari ya Mwingiliano wa Sheria za ardhi, Madini na
Sheria Inayosimamia Maliasili na Mazingira**

MHE. BEATRICE M. SHELUKINDO aliuliza:-

Migogoro inayotokea kwenye baadhi ya Wilaya hususan Wilaya ya Kilindi inatokana na muingiliano wa Sheria zinazosimamia madini, ardhi na sheria ya maliasili na mazingira na hivyo kuleta usumbufu na machafuko makubwa ndani ya jamii, yanayosababisha hata umwagaji damu kwa baadhi ya maeneo hapa nchini:-

(a)Je, Serikali inakubaliana nami juu ya kuwepo kwa muingiliano wa sheria hizo na kama ndivyo ni hatua gani za makusudi na za dharura zinachukuliwa kuondoa tatizo hizo?

(b)Je, Serikali kwa sasa inawaambia nini wananchi ambao tayari wameathirika na muingiliano wa Sheria hizo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA) (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria naomba kujibu swali la Mheshimiwa Beatrice Matumbo Shelukindo, Mbunge wa Kiliindi lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kimsingi hakuna muingiliano wala mgongano baina ya Sheria zinazosimamia masuala ya madini, ardhi, maliasili na mazingira. Kuwepo kwa Sheria hizi zilizotungwa na Bunge lako tukufu ni kwa ajili ya kuhakikisha kuwa maliasili, ardhi, madini na mazingira yetu yanatunzwa na kusimamiwa vizuri kwa manufaa ya Taifa na watu wake.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ardhi na mali ni wazi kuwa migogoro ya ardhi, si rahisi kuiepuka. Hata hivyo, migogoro hii haitokani na uwepo wa sheria hizo bali hutokana na uelewa mdogo wa sheria na wakati mwingine ukiukwaji wa makusudi wa sheria unaofanywa na baadhi ya watu. Serikali kuititia Wizara za Sekta husika ikiwemo Wizara yangu itaendelea kutoa elimu kwa umma juu ya utekelezaji wa sheria hizo ili kuepusha migogoro isiyo ya lazima.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwisha kusema katika sehemu (a) hakuna mwingiliano wa Sheria husika zilizotajwa na Mhesihmiwa Mbunge, iwapo kuna mwananchi au wananchi walioathirika kwa msingi niliueleza hapo juu, wanaweza kuchukua hatua kwa kufikisha malalamiko yao kwa mamlaka husika Serikali au katika vyombo vilivypo kama vile Mahakama na Mabaraza ya Ardhi na Nyumba. Aidha, namshauri Mheshimiwa Mbunge, kama anaona kuna vipengele vinavyokinanza ni vyema akafuata taratibu na hatua za kawaida za kuwasilisha vipengele hivyo kwenye Wizara husika ili tuweze kuziangalia kwa pamoja kati ya Wizara yangu na Wizara za Sekta husika.

MHE. BEATRICE M. SHELUKINDO: Asante sana Mheshimiwa Spika. Kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake ya kinadharia. Ninashangaa kusikia kwamba Serikali hajui mwingiliano kwa sababu hizi sheria zinavyoletwa kwenye Bunge letu tukufu haziletwi kwa pamoja. Zinaletwa leo Wizara hii au kesho Wizara ile. Sasa mimi nilikuwa nashangaa nilikuwa niombe Serikali swali langu la kwanza.

Je, Mheshimiwa Waziri na Serikali haioni kwamba kuna haja sasa kwa sababu tatizo hili lipo na tunaosema ni wawakilishi wa watu tunatoka kwenye maeneo tunasema lipo. Na limesababisha umwagaji wa damu. Haoni kwamba kuna haja wao kuagiza Wizara zote husika zikae pamoja na kuangalia Sheria zote kwa pamoja ndipo wao wawahushe labda mamlaka husika kama watataka taarifa zaidi badala ya kumwomba Mbunge alete taarifa ambaye siyo mtaalam wa Sheria? (*Makofii*)

Swali la pili, Waziri amesema kwamba migogoro hii mingine inasababishwa na uelewa mdogo na ukiukwaji kwa baadhi ya wananchi. Mimi niombe niseme ameahidi kutoa elimu. Hiyo elimu itasaidia wale watendaji ambao kuwadhibiti wale watendaji na wataalam ambao hawaifuati sheria? (*Makofii*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA) (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA): Mheshimiwa Spika, Suala la muingiliano, ardhi ya Tanzania imegawanywa katika mafungu matatu. Fungu la kwanza ni ardhi iliyotengwa kwa ajili ya *National Parks*. Hifadhi zingine, bahari na maeneo tengefu.

Ardhi nyingine ni ile ya vijiji ambayo inamilikiwa na Sheria za Vijiji na wanavijiji wenyewe wanazifahamu sheria hizo na jinsi ya kugawa ardhi yao na kumiliki ardhi yao. Ardhi ya tatu, ni ardhi ambayo haiangukii katika eneo hili la hifadhi , ni lile eneo ambalo ni ardhi ya kawaida ambayo inamilikiwa na Kamishna wa Ardhi na zipo Sheria zinazoeleza jinsi gani ardhi hiyo inamilikiwa.

Sasa mgogoro ambao nilidhania inatokea kati ya wachimbaji labda na wakulima au wanakijji. Mchimbaji anapotaka kwenda kuchimba au kutafuta madini anaomba kibali anapewa kibali anakwenda kwenye ardhi ambayo ye ye mwenyewe ameitambua ame-*identify*. Lakini akifika pale atakuta sasa ama ardhi hiyo inaangukia katika moja ya mafungu haya matatu na ni lazima azingatie sheria zinazohusu ardhi hiyo. Ndiyo maana nasema katika Sheria peke yake hakuna mgongano wowote. Upo sasa mgongano anapopata nafasi hiyo ya kufika pale anavamia au haongei na wanakijji akawaambia nakuja kutafuta madini sehemu hii na *therefore* wakishamkuballia awalipe kinachostahili kuwalipa afanye hivyo.

Sasa hapo si mgongano wa Sheria. Mgongano katika utendaji, Sheria ziko *very very clear*. Sheria za Mazingira zinaweka utaratibu wa jinsi gani ardhi tutaitumia vizuri.

Swali la pili la elimu unasema elimu kweli labda haitamsaidia yule anavunja sheria. Anayevunja sheria dawa yake inafahamika. Tunampeleka mbele ya Sheria na kama kuna watendaji ambao wanavunja kwa makusudi, basi tutawapeleka mbele ya Sheria na tufanye hivyo.

Na. 120

Uboreshaji wa Elimu Kupitia Shule za Jeshi

MHE. RUKIA KASSIM AHAMED (K.n.y. MHE. THUWAIBA IDRIS MUHAMMED) aliuliza:-

Huduma ya elimu itolewayo na shule za jeshi kama Makongo na Jitegemee za Jijini Dar es Salaam pamoja na Luhwiko iliyoko Songea imeleta mafanikio:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupanua huduma hiyo Mikoani na Tanzania Visiwani ili kuboresha elimu?

NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Thuwaiba Idris Muhammed, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania na Jeshi la Kujenga Taifa linamiliki shule za binafsi (*private schools*) za sekondari 9 na shule hizo ni:-

1. Makongo Sekondari, ambayo iko Dar es Salaam;
2. Airwing Sekondari, ambayo iko Dar es Salaam;
3. Kigamboni Sekondari, ambayo iko Dar es Salaam;
4. Jitegemee Sekondari, ambayo iko Dar es Salaam;
5. Kizuka Sekondari, ambayo iko Ngerengere Morogoro;
6. Ruhuwiko Sekondari, ambayo iko Songea;
7. Nyuki Sekondari, iko Zanzibar;
8. Kawawa Sekondari, ambayo iko Mafinga Iringa; na
9. Unyanyembe Sekondari, ambayo iko Tabora.

Mheshimiwa Spika, shule hizi zimekuwa na mafanikio katika kutoa elimu ya sekondari kwa vijana wa Kitanzania. Aidha, wastani wa vijana 2,216 huhitimu elimu ya kidato cha nne na wastani wa vijana 1,883 huhitimu kidato cha sita kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa kanda zilizokwisha kufikiwa na shule za sekondari zinazomilikiwa na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania ni Dar es Salaam, Morogoro, Iringa, Ruvuma, Tabora na Tanzania Visiwani kwa maana ya (Zanzibar).

Mheshimiwa Spika, upo mpango wa kuendelea kupanua huduma ya kutoa elimu katika maeneo wanayofanya kazi wanajeshi kwa ajili ya familia zao na raia wanaozunguka maeneo hayo. Shule za msingi na sekondari zinaendelea kujengwa katika vikosi mbalimbali. Aidha, shule za sekondari zilizopo sehemu zilizobainishwa zinaendelea kuboreshwa na kupanuliwa ili kuimarisha huduma ya elimu kwa wanajeshi na familia zao na wananchi wanaoishi jirani na shule hizo.

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Asante sana Mheshimiwa Spika. Pamoja na majibu mazuri lakini naomba nimwulize maswali mawili ya nyongeza. Shule hii ya Nyuki iliyopo Zanzibar ilikuwa ikitoa wanafunzi wengi sana waliokuwa wakifaulu darasa la nne na kidato cha nne kulikoni sasa. Je, Jeshi lini itairejeshea hadhi yake shule hii kwa kuwapatia walimu wa kutosha pamoja na vifaa vyta maabara?

Swali la pili, kwa kuwa shule hii ya Nyuki imerithi mabanda ya maonyesho yaliyopo Mwanakwerekwe. Je, lini sasa Jeshi itawajengea shule ya kisasa ambayo itakidhi haja? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, kwanza hilo swali la shule ya Nyuki ambayo iko Zanzibar kuongezewa walimu na vifaa vyta kutosha. Labda nijibu tu kwa haraka haraka kwamba ni kweli katika jibu langu la msingi nimeelezea kwamba kuna mpango wa kuendelea kupanua huduma ya elimu. Kwa hiyo labda katika mpango unaokuja Shule ya Nyuki inaweza kuingia katika huo mpango.

Lakini niliseme tu kwa haraka haraka kwamba jukumu kubwa la jeshi kwanza ni masuala ya ulinsi. Haya mengine yanakuja tu pale jeshi inataka kuangalia kuhakikisha inasaidia familia zao pamoja na jamii inayoizunguka.

Lakini lingine hilo la kurithi kwa mabanda. Nadhani na lenyewe pia ninaweza kulijibu katika misingi hiyo hiyo kwamba pale itakapofikia muda wa kupanua shule au kuweza kuendeleza mpango wa kupanua huduma za kupanua za kutoa elimu kwa familia za wanajeshi mbalimbali katika vikosi vyao na hapo pia wanaweza kupata hiyo nafasi kama bajeti ikiruhusu. Asante.

Mradi wa Maji wa World Bank Kuchelewa

MHE. MICHAEL L. LAIZER aliuliza:-

Mradi wa maji wa *World Bank* umechelewa kukamilika na wnanchi wamesubiri kwa muda mrefu:-

- (a) Je, Serikali inachukua hatua gani kuharakisha mradi huo?
- (b) Kama mradi huo umeshindikana, Serikali inawaambia nini wnanchi?

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na washirika mbalimbali wa maendeleo inatekeleza programu ya maendeleo ya sekta ya maji nchini kote ilioanza mwaka 2007. Wakati utekelezaji wa programu unaanza kulikuwa na changamoto zifuatazo:- Uwezo wa watalaam wetu ngazi ya Halmashauri ulikuwa mdogo ikiwa ni pamoja na ukosefu wa vifaa, uwezo wa kuandaa mchakato wa manunuzi ya watalaam washauri kulingana na vigezo vinavyotumika na Benki ya Dunia; na katika baadhi ya Halmashauri hakukuwa na watalaam washauri wa kutosha kwa ajili ya ushindani hivyo kusababisha baadhi ya Halmashauri kurudia mchakato wa manunuzi.

Mheshimiwa Spika, hatua zilizochukuliwa na Serikali ili kuharakisha utekelezaji wa programu ni pamoja na kujenga uwezo wa watalaam ngazi ya Halmashauri, kuwapatia vifaa nya kazi kama vile magari, pikipiki na kompyuta.

Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako tukufu kuwa utekelezaji wa mradi wa Vijiji 10 haujashindikana. Hadi sasa mradi huo uko katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama ifuatavyo:- Halamashauri 60 zimekamilisha usanifu na kutangaza zabuni za kuajiri wakandarasi wa kujenga miundombinu ya kusambaza maji.

Halmashauri 22 zimepata kibali cha kutangaza tenda kwa ajili ya kutafuta wakandarasi kwa aili ya kujenga miundombinu ya kusambaza maji. Halmashauri 50 zipo kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji ikiwa ni pamoja na watalaam washauri kundaa taarifa za zabuni kwa ajili ya kuajiri wakandarasi wa kuchimba visima, kufanya usanifu kwa ajili ya kujenga miundominu na kuandaa taarifa za awali na kuainisha kazi zitakazofanyika (*scoping study*).

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri ya Wilaya ya Longido, mtalaam mshauri *Howard Humphrey (T)Ltd* aliajiriwa mwezi Mei, 2009 na amekamilisha usanifu na kuwasilisha tarifa Wizarani. Ujenzi wa miundombinu utaanza Januari, 2012. Katika mwaka wa fedha 2011/2012 Halmashauri ya Wilaya ya Longido imetengewa zaidi ya shilingi milioni 458 kwa ajili ya utekelezaji wa programu.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala hili la mradi wa maji wa *World Bank* vijiji 10 imekuwa ni suala ambalo Wabunge wengi wanauliza kila siku. Nadhani ina miaka 10 sasa Wabunge wakiuliza maswali kuhusu *World Bank*. Je, Serikali haionti kwamba inadanganya Bunge hili na wananchi kutoana na kutoa jibu moja ambalo siyo sahihi mpaka leo? (*Makofii*)

Swali lingine ambalo ningependa kuuliza ni kwamba kwa vile kuna visima vichache ambazo zimechimbwa na maji yakapatikana. Ni lini *World Bank* watakamilisha miradi hiyo ili wananchi wapate maji? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba niweke wazi kwamba hatuwezi kusema *World Bank* wanadanganya. *World Bank* ni wafadhili washirika wa maendeleo. Serikali na wao tumekubaliana tunafanya pamoja na Serikali.

Kwa hiyo haiwezekani tatizo la vijiji liwe la *World Bank* ni Serikali pamoja na *World Bank*. Katika kutekeleza mradi huu tumekubaliana masharti namna gani tutafanya, tunatutumia manunuzi kwa Sheria ya *World Bank*.

Sasa ukifanya hatua moja lazima kwanza waseme sawa endelea hatua ya pili. Mpaka sasa tuna Halmashauri 132. Sasa unazungumza vijiji 1,320. Ni mradi mkubwa. Sasa tunasema kwamba mpaka sasa tumeshafanya vizuri. Kwa sababu kazi kubwa ni ile usanifu.

Kutafuta maji chini ya ardhi siyo kazi ndogo. Sasa hiyo kazi tumeshawenza kufanikiwa. Sasa tuko katika hatua ya kujenga miundombinu. Sehemu kubwa tumeshachimba visima. Sasa tunaenda kwenye awamu ya kujenga miundombinu ili tuweze kusambaza maji kwenye vijiji.

Kwa hiyo naomba niseme kwamba Serikali haijashindwa na wala *World Bank* haidanganyi tunakwenda kwa pamoja. Ndiyo maana tunawaita washirika wa maendeleo.

Swali lake la pili, kwamba katika visima vichache ambavyo vimeshachimbwa, ndiyo maana nimesema kwamba Halmashauri 60 tayari tumetoa kibali watangaze tenda wapate wakandarasi ili waweze kujenga miundombinu na kusambaza maji kama inavyotegemewa.

MHE. PAULINA P. GEKUL: Mheshimiwa Spika, nashukuru kuniona. Kwa kuwa huu mradi ulianza tangu mwaka 2007, almost kama miaka mitano sasa na maji hayatoki. Mheshimiwa Waziri atuambie ni lini maji yatatoka chini ya mradi huu wa *World Bank* kwa sababu visima vyote havitoi maji?

SPIKA: Mradi wa *World Bank* uko nchi nzima, sasa maji hayatoki wapi? Ni wapi huko?

MHE. PAULINA P. GEKUL: Mheshimiwa Spika, kwa Halmshauri ya Mji wa Babati visima vimechimbwa, mpaka sasa hakuna hata kisima kimoja ambacho kimetoa maji. Kwa hiyo, watuambie ni lini? Kwa sababu, inaonekana mradi huu kwa nchi nzima hauelekei kutoa maji pamoja na kwamba, umekaa kwa miaka mitano?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa anasema visima havitoi maji; mimi nasema kuna hatua ambazo tumeshachimba pamoja na Babati, visima vile vinatakiwa vijengewe miundombinu ndio viweze kutoa maji. Lakini maji yapo, yumepima yapo na tumechimba ile hatua ya awali, hatua ya pili ni kujenga miundombinu.

Sasa kuwa *specific* na Babati, hilo swalii kwa sababu sikuwa nimejiandaa itabidi niweze kulifuatilia njue Babati ni visima vingapi ambavyo vina maji na vingapi ambavyo tunaendelea kujenga miundombinu.

Na. 122

Elimu kwa Wenye Salun Kuhusu Maambukizi ya VVU

MHE. LUCY F. OWENYA aliuliza:-

Moja ya sababu za maambukizi ya *VVU* ni kushirikiana kwa matumizi ya vifaa vyenye ncha kali kama vifaa vya kutengenezea kucha katika saluni za wanawake na mashine za kunyolea katika saluni za wanaume:-

(a)Je, Serikali inaeleza nini juu ya matumizi ya vifaa hivyo na uhusiano katika maambukizi ya *VVU*?

(b)Je, Serikali imeshawahi kutoa elimu kwa wenyre saluni juu ya maambukizi ya *VVU*?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, vifaa vya kunyolea na kusafishia kucha vyenye ncha kali katika saluni za kiume na za kike, vikitumiwa na zaidi ya mtu mmoja vyaweza kuwa hatarishi katika maambukizi ya *VVU*.

Ifahamike kwamba, vifaa vyote vyenye ncha kali, iwapo vitamjeruhi mtumiaji na kubeba majimaji yenye *VVU* na kuchangiwa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwagine, vinaweza kusababisha maambukizi hayo. Hivyo basi, ili kuepuka uwezekano wa kutokea kwa maambukizi, mambo yafuatayo yanatakiwa kuzingatiwa kwa matumizi ya vifaa vyenye ncha kali:-

.Kuepuka kuchangia matumizi ya vifaa vyenye ncha kali.

.Vifaa vyenye ncha kali vinapotumika kwa zaidi ya mtu mmoja, ni vyema vikataswa (*sterilisation*) au kuua vijidudu kwa dawa (*Proper Disinfection*).

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kupertia Bunge lako Tukufu, kutoa wito kwa wananchi wote (wake kwa waume) pale inapowezekana, wabebe vifaa vyao vile vyenye ncha kali kama vile nyembe, sindano, nk wanapokwenda saluni ili kuepuka uchangiaji wa vifaa hivyo.

(b)Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imekuwa ikitoa elimu kuhusu njia za kuzuwa maambukizi ya *VVU* kwa wananchi wote wakiwemo watoa huduma za saluni.

Aidha, ukaguzi katika maeneo mbalimbali ya biashara zikiwemo saluni unaofanywa na Maafisa Afya nchi nzima, husaidia kutoa elimu na maelekezo sahihi jinsi nya kutumia na kutunza vifaa hivi kwa wamiliki na watoa huduma katika saluni juu ya maambukizi ya *VVU*.

Kiujumla, elimu kuhusu ufahamu wa *VVU* na maambukizo yake kwa wananchi imekuwa ikitolewa kwa njia za Radio, Televisiuni, Magazeti, Semina na Mikutano katika ngazi zote nchi nzima. Elimu hiyo imechangia kuongeza uelewa kuhusu *UKIMWI* kwa 98% kwa wanawake na wanaume wenyre umri kati ya miaka 15 – 49, kufuatana na takwimu za viashiria vya *UKIMWI* na malaria za mwaka 2007 – 2008.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini kwa uzoefu wangu masaluni mengi yote ya wanaume na wanawake wamekuwa wakitumia *spirit* kama njia ya kuvitakasa vyombo vile ili kuua vijidudu vya *VVU*. Je, matumizi ya *spirit* yanaweza kudhoofisha au kuua vijidudu vya *VVU*?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Mheshimiwa Waziri, amesema kwamba, wamekuwa wakitoa elimu pia katika masaluni jinsi ya kutumia vyombo hivi; ningependa kujua, Je, kuna mwongozo wowote ambao ulishawahi kutolewa na Serikali, jinsi ya kutumia vyombo hivyo kwa usalamu? Kama haujatolewa. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kutoa mwongozo huo?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Lucy Owenya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli *spirit* haiwezi kukidhi hasa kuweza kuuwa wale wadudu ambao kwenye swalii la msingi liliulizwa, *VVU*. Nimeeleza kwamba, njia ambayo ni sahihi kabisa ya kuweza kuwauwa kabisa au kuwadhibiti *VVU* katika saluni ni kutimia mashine ya *sterilisation* ambayo tumewaelekeza kuititia Sheria ya Afya ya Jamii, *Public Health Act 2009*, kwamba hawa wanaoanzisha saluni ni lazima waweke hivyo vitendea kazi vya kuweza kudhibiti hao wadudu.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika jibu langu la msingi nimeeleza kwamba, huwa hawa watumishi ambao Mabwana Afya, wanapofanya ukaguzi katika sehemu mbalimbali za biashara pamoja na hizo saluni, wao huwa wanapita wanatoa elimu ya ufasaha zaidi moja kwa moja kwa hao ambao wanatoa huduma hizo. Kwa sababu, hatari hiyo ya maambukizo haiko tu nkwa wateja wao, halikadhalika hata wao wenyewe kama wasipokuwa waangalifu kwa matumizi sahihi ya vifaa hivyo nao wanakuwa na uhatarishi wa kupata maambukizi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge ameuliza kuhusu mwongozo. Nimeeleza kwamba, pamoja na mwongozo hii iko ndani ya Sheria ya Afya ya Jamii inayoelekeza wazi, inaoanisha ni namna gani ya kuweza kudhibiti maambukizi ya magonjwa haya katika sehemu mbalimbali ikiwemo na saluni.

MHE. EUGEN E. MWAIPOSA: Mheshimiwa Spika, nishukuru kwa kuniona. Kwa kuwa, inasemekana kwamba, baadhi ya watu ambao wameambukizwa *VVU* nao huwaambukiza wenzao kwa makusudi. Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba, inaweka Sheria kali ya kuwapa adhabu watu hawa?

SPIKA: Huko hukosaluni! Mheshimiwa Dokta. (*Kicheko*)

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Mwaiposa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kudhibiti Maambukizo ya *VVU* kwa makusudi, ipo hii Sheria ambayo imepitishwa na Bunge lako Tukufu. Naomba nimkumbushe tu Mheshimiwa Mbunge, tukitoka hapa nimpe nakala ya Sheria hiyo aisome na vilevile apate nafasi ya kuelimisha Wanajimbo wake.

Na. 123

Ombi la Kivuko Kati ya Kijiji cha Nansimo na Kisiwa cha Nafuba

MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA (K.n.y. MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA) aliuliza:-

Katika mchango wangu wa maandishi katika Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ujenzi ya Mwaka 2011/2012 niliomba Serikali iwapatie wana Mwibara boti ya *MV Ukara* kwa ajili ya usafiri kati ya kijiji cha Nansimo na Kisiwa cha Nafuba, pamoja na Visiwa vidogo vya Sozia na Bugeru.

Je, ombi hilo limefikia wapi?

WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Kangi Lugola, Mbunge wa Mwibara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, boti ya *MV Ukara* ilikuwa mali ya Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe. Baada ya kuharibika na Halmashauri kushindwa kuitengeneza boti hiyo ilikabidhiwa *TEMESA*, Wizara ya Ujenzi ikiwa mbovu. Aidha, ukaguzi wa *SUMATRA* ulibaini vifaa vingi vikiwemo vile vya usalama vilihitajika ili boti hiyo iweze kutoa huduma kwa wananchi kwa usalama.

Mheshimiwa Spika, boti hiyo itawekwa kwenye mpango wa kufanyiwa matengenezo makubwa mwaka 2012/2013. Na pindi itakapokamiliika Wizara italfanyia kazi ombi la Mheshimiwa Mbunge, pamoja na maombi mengine yaliyokwishaletwa Wizarani na Wizara itafanya maamuzi ya wapi boti hiyo ipelekwe.

MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na ninamshukuru pia Mheshimiwa Waziri, kwa majibu mazuri. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, kwanza; kwa vile wananchi wa Jimbo hili la Mwibara, hasa visiwa hivyo vya Nafuba na vingine wameshaleta hili ombi rasmi namna hii, basi ni kwa nini isiwe vizuri wakapewa kipaumbele kupewa Boti hiyo mara itakapokuwa imekamiliika ukarabati?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili; kwa vile suala la visiwa hivyo vya Nafuba ni sawasawa kabisa na visiwa vya Maisome huko Buchosa na Serikali imeshatenga bajeti kwa ajili ya ukarabati wa kivuko cha *MV Geita*. Labda Mheshimiwa Waziri, anajua ni lini ukarabati huo utaanza?

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Dokta Tizeba, Mbunge wa Buchosa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi nimesema mara baada ya kufanyiwa ukarabati kivuko cha *MV Ukara*, Wizara itaangalia ni mahali gani kivuko hicho kipelekwe au Boti hiyo ipelekwe kwa sababu maombi ni mengi. Lakini napenda nimhakikishie Mheshimiwa Tizeba na wananchi wa Mwibara kwamba, *priority* ya kwanza itakuwa ni pamoja na visiwa hivyo ambavyo viliombewa na Mheshimiwa Lugola, katika kuchangia hotuba yetu tarehe 02/08/2011. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu kivuko cha Mesome, katika bajeti yetu ya Wizara ya Ujenzi iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu, tulipitisha bilioni 1.271 kwa ajili ya kununulia kivuko Kipyaa cha Mesome pamoja na llagala. Lakini wakati hatua hizo zikiendelea tumeanza kufanya matengenezo ya kivuko cha *MV Geita* ambacho kinaweza kikaendelea kutoa huduma kwenye sehemu ya Mesome, mara kitakapokamiliika kivuko hicho tutakipeleka katika Jimbo la Mheshimiwa Dokta Tizeba ili kikaweze kutoa huduma kwa wananchi wa Mesome ambaa hawana usafiri.

MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Swalii alilouliza Mheshimiwa Tizeba, linafanana sana na suala la Kigamboni. Kwa sasa hivi pantoni ambazo zipo pale Kigamboni, hazitoshelezi mahitaji kutokana na ongezeko kubwa sana la watu. Na ninatambua kwamba, Serikali inatarajia kujenga daraja Kigamboni, mapema mwakani; lakini bado tunahitaji kuwepo na kivuko Kingine pale Kigamboni. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza kivuko pale?

Mheshimiwa Spika, lakini swalii la pili; nilikuwa nataka kujuu pale Kigamboni, upande wa Kigamboni, sehemu ya kusubiria abiria ni ndogo sana. Je, Serikali ina mpango gani wa kupanua? Na ni lini itafanyika?

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dokta Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali na Wizara kwa ujumla inatambua umuhimu wa vivuko katika maeneo ya Kigamboni. Na ndio maana katika bajeti ya mwaka huu zimetengwa milioni 799.415 ambazo zitatumika kwa ajili ya kufanya ukarabati wa kivuko cha *MV Halina*, lakini fedha nyininge zitatumika pia kufanya ukarabati wa kivuko cha *MV Pangani I*, kilichopo huko Tanga.

Mheshimiwa Spika, wakati juhudii zikiendelea za kutengeneza daraja la Kigamboni, Wizara itaendelea kusimamia vizuri vile vivuko ambavyo vinafanya kazi vya *MV Kigamboni* na *MV Halina*, ili viendelee kuvusha watu kwa wakati wote, kwa masaa yote. Na katika eneo ambalo anasema halitoshi, kwa upande wa Kigamboni kule watu wameshalipwa fidia; ningemuomba Mheshimiwa Ndugulile, awashauri wananchi wa kule ambaa wamekaa karibu na maeneo ya kivuko waanze kuondoka ili kusudi wapishe eneo hilo kwa ajili ya kutengeneza eneo kubwa la kupaki *ferry* na kufanya maeneo mazuri kwa ajili ya wanaovuka kwenye *ferry* hiyo.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda pia umeisha.

MHE. MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika!

SPIKA: Jamani, Spika akisimama msimuambie Mwongozo. Maana hata Kanuni ukisoma inasema, kama hakuna aliyesimama! Tena aliyesimama Spika, humpigi Mwongozo!

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni ambao tunao hapa Bungeni. Kuna mgeni wetu Profesa Emmanuel Kilima Bavu, ni mstaafu wa Utumishi wa Umma na wako pamoja na Dokta Kawambwa. Naomba Profesa Bavu, asimame. Sijui amekaa wapi? Kumbe wamekuweka pale! Ulipaswa kukaa *Speaker' Gallary* pale. (*Makofi*)

Profesa pamoja na Kawambwa, wameandika kitabu kimoja ambapo mtagawiwa ninyi hapa. Kinaitwa *Culture of Maintainance, a Sustainable for Development*; atatugawia, wametengeneza kitabu chao kwa muda mrefu. Si mnajua tena sisi watanzania *culture ya maintainance* haipo! Kwa hiyo, kitabu hiki wametupa kama *complementary* na ninadhani mukikipata, mtakisoma vizuri sana. Tunakushukuru sana Profesa na Dokta Shukuru Kawambwa. (*Makofi*)

Halafu nina wageni wengine, wapo wanafunzi 80 na walimu 8 kutoka Shule ya Msingi ya Mlimani Dodoma. Wako wapi walimu na wanafunzi? Ah haa, asante sana, msome kwa bidii. (*Makofi*)

Halafu tuna washiriki 31 wa *Miss Utalii*, kutoka Vyuo Vya Elimu ya Juu, Kanda ya Kati Dodoma, wakiongozwa na Rais wa *Miss Utalii Tanzania*, ndugu Gidion Chipungahelo. Huyo Rais yupo wapi? Gidion Chipungahelo? Wako huku, *okey*. Na wote hawa wengine washiriki wasimame. Haya asante, tutawaona kwenye screen maana huko nyuma kwingine hakuonekani. (*Makofi*)

Tunao wanafunzi 50 kutoka Chuo Cha Elimu ya Biashara, *CBE Dodoma*, naomba wasimame wanafunzi hao walipo! Asante, hawa ni majirani zetu hapa, tunaomba mufanye kusoma kwa bidii sana. Tunao wanafunzi 50 kutoka Chuo Cha Elimu ya Biashara, *CBE Dar-es-Salaam*, na wenyewe wasimame walipo! Ah haa, asante sana tunawatachia musome vizuri. (*Makofi*)

Tuna wanafunzi saba wanaosoma Shahada ya Uzamili, Uhusiano wa Kimataifa, kutoka *UDOM*; hawa wako wapi kutoka *UDOM*? Asante sana, msome kwa bidii, ndio mtakuwa Mabalozi wetu. (*Makofi*)

Tuna viongozi wanne wa Kongamano la Wanafunzi wa Vyuo Vikuu vya Dodoma, hawakutaja ni viongozi wa namna gani! Naomba wasimame hao viongozi wetu hao! *Okey*, wako upande huu. (*Makofi*)

Tuna wanafunzi saba kutoka *Nuru Education Centre Dodoma*, hawa nao wako wapi? Wako maeneo ya huko nyuma! (*Makofi*)

Nina wageni wangu kwenye *Speakers' Lounge*, lakini hamkunipa majina! Naomba mfanye hivyo, nitayatangaza baadaye, maana mimi hapa siwaoni.

Halafu, matangazo ya kazi; Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo kutakuwa na Kikao cha Kamati kitakachofanyika katika Ukumbi wa *Basement* saa 10.00 jioni. Wajumbe wote wanaombwa, Kikao hiki kitafanyika saa 10.00 jioni, kwenye *basement* yetu pale.

Halafu, kuna Mwenyekiti wa Kikundi cha Wabunge Maskauti, huyu ni Mheshimiwa Abdulkarim Shah! Sasa mimi sijajua kama kuna Wabunge Maskauti, leo ndio nimejua. Naomba niwatangazie Wajumbe wa Kikundi cha Wabunge Maskauti kuwa, leo saa 7.15 mchana,

kutafanyika kikao kifupi cha kikundi hicho katika eneo la *Basement*. Sina uhakika kama saa hii ni sawasawa, kwa sababu kuna shughuli ya *TAPAC* kwa hiyo, mtajipanga wenyewe kadiri inavyofaa.

Kwa hiyo, kwa maana hiyo pia, ngoja niseme hapa, Mheshimiwa Missanga, yeze ni Mwenyekiti wa Wanayanga Bungeni, anasema hivi; ninaomba uwatangazie Wanachama na Wapenzi wa *Club* ya Yanga, kuwa kutakuwa na kikao kifupi lakini muhimu kitakachofanyika katika Ukumbi wa Msekwa leo mara tu baada ya kumalizika kwa shughuli za Uzinduzi wa *TAPAC*. Kwa hiyo, ninadhani ninyi mtalewana huko huko. (*Makofi*)

Hawa wanaoandika kwa mkono mimi siwapendi, kwa sababu kila mtu anajua mwenyewe anavyoandika. Anasema Mwenyekiti wa *Club* ya Ngumi Bungeni na Katibu wa Ngumi Bungeni, Mheshimiwa Mangungu na Mlezi wao Mheshimiwa Wasira eti na kocha wao ninasikia ni Mheshimiwa Abuu Hamoud Jumaa, sasa wachezaji hao ni Mheshimiwa Abas Mtemvu, Mheshimiwa Mussa Zungu, Mheshimiwa Amos Makalla, Mheshimiwa Saidi Mtanda, Mheshimiwa Capt. John Komba, Mheshimiwa Salim Hassan Abdallah Turky, Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mheshimiwa Yusuph Abdallah Nassir, Mheshimiwa Livingstone Lusinde, Mheshimiwa Adam Malima na Mheshimiwa Ismail Rage, wanatangaziwa kwamba, kutakuwa na mazoezi leo uwanjani, saa kumi, lakini saa kumi na moja muwe hapa. (*Kicheko/Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, tunaendelea na shughuli inayofuata; Mheshimiwa Vita Kawawa.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninaomba mwongozo wako kuhusiana na usalama wa sisi Wabunge na Watumishi wa Bunge lako na ufanisi wa kazi za Shughuli za Bunge. Kwanza, ninaomba niushukuru sana Utawala, kwa kuimarisha kila siku usalama wetu wa sisi Wabunge.

Tume-experience kwenye Kamati yetu, Bunge linaendelea kuimarisha milango kwa kuweka *electronic door*, lakini katika Kumbi za *Administration*, jana tulipokuwa Ukumbi Namba 133 kwenye kikao chetu, Katibu wetu wa Kamati ilikuwa kazi yake ni kwenda kufungua mlango, kwa sababu alikuwa peke yake mwenye *access* ya ufunguzi wa mlango huo kwa kutumia *electronic card* yake. Kila aliyekuwa anaingia ndani, ilikuwa lazima yeze anyanyuke na alikuwa anashindwa ku-concentrate kwenye kazi ya Kamati. Kiusalama pia siyo vyema, kama lolote linaweza kutokea, mtu mmoja tu ndiyo mwenye *access* ya kufungua mlango, tunaweza kupata madhara Wabunge. (*Makofi*)

Vilevile jana nili-experience kupata huduma katika Ofisi za Utawala, shughuli ambayo ilitakiwa nipate kwa dakika tatu, nilitumia dakika 20, kwa sababu aliyekuwa ananihudumia ndiyo kila mtu aliyekuwa anataka kuingia anakwenda kumfungulia mlango na anayetoka ndiyo aliyekuwa anakwenda kumfungulia mlango. (*Makofi*)

Kubwa zaidi, humu ndani lazima tutumie kadi wakati wa kutoka; mimi ninakubaliana kabisa na kuingia kwa kutumia kadi zetu, lakini wakati wa kutoka, Utawala unaweza kumwelekeza mkandarasi aliywewka *electronic lock* tutumie vitufe kufungulia milango; kama lolote linaweza likatokea humu ndani Wabunge tukihamanika, tutashindwa kutoka tutatumia mlango mmoja tu na tunaweza tukapata madhara makubwa. Ninaomba mwongozo wako Mheshimiwa Spika. (*Makofi*)

SPIKA: Litaangaliwa na Utawala.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Nimesema litaangaliwa na Utawala. Mwongozo kuhusu nini tena.

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO: Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 47.

SPIKA: Isome.

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO: Baada ya muda wa maswali kwisha, Mbunge yeoyote anaweza kutoa hoja kuwa, Shughuli za Bunge kama zilivyooneshwa kwenye Orodha za Shughuli ziahirishwe ili Bunge lijadili jambo halisi la dharura na muhimu kwa umma.

Mheshimiwa Spika...

SPIKA: Dakika moja unieleze ni nini hicho cha dharura.

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO: Mheshimiwa Spika, Wakulima wa Nyanda za Juu Kusini wamelima mahindi mengi sana na Serikali imekuwa ikinunua, lakini kwa sasa Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, ameandika Waraka mahindi hayo yasinunuliwe tena, wakati hao wakulima wamekodi magari kutoka kilomita 30 mpaka 50 kupeleka hayo mahindi kwenye maghala hayo. Wakulima hao sasa wamehamanika na hawajui cha kufanya na muda mfupi ujao Wizara ya Kilimo itapeleka pembejeo ya ruzuku na hawa Wakulima watakuwa hawana fedha za kununua.

Ninaomba mwongozo wako. (*Makofii*)

SPIKA: Anayoyasema Mheshimiwa Mbunge ni kweli yamejitokeza, sasa Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo itayafanya kazi. Dharura siyo ya aina hii. Kwa hiyo, tunaendelea na kazi, Serikali imesikia na itachukua hatua itaeleza inavyostahili. Katibu kwa hatua inayofuata.

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa Mwaka 2011
(*The Constitutional Review Act, 2011*)

(*Majadiliano yanaendelea*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika ukurasa wa 27 wa Taarifa inaonesha kwamba Muswada huu Unasomwa kwa Mara ya Pili, kitu ambacho binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu sikubaliani nacho kwa sababu Muswada huu ulipoletwa kwa Mara ya Kwanza haukuwa umekidhi vigezo hali iliyopelekea urudishwe. Kwa kuwa sasa hivi ndiyo umekidhi vigezo, basi ni vizuri kama ungesomwa kwa Mara ya Kwanza. Kwa hiyo, namwomba Waziri anieleze ni sababu zipi zinazopelekea Muswada huu Usomwe kwa Mara ya Pili na siyo Mara ya Kwanza kama Watanzania wengi wanavyotaka hasa ukizingatia kwamba, Bunge hili linawakilisha mawazo ya wananchi wote.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne, utaratibu wa utendaji kazi wa Tume kifungu cha 16 (b) kinasomeka kwamba, "Tume itaitisha na kusimamia mikutano au Mabaraza katika sehemu na nyakati mbalimbali kama ambavyo itakavyoamua". Kipengele hiki nakiona kama kinaipa Tume uhuru wa kuchagua wapi pa kufanya mikutano na Mabaraza ya kukusanya maoni na hivyo sehemu zingine wanaweza wasipate nafasi ya kuchangia maoni yao kwani itakuwa inategemea uamuzi wa Tume. Kwa kuwa mchakato huu unagusa wengi ni kwa nini kipengele hiki kisisomeke katika hali ya kuirazimisha Tume kuhakikisha inaitisha na kusimamia mikutano au Mabaraza nchi nzima ili kila Mtanzania apate fursa ya kutoa mawazo yake?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Watanzania wengi wamekuwa hawaridhishwi na jina la Muswada kuitwa 'Sheria ya Mabadiliko ya Katiba' na kupendekeza iitwe 'Sheria ya Kutunga Katiba Mpya', je, kwa nini Serikali isisikie kilio cha Watanzania na kuheshimu mawazo yao hasa kwa kuzingatia kwamba wao ndiyo msingi wa mamlaka zote kwa mujibu wa Ibara ya 8 ya Katiba iliyopo?

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatoo, kifungu cha 15 kinampa uhuru Mjumbe wa Tume au Sekretarieti asishtakiwe yeeye binafsi kwa shauri la madai au jinai kutokana na jambo lolote au kitu

chochote atakachofanya au kutofanya kwa nia njema kama Mjumbe wa Tume au Sekretarieti katika utekelezaji wa majukumu na utumiaji wa mamlaka yake chini ya Sheria hii. Namwomba Mheshimiwa Waziri afafanue vizuri hasa ukizingatia kwamba, inawezekana Mjumbe mmoja au zaidi wakawa na uhasama na raia tangu zamani akaamua kutumia Sheria hii hasa kifungu hiki kumlinda na akamdhuru raia na asishtakiwe kwani hajaeleza wazi ni namna gani tutajua kwamba, makosa haya kwa Mjumbe iwapo yaktitea anakuwa anatimiza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu, kifungu cha 4(a), mtu hawezi kuwa Mjumbe wa Tume kama ni Kiongozi wa Chama cha Siasa kwa ngazi zote za Taifa, Mkoa au Wilaya. Lakini nchi hii ni ya wote wakiwemo wanasiwa na mawazo yao pia ni muhimu kwa ustawi wa nchi yetu. Kama hali ndiyo hivyo na inatekelezwa kwa nchi yetu, inakuwa ngumu kwani Muswada huu unamtaja Rais sana kama mhusika mkuu na wakati huohuo yeze ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM). Kwa hiyo, yeze ni kiongozi wa Chama cha Siasa Taifa. Naomba ufanuzi kama Sheria hii hajavunjika au la, kwani yeze kuwa Rais wa nchi haiondoi ukweli kuwa hata yeze bado ni Mwenyekiti wa Chama cha Siasa Taifa.

MHE. DKT. MAUA A. DAFTARI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naunga mkono hoja ya kuupitisha Muswada huu. Hongera Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri ya kuonesha njia. Uamuzi wako wa kutaka kuipitia upya Katiba yetu iendane na wakati tulionao ni wa busara sana na hautokani na *pressure* ya mtu yeoyote.

Mheshimiwa Spika, napenda nilaani kwa nguvu zangu zote kwa niaba ya wapiga kura wangu, manyanyaso yaliyotolewa na Mheshimiwa Tundu Lissu, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani katika Wizara ya Katiba na Sheria. Maneno yake ya kutunyanyasa Wazanzibari ni mwelekeo tosha unaotunesha chuki ya hali ya juu walijonayo Kambi ya Upinzani kwa upande wa pili wa Muungano. Kambi ya Upinzani ielete kuwa Wabunge wa Zanzibar hawapo Bungeni kwa hisani, ila wapo Kikatiba na wajizue kusema mambo yasiyo ya ukweli.

Mawaziri walioeteuliwa na Rais ni kama ifuatavyo:

- (i) Mawaziri wanne (4) kati ya Mawaziri thelathini na wawili (32); na
- (ii) Naibu Mawaziri watatu (3) kati ya Naibu Mawaziri ishirini na moja (21).

Mheshimiwa Spika, Zanzibar hajadai kuongezewa mgawo wa Mawaziri licha ya kuwa Muungano wetu ni wa nchi mbili zilizokuwa na haki sawa Kimataifa. Tunaelewa katika kuungana na Wizara chache tu ndizo zilizoguswa kama walivyokubaliana wakati wa Muungano.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 17 wa hotuba ya Msemaji huyo wa Kambi ya Upinzani, para ya mwisho nanukuu:-

"Uwakilishi mkubwa wa Zanzibar katika Bunge la Jamhuri ya Muungano umetumika kihistoria kwa lengo la kuwatuliza Wanzibari wakati wa Serikali ya Mwalimu Nyerere ilipokuwa inamomonyoa uhuru wa Zanzibar kwa kuongeza orodha ya mambo ya Muungano kwenye Katiba ya Muungano."

Mheshimiwa Spika, maneno yanayofuatia katika para hiyo ni ya kuchochea chuki baina ya ndugu zetu wa Zanzibar na ndugu zao wa Tanzania Bara. Kama hilo linawekera si wapitishe huu Muswada na walizungumzie na kulitolea maoni wakati wa uundwaji wa Katiba Mpya? Nafasi ipo waitumie. Muswada huu hauoneshi upendeleo wowote kwa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 18, Msemaji wa Upinzani anaendelea kusema katika mstari wa mwisho wa hotuba yake, "Yaani ni ujinga kudhani kwamba Bara linawenza kutawaliwa millele na kisiwa kwa sababu utaratibu wa asili haujawahi kufanya kitegemezi kuwa kikubwa kuliko Sayari yake ya msingi." Je, huo ujinga wa Zanzibar umeanza lin? Je, hii ndiyo lugha anayofundisha katika Chama chake?

Mheshimiwa Spika, wakati mwafaka ukifika wa kuunda Katiba Mpya mawazo yake na yale ya Chama chake ya kutaka kuwa na Serikali ya Tanganyika basi wayatoe. Sasa tunaweka misingi ya kufika huko ambako watapata nafasi ya kusema hayo.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Muswada huu pamoja na mabadiliko tuliyoyafanya. Hata hivyo, ninayo maoni machache tu yafuatayo:-

Kwanza, kifungu cha 20(2)(a) – (e). Kipengele cha (a) - (d), ni Wajumbe wanaoingia katika *Constituent Assembly* kwa nyadhifa zao haihitaji *one third* (1/3).

Kipengele cha (e) pekee ndicho kingekuwa sahihi kutaka kiwe na *one third* (1/3) ya Wajumbe 116 wa Tanzania Zanzibar. Hivyo, kipengele (e) kianishwe wazi kuwa ndicho kinachohusika na badala ya kuwa na 1/3 iwe ni sawia kwa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar yaani 50:50.

Pili, katika kuchagua Wajumbe washiriki 116 katika (e) kutoka *institutions* mbalimbali ninatoa angalizo kuwa:-

- (i) *NGO* ziko political affiliated, zichaguliwe zile zinazohusu mambo ya jamii na zisizo za siasa.
- (ii) *Faith based organizations* – siku hizi baadhi ya Mapadri na Masheik ni wanaharakati kweli katika vyama mbalimbali, hilo litazamwe.

MHE. SAIDI M. MTANDA: Mheshimiwa Spika, namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kukubali na kuridhia Muswada huu kuletwa hapa Bungeni kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, pia nawapongeza Watendaji wa Wizara hii ya Katiba na Sheria kwa kazi nzuri ya kuandaa Muswada huu. Muswada umeeleweka vizuri na wale wanaobezza juhudhi hizi wana lao jambo.

Mheshimiwa Spika, ukisoma Muswada huu Sehemu ya Pili, kifungu cha 4 (a) – (k) vinaeleza wazi madhumuni ya Muswada huu. Wanaosema wananchi hawakushirikishwa nadhani hawasemi ukweli.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uteuzi wa Wajumbe, kifungu cha 6 (3) (e), Rais atateua Wajumbe kwa vigezo fulani lakini kifungu cha 6(3)(e) kinasema atateua kwa kigezo anachoona kinafaa. Nadhani kifungu hiki kifutwe na sifa zote zitajwe kwenye sheria.

Mheshimiwa Spika, kuhusu makosa na adhabu, kifungu cha 19(1) – (2) adhabu inayopendekezwa hapa ni kubwa sana nashauri ipunguzwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bunge la Katiba, kifungu cha 20 (2) (c) – (d) na (e) kinataja Wajumbe wa Bunge la Katiba wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, lakini Waziri na Mwanasheria Mkuu wanatajwa tena wakati wao ni Waheshimiwa Wabunge. Sioni haja ya kurudia kuwataja tena kwa nyadhifa zao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu haki ya kupiga kura katika kura ya maoni. Kifungu cha 30 kinataja wananchi wenye haki lakini wapo wananchi ambao wana sifa za kuwa wapigakura lakini hawamo kwenye daftari. Je, ni utaratibu gani umewekwa kwa watu wa namna hii?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Spika, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais Kikwete kwa kuridhia au kuamua kuwa na mjadala wa marekebisho ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, kwa ujasiri na kazi nzuri aliyofanya katika maandalizi ya Muswada huu. Historia itaandika jitihada za Waziri Mwanamke katika kusimamia mabadiliko ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, jambo la kusikitisha ni upotoshaji mkubwa unaofanywa na CHADEMA, Wanaharakati, pamoja na vyombo vya habari kwamba, hatua ya sasa ni kuandaa Katiba Mpya wakati Muswada uliopo sasa ni wa kuandaa mchakato wa kuelekea kwenye untengenezaji wa Katiba kuititia Tume itakayoundwa. Upotoshaji huu una lengo la kuwahadaa Watanzania na kuleta fujo na vurugu nchini, jambo ambalo Tanzania hatukuzoea na tusingependa kufika huko.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali isiwaonee haya wakorofi na kuwabembeleza watu wanaotaka kuvuruga amani na utulivu uliopo nchini. Tabia ya kulea uovu ndiyo inayofanya watu wachache wafanye mambo ya hovyo.

Mheshimiwa Spika, madaraka aliyonayo Mheshimiwa Rais yanamruhusu kuunda Tume bila ya kushirikisha Bunge au mtu yejote. Hivyo, ni vyema tumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais Kikwete, kwa kutupa heshima ya kutoa mchangano katika uundaji wa Tume na kutunga Sheria itakayowezesha Tume kuundwa ili hatimaye wananchi watoe maoni yao bila hofu. Nafasi iliyotolewa na Mheshimiwa Rais ni ya kihistoria na haijawahi kutokea.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwamba Rais ana madaraka makubwa haina mashiko yoyote kwa kuwa Katiba ya sasa ya mwaka 1977 tayari imempa madaraka hayo. Izingatiwe kuwa Rais ni Mkuu wa Nchi na Amiri Jeshi Mkuu, hivyo ndiye mwenye haki ya kuteua Tume na si mtu mwingine. Aidha, izingatiwe kuwa Rais Kikwete amechaguliwa na wananchi walio wengi kuwa kiongozi na Mkuu wa Nchi.

Mheshimiwa Spika, tarehe 12/11/2011, Rais Mstaafu wa Kenya alihutubia Mkutano wa hadhara na kuoneshwa na ITV akasema kuwa, Katiba ya sasa ya Kenya ina mapungufo mengi hasa kwa kupunguza madaraka ya Rais wa Kenya, jambo ambalo litakuwa na athari. Hivyo, tumwachie Rais madaraka yake ya Kikatiba. Watanzania tuwapuuze CHADEMA kwani hawaitakii mema nchi yetu. Tubaki na amani yetu na utulivu uliopo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. BERNADETA K. MUSHASHU: Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Waziri wa Katiba na Sheria, Mwanasheria Mkuu na Kamati walioandaa na kuendelea kuboresha Muswada huu. Nawapongeza sana wadau wote na Waheshimiwa Wabunge amba wameendelea kutoa maoni yao ya kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Wabunge ni wawakilishi wa wananchi, tumeletwa hapa na wananchi hivyo inabidi tutimize matakwa yao. Watu wanataka Katiba hivyo ni jukumu letu kuhakikisha tunaandaa mazingira mazuri ya kuwezesha mchakato uanze.

Mheshimiwa Spika, wenzetu wa CHADEMA walizira wakaondoka, hii ina maana hawataki Katiba Mpya, wanawanyima wananchi haki yao. Kama ni kweli hawataki kushiriki kwenye mchakato mbona mwakilishi wao Mheshimiwa Tundu Lissu alisoma maoni yao? Mimi kwangu naona hii ni fujo, wanalahai umma na vitendo hivyo vinaweza kuchochea fujo nchi nzima. Kuna watu wanachezea amani ya nchi hii. Ni lini Wabunge wa CHADEMA wataacha tabia ya kuzira na kuondoka Bungeni wakati mambo muhimu yanajadiliwa?

Mheshimiwa Spika, kuna upotoshwaji mkubwa unaendelea. Wananchi wanadanganywa kuwa sisi Wabunge tupo hapa tunatunga Katiba Mpya, hii si kweli. Sisi tupo hapa tunajadili na tunaboresha Muswada wa Sheria amba madhumuni yake yako wazi. Ibara ya nne (4) ya Muswada huu inabainisha wazi kuwa madhumuni ya Sheria hii yatakuwa ni:-

- Kuweka utaratibu wa kuunda Tume itakayokusanya na kuratibu maoni ya wananchi.
- Kuweka utaratibu utakaoruhusu wananchi kushiriki kwa mapana na katika kutoa na kuwasilisha maoni yao kuhusu Katiba.

Mheshimiwa Spika, Tume hii ikishaundwa itakwenda kwa wananchi, wananchi watatoa maoni yao yote ambayo wangependa yawe kwenye Katiba. Hivyo tuandae Muswada huu wa Sheria, Tume iundwe ili watu waweze kutoa maoni yao.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 6(1), inasema Rais baada ya kushauriana na kukubaliana na Rais wa Zanzibar atateua Wajumbe wa Tume. Madaraka haya Rais anapewa na Katiba, Ibara ya 37(1) ya Katiba ambayo inabainisha kuwa Rais atakuwa Mkuu wa Nchi, Kiongozi wa Serikali na Amiri Jeshi Mkuu, wale wanaohoji mamlaka makubwa ya Rais watambue kuwa Rais amechaguliwa na wananchi, yeze ni Mkuu wa Nchi, madaraka haya kapewa na Katiba. Kama kuna wanaofikiri Katiba iliyopo ilimpa madaraka makubwa basi tupitishe Muswada huu, Tume iundwe ili wananchi watoe maoni yao juu ya hilo.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa Katiba Mpya utakuwa na hatua mbalimbali kama Muswada huu wa Sheria ya Katiba ya mwaka 2011 unavyoonyesha. Kutakuwa na kuandaa Muswada wa kuunda Tume, ukusanyaji wa maoni, uundwaji wa Bunge la Katiba na kura ya maoni. Naomba elimu ya kina itolewe kwa kutumia *radio*, *TV*, magazeti, machapisho mengine na mikutano ili wananchi waelewe vizuri umuhimu na kinachojiri katika kila hatua. Angalizo, *NGOs* ambazo zinachochea fujo zisiruhusiwe kushiriki.

MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru sana kwa kupata nafasi hii angalau kuchangia kwa maandishi Muswada huu ulioletwa kwetu Bunge na wawakilishi wa wananchi.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa kuamua kuleta Muswada katika kipindi muafaka ili kuweza kupata muda wa kufanya mabadiliko ya Katiba wakati utakapofika.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya kuletwa kwetu ni kuujadili, kuufanya marekebishes pale inapobidi, lakini pia kabla ya kuja Bungeni hapa kwa utaratibu ulipitia Kamati husika na kushirikisha wadau wa pande zote mbili ili kuweza kutoa marekebishes. Baada ya kuititia maeneo hayo Kamati imefanya marekebishes kutokana na michango mbalimbali iliyotolewa na wadau wa maeneo tofauti na wa pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Spika, nawaomba wananchi kuwa makini na kasoro mbalimbali zinazotolewa na wanaharakati kwa maana ya upotoshaji Taifa. Muswada kwa sasa upo Bungeni tunajadili kwa niaba yao na baadaye kuupitisha ili uweze kutiwa saini na Mheshimiwa Rais, baadaye uwe Sheria itakayoruhusu mchakato wa kukusanya maoni ya wananchi kuhusu mabadiliko ya Katiba yao ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, napenda niungane na maneno ya Kamati ya Katiba na Sheria walioyatoa na kuyawasilisha Bungeni hapa baada ya mtoa hoja kumaliza hotuba yake. Naomba marekebishes yazingatiwe kwa kina ili kusaidia Sheria hii kutumika bila vikwazo. Pia nawaomba wananchi kutokusikiliza dhana za upotoshaji zinazoendelea kujitokeza kwani fikra hizo zinawenza kuapelekeea pabaya na lengo ni kutoa maoni yao kuhusu Katiba hapo baada ya Sheria hii kuitishwa na Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, naomba niwaombe Wazanzibar wote kuungana nasi katika kuitisha Sheria hii ili iweze kuwa Sheria baada ya kutiwa saini na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, mambo mengine ni vyama, waipitie kwa umakini mkubwa Katiba iliyopo ya Jamhuri ya Muungano ili kuona changamoto zinazoikabili Zanzibar kwani bila kusoma Katiba huwezi kutoa maoni kwa uhakika.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 20 inayohusu uundwaji wa Bunge la Katiba, Muswada haujaaeleza pahali Bunge hilo litakutana. Pia, Ibara ya 20(2)(e) kuhusu Wajumbe mia moja na kumi na sita watakaoteuliwa kutoka (i), (ii), (iii), (iv) na (v), Muswada haujaaeleza kila asasi zisizokuwa za Kiserikali watakuwa wangapi, asasi za kidini wangapi, Vyama vya Siasa kila Chama watakuwa wangapi, Taasisi za Elimu ya Juu wangapi pamoja na makundi mengine.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo machache, naunga mkono hoja.

MHE. ABDUL R. MTEKETA: Mheshimiwa Spika, napenda kwanza kutoa sifa nyingi kwa Ris wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya M. Kikwete, kwa kukubali Muswada wa Katiba kujadiliwa na wananchi wote.

Mheshimiwa Spika, kitu cha kwanza kabisa nachopenda kuongelea ni elimu ndogo waliyonayo wananchi ya uelewa wa mambo ya Katiba, hayo yote yanafuatia na Chama pinzani kuelezea kinyume na inavyokusudiwa. Kwa kifupi wananchi wengi hawajui kama Muswada huu umeshapitishwa au ndiyo umekuja Bungeni kupitishwa. Ndiyo maana umeleta matatizo.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Serikali ifanye kila njia na iwe wazi zaidi kwa kuwaelimisha wananchi kuwa sasa ni wakati wao wa kutoa maoni yao yaliyo moyoni mwao bila woga ili wananchi wa Tanzania wapate Katiba yao na tunawahamasisha kwamba nafasi hii hutokea mara chache katika maisha na kila mwananchi ajivunie kutoa mchango wake. Sijui hao wenzetu wanaitakia nini nchi hii, kama Uhuru tumeshaupata mwaka 1961, je, hao wenzetu wanataka uhuru gani? Naomba Serikali ilikazie macho jambo hili, tusiache amani tuliyonayo ikapotea na watu wenye uchoyo wa madaraka. Kama ningekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani, naona hayo yangeisha, kwa nini watuchezee hivi? Wanafanya wanavyotaka, wao ni nani? Kwa nini tunawaonea haya? Hao wanataka tuwaonyeshe mfano kidogo washike adabu siyo kulitia Bunge letu Tukufu hasara kila siku mara wamo ndani mara nje. Naona tutunge Sheria waondokao au wasusao Bungeni bila sababu ya maana wasije vikao vitatu posho na mshahara wasipate.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Mungu ibariki Tanzania, Mungu ubariki Muungano.

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Spika, naomba niruhusu nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Katiba, Mwanasheria Mkuu wa Tanzania Bara, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Tanzania Bara na Watendaji wote wa Wizara ya Sheria. Pia niruhusu nimpongze Waziri wa Sheria Zanzibar, Mwanasheria Mkuu wa Sheria Zanzibar, Mwanasheria Mkuu Zanzibar na Watendaji wote wa Wizara ya Sheria Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizi, ninayo machache ya kuchangia na kuboresha Muswada huu. Kwanza, nitamke wazi kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuhusu hadidu za rejea za Tume. Nakubaliana na hadidu za rejea kama zilivyowekwa kwenye Muswada na itakuwa ni vema Tume ikazingatia wakati inafanya kazi zake. Tatizo naloliona hapa ni kwa nini hadidu za rejea zikae ndani ya Muswada badala ya kukaa kwenye jedwali (*schedules*). Faida ya kuweka hadidu za rejea kwenye jedwali (*schedules*) ni kwamba itakapotokea mahitaji ya lazima ya kuongeza hadidu za rejea, Waziri mwenye dhamana atakuwa na uwezo wa kisheria kuongeza hadidu za rejea bila kulazimika kuleta Bungeni Muswada wa mabadiliko na kwa kuwa kazi ya Tume inaweza kuanza mwezi Desemba, 2011 wakati Bunge liko likizo hadi Februari, 2012 hivyo kutokuwepo nafasi ya kutosha kufanya mabadiliko ya Sheria hii.

Mheshimiwa Spika, pili, ni Katibu wa Sekretarieti. Katibu wa Tume inapendekezwa kuteuliwa na Rais. Kwa kuwa Katibu huyu atatakiwa kuwajibika kwa Tume ya kukusanya na kuratibu maoni, ni vema Katibu wa Tume akaajiriwa na Tume kwa vigezo ambavyo Tume itaviweka. Nafasi ya Katibu wa Tume itangazwe na ishindanishwe ili tumpate Katibu bora na mwenye sifa kamili.

Mheshimiwa Spika, tatu ni kuhusu malipo ya wajumbe wa Tume. Malipo ya gharama za Tume yatalipwa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina na malipo ya Wajumbe wa Tume na Sekretarieti watalipwa kwa kadri Waziri atakavyoamua kulingana na Sheria na Kanuni za nchi. Swali langu la msingi sana, Mswada huu hauelezi juu ya malipo ya Wajumbe wa Bunge Maalum. Ni vizuri Muswada uweke kipengele kuhusu malipo ya wajumbe wa Bunge Maalum kwani hili litakuwa ni Bunge la aina yake tofauti na Mabunge yetu ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, nne, ni Katibu na Watumishi wa Bunge Maalum. Nakubaliana na kifungu hiki kinachoruhusu Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano na Katibu wa Baraza la wawakilishi kwa mujibu wa Sheria hii, kuwa Katibu na Naibu Katibu wa Bunge Maalum au kinyume chake. Hii ni sahihi kuwatumia kwa sababu Makatibu hawa wawili wanao uwezo na uzoefu mkubwa sana katika masuala ya uendeshaji wa shughuli za Bunge hivyo watasaidia kwa kiasi kikubwa kazi za Bunge Maalum.

Mheshimiwa Spika, tano, kazi za Tume. Mojawapo ya kazi za Tume ni kuratibu na kukusanya maoni ya wananchi wote hasa raia wa Tanzania. Naomba kushauri Tume ifike kila kijiji hasa maeneo ya pembezoni kama vile vijiji vya Chamuchuzi, Kahanga, Kigarama, Kafunjo, Ruhita, Mushabaiguru, Kanoni, Kandegesho na kadhalika Wilayani Karagwe.

Mheshimiwa Spika, sita, viapo vya Wajumbe wa Tume vitokane na utaratibu utakaowekwa na Bunge Maalum la Katiba kwa sababu humu ndani tunaapa kuilinda na kuitetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa kuwa Katiba hii tunayoapa kuilinda ndiyo tunayokusudia kivunja au kuiua, hivyo Wajumbe wa Tume na Wajumbe wa Bunge la Katiba waape kwa viapo maalum vitakavyowekwa na Tume Maalum.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ABIA M. NYABAKARI: Mheshimiwa Spika, Serikali ihakikishe inaimarisha Sheria zaidi kwani uharibifu umekuwa mkubwa wa kufaja mali za umma, bila hatua zozote kuchukuliwa na uonevu uliokithiri na hasa Mahakamani na vyombo vya Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Spika, Serikali iweke Sheria itakayowazuia (wabana) wezi wa mali za umma kuliko wanavyofikiria sasa kwani Sheria zilizopo sasa zinawapa uhuru uliopitiliza.

Mheshimiwa Spika, Sheria iwekwe ya mtumishi wa Serikali ngazi za juu kutokukaa au kushika nafasi ya utendaji kwa miaka minge hasa Makatibu wa Wizara na Wahasibu wao. Uwepo utaratibu wa watumishi kuzoea kupanda na kushushwa katika utumishi wao.

Mheshimiwa Spika, nchi haiwezi kwenda mbele kwa Sheria zilizozorota hata Mtendaji wa Kijiji au Kata akichangisha na kula hakuna Sheria inayombana na matokeo yake huhamishwa kwenda eneo lingine ikiwa wananchi watalalamika.

Mheshimiwa Spika, kila mwenye Mamlaka ya kushika hela tulipofikia sasa ni yake siyo tena ya Serikali hata taarifa zao utafikiri zimeandikwa Mbinguni zikionyesha maendeleo ya hali ya juu wakati hela zote zikiwa zimeliwa. Hii hupelekea wananchi kushikwa na ghadhabu na kukichukia Chama kilichopo madarakani.

Mheshimiwa Spika, kumweka mtu madarakani hasa nafasi moja mwenye cheo kikubwa chenye maslahi ni kujichimbia kaburi na unapomwondo katika madaraka unatafuta kifo wewe.

Mheshimiwa Spika, nashauri, kwanza, Makatibu Wakuu wa Wizara wawekewe utaratibu maalum si wa muda mrefu. Pili, Sheria ya Fedha za maendeleo ya vijiji ziwe hadharani, wananchi waambiwe kuepuka uchakachuzi. Tatu, kuweka Sheria kwenye miradi yote kuwa wazi kuepuka uchakachuzi wa fedha na uwepo usimamizi wa Serikali na kijiji wakati Mkandarasi anapofanya kazi husika kama vile Wakandarasi na Wataalam wanavyoshirikiana kujenga barabara za lami, kila mtu kwa nafasi yake huwa makini wanapoangalia uchanganyaji wa *ratio*.

MHE. CLARA D. MWATUKA: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii illi nami niweze kuchangia walau machache.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kukubali suala zima la kuwepo kwa Katiba Mpya. Kikubwa ni kumwomba Mwenyezi Mungu ambaye ndiye mweza wa mambo yote.

Mheshimiwa Spika, pamoja na yote, kwanza napenda kutoa ushauri juu ya hali iliyopo Bungeni. Inaonekana badala ya kufanya lililokusudiwa, tunachukua muda mwangi kwa malumbano, jambo ambalo linaleta sura na picha mbaya sana. Inafahamika wazi juu ya watu hawa CHADEMA, sasa mtu ukimjua hakusumbui.

Mheshimiwa Spika, mimi ombi langu, pamoja na kwamba yasemwayo na Wapinzani daima sio ya maana kwa Chama Tawala lakini ni wazi kwamba yapo yasemwayo yaliyo ya maana, hivyo sio vema kupuuza kila jambo. Tupunguze dharau na jazba, kwani yote yana Mungu. Tusione kwamba nchi ipo mikononi mwetu tu kwani kila kilicho na mwanzo kinakuwa na mwisho. Tunaweza kujambia kwamba hali hii ni ya milele lah! Inawezekana ikabadilika na ikawa kinyume na matarajio. Tunasikia nchi mbalimbali ambazo zinachukuliwa na Wapinzani, sasa tukiwa kama tunavyoamini, tukajijengea kwa upande wetu, ikitoea ikawa sivyo, tutajilaumu, itakuja kuwa kilio. Kama kweli imekusudiwa Katiba Mpya, basi iwe mpya kwelikweli itakayokuwa ni ya nchi yaani isiyoelemea upande Fulani. Kwa walio Wakristo, kuna habari katika Biblia ya Modekai na Naaman, ambayo kama Katiba ikielemea upande wa ni yetu basi mfano huo utakumbukwa.

Mheshimiwa Spika, nia yangu ilikuwa ni hiyo tu ya kutoa ushauri na angalizo kwamba tutoe michango yetu tukiwa na lengo la kuitakia nchi amani na utulivu ili sifa ya nchi yetu ambayo imedumu kwa muda wote isipotee. Mungu wetu atupe hekima na busara ili lengo lililokusudiwa litimie.

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA: Mheshimiwa Spika, naomba fursa hii kwa namna ya kipekee kumpongeza na kumshukuru Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa maamuzi yake yaliyo ya busara tele kwa kusikiliza kilio na malalamiko ya Watanzania na kukubaliana nao kuleta Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, sisi Watanzania kwa namna ya kipekee tunatakiwa kujivunia sana jinsi Muswada huu ulivyoletwaha papa Bungeni. Nchi nydingi duniani huwa zinashughulikia Miswada kama hii nchi zao zikiwa katika machafuko makubwa. Sisi tumepata fursa ya kushughulikia Muswada huu nchi yetu ikiwa katika amana na upendo mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa sana, kuna baadhi ya Wabunge wenzetu pamoja na wananchi wameamua kupotosha ukweli pamoja na kuchochea vurugu. Jambo hili naomba tulilaani na tuombe vyombo vyaya dola vifanye kazi yake pale inapotokea Mbunge au mwananchi kwa maslahi yake binafsi anaamua kuchochea vurugu kama tulivyowasikia wenzetu wanaharakati walivyochochea na kurusha katika kipindi cha ITV- kama Muswada huu utapitishwa wataandaa mandamano nchi nzima. Huu ni uvunjaji wa Sheria sababu ni uchochezi ambao utaleta madhara makubwa sana katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, natamka kuwa naunga mkono hoja hii ya Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya mwaka 2011.

MHE. NEEMA M. HAMID: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kunipatia nafasi nami kuweza kuchangia hoja iliyo mbele yetu inayohusu kujadili Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, nami nikiwa kijana ambaye kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu *Inshallah* nitaona miaka mingine 50 hivyo basi nimeona kuna hoja ya kutoa maoni yangu katika hoja hii ya kujadili Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wangu, naomba nijikite kwenye maeneo mawili makubwa ambayo yamefanyiwa upotoshaji mkubwa. Kwanza, ni kuhusu Muswada ultakiwa Usisomwe Mara ya Pili na badala yake Usomwe Mara ya Kwanza. Hili linanisikitisha sana kwamba kuna watu wamefikia hatua ya kusema kwamba Ukiomwe kwa Mara ya Pili wataitisha maandamano nchi nzima. Naomba niwatoe wasiwasi vijana wenzangu na Watanzania kwa ujumla kuwa Muswada huu umefuata taratibu zote zilizopo za kuwasilisha Muswada Bungeni. Kwa maoni yangu, nilivyoupitia Muswada huu, nimeona maudhui yamebaki yaleyale, kwa hiyo, mimi

nashangaa wenzetu wanatumia Sheria au Kanuni gani ya Bunge. Kwa hiyo, maoni yangu ni kwamba tuko katika *right process* hivyo tuendelee kujadili Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, suala la kwanza linalolalamikiwa ni kuhusu mamlaka aliyopewa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuanzisha Tume na kuteua wajumbe katika Tume hiyo ambayo ipo katika kifungu cha 3(5)(6) cha Muswada huu. Mimi sio Mwanasheria lakini nimeapa kuwa nitailinda na kuitetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katiba hiyo hiyo ndio inampa madaraka Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 33(2) ya Katiba inasema Rais atakuwa Mkuu wa Nchi, Kiongozi wa Serikali na Amiri Jeshi Mkuu. Jamani vijana wenzangu tuko watu karibu milioni 40, hivi kweli sisi watu wote kwa wingi wetu tunaweza kuunda hiyo Tume? Mimi nawaomba vijana wenzangu tusikubali kutumiwa vibaya katika hili.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaenda mbali, wasiwasи wangu ni kwamba katika vile vigezo vya uteuzi wa wajumbe kuna sifa zimeainishwa kama vile uzoefu, jiografia, maslahi ya umma, umri na jinsia. Naomba nijikite kifungu cha 6(3)(d) kinachozungumzia umri, mimi wasiwasи wangu ni vipi vijana wataweza kuteuliwa kuwa wajumbe sababu wengi wetu uzoefu hatuna lakini sisi vijana wa chini ya miaka 30 ndio kundi muhimu kushirikishwa katika mchakato huu kwani tunaweza kuona miaka mingine 50 ijayo. Mheshimiwa Waziri naomba ufanuzi katika suala hili wakati wa kufanya majumuhisho yako.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

MHE. KHERI KHATIB AMEIR: Mheshimiwa Spika, Ibara ya 96(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano inaelezea kuundwa kwa Kamati mbalimbali na sharti zilizowekwa.

Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, kwa vile tarehe 5 Aprili, 2011, rasimu ya kwanza ya Muswada huu illetwa Bungeni na Kusomwa kwa Mara ya Kwanza na hii ni kutekeleza sharti la Kanuni ya 84(1) la Kanuni za Bunge, toleo lilitotajwa hapo juu. Kwa hiyo, hoja ya Kambi ya Upinzani haina mshiko kwani imekidhi masharti yanayotakiwa.

Mheshimiwa Spika, uundawaji wa Tume. Mimi nakubaliana na mapendekezo ya kwamba Rais aachiwe kuunda Tume kama Katiba ya Jamhuri ya Muungano 1977, Ibara ya 36 inavyosema. Zaidi sioni sababu ya Rais kuwekewa ulazima wa kushauriana na Mwanasheria Mkuu Bara na Zanzibar kwa vile Rais ni Taasisi na sio kama dhana iliyopo ya kuwa Rais ni mtu. Hii ina maana Rais aachiwe nafasi bila kuwekewa sharti nani wa kumsaidia au kumtaka ushauri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uteuzi wa Tume, nakubaliana na mapendekezo ya Kamati ya Sheria na Katiba ya Bunge kufutwa kwa kifungu cha 6(3)(c) na 6(3)(e) na sikubaliani na mashauri ya Kambi ya Upinzani kuwa uteuzi huo uende na mifumo ya kuzingatia Vyama (*Multiparty Commission*). Je, wale wasio na Vyama watawakilishwa na nani? Sio sahihi na wala sio kweli eti wateuliwa wa Rais watakuwa hawana uhuru kwa vile ni waajiriwa wa Serikali kwani wale wa Chama nao si watakuwa wanafuata mkono na maelekezo ya Vyama vyao?

Mheshimiwa Spika, kuhusu uhuru wa kifalme, Ibara ya 18(2), mimi nadhani Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wamepoteza mwelekeo wanasema Tume isiwasilishe ripoti yao kwa Rais wa Tanzania Bara na Zanzibar, ni mzaha, kumbe wapeleke wapi? Marais ambao ndio wanaunda Tume na wao ndio wanaowajibika kwa mujibu wa Ibara ya 18(2), hili ni sharti la Katiba, nadhani wamechanganyikiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ushiriki wa Zanzibar, mimi nakubaliana na pendekoz la Kamati ya Katiba Sheria na sikubaliani kabisa na mapendekezo, mawazo yote ya Tundu Lissu kwani bila Zanzibar, Tanzania haipo. Kwa hiyo, nchi hizi zote hizi ni sawa na nchi mbili zilizoungana lakini zaidi Tundu Lissu ni Mtanzania na siyo Mtanganyika.

MHE. INNOCENT E. KALOGERIS: Mheshimiwa Spika, nami naomba kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu. Napenda vilevile kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa moyo wa uzalendo waliouonyesha katika dhamira ya upatikanaji wa Katiba Mpya kwa Watanzania wakati tunatimiza miaka 50 ya uhuru wetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria wa Serikali ya Muungano na wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, kwa jinsi kila mmoja alivyochangia uwepo wa Muswada huu mbele yetu leo hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kuwatangazia Watanzania kupitia Bunge lako kuwa uchaugzi umekwisha, CCM ndio Chama kilichopewa ridhaa na Watanzania kuiongoza nchi kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba Serikali iwaambie Watanzania nchi yetu hajatoka vitani, ni juzi tu uchaguzi umekwisha na Rais amepatikana toka Chama cha Mapinduzi ili kuongoza Serikali zote mbili ya Muungano na Mapinduzi Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, dhana ya mchakato wa kuundwa au upatikanaji wa Katiba Mpya kama matakwa ya Watanzania yanavyotaka, ni lazima yaendane na Katiba iliyopo sasa ambayo inampa mamlaka Rais aliyepo madarakani bila kujali Itikadi au anatoka Chama gani?

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu, wagombea wote wa nafasi ya Urais, Ubunge na Udiwani, ni lazima watokane na Chama cha Siasa.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo Rais ye yeyote atakayepatikana baada ya uchaguzi lazima atatokana na Chama chochote cha Siasa. Mfano aliyeshinda kwa sasa na tangu tumepata uhuru, ni TANU na sasa CCM.

Mheshimiwa Spika, kutotaka kutambua mamlaka ya Rais kwa mujibu wa Katiba yetu ambayo imetufikisha hapa, ni kitendo cha uhaini amba kwa mujibu wa Katiba hiyohiyo wote amba kwa makusudi wanapotosha au kupingana na Katiba hii wanatakiwa kushtakiwa.

Mheshimiwa Spika, kukwepa kuitumia Katiba iliyopo katika kupitisha Muswada ambao upo mbele yetu, ni kuvunja Katiba ambayo tumeapa kuitetea na kuilinda wakati tunaapa kama Wabunge.

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni kwetu sisi Wabunge na wananchi, tunasaidiana vipi ili kufanikisha upatikanaji wa Katiba Mpya ambayo itatutoa hapa tulipo na kutupeleka kule tunakotaka kwa matakwa ya wakati tulionao na wakati ujao.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kamperi za uchaguzi zilizopita, viongozi wa CHADEMA na Wabunge wao waliahidi Watanzania kuwa kama wataingia Ikulu wangekamilisha upatikanaji wa Katiba mpya ndani ya siku 100. Imani yangu, Katiba iliyopo ndiyo ingewasaidia kupatikana Katiba hiyo. Ombi langu kwao, naamini walishajiandaa na upo uwezkano wanayo nakala ya Katiba hiyo, watupatie Watanzania tuijoni, tuijadili na tuone kama inakidhi matakwa yetu tuitumie, ili tupunguze hayo maandamano, malumbano na mengineyo ambayo hayana tija kwa ustawi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba niiombe Serikali kuchukua hatua za dhati katika kupambana na watu wachache amba kwa tamaa ya madaraka wanataka kutumia mjadala huu wa Katiba kuharibu amani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. AMINA MOHAMED MWIDAU: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nianze kwa kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa busara na hekima zake, kwa kuruhusu Muswada utakaopelekea mchakato wa Katiba kuanza kuletwa humu Bungeni na kujadiliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mtazamo wangu, Muswada huu una upungufu ufuatao:-

Kwanza, kwa mujibu wa Ibara ya 7(2) ya Muswada, Spika wa Mwenyekiti wa Makamu Mwenyekiti watateuliwa na Rais; ninapendekeza Ibara hiyo irekebishwe na itamke wazi kuwa, mara tu baada ya Wajumbe wa Tume kuteuliwa na kuapishwa ndani ya siku saba, wataamua na kuchagua Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti kutoka mionganii mwao kwa kuzingatia kuwa, iwapo Mwenyekiti atatoka upande mmoja wa Muungano, basi Makamu Mwenyekiti atoke upande mwingine wa Muungano.

Pili, idadi ya Makamishna wa Tume iongezwe. Ibara ya 7(1)(c) inaeleza kuwa, Makamishna wasiozidi thelathini. Kwa kuwa Tume itakuwa na kazi kubwa hadi kupatikana kwa Katiba Mpya na kwa kuzingatia jiografia ya nchi na miundombinu ya mawasiliano; ni vyema Tume ikawa na Makamishna 60 ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu yake.

Tatu, baadhi ya nyaraka zilizoainishwa katika Ibara ya 16(4) ya Muswada kutoonesha mwaka ambazo nyaraka husika ilitolewa. Ninapendekeza Ibara hii irekebishwe ili nyaraka zote ambazo hazijaonesha mwaka, zioneshe. Nyaraka hizi ni pamoja na Hati za Muungano wa Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar, Ibara ya 16(4)(e), Ripoti ya Pamoja ya Tume ya Fedha na Ripoti ya Shellukindo juu ya Changamoto za Muungano, Ibara ya 16(4)(j) na Ripoti ya Wangwe juu ya uharakishaji wa Shirikisho la Afrika Mashariki, Ibara ya 16(4)(k).

Mheshimiwa Spika, kutaja miaka katika nyaraka hizi kutakuza historia na kuwezesha kizazi cha sasa na vizazi vijavyo kutambua mambo muhimu yaliyowahi kuchapishwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Muswada hauweki ulazima wa Tume kuunda Kamati na hautamki aina ya Kamati ambazo zinaweza kuundwa na Tume. Ibara ya 16(10) inatamka kuwa, ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, Tume inaweza kuunda Kamati na inaweza kuipatia Kamati yoyote iliyoiunda kazi za jumla au kazi maalum za kufanya.

Ninapendekeza marekebisho yafanyike ili iwe ni lazima kwa Tume kuunda Kamati kwa ajili ya kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya Tume ya siku hadi siku. Muswada uboreshwwe kwa kutamka wazi aina ya Kamati zitakazoundwa na Tume; mfano, Kamati ya Elimu ya Uraia, Kamati ya Fedha na Utawala, Kamati ya Utafiti na Kamati ya Usafiri, Mawasiliano na Uhusiano na Vyombo vya Habari.

Mheshimiwa Spika, ni vyema pia Muswada ukaweka makadirio ya Wajumbe wa kila Kamati itakayoundwa; mfano, Kamati iwe na Wajumbe watatu hadi watano au saba na kadhalika; na pia ielete iwapo Mjumbe anaweza au hawesi kuwa Mjumbe wa Kamati zaidi ya moja na kadhalika.

Tano, Muswada haujaweka kifungu chochote juu ya mambo yanayoweza kusababisha Mjumbe wa Bunge la Katiba kupoteza sifa za kuwa Mjumbe na namna uteuzi wa Mjumbe mwingine kuziba pengo la Mjumbe aliyekosa sifa (*cease*), utakavyofanyika na kwa kuzingatia muda. Ili kuwa na Bunge la Katiba lillio katika mfumo wa kidemokrasia na unaotekelzeza ni vyema pawe na kifungu/vifungu vinavyoainisha wazi namna Mjumbe wa Bunge la Katiba anavyoweza kupoteza sifa na hivyo kukoma kuwa Mjumbe wa Bunge la Katiba. Mfano, kwa kufariki dunia, kuijuzulu na kadhalika. Kwa maana hiyo, pawe na kifungu kinachoonesha namna Mjumbe wa kuziba nafasi anavyoweza kupatikana.

Sita, Tume kutoshtakiwa kwa kosa lolote kwa mujibu wa Ibara ya 10 na 19 ya Muswada. Pendeleko ni kuwa ni vyema Tume ikapewa hadhi ya kuwa mtu kisheria (*legal personality*) ili iwe na sifa zote za kishtaki kwa kutumia jina lake au pale inapobidi kushtakiwa ili kudumisha ufanisi wa utendaji kazi wa Tume na Wananchi kuwa na imani nayo kadiri itakavyokuwa.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, ninampongeza Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Celina Kombani, kwa kuwasilisha vyema Muswada huu Bungeni. Vilevile ninatumia fursa hii kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Mama Pindi Chana na Wanakamati wote, kwa kazi nzuri na ngumu walijofanya toka walipokabidhiwa kazi ya Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maoni mengi yaliyotolewa na Wabunge wenzangu, mimi nina maoni katika kifungu cha 21(4). Kwa kuwa Wabunge wa Bunge la Katiba watafanya kazi maalum ni wajibu kuweka au kuongeza kifungu kidogo cha (b) au vinginevyo ili kutaka Wabunge wa Bunge la Katiba nao wale kiapo kama Spika na Naibu Spika wa Bunge la Katiba watakaochaguliwa na Wabunge hao kabla ya kuanza kazi yao.

Mheshimiwa Spika, hii itasaidia sana sababu tusichukulie Wabunge wa Jamhuri ya Muungano na Wawakilishi wa Baraza kwa kuwa wao walishaapa mbele ya mamlaka zao basi tena. Kuna umuhimu wa wao kuapa tena na pia kutakuwa na Wajumbe wengine wasiopungua 116 kutoka Taasisi mbalimbali ambao wakishateuliwa watakuwa Wabunge halali wa Bunge la Katiba kwa mujibu wa Muswada huu; hivyo, hawana budi nao wawe wameapa na kula yamini kabla ya kuanza kazi.

Mheshimiwa Spika, sasa tupo katika mchakato wa mwanzo wa kutunga sheria itakayolinda utaratibu mzima wa zoezi hili la mabadiliko ya Katiba. Tunachotakiwa hapa ni kuendelea kuaminiana na sisi ndiyo mliotuchagua kisheria kabisa ili tuweze kufanya kazi ya uwakilishi wenu katika kutunga sheria na kusimamia Serikali kwa mujibu wa taratibu tulizojiwekea wenye, mojawapo ni Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Spika, jambo lolote linaloletwa na kuwekwa Mezani humu Bungeni, linaendeshwa kwa mujibu wa Kanuni tulizojitungia sisi wenye, Wabunge ili kuendesha Shughuli za Bunge. Sasa, Muswada huu uliletwa na Kusomwa kwa Mara ya Kwanza na kwa mujibu wa Kanuni, Muswada ukishasomwa Mara ya Kwanza unatakiwa pia uende katika Kamati na kujadiliwa pia na *Public Hearing* na kuchukua mawazo yao.

Katika Muswad huu hili ilifanyika na kwa mujibu wa Kanuni, kazi za Bunge zinafanyika Dodoma, Dar es salaam na Zanzibar na kazi hii ilifanyika katika vituo vyote hivyo na Wadau walitoa michango yao wakiwemo Wananchi wa Kawaida na Taasisi za Kiraia, Chama cha Majaji Wastaafu, *TLS*, *TGNP*, *TAWLA*, *WILAC*, *LHRC*, *NOLA*, *TUCTA*, Mfuko wa Mwalimu Nyerere, *UDSM*, *UDOM*, *UZNZ*, *U-Mzumbe*, Chuo cha Mipango na Chuo cha Elimu ya Blashara (*CBE*).

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichukua mawazo na kuyaingiza katika vipengele vingi na umebadilishwa kwa utaratibu wa Kibunge, kwa mujibu wa Kanuni umeletwa kwa mara ya pili sasa tuujadili kwa taratibu za Kanuni za Bunge la Wananchi ambao wamewachagua; na kama kuna jambo Mwananchi anaona lingehitaji kuongezwa au kurekebishwa, tumieni Wabunge ili sasa walete kwa utaratibu wa Kibunge na kujadiliwa humu ndani.

Mheshimiwa Spika, sasa kama Mbunge wako ametoka kwa kususa haisaidii, anawanyima haki yenu ya Kikatiba, Kisheria na Kikanuni ya kuwakilisha mawazo yenu. Bunge hili ni la watu wote wa Tanzania na ndiyo mliotuchagua. Ninataka niwahakikishie haki yenu ya kutoa michango yenu ya mabadiliko ya Katiba ipo pale pale. Tunachoandaa ni utaratibu wa Wananchi kutoa maoni yao kwa mujibu wa sheria. Tulio wengi, mliotupa ridhaa, Wabunge wa CCM tumekuwa tukitambua haki ya Wananchi ya msingi kwa miaka mingi toka tupate Uhuru. Tutaendelea kuilinda na kuiheshimu haki hiyo.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu muhimu sana wakati huu; ni muda mwafaka sambamba na kusherehekea Miaka 50 ya Uhuru wetu. Ninampongeza Mheshimiwa Waziri na Mwanasheria Mkuu, kwa kusimamia vyema mchakato wa Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja na ninashauri tusonge mbele (*aluta continua*), ili Mheshimiwa Rais aweze kuunda Tume husika itakayokusanya maoni ya Wananchi kwa pande zote za Muungano. Mheshimiwa Rais, anayo nia nzuri juu ya kupata Katiba Mpya. Alitatua mgogoro wa Zanzibar mpaka mwafaka ukapatikana; kwa nini CHADEMA hawamwamini Mheshimiwa Rais?

Mheshimiwa Spika, Wabunge wa CHADEMA hawaelewii dhana nzima ya uwakilishi. Rais, Wabunge na Madiwani ndio Wawakilishi halali wa Wananchi na si Wanaharakati.

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kuendesha mambo ya Kitaifa kiholela; Rais ni lazima asimamie suala hili nyeti kwa kuunda Tume na hatimaye kupokea Ripoti juu ya Maoni ya Wananchi.

Mheshimiwa Spika, ninawasilisha.

MHE. RIZIKI OMAR JUMA: Mheshimiwa Spika, ninaomba nitoe mchango wangu kwa kuanza kuunga mkono hoja iliyoko mbele yetu kwa asilimia mia moja. Pia ninataka nitumie nafasi hii, kumpungeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutuwekeea historia katika nchi yetu, kwa kukubali kutuletea Muswada huu ambaa utapelekea kuundwa kwa Tume itakayotuwezesha kufikia kwenye kuandaa Katiba Mpya ya nchi yetu. Nitumie nafasi hii vilevile kuwasihii Watanzania wakubali tuupitishe Muswada huu kwani ndio utakaopelekea wao kupata fursa ya kutoa maoni yao kuhusu Katiba gani ambayo wangependa kuwa nayo, kwani nyumba bila msingi haiwezi kuwa madhubuti. Kupitisha Muswada huu ni mwanzo wa kuandaa Katiba yetu. Hivyo basi, wasikubali kuyumbishwa na watu wachache wasioitakia mema nchi yetu. Tukatae mawazo yao kwa nguvu zetu zote.

Mheshimiwa Spika, kwanza, ninaomba ufanuzi katika kifungu cha 6(4)(b) kuhusu kukosa sifa za kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Tume. Kifungu hicho kimemtaja Mtumishi wa Vyombo vya Usalama. Hawa ni watu ambaa kwa kawaida hawatambuliki ovyo ovyo; je, tutahakikishaje?

Pili, Wajumbe wa Tume, Kifungu cha 7(1)(c), Makamishna wasiozidi thelathini; je, watapatikana kwa mgawanyo upi?

Mheshimiwa Spika, tatu, Kifungu cha 4(2), Wajumbe wa Tume na Sekretarieti kulipwa kwa kadiri Waziri atakavyoona. Ninaomba Waziri aweke kiwango maalum.

Mheshimiwa Spika, sina wasiwasi na Muswada huu.

MHE. MODESTUS D. KILIFI: Mheshimiwa Spika, ninaomba kuchangia Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa Mwaka 2011. Ninampungeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuridhia Muswada huu uweze kujadiliwa na Watanzania ili kutoa maoni yao kadiri watakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Spika, Katiba ni uhai wa Taifa lolote Duniani. Kamwe tusikubali baadhi ya watu (kikundi cha watu), kubeza maandalizi ya mabadiliko ya Katiba. Matokeo ya kuacha makundi ya baadhi ya watu kuendelea kubeza na kuwadanganya Watanzania juu ya nia nzuri ya Serikali na Wabunge ya kutaka kuunda utaratibu mzuri wa namna gani fursa zitatolewa kwa Watanzania ili kuchangia hoja hii muhimu, ni hatari kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, ninashauri jitihada za kuendelea kuwaelimisha Wananchi juu ya ukweli wa jambo hili muhimu Kitaifa, ziendelee kwa nguvu zote. Aidha, amani, upendo na utulivu wa Watanzania tulio nao, tuutetee bila kuwaonea haya wanaotaka kutupeleka pabaya. Gharama ya kuvirejesha tukishapoteza ni kubwa mno. Tusikubali, Mkuu wa nchi hii ni mmoja tu; tumtii atuongoze hadi mwisho wa mjadala huu.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

MHE. AMOS G. MAKALLA: Mheshimiwa Spika, kwanza, ninachukua fursa hii kuunga mkono hoja hii. Ninampongeza Rais kwa uamuzi wa busara kukubali wazo la kufanya marekebisho ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ni mzuri. Kamati ya kukusanya maoni itakapoundwa, iyafikie makundi yote muhimu; Wakulima, Wafugaji, *NGOs*, Wawakilishi wa Dini zote, Wasomi, Wanafunzi wa Vyuo na Sekondari na Wananchi wote mpaka Vijijini. Watakaota maoni wawe huru kwa lengo la kuboresha Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wajumbe 116 watakaoteuliwa na Rais, pamoja na kuzingatia sifa zilizotajwa, uteuzi uzingatje jiografia na Muungano.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninapenda kuipongeza Serikali yangu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uamuzi wake wa busara wa kufanya maamuzi ya kuwa na Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu katika hoja iliyopo juu utajikita katika maeneo yafuatayo: Umuhimu wa Katiba; nafasi ya Mheshimiwa Rais; upotoshwaji wa taarifa; na wito kwa Wanawake.

Mheshimiwa Spika, kwanza, ninapenda nichangie kuwa ni muhimu kuwa na Katiba Mpya. Kwa kuwa tumefikia Miaka 50 ya Uhuru ni bora tukawa na Katiba Mpya inayօenda na wakati tulionao. Tumekuwa na mambo mengi yanayohitajika kuingia katika Katiba.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchukua nafasi hii kuomba Wananchi waweze kutambua Rais ni nani na ana wajibu wake kwa nchi yake.

Mheshimiwa Spika, madaraka aliopewa Rais siyo makubwa lakini ni yake na anastahili kupewa madaraka na maamuzi yake ndiyo maamuzi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na upotoshwaji wa Taarifa na hasa katika Mikoa yenye Miji Mikuu; kumeandaliwa majukwaa yasiyo na ukweli ambayo wanatishia Wananchi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali yetu iwe na meno kwa wale wanaosema ovyo na kuchanganya Wananchi waache mara moja tabia mbaya ya kupotosha Wananchi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nichukue nafasi hii kuwaambia Wanawake wenzangu wa Mkoa wa Dar es Salaam na Tanzania kwa ujumla kuwa, tufanye kazi kwa bidii tuinue uchumi wa nchi yetu. Utakapofika wakati wa kupeleka maoni yetu katika Tume kuomba uwakilishi wa Wanawake katika makundi mbalimbali ikiwemo Wakulima, Wafanyakazi, Wajasiriamali na Vyama vya Walemaru, tujitokeze kwa wingi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, Muswada upite twende kwenye mchakato wa kupata Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS: Mheshimiwa Spika, jina la Muswada ni refu lakini limejitosheleza kulingana na maudhui ya Muswada huo, limekidhi haja.

Mheshimiwa Spika, jinsi Muswada ulivyoandaliwa tayari umekidhi haja kwani hadidu za rejea zipo katika kifungu cha 8, 9 na 16. Pia ilibidi zilandaliwe ili ziingizwe kwenye Jedwali kupunguza kelele na kuipunguzia kazi Tume itakapoanza kazi ikute majukumu yapo tayari.

Mheshimiwa Spika, Kifungu namba 24, wakati Bunge Maalum, linapitisha Rasimu ya Katiba, itabidi kupiga kura pande zote mbili na kila upande upate theluthi mbili; je, kama haikufikiwa kat

ya upande mmoja hatma yake itakuwa nini; na hapo siyo kukwama kwa mchakato mzima wa Rasimu ya Katiba? Ningeliuomba ulizungumzie kwa kirefu ili kuwaondolea Wananchi utata.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 30 kinazungumzia juu ya kupiga kura ya maoni; pande zote zinatakiwa kutumia Daftari la Kudumu la Wapiga Kura hilo, halina mjadala. Kifungu namba 32 kinasema kwamba, matokeo ya kura za maoni yatatangazwa na Tume ya Taifa (*NEC*) tena iheshimiwe. Ningeliomba na *ZEC* ya Zanzibar ishirikishwe wakati wa kutangaza matokeo ili nayo iweze kutoa baraka zake, isiwekwe kando baada ya kumaliza uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Wawakilishi wanaingia kwa nafasi zao kwenye Mchakato wa Bunge Maalum. Kwa kuwaingiza Waheshimiwa Mawaziri wa Sheria na Wanasheria kuingia kwa vyeo vyao, hilo halikubaliki kwani Vlongozi wote ndani ya Bunge Maalum ni sawa na Vlongozi wao ni Mwenyekiti na Naibu Mwenyekiti na Waziri wa Sheria na Wanasheria wawe ni Wajumbe kama walivyo Vlongozi wengine.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE: Mheshimiwa Spika, kwanza, ninaipongeza Serikali na hasa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Kikwete, kwa kuwa Muungwana wa hali ya juu, kwa kuruhusu Muswada huu uletwe mbele ya Bunge na kujadiliwa. Kwa kufanya hivyo, Rais Kikwete ametuthibitishia kuwa yeye ni mpenda demokrasia kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, pili, ninaomba Watanzania watambue kuwa, Rais ni Mkuu wa Nchi kama Katiba inavyotuelekeza na ndiyo maana ye ye anabeba dhamana ya kutuongoza Watanzania wote. Hivyo, lazima Rais apewe mamlaka makubwa ili aweze kupata nguvu ya kututumikia. Rais ni lazima awe na mamlaka, hata ndani ya nyumba baba ndiyo anayebeba dhamana ya kuongoza nyumba. Wanaopinga mamlaka ya Rais wana lao jambo.

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, kutohana na maoni yangu, Katiba Mpya inawezekana kuwepo na kuwa shida. Kwa sasa Katiba Mpya ni gharama kubwa, wakati Tanzania hatujitoshelezi kwa uchumi, msimamo wangu nilihitaji kwa sasa tushughulikie madai ya Watanzania wanaodai Katiba Mpya ni gharama kuwa kuna nchi zilifilisika kwa gharama kubwa ya kuandaa Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, pili, haiwezekani Rais akapunguziwa madaraka wakati ye ye ni Amiri Jeshi Mkuu; kwa nini asiwe na madaraka makubwa? Kwa maoni yangu, kwa kuwa kwa sasa Tanzania hakuna pesa za kutosha na mchakato mzima unahitaji pesa, ninaomba mchakato huu upunguze watu wawe wachache katika kujadili Katiba.

Mheshimiwa Spika, ninapendekeza kwamba, hakuna haja ya Katiba Mpya ila baadhi ya vipengele vyake vifanyiwe marekebisho tu.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja mia kwa mia.

MHE. BRIG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI: Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, kwa sababu ya vigezo vyote ambavyo vimekusudiwa kulifikisha Taifa kuanzisha na kumaliza mchakato wa kupata Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ninawasilisha.

MHE. WARIDE BAKARI JABU: Mheshimiwa Spika, kwanza, ninapenda kutoa pongezi kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuleta Muswada wa Mabadiliko ya Katiba na kutunga Sheria ya Kuundwa Tume ya Mabadiliko ya Katiba kwa faida ya Nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ninatoa mapendekezo yafuatayo:-

Kutokana na Jina Refu la Muswada huu, ninashauri jina liliopendekezwa lipunguzwe au likarabatiwe na liwekwe katika mfumo wa maana iliyokusudiwa na kwa ufupi.

Ibara ya 16, sehemu ya nne - Utaratibu wa Utendaji kazi wa Tume; ninaishukuru Sheria kwa kuweka utaratibu katika Ibara hii na vipengele vingi vinatekelezeka isipokuwa ninashauri kutungwe Sheria Maalum ya Kinga kwa watakaoshiriki kwenye Bunge hili la Katiba; na pia kuwepo na Sheria au Miongozo Maalum ya Kura za Maoni.

Ibara ya 18 - uwasilishaji Ripoti ya Tume; ninashauri badala ya Rais kumwagiza Waziri kuwasilisha Muswada kwa Waziri, ninaomba Muswada huu Rais amwagize Mwenyekiti wa Tume kuwasilishwa Muswada wa Katiba katika Bunge la Katiba.

Kuundwa Bunge la Katiba: Ninashauri Sheria hii ifafanue zaidi pale kifungu cha 20(e) Wajumbe 116 watakaoteuliwa haikutajwa Wanawake watakuwa asilimia ngapi katika kundi hilo na sifa za hao watakaochaguliwa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. HUSSEIN NASSOR AMAR: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninaunga mkono hoja iliyoko mbele yetu kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, ninaomba mchakato huu tuubariki ili Mheshimiwa Rais aunde Tume yake ianze kazi mara moja.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kusema kuwa, ninaungana na wote ambao wameunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

MHE. RAMADHAN HAJI SALEH: Mheshimiwa Spika, ninaomba nichukue nafasi hii nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuweza kutufikisha hapa Bungeni tukiwa katika hali ya uzima.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umekuja kwa wakati mwafaka kwa Watanzania ambao wanahamu na maendeleo ya nchi yao.

Mheshimiwa Spika, ukiisoma Hotuba ya Mheshimiwa Tundu Lissu ni ya upotoshaji sana. Hotuba ambayo haiwatakii mema Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, katika kuliona hilli, ninaomba Serikali iwe macho kuwaelimisha Watanzania waweze kuelewa madhumuni ya Muswada huu; kwa kuwa Watanzania wengi hawafahamu Katiba ni nini na hasa Wananchi ambao wanaishi Vijijini.

Ninaomba nijikite kwenye Muswada, kifungu cha madaraka ya Rais, kama wanavyodai Wapinzani kuwa apunguziwe madaraka. Madaraka ya Rais, ninaomba yasiingiliwe na yaachwe kama yalivyo. Rais ndiye Mkuu wa Nchi na Rais huyo huyo ndiye Amiri Jeshi Mkuu wa Nchi, kumtaka apunguziwe madaraka, huko ndiko kumdhihaki Kiongozi wa Nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa maoni yangu na kwa kuwa Wabunge wengi wameshachangia mengi, ninaomba niseme Muswada huu umekuja wakati mwafaka na ujadiliwe ili hatua zinazofuata ziendelee.

MHE. MUSSA HASSAN MUSSA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninachukua nafasi hii kumshukuru Mungu nami kwa kupata nafasi walau ya kuchangia Muswada huu kwa maandishi.

Pamoja na kutupa muda wa siku tatu kuchangia Muswada huu, bado muda huo haukumruhusu kila Mbunge kuchangia kwa kuzungumza. Hii ni kutokana na umuhimu wa suala lenyewe.

Mheshimiwa Spika, pili, ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Wizara ya Katiba, kwa umakini wake na uzalendo wake, kufanikisha Kusomwa kwa Mara ya Pili kwa Muswada huu, pamoja na *pressure* za Wanaharakati na upotoshaji wa makusudi ambao hauitakii mema Nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ninaomba niende moja kwa moja kwenye mchango wangu, juu ya Muswada ambao uko katika Meza yako au Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kipengele namba 20(1) na (2) katika Tamko la Bunge la Katiba, kwenye vipengele (a) – (e) kuhusiana na namna ya kupatikana Wajumbe; ninaomba kupendekeza kwamba, kwenye kipengele (e), mgao uwe nusu kwa nusu kwa pande hizi mbili za Muungano kwa maana ya idadi 58 bila kujali wingi na uchache wa watu katika nchi hizi.

Mheshimiwa Spika, ahsante na ninaomba kuunga mkono hoja.

MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninampongeza Waziri wa Katiba na Sheria kwa Hotuba nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuleta Muswada huu Bungeni ili ujadiliwe.

Mheshimiwa Spika, sote tunajua kuwa, Muswada huu unalenga kuweka utaratibu utakaowezesha Taifa letu kupata Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na mapendekezo ya Muswada kwamba, Rais kwa mamlaka yake kama Mkuu wa Nchi, aachiwe madaraka ya kuunda Tume anayopewa na Ibara ya 33 na 34 kuhusu mamlaka ya Rais na Ibara ya 36 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Mheshimiwa Spika, Tume hii itakusanya maoni ya Wananchi na ipewe muda wa kutosha kupitia makundi yote, kwani wao wenyenchi hii Mijini na Vijiji.

Mheshimiwa Spika, pia Elimu itolewe vya kutosha ili Watanzania waelewe kwani wengi wanapotoshwa, Muswada huu upelekwe vizuri ili tupitishe Muswada huu vizuri.

Mheshimiwa Spika, Watanzania tunahitaji amani na utulivu, kwani kuna wachache wanaotaka kutuharibia amani hii tunayoiensi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ninamalizia kwa kusema ninaunga mkono hoja hii.

MHE. SAIDI R. BWANAMDOGO: Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja. Hata hivyo, nina maoni kadhaa katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, nina hisia za nchi mbalimbali kuingilia mchakato huu kwani kuna taarifa kuwa, kuna Kiongozi mmoja wa nchi fulani, jana tarehe 15 Novemba, 2011, alikutana na Wabunge wa CHADEMA huko VETA Dodoma. Hivyo, ni vizuri Serikali ikalifuatilia jambo hili.

Pili, hoja juu ya madaraka ya Rais; Kifungu hiki kiko sawa na hakuna haja ya kuyapunguza majukumu ya Rais. Wanaohoji madaraka ya Rais ni kutokana na chuki binafsi tu ama za kisiasa au vyovoyote vile. Rais ni Taasisi na siyo vizuri Rais kumwona kwa jina lake au kwa Chama chake.

Tatu, Ibara ya 20; ninaomba kujulishwa Kanuni iliyotumika kuwapata Wajumbe 116; kwa nini wasiwe zaidi au pungufu ya waliotajwa?

Nne, Jukwaa la Katiba; kikundi hiki kwa mtazamo wangu hakina nia njema na jambo hili. Juzi, Jumapili, niliwasikiliza wachangiaji kwenye Mkutano ulioandaliwa na Jukwaa la Katiba,

nilichokiona ni kwamba, wachangiaji wote walikuwa na sura ya uharakati tu. Serikali iwaangalie sana waandaaji wa Jukwaa la Katiba.

MHE. JITU VRAJLAL SONI: Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchukua nafasi hii, kwanza kabisa, kuishukuru Serikali kwa kuleta Muswada huu muhimu wa kubadilisha Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Kamati ya Bunge pamoja na Wizara ya Katiba na Sheria kwa kazi nzuri waliyofanya.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na ushauri; ninaomba katika vipengele vyta Mwanasheria wa Jamhuri na Zanzibar, waondolewe katika kumshauri na kuchagua Tume ya kuratibu maoni ya Wananchi kuhusu Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, pia ningeshauri liangaliwe upya suala la theluthi mbili na ili pasiwe na mashaka au mgongano; itumike *simple majority* pande zote mbili za Jamhuri.

Mheshimiwa Spika, pia ninashauri Serikali itoe tamko maalum kuhusu upotoshaji unaotolewa na baadhi ya Taasisi na Viongozi wa Kisiasa kuhusu mpango mzima wa kufikia kuundwa Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, ninaomba ufanuzi; sijaelewa kabisa Mbunge anapotamka hapa Bungeni kuwa Rais amepewa Mamlaka makubwa na ni Rais Mfalme na asiteue Tume na kuunda Bunge la Katiba; je, kwa Katiba ya sasa na Sheria zilizopo nani mwingine ana mamlaka ya kuitisha Tume na kuteua Wajumbe zaidi ya yeye Rais wa Jamhuri na Kiongozi Mkuu wa Nchi?

Mheshimiwa Spika, Bunge la Katiba lipange na lijamulie Kanuni bila sisi kuingilia haki yao.

Mheshimiwa Spika, ningeshauri Elimu na Tamko la Serikali kuhusu maamuzi na malengo ya Muswada huu itolewe kwa Raia wote na hasa Vijijini ili wasipotoshwe.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja na tusonge mbele.

MHE. KAIKA S. TELELE: Mheshimiwa Spika, kwanza, ninaunga mkono hoja. Kwa kuwa Muswada huu unatumwi na Wapinzani kupotosha Umma na kujitafutia umaarufu wa kisisasa, ninashauri upitie hatua zote za Kisheria na uwekwe wazi na Tume kwa Wananchi kuujadili kwa kina na kwa muda wa kutosha ili kuondoa hisia mbaya. Muswada upitishwe haraka ili hatua zingine muhimu zianze bila kuchelewa wala kuendelea kulumbana.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Muswada unaopendekezwa utambue na kuthamini nafasi ya wafugaji katika nchi hii. Sheria ilinde maeneo yao ya malisho yasipokonywe na Serikali yenye, wawekezaji wala kugeuza maeneo hayo kuwa Hifadhi za Taifa za Wanyamapori. Pia fidia ya kutosha itolewe kwa watu wa mifugo (*Restocking*) kutoptana na majanga ya ukame ya muda mrefu na kuuliwa/kuumizwa (kupata ulemavu), kwa Wananchi wanaoishi ndani au nje ya maeneo ya Wanyamapori kama Ngorongoro na kwingineko.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Spika, ninaomba nichukue fursa hii, nichangie Muswada huu wa Maandalizi ya Kuruhusu Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Rais, kwa ujasiri mkubwa wa kuanzisha mchakato huu wa Katiba inayowahusisha Wananchi moja kwa moja, kwa kuwapa nafasi ya kipekee waweze kutoa maoni yao juu ya mustakabali wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, huu ni wakati mwafaka wa kuruhusu Muswada huu ili uweze kujadiliwa, kwani ningependa tutoe kipaumbele juu ya Uzalendo wa Nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pili, tuangalie juu ya kuendeleza historia ya nchi yetu kwa kutoubeza Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Muungano ni kwa manufaa ya Watanzania ambao tunaishi kwa kuthaminiana; Watanzania wanaoishi Zanzibar na wanaoishi Tanzania Bara, wote ni jamii moja. Hivyo, yeyote yule anayetaka kuupotosha Umma juu ya kuuvunja Muungano huu hatufai.

Jambo lingine ni juu maudhui ya Muswada ambao ameuwasilisha Mheshimiwa Waziri wa Katiba. Huu ni msingi wa mchakato wa kuunda Katiba Mpya, lakini kumekuwa na upotoshaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuwapotosha Wananchi na kutafuta umaarufu sana juu ya ukweli uliowakilishwa na Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuchangia kifungu cha 19, juu ya utaratibu wa kuwapata Wajumbe watakaouna Baraza la Katiba, uwe wazi na uhushe watu wenyewe sifa maalumu na si vinginevyo. Tukifanya hivyo, tutakuwa tumewatendea haki juu ya kutokuwakilishwa vyema kwa Wananchi kama wenzetu wa Upinzani; siyo kweli kwani sisi Waheshimiwa Wabunge ndiyo tuliopeba dhamana na kutoa uwakilishi wa Wananchi ambao tumewawakilisha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wapi Ripoti itawakilishwa; mimi ninaamini mahali panapostahili ni kwa yule aliyepewa dhamana ya kuunda Katiba kwa mujibu wa taratibu za Katiba ya Nchi yetu, inayomtaka Mheshimiwa Rais aunde au kuteua Katiba hii.

Mheshimiwa Spika, kama wachangiaji wengi walivyochangia, mimi ninaunga mkono hoja hii.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninamshukuru Mwenyezi Mungu, aliyejipendeza kuingia katika Bunge lako Tukufu kwa siku ya leo.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, ninaipongeza Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa kazi nzuri waliyofanya. Sasa ninaomba Wananchi waelewe hapa Bungeni tunafanya nini.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unahu Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya Mwaka 2011. Sheria hii ni kwa ajili ya kuunda Tume ya Kukusanya Maoni kutoka kwa Wananchi. Muswada huu ukishapitishwa, Mheshimiwa Rais atawezekuunda Tume, ambayo itajikita katika kutafuta maoni au mawazo kutoka kwa Wananchi, jinsi wanavyoona na wanavyopenda wao wenywewe kipi kiwekwe kwenye Katiba Mpya na kipi kiachwe kuhusiana na maoni yao. Kwa hiyo, Muswada huu utufuatana na ni matakwa gani yamewekwa au yawekwe au yawemo kwenye Katiba kama anavyotaka Wananchi mwenywewe.

Mheshimiwa Spika, kwa Wananchi, inapaswa waelewe kuwa, wamewakilishwa kwani kila Mbunge hapa anawakilisha Wananchi wake. Kwa mfano; nikiwa Mbunge wa Viti Maalum Morogoro, ninawawakilisha Wananchi wote wa Mkoa wa Morogoro. Ninawasihi Wananchi watuelewe.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninawaomba sana Wananchi wote wa Mkoa wa Morogoro na Wananchi wengine wa mikoa yote ya Tanzania; Wanawake, Wanaume, Vijana na Watoto, waelewe kuwa hadidu za rejea zipo wazi. Ninawasihi Wananchi mtoe maoni yenu mara tu mchakato utakapoanza. Ndugu zangu Wananchi, wakati ndiyo huu, muwe tayari nyote kutoa maoni yenu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Wananchi wasipotoshwe, waelewe kuanzia mwanzo kuwa nchi yetu ya Tanzania tumethubutu, tumeweza na tunazidi kusonga mbele na hivyo tuwe tayari kuunda Katiba Mpya. Wananchi inabidi tukubali na kuelewa kuwa, Mkuu wa Nchi ya Tanzania ni Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais baada ya kuitishwa Muswada huu, ataunda Tume kwa kufuata vigezo vilivyowekwa kwa uwakilishi ili ipate fursa ya kukusanya maoni kutoka kwa Wananchi.

Mheshimiwa Spika, ninaauliza sasa tatizo ni nini? Inabidi Wabunge wote tuelewe, tuukubali na kuupitisha Muswada huu kusudi Wananchi wapate nafasi ya kutoa maoni yao kufuatanana na wao wenywewe wanavyoona kufuatanana na mabadiliko ya Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, wale wachache wanaojidai kujua kumbe wanawapotosha Wananchi wenye dhamana ya kutendewa haki kwa kutoa maoni yao, waache kabisa kuwapotosha Wananchi, badala yake wawaongoze kwa kuwaonesha njia, kuwaeleza vizuri jinsi ya kutoa maoni, ili wawe tayari kutoa maoni yao vizuri. Tafadhalii Wananchi wa Tanzania, wakati ndiyo huu, hao watu wachache wasiwatoshe, kuweni tayari kutoa maoni yenu bila hofu.

Mheshimiwa Spika, ieleteke kuwa, kwanza kabisa, Wabunge wa Vyama vyote, tayari wametoa maoni yao ndani ya Bunge lako Tukufu. Kwa hiyo, ninaona tunachelewa. Waheshimiwa Wabunge, toeni mapendekezo twende kwa pamoja kwa kushirikiana kusudi Muswada huu upite na Wananchi watoe maoni yao kuhusu Katiba yao wanataka iweje. Baada ya hapo, maoni ya Wananchi yataangaliwa na kuwekwa sawa na hapo Katiba Mpya ya ushiriki ya Wananchi mwisho wake itaundwa (2011).

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kupitisha Muswada huu, Sheria sasa ya kuunda Tume, Wananchi wote ninaomba tuwe pamoja, tuweze kutoa maoni yetu kwa nafasi adimu na kubwa tuliyopewa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo yote, ninaomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. ZARINA S. MADABIDA: Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Serikali, ikiwa ni pamoja na Mheshimiwa Rais, Waziri na Watendaji, kwa kuleta Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuipongeza Kamati ambayo ina Wajumbe makini, ambao wameuchambua Muswada huu na kuleta mwelekeo mzuri ulioiwezesha hata Serikali kuleta *Schedule of Amendment*, ikiwa imezingatia maoni ya Wadau wengi walioshiriki wakiwemo Wanasheria, Wanaharakati, Wanavyuo, Wananchi, Wanasiaya, Viongozi wa Dini na waliojiita Jukwaa la Katiba na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na upotoshaji mkubwa sana kutoka kwa baadhi ya waliochangia, kuwapotosha Wananchi kwa makusudi wakiwaambia kuwa, Muswada huu ndiyo wa Katiba na kuleta maneno ya uchochezi. Wapo walioota maneno ya kashfa kwa Serikali, lakini pia kuhimiza vurugu kwa Wananchi kwa sababu za uongo, wakishinikiza Muswada uanze upya kwa Kusomwa Mara ya Kwanza, wakati Muswada umekuja kwa Mara ya Pili, ukiwa na madhumuni na maudhui yale kama yaliyoletwa wakati unasomwa kwa Mara ya Kwanza.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hii, ninaomba vitu viwili:-

- (i) Serikali itoe elimu kwa Wananchi ili waelewe kuwa Muswada huu ni nini; lakini pia wahakikishe wanapata elimu kuhusu Tume na fursa yao ya kutoa maoni kuchangia kutunga Katiba yao mpya; na
- (ii) Serikali itoe ulinzi wa kutosha na iwashughulikie wale wote wanaotaka kupotosha Wananchi na inawezekana wakawazuia Wananchi kushiriki kikamilifu na kuhakikisha hawatishwi katika ngazi yoyote ya mchakato huu.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huu, ninaomba kifungu cha 19 cha Makosa na Adhabu kisiishie tu kwa Wajumbe wa Tume au Sekretarieti, bali pia kiwahuus Wananchi ambao kwa namna yoyote wanaweza kufanyiwa fujo. Adhabu iangaliwe ili iwe kali zaidi ili kuhakikisha zoezi linadumisha amani na hakuna bughudha. Ninapendekeza faini iwe isiyopungua shilingi milioni tano au kifungo kisichopungua miaka miwili au vyote kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa Muswada huu, umetusaidia kuweza kufahamu makundi ambayo yanaashiria vurugu, jazba na kuhimiza uvunjifu wa amani na kuleta tararuki. Ili kuhakikisha Tume yetu inakuwa haina Mjumbe ye yoyote anayeweza kuashiria niliyoyataja hapo juu, ninapendekeza sehemu ya sita, kifungu cha 4(a) kitamke wazi kama kiliviotamka juu ya Viongozi wa Siasa, basi iongezwe pale kwamba, Wanaharakati, Wanajukwaa la Katiba na wote ambao

wameonesha msimamo wao wakati wa mchakato wa Muswada huu, wasiwemo kwenye Ujumbe wa Tume.

Mheshimiwa Spika, Tume iwe na Viongozi walioonesha uvumilivu, hekima, busara na walio tayari kusikiliza na kuongoza Wananchi kwenye zoezi lao muhimu sana la kupata Katiba Mpya, kwa manufaa ya sasa na vizazi vijavyo.

MHE. DKT. WILLIAM A. MGIMWA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nachukua fursa ya kukupongeza wewe Mheshimiwa Waziri binafsi na Wizara yako kwa kazi nzuri mnayofanya. Naomba kuchangia kama ifuatavyo ili kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, *commencement of the Act, Section 1(2)*. Muswada unaelekeza kwamba Sheria hii itaanza kutumika tarehe 1/12/2011. Mimi naomba kwamba kwa hali halisi tarehe hiyo siyo sahihi kulingana na mchakato wa kuitishwa Muswada huu, kwa hali hiyo napendekeza matumizi ya Sheria (*commencement*) yaanze punde tu Mheshimiwa Rais anapotia sahihi.

Mheshimiwa Spika, *Terms of Reference, section 8(1)*. Kifungu hicho kinasema Mheshimiwa Rais ndiye atakayetoa *Terms of Reference* kwa *Commission*. Maoni yangu, Bunge hili tupewe *details of terms of reference* ili kuondoa shaka yoyote ya mambo yatakayofungwa na Tume.

Mheshimiwa Spika, *Proclamation of the Constituent Assembly section 20(2) (e)*, kipengele hiki kiboreshwe kwa kutamka *minimum number of representatives from each group (i) to (v) out of 116 people*.

MHE. BENEDICT N. OLE NANGORO: Mheshimiwa Spika, moja, natoa pongezi kwa Waziri wa Katiba na Sheria, Katibu Mkuu na wataalamu kwa kuandika Muswada mpya wa mabadiliko ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, pili, Muswada huu naunga mkono mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, tatu Bunge Maalum la Katiba lijitungie ratiba ya kazi ya kukusanya maoni, kuchambua maoni hayo na kuiandika rasimu ya Katiba mpya.

Mheshimiwa Spika, nne, Bunge Maalum la Katiba liunde Tume ya Elimu kwa Umma itakayoelewesa umma juu ya yale yaliyomo kwenye rasimu ya Katiba mpya.

Mheshimiwa Spika, tano, maoni ya watu juu ya rasimu yatumike kuboresha rasimu hiyo na mwishoni kuandika na kuchapa "*o*" *draft* ya Katiba mpya.

Mheshimiwa Spika, sita, kura ya maoni ipigwe juu ya kukubali ama kukataa "*o*" *draft* ya Katiba mpya.

Mheshimiwa Spika, saba, hesabu ya kura za maoni juu ya kukubali ama kukataa "*o*" *draft* itumie Kanuni ya "*simple majority*" badala ya *two third*.

MHE. ENG. ATHUMAN R. MFUTAKAMBA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Celina O. Kombani, Mbunge, Waziri wa Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Igalula wote kwa ujumla wanaunga mkono hoja hii kupitia mwakilishi wao halali mimi. Hoja ya Upinzani haina mashiko kwani inalenga upotoshwaji wa Muswada huu kwa sababu zifuatazo:-

Baada ya CHADEMA kushindwa Uchaguzi Mkuu 2010 na Igunga Oktoba, 2011 uchaguzi mdogo, sasa mjadala wa Katiba unaongozwa na Chama Tawala (CCM) badala ya CHADEMA, Mheshimiwa Rais Dokta Jakaya M. Kikwete, wao wanaona wateke nyara Muswada ili ndoto zao za mwaka 2015 kuingia ikulu (haiwezekani) waweze kuanza mchakato wa kuunda Katiba mpya.

Ubinafsi wa CHADEMA hautofanikiwa kwani Muswada huu utatoa fursa ya wananchi wengi ambaeo ni sauti ya Mungu. CHADEMA inawakilisha 14% ya Wabunge na kwa sababu wengi ni ndugu wa damu, uwakilishi wao ni mdogo. Hivyo Muswada utapita na baadae Katiba itapatikana.

Precedence: Kenya, Uganda, Ghana na kwingine duniani utaratibu wa kupata Katiba mpya ni sahihi Tanzania kuufuata.

Mchangiaji wa Kambi ya Upinzani CHADEMA anavunja Katiba kwa kuhoji Mamlaka ya Rais kama walivyofanya Desemba, 2010 kutoka nje ya Bunge Rais alipokuwa akihutubia.

Tundu Lissu hana hoja bali ana matusi tu kwani ameona ajenda yao inashindwa wana lao jambo ovu.

Mheshimiwa Spika, hawa wanaofadhili CHADEMA hawatutakii mema, wana vivu na amani na utulivu wetu. Tuwabaini na tuwaambie hawatafanikiwa kamwe. Tumethubutu, tumeweza na tunasonga mbele.

Mheshimiwa Spika, Tume zimeundwa na Marais wastaafu Mzee Mwinyi (1991- Nyalali), Mzee Mkapa (1998 - Kisanga), leo Rais Dokta Jakaya Mrisho Kikwete ametoa fursa ya Muswada wa kurekebisha Katiba, CHADEMA wanang'aka, wana lao jambo. Wametumwa, tuwakatae.

Baadhi ya ufadhili wamediriki kusema CCM imetawala kwa muda mrefu ipatikane njia ya kuiondoa madarakani. Wanadhani hii nia ya Muswada wa kuvuruga watafanya nchi isitawalike ili watwae madaraka. Hawatoweza kamwe hawa vibaraka CHADEMA.

Mheshimiwa Spika, CHADEMA haina wawakilishi kule Zanzibar? Iweje hawataki Muungano? Hiki chama kweli ni cha familia isiyo na demokrasia! Balaa tupu. Ewe Mungu tuepusha na dhamana hii tuendelee na amani, mshikamano na utulivu.

MHE. ROSWEETER F. KASIKILA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mungu kwa afya anayonijalia na kuniwezesha nami kuchangia juu ya hoja hii.

Mheshimiwa Spika, naanza kwa kumpongeza Waziri mwenye dhamana, watendaji katika Wizara ya Katiba na Sheria, lakini pia niwapongeze Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa kazi nzito ya kuuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, nami naunga mkono Muswada uliopo mezani. Naomba kuchangia juu ya mabadiliko kuwa:-

Kifungu cha Marais wote wawili wasipate ushauri wa Wanasheria Wakuu (*Attorney Generals*) wa Zanzibar na Tanzania Bara wawaachie Marais wao husika.

Bunge Maalum litakaloundwa ndio lipewe jukumu la kuweka utaratibu wa ni vipi Tume itaundwa na hata juu ya theluthi mbili Bunge Maalum liachiwe kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia zote mia moja.

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Mheshimiwa Spika, kabla yote napenda niseme kuwa naunga mkono hoja ya Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba mia kwa mia.

Watanzania tulidai Katiba Mpya siku nyingi, ambayo itakidhi matakwa ya Vyama vingi. Mimi nampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Tanzania kwa dhamira yake njema ya kuleta Muswada huu. Nashangaa sana kuwaona wenzetu wa CHADEMA kuukataa Muswada huu. Hii inaonyesha dhahiri kuwa hawatikii mema nchi hii. Tena nawaonea huruma sana wale Wabunge wenzetu waliomo kwenye chama hiki ambaeo ni Wazanzibar. Natoa wito kwa Wazanzibar wote waielewe CHADEMA ni chama cha aina gani. Chama hiki hakitaki pawe na Muungano, chama hiki kama kungetokea siku kikaongoza nchi basi watatufikisha pabaya sana.

Mheshimiwa Spika, ikiwa kweli tunaona Rais amepewa madaraka makubwa, chombo pekee kitakachowea kupunguza madaraka haya ni Katiba. Mwisho uchomeapo ndipo utokeapo, Katiba tuliyonayo ndiyo iliyompa Rais madaraka haya. Hatuwezi kupata Katiba Mpya kwa kuandamana barabarani, Katiba itapatikana kwa kukaa pamoja Wabunge tukajadili Muswada huu na kuelekea kwenye mchakato wa kupata Katiba Mpya.

MHE MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata fursa hii ya kuchangia Muswada huu. Mchango wangu hauna jipya sana zaidi ya kutoa pongezi kwa Wizara kwa kuandaa Muswada huu na kuufikisha hapa Bungeni.

Pamoja na pongezi hizo naomba kutoa maoni kwamba Serikali iangalie umuhimu wa kutoa elimu kwa wananchi juu ya namna watakavyotoa maoni yao na hatma ya namna Katiba Mpya itakavyopatikana. Kwani nina mashaka sana na baadhi ya wanasiisa na wanaharakati kupotosha umma wa Watanzania na wakiwakosesha haki zao ya msingi ya kutoa maoni yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja.

MHE. FAITH M. MITAMBO: Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja. Suala la kuunda Tume ya kukusanya maoni juu ya Katiba Mpya. Ni muhimu na ndiyo mwanzo hasa wa upatikanaji au kutopatikana kwa Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, Katiba Mpya haitaweza kupatikana kwa kufanya mikutano ya hadhara bali ni kwa njia ya kukusanya maoni mbalimbali kutoka kwa wadau wote wa Katiba hiyo ambayo ni Watanzania wote. Turuhusu Tume ya kukusanya maoni ya Katiba Mpya iwepo ili sisi Watanzania wote tutoe maoni na mawazo yetu kwa uhuru na kwa utaratibu mwema ili hatimaye mwisho wa zoezi hili tutakuwa tumepata mawazo ya msingi na ya kweli, Watanzania wanasema nini kuhusu Katiba na lipi lirekebishwe na lipi libaki kama lilitivo na upi uondolewe katika Katiba hiyo.

Mheshimiwa Spika, niwaombe Watanzania kutosikiliza tabia ya uchochezi inayoendelea sasa mionganini mwetwa kwa nia ya kutuharibia na kupotosha ukweli na dhana yenye kazi Tume hiyo na hatimaye kutufanya sisi Watanzania kutopata haki yetu ya kimsingi na Kikatiba.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia.

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali hususan Rais wa nchi kwa kutamka tunahitaji Katiba Mpya. Kwenye Muswada tumeona Rais angepewa mamlaka mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika Kifungu cha 5, Rais amepewa mamlaka ya uteuzi akishirikiana na Rais wa Zanzibar. Kifungu cha 6 atateua Wajumbe wa Tume na Kifungu cha 8 amepewa mamlaka ya kuandaa hadidu rejea.

Mimi binafsi naamini Rais ni Mkuu wa nchi na Katiba ya nchi Ibara ya 33 imempa mamlaka hayo, lakini naamini Watanzania watapewa nafasi ya kutoa maoni yao na hatimaye kupata Katiba ya nchi wanayoitaka wao. Iwe kuongeza au kupunguza madaraka. Hivyo sioni sababu ya kugomea Muswada uliopo ndani ya Bunge letu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. JUMA SURURU JUMA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Kifungu 9(2)(a) – (h) naomba kusisitiza kwamba misingi mikuu ya Kitaifa na maadili ya jamii ipewe msukumo na umuhimu mkubwa ili kulinda Muungano na Mapinduzi ya Zanzibar. Naomba hili lipewe umuhimu katika kazi ya Tume itayaoundwa.

Kifungu cha 20, naomba katika uteuzi wa Wajumbe kutoka kwa Marais wawili ni vyema wakateua kwa fikra zao wenyewe bila ya kushurutishwa wala ushauri wa Wanasheria walotajwa katika mapendekezo.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Spika, hakuna mabadiliko yoyote ya sheria yanayoweza kutokea kutoka hewani na kuanguka kama mvua bila kuwa na chanzo chake. Hivyo mabadiliko yoyote ya kisheria lazima yaanzishe na kiongozi/viongozi au mtu yeoyote maadam tu awe amefuata, utaratibu, kanuni au miongozo mbalimbali iliyowekwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba hii natoa pongezi zangu za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa busara yake ya kukubali kusikiliza maoni ya wadau mbalimbali ya kutaka kuwa na Katiba Mpya na hatimaye Mheshimiwa Rais kutamka rasmi tarehe 5 Februari, 2011 wakati wa sherehe ya kuzaliwa CCM.

Mheshimiwa Spika, ninawashauri wananchi watumie fursa hii muhimu katika kutoa maoni.

Mheshimiwa Spika, uundaji wa Tume ya Mmchakato ufanywe na Mheshimiwa Rais kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais hakujiweka katika madaraka aliyonayo bali amewekwa na wananchi kwa kuchaguliwa. Hivyo, sioni sababu ya kuhofia Rais juu ya uteuzi wa Tume.

Mheshimiwa Spika, katika Muswada huu wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba iwepo nafasi au muda wa kutosha kuhakikisha wananchi wote na kwa makundi mbalimbali wamefikiwa ili kutoa maoni yao.

Mheshimiwa Spika, Tume itakayoundwa kuwe na utaratibu wa kuhakikisha Tume hiyo inatoa elimu ya kutosha ili kuwezesha watu wote wenye sifa ya kupiga kura ya maoni wamepiga kura.

Mheshimiwa Spika, mamlaka tuliyopewa na Wananchi, Tume bila hofu yoyote ni mamlaka halali, tuitumie ipasavyo ili mradi hatuvunji sheria.

Mheshimiwa Spika, lazima tuwe macho na Serikali ichukue hatua kwa mtu yeoyote anayetaka kuvuruga wananchi na kuvunja amani kwa sababu ya kutafuta madaraka kwa nguvu. Sheria ichukue mkondo wake.

Mheshimiwa Spika, hivyo nawasihi wananchi wenzangu muwasusie watu hao wanaotaka kuvunja amani tuliyonayo.

Mungu ibariki Tanzania, Mungu ibariki Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. FATUMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kuhusu Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa mwaka 2001. Kwanza ninaunga mkono mia kwa mia. Hongera kwa kuwa na Muswada huo ulio makini sana hasa kwa kuangalia madaraka ya Rais, suala la Wazanzibari kushirkishwa kikamilifu, hongera sana.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya Katiba ni kitu cha kawaida, kwa hiyo, Tume iundwe lakini pia ishirikishe aina zote za jamii nchini; wasomi, wasiokuwa wasomi, wa mijini, wa vijiji, wazee, vijana, wake, waume, wakristo, waislamu, *NGOs* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, wananchi waelimishwe kati ya Muswada wa Sheria, yaani uundwaji wa Tume ni tofauti na masuala mazima ya kuunda Katiba mpya, maana inaelekea watu, raia, wananchi wanashindwa kuelewa kati ya mambo hayo mawili hapo juu yaani Muswada wa Sheria ya Marekebisho na kutunga Katiba Mpya.

MHE. JASSON S. RWEIKIZA: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kuhusu Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba kuwa Muswada huu ni mzuri, una maana kubwa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, jina fupi la Muswada libadilishwe lisiwe "Sheria ya Marekebisho ya Katiba ya mwaka 2011," liwe ni "Sheria ya Kutunga Katiba Mpya." Neno "Mabadiliko" lina maana hata pale unaporekebisha au kusahihisha au "kuweka kiraka" au kubadili kifungu au vifungu katika Katiba hiyo hiyo ya zamani; sisi tunazungumzia kutengeneza Katiba mpya, tuseme hivyo basi. Suala la kwamba tulikuwa tuna Katiba ya sasa halibadiliki. Neno "Mpya" lina maana ni badala ya hiyo ya sasa/ya zamani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bunge la Katiba/Maalum, Bunge hili lifutwe, hatuhitaji Bunge Maalum, wakati huo huo kuna kura ya maoni (*referendum*). Demokrasia tulyonayo ni ya aina mbili ambazo hufanya kazi kwa aina moja au nyngine; sio zote kwa wakati mmoja. Demokrasia hiyo ni ile ya moja kwa moja (*direct*) au ile ya uwakilishi (*representative*). Tukifanya Bunge la Katiba na *referendum*, ina maana tumefanya zote mbili. Hatuna sababu ya msingi ya kufanya demokrasia zote mbili ambazo zitatugharimu sana kifedha na kisiasa. Tuchague moja na mimi naona kwa kuwa jambo lenyewe ni kubwa sana, tuchague ile demokrasia ya moja kwa moja, (*direct*) yaani kura ya maoni (*referendum*).

MHE. EUSTACE O. KATAGIRA: Mheshimiwa Spika, nawapongeza wote waliohusika na uandaaji wa Muswada huu hasa Mheshimiwa Waziri na Kamati husika, wamefanya kazi kubwa. Natoa shukrani kwa Mheshimiwa Rais, kwa kuridhia mchakato huu wa Katiba mpya.

Mheshimiwa Spika, mambo muhimu yamezingatiwa. Kuhusu Tume; utaratibu wa uundaji Tume unaridhisha na shughuli zake ni muhimu. Wachaguliwe vizuri watu wenye *high credibility*.

Mheshimiwa Spika, Bunge la Katiba, utaratibu uliowekwa ni muafaka. Ile nyongeza ya ziada ya Wajumbe 116 ni suala muafaka kabisa na kwa kutoka maeneo muhimu; taasisi za kidini, vyuo, na kadhalika. Ni muhimu hili litazamwe na kutangazwa sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kura za maoni, huu ni utaratibu mzuri na inawapa wananchi kauli ya mwisho kuikubali Katiba au kuikataa. La msingi ni tuendelee kuwaelimisha wananchi juu ya fursa hii waliyonayo na inayowaongezza "*ownership*" ya Katiba hiyo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SALOME D. MWAMBU: Mheshimiwa Spika, naomba nitoe maoni yangu kuhusu Muswada wa Katiba kwa ajili ya kuboresha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuchagua Wajumbe wa Tume naomba au nashauri ushirikishwaji wa makundi yote ya kijamii yazingatiwe. Mfano, wakulima na wafugaji, vijana na wazee, watumishi wa Serikali, wafanyakishara na wafanyakazi, wanafunzi wa *higher learning institutions* na kadhalika. Nasemea makundi haya ni muhimu sana kwani ndiyo yanayoilalamikia Serikali kuhusu masuala mengi katika jamii.

Mheshimiwa Spika, naomba kushauri kwamba katika mchakato mzima Rais apewe heshima kama mkuu wa nchi na kuwa ana mamlaka ya kuteua bila kupingwa. Kwa hiyo, asiingiliwe katika uteuzi wa Tume.

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe angalizo kuhusu Wanaharakati, kwanza wasiingilie mapendekezo yatakayotolewa na wananchi katika mchakato mzima wa kutoa maoni. Watakaopotosha kwa njia moja au nyngine wachukuliwe hatua za kisheria.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga hoja Muswada upite asilimia 100. Naomba kuwasilisha.

MHE. SYLVESTER M. MABUMBA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ile ya Mapinduzi ya Zanzibar. Pia naipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa kupitia na kuchambua kwa kina hatimaye kuwezesha Muswada huu kuwasilishwa kwa mara ya pili katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, Tanzania kwa mara nyingine inauthibitishia ulimwengu kwamba amani iliyopo nchini imepatikana kutokana na misingi madhubuti ya kidemokrasia iliyojengwa na waasisi wa Taifa letu. Utaratibu huu wa kulishirikisha Bunge ambalo ndio chombo halali kinachowakilisha Watanzania wote ni dalili njema kwa mustakabali wa nchi yetu. Utaratibu huu wa kulishirikisha Bunge kujadili namna Tume ya kukusanya, kuratibu na kuchambua maoni ya wananchi utaiwezesha Tume itakayoundwa kuwa na nguvu za kisheria na baraka za Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia sehemu ya tatu ya Muswada, hasa Ibara ya 6(3). Naiomba Serikali katika kufanya uteuzi wa Wajumbe wa Tume, pamoja na kuzingatia uwakilishi ulio sawa kwa pande zote mbili za Muungano, naomba sana wasiteuliwa Wajumbe ambao msimamo wao ni kuvunja Muungano wetu. Vyombo vya ulinzi na usalama vitumiwe ipasavyo kuwachunguza wote watakaopendekezwa kabla ya kuteuliwa. Pamoja na utaalamu wao juu ya mambo ya Katiba na Sheria, nashauri kigezo cha uzalendo na mapenzi kwa Muungano iwe ndiyo sifa mama itakayotumika kuwa tena Wajumbe wa Tume. Minong'ono inayoendelea hasa kutoka upande wa Zanzibar ni kushinkiza kuunda Serikali tatu ambazo hatima yake ni kuvunjika kwa Muungano. Serikali isiruhusu hili kutokea.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana kabisa na Ibara ya 9 ya Muswada huu inayozungumzia kazi za Tume. Nashauri Ibara ya 9(2) izingatiwe ipasavyo ili kuhakikisha Muungano wetu unaendelea kuwepo kwa gharama yoyote kwa manufaa ya watu wetu. Nashauri wananchi waelimishwe kuhusu umuhimu wa umoja tulionao kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 14(1) inazungumzia gharama za shughuli za Tume; kwamba zitalipwa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina. Naomba gharama zichangiwe na Hazina zote mbili ya SMT na SMZ kwa sababu, sehemu zote za Muswada huu zimeelezea waziwazi kwamba maamuzi yote yatafanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano baada ya kushauriana na kukubaliana na Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hivyo haitakuwa vizuri gharama za shughuli za Tume zikaghari miwa na Mfuko Mkuu wa Hazina ya Jamhuri ya Muungano. Zanzibar ipewe haki yake ya kugharimia, hii ndiyo haki na usawa, tunaomba kwenye Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 23(1) inasema kwamba, "Bunge la Katiba, litakuwa na Mamlaka na litatumia mamlaka hayo kutunga upya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kutunga masharti yatokanayo, masharti ya mpito na vilevile kutunga na kuweka masharti mengine kama Bunge la Katiba litakavyoona inafaa." Kwa nukuu hii, Bunge la Katiba litakuwa na nguvu zote na kwa vile litakuwa limeundwa kwa utaratibu unaokubalika. Hivyo nashauri Ibara ya 24(3) ifutwe kwenye Muswada huu ili kulipatia fursa Bunge la Katiba kuijiwekea utaratibu unaofaa katika kupiga kura za uamuzi na maamuzi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 27(1) na (2), zinaelezea uendeshaji wa kura ya maoni. Nakubaliana kabisa na maelezo hasa ya Ibara hiyo ya 27(2) kwamba, Tume ya Uchaguzi Zanzibar kwa upande wa Zanzibar, ikasimamia zoezi lote la upigaji wa kura za maoni na kuwasilisha kwenye Tume ya Taifa ya Uchaguzi matokeo ya kura zilizopigwa Tanzania Zanzibar. Hata hivyo, nashauri kwamba daftari la kudumu la wapiga kura lililopo Zanzibar, likaheshimiwe na vyama vya siasa vilivypopo Zanzibar. Kuna maneno yasiyofaa kwamba daftari hilo lina majina ya watu ambao siyo Wazanzibari. Maneno hayo ni ya hatari na ya kipuuzi na hayana nia njema kwa zoezi zima litakaloendeshwa kukusanya maoni ya wananchi. Serikali zetu naziomba zisikubali maneno hayo ya upotoshaji.

Mheshimiwa Spika, nashukuru na naunga mkono hoja.

MHE. ALBERT O. NTABALIBA: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia Muswada huu kwa kuanza kuunga mkono. Napenda kuipongeza Wizara ya Katiba na Sheria na Kamati ya Bunge, kwa kuufanya kazi kubwa Muswada huu uliowasilishwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, nashauri kuhusu amani na utulivu, naomba Serikali iwe na kazi sana ya kusimamia ishara zote zinazojitokeza kutaka kutokea hapa nchini zinazoratibiwa na Chama cha CHADEMA, pia Wanaharakati wanaosema hadharani. Serikali iendelee kuhakikisha vibali nya mikutano nchi nzima kwa vyama nya siasa, vibali vitolewe kabla ya kurusha vipindi nya *television* kwa kila mwanaharakati na kila *NGO*, wanaharakati, watoe gharama za kuendesha shughuli zao zinazohusu mambo ya Katiba ili kubaini nani ni wafadhilli wa kongamano hilo.

Mheshimiwa Spika, semina mahususi itolewe kwa vyombo nya habari juu ya mchakato wa Katiba ili kupunguza upotoshaji unaochangiwa pia na wanahabari.

Mheshimiwa Spika, kuna haja kubwa ya kuimarisha imani ya Watanzania inayopotea mionganii mwa wananchi juu ya kiongozi wa nchi na Serikali yao, inayochochewa na vyama nya siasa na wanaharakati.

Mheshimiwa Spika, namna ya kuimarisha imani; kwanza Serikali ijitokeze mara moja jambo linapotoka nchini bila kukawia, pili, vyombo vinavyosaidia Serikali; Wakala kama *EWURA* au *SUMATRA*, wananchi hawawatambui sana kama Serikali. Basi Serikali ijitokeze mara moja kuingilia na kutoa wasiwasi kwa wananchi, tatu Serikali fungeni watu wakorofii kuwa fundisho na nne, mchakato wa Katiba; Tume itakapoundwa, ifike Jimbo la Manyovu kupata maoni ya wananchi kwani wanasubiri kwa hamu kubwa.

Tano, kuhusu upinzani; maoni ya Wapinzani yametolewa na Mheshimiwa Tundu Lissu, haya yachukuliwe kama yametayarishwa na wote. Hivyo, maoni hayo hayatasaidia nchi hii kwa namna yoyote ila ni uvunjifu wa amani. Tujiandae na misukosuko katika nchi kwani, dhamira yao siyo njema.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii na nimeridhika na yote waliyoyasema Wabunge wenzangu.

MHE. CNYTHIA H. NGOYE: Mheshimiwa Spika, awali kabisa naomba kuipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuleta Muswada huu kwa wakati huu muafaka.

Naunga mkono nafasi ya Rais kutambuliwa katika hatua za uundwaji wa Katiba yetu akishirikiana na Rais wa Zanzibar. Kila jambo lazima liwe na mwenyewe. Kifungu cha 6 kinazungumzia uundwaji wa Tume ambayo kwa kiwango kikubwa itafanya kazi hii kubwa na kifungu cha 6 kinataja aina ya Wajumbe watakaoteuliwa. Naomba kusisitiza kuhusu uteuzi utakaofanyika kuzingatia jinsia. Kifungu hiki ni muhimu na ninashauri uzingatiaji wa kuwashirikisha wanawake wenye uwezo ambao wataweka maslahi ya wanawake na watoto wakati wa ukusanyaji wa maoni ya wananchi. Suala la Katiba ni maisha ya watu hivyo ni muhimu kuyawekea kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 12(3) napendekeza Mjumbe wa Tume wa aina hiyo pamoja na kuondolewa kwenye orodha ya Wajumbe, pia achukuliwe hatua za kinidhamu. Kifungu cha 29(2) napendekeza suala la kuelimisha na kuhamasisha wananchi kuhusu kuipigia kura za maoni Katiba inayopendekezwa kazi hiyo ifanyike na Tume. Kwa hatua hii vyama nya siasa vishirikishwe kwani nafasi hii inaweza kutumika vibaya na vyama kwa kuacha ajenda ya Katiba na kujilingiza katika masuala ya siasa.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kusisitiza mambo ya ujumla yanayohusu Muswada huu. Naomba kusisitiza kuhusu suala la uadilifu wa hali ya juu sana hasa wakati wa ukusanyaji wa mawazo ya wananchi ili kuheshimu mawazo ya kila mtu na kuyafanya kazi. Pili, ni vizuri Wizara hii iendelee kusisitiza kuhusu Watanzania wenyewe kuachiwa nafasi ya kutoa mawazo yao kuhusu Katiba yao bila kuingiliwa na wageni.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba Serikali iangalie uwezekano wa kuwatambua Watanzania raia wa Tanzania waishio nje ya nchi nao watoe mawazo yao kuhusu Katiba yao. Kwa njia hii tutakuwa tumeputa uwakilishi wa kutosha na kutoka makundi yote ya binadamu.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia naomba kazi hii ifanyike kikamilifu kwa mujibu wa Katiba.

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hoja hii.

MHE. CATHERINE V. MAGIGE: Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali pamoja na Mheshimiwa Rais kwa kutamka tunahitaji Katiba Mpya.

Katika Muswada tumeona Rais kapewa mamlaka mbalimbali. Mimi binafsi naamini madaraka hayo ni sawa kabisa natumaini na Rais mimi na Watanzania wenzangu na ndio maana tukamchagua awe Rais wa nchi yetu. Kwenye Muswada tumeona Rais amepewa madaraka mbalimbali. Katika Ibara ya 33 imempa madaraka hayo kuwa Rais ni mkuu wa nchi na Katiba ya nchi. Katika Muswada Rais amepewa mamlaka mbalimbali.

Kifungu cha 5, Rais kapewa mamlaka ya uteuzi akishirikiana na Rais wa Zanzibar. Kifungu cha 6 Rais atateua Wajumbe wa Tume na Kifungu cha 8 Rais kapewa mamlaka kuandaa hadidu rejea.

Mimi naamini madaraka ya Rais ni sawa kabisa na nchi lazima iwe na kiongozi. Tumeona nchi nydingi kama Zambia, Kenya na Ghana wakati wanaunda Katiba Mpya, Marais wao walipewa madaraka kama leo hii aliyopewa Rais wetu. Watanzania waelewe, wasikubali kupotoshwa katika suala hili la Katiba, madaraka anayopewa Rais ni sawa kabisa.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuunga mkono Muswada 100% kwani kutokana na maendeleo ya kijamii kiuchumi na kisiasa kwa nchi yetu ni muhimu kuiangalia Katiba na kuiweka ilingane na mazingira ambayo tumefikia kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kusema kidogo juu ya wenzenetu wa Chama cha CHADEMA kususia Muswada siyo sawa, wangeweza kutoa hayo mawazo yao Watanzania wangewasikia na pengine wangeyafanya kazi, wamekosea sana.

Mheshimiwa Spika, naanza na kuiangalia Ibara ya 5 katika Muswada inayosema Rais wa Jamhuri kushauriana na Rais wa Serikali ya Zanzibar kupata ushauri toka kwa Wanasheria Wakuu. Sijaona umuhimu wake pengine kwa mawazo yangu kuondolewa sioni sababu ya viongozi hawa kwenda kupata ushauri kwa Wanasheria.

Suala la pili ni kuhusu Bunge la Katiba, chombo hiki kiwe ndio chombo cha mwisho kuhalalisha Katiba. Kinachowezekana ni kuongeza uwakilishi uwe mkubwa zaidi kwa makundi mbalimbali yanayojenga utaifa wetu na kama njia hii haitatumika basi lazima ipelekwe moja kwa moja kwa wananchi kupigiza kura kwa msingi huu, hakuna sababu kupeleka rasimu kwenye vyombo viwili vikubwa na vitakavyotumia gharama kubwa sana lakini pia inaweza kuwa maeneo yanayoweza kuzua mgawanyiko ambao ungeepukwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hoja hii.

MHE. PEREIRA AME SILIMA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nikushukuru kwa kunipa fursa nami nishiriki katika wachangiaji wa Muswada huu.

Kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuridhia mchakato shirikishi wa kuwa na Katiba Mpya ya miaka 50 inayokuja kwa Uhuru wa nchi.

Mheshimiwa Spika, napenda nizipongeze Serikali zetu mbili na kupitia kwa Wanasheria Wakuu wa Serikali hizi:-

Kwanza kuja na mapendekezo mazuri kwa ajili ya mchakato wa kutafuta maoni na hatimaye kuandaa rasimu ya Katiba Mpya. Pili, kwa kuleta mapendekezo mazuri ambayo kimsingi yametambua uwepo kwa pande mbili za Muungano na kwa kiasi kikubwa kutoa haki kwa pande zote hizo.

Mheshimiwa Spika, naomba kwanza niunge mkono hoja mia kwa mia. Pamoja na kuunga mkono naomba nichangie katika maeneo yafuatayo:-

Ibara ya 32 imependekeza kwamba iwapo kura za ndiyo hazikutosha uchaguzi utarudiwa baada ya kutoa muda wa kushajiisha wapiga kura. Ipo haja ya kuonesha ni mara ngapi marudio yatafanya na baada ya mara ngapi marudio haya yatafanya baada ya kufanya maamuzi mengine.

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe angalizo kwa Serikali kupidia kwako iangalie vitendo vya Kambi ya Upinzani na hususan Mnadhimu wake Mheshimiwa Tundu Lissu. Kinachoonekana ni kupanda mbegu za chuki hususan kwa upande mmoja wa Muungano Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SARA M. ALLY: Mheshimiwa Spika, naomba nichangie maeneo yafuayato nikianza na sehemu ya tano ya Muswada, Ibara ya 20 inayozungumzia kuundwa kwa Bunge la Katiba. Nakubaliana na Rais wa Jamhuri kwa kushirikiana na Rais wa Zanzibar kuunda Bunge la Katiba. Lakini Mwanasheria Mkuu wa Serikali kutoka pande zote mbili za Muungano nashauri waondolewe wasiwe washauri wakuu.

Mheshimiwa Spika, hawa Wanasheria kutokana na nafasi zao ni Wajumbe katika Bunge la Katiba. Rais anaunda Bunge la Katiba kutokana na mamlaka aliyonayo Kikatiba (*he is the head of state*). Aidha, muundo wa Wajumbe wa Bunge la Katiba hauhitaji *application* ya sheria kupata Wajumbe wake.

Ibara ya 23(3) inaeleza masharti ya Muswada wa Katiba yapate kupidishwa katika Bunge la Katiba yatahitaji kuungwa mkono kwa wingi wa theluthi mbili ya idadi ya wajumbe wote kutoka kila pande ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, hofu yangu ni kwamba endapo upande mmoja haujatimiza idadi inayotakiwa ya wajumbe ndiyo itakuwa mwisho wa mchakato wa kupata Katiba Mpya? Je, Serikali haioni inawanyima wananchi fursa ya kushiriki? Naomba Serikali ilitazame upya.

Mheshimiwa Spika, muundo wa Sekretarieti, Katibu wa Sekretarieti atateuliwa na Rais baada ya kukubaliana na Rais wa Zanzibar. Katibu anatakiwa kuwa na taaluma ya sheria, uzoefu wa kazi wa miaka 10, awe mtumishi wa umma awe na mwenendo na tabia nzuri.

Mheshimiwa Spika, Sekretarieti itakuwa na idadi ya watumishi wa umma kwa kadri itakavyohitajika. Naijuliza tabia nzuri anazotakiwa kuwa nazo Katibu ni zipi? Naomba ziorodheshwe, naijuliza ni lazima Katibu na Sekretarieti yote itokane na utumishi wa umma?

Nashauri Sekretarieti iwe na uwiano sawa na idadi ya watumishi wa umma na kutoka taasisi nyingine za kijamii. Hii itasaidia kujenga imani kwa wananchi na makundi mbalimbali katika jamii.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa kupata Katiba Mpya. Kwanza Bunge la Katiba, wajumbe kupiga kura za theluthi mbili kila upande wa Muungano. Pili, kura za maoni wananchi kupiga kura za ndiyo au hapana ambayo itasimamiwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Tume ya Uchaguzi Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwa vile Tanzania ni mwanachama wa Jumuiya ya Madola na sasa tuanelekea kuwa na Shirikisho la Afrika Mashariki, naiomba Serikali itazame upya utaratibu

huu, michakato yote miwili kwa wakati mmoja na kwa jambo moja la kufikia malengo ya kuwa na Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, mchakato huu utachukua muda mrefu na ghamama zake ni kubwa. Naomba tuangalie nchi za wenzetu ambao wana Katiba Mpya mfamo Kenya, Uganda na Ghana ambao walitumia kura za maoni tu na wakafanikiwa. Basi nasi Tanzania tutumie utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, mamlaka ya Tume ibara ya 10, Tume itakuwa na mamlaka na uhuru katika utekelezaji wa majukumu yake na haitaingiliwa na mtu au mamlaka yoyote. Hivyo natoa wito kwa Watanzania hususani vijana na wanawake kutumia fursa hii kutoa maoni yao kwa uhuru na kuhoji mamlaka ya Rais, haki ya kumiliki mali na ushirikishwaji wao kutumia asilimia za nchi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR: Mheshimiwa Spika, Zanzibar ni sehemu ya Muungano. Hii inatokana na kuwa Jamhuri ya Muungano imepatikana kwa kuungana nchi huru mbili yaani Jamhuri ya Zanzibar na Jamhuri ya Tanganyika. Hivyo Zanzibar ina haki sawa katika kuchangia Bunge la Katiba.

Vilevile ni haki yake Zanzibar kushauriwa katika kutozwa ushauri kwa hatua zote za utekelezaji wa zoezi. Inasikitisha kuwa Kambi ya Upinzani inatoka nje na haishiriki katika mjadala huu. Kambi ya Upinzani ina malalamiko mengi yakiwemo nguvu nyingi alizokuwa nazo Rais katika kuongoza nchi. Hii ilikuwa nafasi nzuri kwa Kambi ya Upinzani kuweza kuyajadili haya kwa azma ya kuyaingiza katika Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, lazima iwekwe wazi katika Muswada ikiwa matokeo ya kura hayakufikiwa theluthi mbili katika kura ya Bunge la Katiba yaani ikiwa hakuna upande utakaopata theluthi ya kura lazima pawekwe kipengele kitakachotoa *way forward*. Kipengele hiki hakimo katika Muswada huu unaendelea.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Mheshimiwa Celina Kombani, Waziri wa Sheria na Katiba, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa Muswada huu wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa mwaka 2011 akiwemo Mwanasheria Mkuu wa Serikali na timu nzima ya watendaji wake. Ukweli wamefanya kazi nzuri ambayo ninaiunga mkono mia kwa mia, nina matumaini Waheshimiwa Wabunge pia wanaunga mkono.

Mheshimiwa Spika, Tume kuundwa na Mheshimiwa Rais wa nchi nimesikitika sana kuona baadhi wanasiasa wanabeza Mheshimiwa Rais kuunda Tume itakayokusanya maoni kwa wananchi yatakayosaidia kutengeneza Katiba Mpya ambayo italicinda uhuru, haki na maslahi ya Watanzania bila kujali itikadi, jinsia, dini, kabilia na kadhalika wakiwemo wanawake.

Hivi hata katika akili za kawaida ni baba gani anayeweza kuachia mambo ya nyumbani kwake yaende hovyo hovyo, jibu ni kwamba hakuna. Hata hivyo Mheshimiwa Rais ni sehemu ya Bunge hili hakuna sheria ambayo inaweza kuwa sheria bila yeye kusaini. Leo imekuwa ajabu gani Mheshimiwa Rais kuunda Tume ya kukusanya mawazo?

Mheshimiwa Spika, mshangao wa Watanzania kwa Chama cha CHADEMA kukataa kujadili Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya mwaka 2011. CHADEMA ni chama ambacho kilikuwa mstari wa mbele kupiga kelele Serikali kuleta Bungeni Muswada wa mabadiliko ya Katiba wa mwaka 2011, waliendesha makongamano na maneno mengi ya kuishinikiza Serikali kuleta Muswada wa Sheria ya mabadiliko ya Katiba wa mwaka 2011 leo hawataki kujadili walitoka nje.

Mheshimiwa Spika, hii inatoa picha kuwa wenzetu hawa ni kweli wanafiki na wamestahili sifa tatu za mnafiki yaani kwanza akisema husema uongo, akiahidi hatekelezi na akiaminiwa haaminiki.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono kwa asilimia mia kwa mia maneno haya yaliyosemwa na Mheshimiwa Dokta Augustine Mrema, Mbunge wa Jimbo la Vunjo.

Ushauri kwa Serikali, napenda kuishauri Serikali kuwa Tume itakapoundwa ipewe angalizo kuwa itakapoenda kukusanya maoni itumie muda mwangi sana majibu yanayowakilishwa na Wabunge wa chama cha CHADEMA kwani ni dhahiri wameshapotoshwa vy a kutoshwa na Wabunge wao kama ilivyodhihirika jana hapa Bungeni wakati Mheshimiwa Tundu Lissu, Mbunge wa Jimbo la Singida Mashariki wa chama cha CHADEMA. Mchango ulijaa ushabiki, kebehi, dharau hata kwa viongozi wakuu wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, maoni yangu, nilitegemea wote tungeungana kuipongeza Serikali kuleta Muswada wa Sheria ya Katiba. Tuupitisho haraka ili Watanzania wapate nafasi kuchangia mambo muhimu yatakayowasaidia Watanzania kupata haki zao na maslahi yao wakiwemo wanawake ambao wanahitaji sheria zinazowagandamiza wanawake zirekebishwe haraka mfano Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 na nyngine nyngi.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda nimalize kwa kurudia tena kuwa ninaunga mkono hoja.

MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA: Mheshimiwa Spika, nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa msimamo wako thabiti katika kusimamia mchakato wa Muswada huu na kwa kushirikiana na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala katika kuuboresha Muswada.

Mchango wangu ni mdogo kwanza, naiomba Serikali iendelee kuwa na msimamo thabiti katika kusimamia na kuratibu mchakato wa Serikali iendelee kuelewesha Umma wa Tanzania kwamba huu ni Muswada wa kuunda Sheria itakayomwezesha Rais kuunda Tume ya kuratibu na kukusanya maoni ya wananchi kuchagua aina ya Katiba wanayohitaji. Katika suala hili la kuwaelimisha wananchi Serikali iwaombe Waheshimiwa Wabunge wa CCM na CUF washiriki kikamilifu.

Kuna mambo ambayo nayaona kama changamoto. Tume itakapoanza kukusanya maoni ya wananchi watagawanyika. Zanzibar karibu yote inataka kuwepo kwa Serikali tatu (*Federal Government*) Zanzibar State na Tanganyika State. Hata Watanzania wa Bara wengi watapenda Serikali tatu. Lakini swali ninalojuliza ni je kama Wazanzibar wote watataka Serikali tatu wakati wa maoni Serikali itafanya nini? Maoni yangu itabidi tukubali Serikali tatu. Bado tutakuwa pamoja katika mfumo tofuti. Maneno ya mwasisi mmoja wa Muungano Mzee Hassan Nassor Moyo yanaashiria mwelekeo wa mawazo ya Wazanzibar naomba nimnukuu.

"Waache vijana wajadili aina ya muungano wanaoutaka kwa maana uliopo ulianzishwa na waasisi wawili Nyerere na Karume kwa malengo yao. Watu hao wawili hawapo tena." Hii maana yake ni kwamba Wazanzibar hawautaki Muungano kama ulivyo sasa. Muundo wa Muungano tusiendelee kuuona kama ni msahafu (Biblia au Koran).

Jambo jingine ambalo nimekuwa nikilisisitiza na kuiomba Serikali ya Muungano isiyumbishwe na mtu yoyote ni ile ya uhuru wa kuabudu, kipengele cha uvumilivu wa dini nyngine asikirudishe mtu yoyote. Jambo jingine ninalolisitiza ni wananchi kupewa elimu juu ya Katiba iliyopo ili baadaye waweze kuchangia mabadiliko wanayoyataka. Kusema kweli tunahitajikutoa elimu ya Katiba kwa vijana wetu mashulen. Pia naiomba Serikali iwe makini sana katika uteuzi wa Mwenyekiti wa Tume. Mtu huyo awe ni *Judge* itapendeza zaidi kumteua Chief Justice Mstaafu ambaye ameendelea kuwa mwadilifu na mwaminifu kwa Serikali. Nafasi ya Katibu wa Tume pia ni muhimu sana. Ateuliwe mtaalam mzuri wa Sheria mwenye miaka mingi ya uzoefu. Nafasi ya Mwenyekiti, wa Bunge maalum pia ni muhimu na uteuzi wake uzingatie uzoefu na uzalendo.

Mwisho, Serikali iwe kali kwa wanaharakati na vyombo vy a habari. " *Effective Management of the building of the Constitution.*"

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuruhusu uundwaji wa Katiba mpya. Pia nampongeza Mheshimiwa Anne Makinda kwa kusimamia maoni ya kuandaa rasimu ya Muswada wa Mabadiliko ya Katiba, pamoja na shukrani hizo pia napendekeza yafutayo kuhusu mjadala huu.

. . . Kwa ujumla madhumuni ya Muswada wa Sheria hii yanaeleweka wazi ila nasisitiza kuwa mwafaka wa kitaifa na hasa hasa suala la Muungano litiliwe kipaumbele. Hivyo suala la uzalendo lizingative katika madhumuni yaliyoorodheshwa.

. . . Wajumbe wa Tume, kwanza wawe wazalendo. Pili waweke maslahi ya taifa mbele. Tatu wasiwe ving'ang'anizi waliowahi kuitaka Serikali ya Tanganyika kwa maslahi ya vyeo vyao. Nne wasiwe na tamaa ya madaraka, utajiri na kadhalika. Tano wasiwe na historia mbaya katika nchi hii. Hivyo namshauri Mheshimiwa Rais na Rais wa Zanzibar wawe makini katika kufanya mapendekezo ya wajumbe.

. . . Washiriki wa wajumbe katika Tume. Licha uzalendo kuwa kigezo kikubwa lakini makundi ya watu mbalimbali yashirikishwe. Mfano: Wanataaluma, vijana, wakulima, wafugaji, wavuvi na kadhalika. Ongezeko la washiriki toka makundi mbalimbali yataimarisha maoni toka pande zote za uwakilishi.

. . . Sheria kali itumike kwa mtu yoyote atakayepatikana na kosa la kuvunja masharti atakayekwamisha kumkwaza au kumzuia mjambe wa tume au sekretarieti kutekeleza majukumu yake. Naishauri Serikali kuwa kifungo cha mwaka mmoja au faini ya shilingi milioni tano ni kidogo sana. Ili kazi hii ifanyike vizuri na kwa kuwa kuna wanaharakati wengi ni bora faini iwe shilingi milioni kumi pamoja na kifungo cha miaka miwili jela. Hali hii itawafanya wanaharakati waheshimu utendaji wa tume.

. . . Mwisho napendekeza gharama za shughuli za Tume wakati wa mchakato wa mapitio ya Katiba kwa mujibu wa Sheria hii zitalipwa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina. Naunga mkono kuwa gharama zote ziwe chini ya Hazina kama ilivyopendkezwa na Waziri asihusike katika malipo hayo.

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Naomba kuwasilisha.

MHE. SAID MUSSA ZUBEIR: Mhesimiwa Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Naipongeza Kamati kwa Muswada huu pamoja na Waziri wa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, ninapendekeza kubadilishwa kwa kifungu cha *two third* kinachohusu Bunge Maalum la Katiba badala yake iwe asilimia hamsini kwa hamsini au waachiwe wenyewe Bunge Maalum la Katiba waamue utaratibu gani utumike.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Katiba na Sheria na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria na wote waliohusika na maandalizi ya Muswada huu. Suala la kuwa na Bunge la Katiba na kuwa na Kura ya Maoni liangaliwe upya kama ni lazima kuwa na vyote viwili. Muswada uwe wazi katika kueleza cha kufanya pale ambapo upande mmoja wa Muungano utakataa kupitia kura ya maoni.

MHE. SHAWANA BUKHETI HASSAN: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunapongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa usikivu wake wa kero na malalamiko ya Watanzania katika suala zima linalohusiana na Katiba mpya, hatimaye kuamua kuanza mchakato wa Katiba uanze ili wananchi wa Tanzania watoe maoni, kero ili Muungano wetu uwe katika muundo gani na utaratibu wa upi. Tunapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kutuletea Muswada huu wa Sheria wa kuunda Tume ya Mabadiliko ya Katiba kwa madhumuni ya kuratibu na kukusanya

maoni ya wananchi na kuweka utaratibu wa kuunda Bunge la Katiba ili kupatikane Katiba mpya. Pia tunapongeza Kamati ya Katiba na Sheria kwa kazi kubwa na nzuri waliofanya hadi kufikia Muswada huu kuletwa kwenye Bunge letu Tukufu. Kwa maana hiyo tunachukua nafasi hii kuunga mkono Muswada huu kwa asilimia mia moja.

Maoni na ushauri ndani ya Muswada. Kifungu cha 18, uwasilishwaji wa Ripoti ya Tume. Baada ya Tume kumaliza kazi yake itawasilisha Ripoti kwa Rais na Rais wa Zanzibar. Nashauri neno Rais likamilishwe; liandikwe Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar.

Kifungu 20 (2)(v) neno makundi yenyenye mahitaji maalum katika jamii. Nashauri makundi yaliyokusudiwa yatolewe uchambuzi ili yaeleweke. Kwa nini?

Kuna malalamiko kwamba kuna makundi mengi hayakushirikishwa kwenye Bunge hilo la Katiba. Kwa mfano vijana, walemvu, wazee na kadhalika. Pia Kifungu 20(3) Kifungu hiki nakiunga mkono sana na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wameridhia na wanakupongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuliona hili.

Mwisho, tunakushukuru sana kwa ule upungufu amba Zanzibar ilikuwa haikushirikishwa katika maeneo ya Muswada huu kuwa umekubali kuyafanya kazi na kuyajumuisha ndani ya Muswada kwa niaba ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, tunasema ahsante sana. Namaliza tena kwa kusema naunga mkono hoja kwa asilimia 100.

MHE. NIMROD E. MKONO: Kwanza kabisa, naunga mkono hoja hii.

Kwa kuwa sababu kuwa ya Muswada huu ni kutaka kupata maoni ya wananchi kuhusu mchakato mzima wa kupata Katiba mpya, ningetarajia kwamba mchango wa Wabunge ambaa ndio Wawakilishi wa wananchi wangeongezewa muda wa kuongea Bungeni. Nchi nydingi duniani kote Bunge huwa linakaa *full time*, kwetu Tanzania linakaa *part time*. Je, isingekuwa vyema Wabunge tukapewa *unlimited time* kutoa maoni yetu kuhusu Muswada huo badala kupewa dakika 15 za kusema?

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Budget ya vikao vya Bunge ni finyu, kwa nini wafadhili *UNDP* wakaombwa kutoa fedha ili kuwezesha Wabunge wakaketi mfululizo kwa miezi hata mitatu bila ya kutakiwa wakae foleni ili kupata muda wa kuchangia ili tukalimaliza jambo hili mara moja.

Kama fedha za kuwezesha Wabunge kukaa na kujadili kwa kina jambo hili fedha za kutembea nchi nzima kukusanya maoni ya wananchi waishio Tanzania tu zitatoka wapi?

Watanzania walioko nje ya nchi ningedhani pia wangefikiriwa. Je, hawa *diaspora* watafikiwa vipi?

MHE. ABDALLAH SHARIA AMEIR: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ningependa kumshukuru Muumba mbingu na ardhi na viliviyokuwemo ndani yake kwa kuniwezesha kuwa Mbunge na kunipa fikra za kuchangia Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, pili naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kukubali kufanyika kwa mchakato huu wa Katiba kwa roho njema kabisa. Nasema kuwa suala la Muungano ni suala la kutumia akili sana, ni suala la kutumia akili sana na hili si suala la kulfanyia mchezo wa aina yoyote ile.

Mheshimiwa Spika, Msemaji wa Kambi ya Upinzani haelewi kabisa maana ya Muungano huo na anaonekana ana umri mdogo sana chini ya miaka ya Muungano huo wa Tanganyika na Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, mimi nina wake wawili na kila mmoja ana haki kwangu na watoto wake kwa maamuzi madogo na makubwa kwa wakati wote na sio baba mdogo au jirani mwema, hivyo Rais ndiyo mhimili mkuu wa nchi hii, kwa hiyo ye ye ndie anastahili kuunda Tume

hiyo na kuweka Baraza la kupertisha Katiba mpya kama ilivyo kwani kumpa Mbewe, Slaa, na Tundu Lissu hili haliwezekani hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu, Muungano uendelee kuwepo, Rais awe mhimili mkuu wa Taifa letu kwa lolote lille, Muswada upitishwe kama ulivyopangwa na kama kuna haja ya kufanya kwa utaratibu tuliozoea. Mwisho, naomba kusitiza Tanzania ni lazima iwe na amani ya kudumu.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, naunga mkono hoja tena kwa asilimia mia moja.

MHE. LOLEIA J.M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri wa Katiba na kwa kazi kubwa na nzuri iliyofanyika ya kuandaa Muswada huu wa Mabadiliko ya Katiba. Pia naipongeza Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kwa mchakato mzima wa kupata maoni mbalimbali kutoka kwa Watanzania na hatimaye kuwawezesha kuboresha Muswada huu. Nimepitia kipengele kwa kipengele kwa Hakika Muswada umegusa maeneo yote ya muhimu. Nikiangalia mpangilio wa vifungu vyote vimekaa vizuri kabisa. Naunga mkono kwa Rais kuteua Wajumbe wa Tume kwa sababu kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Rais ndiye Kiongozi Mkuu wa Nchi.

Mheshimiwa Spika, ninachopenda kushauri ni katika sehemu ya sita ambayo ni uhalalishaji wa Katiba inayopendekezwa. Mara nydingi usoefu katika uchaguzi unaonesha kuwa idadi ya wananchi wanaojiandikisha katika Daftari la Kupiga Kura wanakuwa ni wengi ukilinganisha na wale wanaojitekeza kupiga kura. Kwa kuwa uhalalishaji wa Katiba iliyopendekezwa inapitishwa kwa kupigwa kura ya maoni, napendekeza kuwepo na elimu ya kutosha ikiwezekana Tume ya Katiba iweke utaratibu mahususi wa kufanya kampeni ya kuwaelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kupiga kura ya maoni. Wananchi walio wengi hasa vijijini wanahitaji kuelimishwa ili waweze kujua haki yao ya msingi ya kupiga kura, pengine itasaidia kuwafanya Watanzania walio wengi kushiriki kikamilifu katika mustakabali wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Kwanza nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kusikiliza kilio cha wananchi cha mahitaji ya Katiba mpya. Pia naipongeza Serikali kwa ujumla kwa kuhakikisha kwamba Muswada wa Mabadiliko ya Katiba unapitishwa na Bunge mwaka huu. Nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria kwa uwasilishaji mzuri sana. Maeneo mengi yamekwishachangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi, hivyo nisingependza kurudia.

Mheshimiwa Spika, moja tu ambalo ningependa kuchangia, ni kifungu cha 8(2) kinachohusu kuongezea Tume muda usiozidi miezi mitatu kama itahitajika ili kuwawezesha Tume kukamilisha na kukamililisha ripoti. Ningependa nipate ufanuzi kwamba ni kwa msingi upi Rais apangiwe muda usiozidi miezi mitatu. Je, kama Tume itahitaji muda zaidi, Serikali haioni kwamba itakuwa imeweka kikwazo cha kuikamilisha kazi ya Tume vizuri? Sheria haikumpangia Rais muda wa kuipa Tume wa kuifanya kazi ya kukusanya maoni, ni kwa nini sasa Sheria isimwachie Rais uhuru wa kuongeza muda kwa kadri atakavyoona inafaa au ni kwa nini aslongeze muda usiozidi miezi sita? Naomba ufanuzi.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Spika, Ibara ya 13 ya Muswada, Kifungu cha 13(1) napendekeza kuongeza maneno: "Atakayesaidiwa na Naibu Katibu", mbele ya neno la mwisho Katibu.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 13(2) napendekeza kuongeza maneno yafuatayo baada ya neno Katibu, yaongezwe maneno: "Na Naibu Katibu ambapo Katibu akitoka upande mmoja wa Muungano basi Naibu Katibu atoke upande wa pili wa Muungano".

Mheshimiwa Spika, watendaji hawa wakuu watakuwa karibu na Rais wa *SMT* na Rais wa *SMZ* ili viongozi hawa kuwa na urahisi wa kupata taarifa kwa haraka bila ufumbuzi wowote.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali itoe nakala za Katiba ya Jamhuri ya Muungano na kuzipeleka katika Kata mbalimbali ili wananchi wapate nafasi ya kuilewa Katiba ya sasa. Kwani imebainika Watanzania wengi hawailewi Katiba ya sasa jambo ambalo halitaleta ufanisi wa kutosha katika mjadala wa kutoa maoni ya wananchi baada ya kuundwa Tume na hatimaye kura ya maoni kwa njia ya kura.

MHE. AGNES E. HOKORORO: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, Katiba ni mali ya Watanzania na Watanzania walio wengi wanahitaji Katiba ya sasa ifanyiwe mabadiliko, upo umuhimu na mahitaji ya kupatikana kwa Katiba mpya kwa manufaa ya Watanzania na Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba una umuhimu wa kipekee kwa Taifa letu kutokana na kuwepo kwa malalamiko kadhaa yanayotolewa kuhusiana na Katiba iliyopo sasa, ni vema Muswada huu ukapitishwa ili Katiba mpya ijumuise mambo yote ambayo wananchi wanayataka yawepo katika Katiba yao.

Mheshimiwa Spika, wanawake wa Tanzania wanahitaji sheria ambazo haziwakandamizi. Muswada huu ukipitishwa na Bunge lako Tukufu utatupa nafasi wanawake wa Tanzania kuweka katika Katiba yetu mpya taratibu tunazotaka ziwepo katika sheria zinazohusu wanawake kwa kuwa Katiba ni Sheria Mama.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya Muswada huu ni mazuri yaani kuweka utaratibu wa kuunda Tume itakayokusanya na kuratibu maoni ya wananchi. Kwa maoni yangu, ni vema sheria hii ikapitishwa na Bunge ili kuwapa wananchi fursa ya kutoa maoni yao kuhusu Katiba mpya.

Mheshimiwa Spika, kama Tume haitaundwa, ni nani atakayeratibu maoni ya wananchi? Hakuna jamii inayoheshimu utawala bora isiyo na utawala kamili na uongozi, ni lazima kuwepo na namna ya kufanya mambo na kwa suala la Katiba, lazima Tume iundwe na mamlaka inayohusika ambapo Katiba ya sasa inaelekeza Rais anayo mamlaka hayo.

Mheshimiwa Spika, maoni ya wengine ya kwamba Rais ana mamlaka makubwa na kwamba hapaswi kuteua Tume, hawaoni kama kwa kutompa Rais mamlaka ya kuteua hiyo Tume wanataka iteuliwe au iundwe na nani? Hawaoni kuwa watakiuka Katiba ambayo tunayo sasa na tunaendelea kuitumia mpaka itakapopatikana Katiba mpya? Huo ni ukiukwaji wa Sheria mama ambayo ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ni wakati muafaka sasa wa Muswada huu kupitishwa ili Watanzania hususan wanawake tuweze kuwasilisha maoni yetu kwa Tume itakayoratibu Katiba mpya ili haki ambazo tunahisi tunazikosa ziweze kupatikana moja kwa moja kutoka Sheria Mama kuliko ilivyo sasa ambapo hata Sheria nyingi zinazohusu wanawake zinashindwa kufanyiwa marekebisho kutokana na ukinzano uliopo baina ya Sheria Mama na Sheria zingine.

Mheshimiwa Spika, naomba Watanzania wawe macho, wasikubali kucheleweshwa na watu wachache kwa kutotaka mabadiliko haya yafanyiwe. Katiba mpya inahitajika, wakati uliokubalika ni sasa, Tume iundwe ili wananchi watoe maoni yao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu (*Subhanah Wataala*) kwa rehema na neema zake alizoneemesh. Namshukuru zaidi Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa ni mionganini mwa Wabunge wanaojadili Muswada huu muhimu kwa mustakabali wa nchi yetu. Pia napenda kumshukuru na kumpongeza

Rais wetu Mheshimiwa Dokta Jakaya Kikwete kwa uadilifu, wema, ubora na upeo wake uliompeleka kufanya maamuzi sahihi ya kuanzisha mchakato wa upatikanaji wa Katiba mpya ambayo tunatarajia iwe bora zaidi ya Katiba tuliyonayo sasa.

Mheshimiwa Spika, huwezi kujua ubora wa kitu mpaka kitu hicho uwe nacho na baadaye kikutoke! Bila ya kuuona sasa na kuuthamini ubora na upeo wa Rais wetu, tutakuja kuuona baada ya kupatikana Rais mwingine ambaye hatapatikana kutokana na Katiba mpya!

Mheshimiwa Spika, Mtume Muhammed (*Swallah Alayh Wasallam*) Kiongozi wa umma huu anasema:- Asiyemshukuru mtu kwa wema, basi huyo hata Mwenyezi Mungu hawezি kumshukuru! Hatuna budi tumshukuru Rais wetu kwa upeo wake, busara, hekima na uadilifu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tatizo la mamlaka ya Rais. Kama Raisi ana madaraka makubwa ni kwa mujibu wa Katiba iliyopo, hakuyanunua dukani! Hapana budi Wabunge tuchangie Muswada huu, tuupitishe na uende kwa wananchi ili waamue Rais awe na madaraka gani! Madaraka ya Rais hayawezi kupunguzwa kwa maandamano wala hayawezi kupunguzwa kwa kukatwa na msumeno au panga lenye makali sana!

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu uliomo kwenye Muswada ndio utumike, yaani tufanye mambo yote mawili, Bunge la Katiba na Kura ya Maoni. Tanzania ni kioo cha Afrika na ndio maana anashauri tufanye yote mawili ili tupate Katiba nzuri yenye ridhaa halisi ya wananchi. Tanzania ni nchi ya kuigwa na sio ya kuiga!

Mheshimiwa Spika, hadidu za rejea zisiwe siri, ziwe wazi kama zilivyoainishwa kwenye Muswada na Waziri asiwe na nafasi ya kuziongeza. Hadidu za rejea ndio moyo wa Katiba mpya ambayo tunategemea iwe bora na vizuri zaidi ya tulivyo nayo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu muundo wa Tume. Napendekeza kifungu cha 14(2) kibadilishwe na kisomeke Wajumbe wa Tume na Sekretarieti watalipwa kwa mujibu wa Kanuni za malipo ya watumishi kwa ngazi husika. (Mamlaka ya malipo ya wajumbe wa Tume na Sekretarieti yasiwe mikononi mwa Waziri, kuwekwe utaratibu rasmi wa malipo yao).

Mheshimiwa Spika, napenda kuzipongeza timu mbili za wataalam ya Tanzania Bara na Tanzania Visiwani kwa kazi nzuri waliyoifanya na marekebisho ya Muswada huu. Tumefika mahali pazuri sana.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila bila kukupongeza wewe binafsi, Ofisi yako pamoja na Kamati ya Kudumu ya Katiba na Sheria ya Bunge lako, kwa kazi nzuri ya kizalendo mliyoifanya bila kuchoka mpaka hapa tulipofika.

Napenda pia kuziasa Tume zetu mbili za Uchaguzi, ya Bara na Visiwani wawe makini, wazalendo na wenye uchungu na nchi yao. Warekebishe madaftari ya wapiga kura ili wote wenye haki waingizwe na asiyekuwa na asilingizwe kwa hali yoyote. Kama wameingizwa kabla watolewe ili tupate Katiba halisi ya Watanzania isiyo na ushawishi wa wageni ambao hawaiiakii mema nchi yetu. Mungu ibariki Tanzania, Mungu ibariki Afrika, wabariki watoto wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii nitoe maoni yangu binafsi kuhusu hoja iliyombele ya Bunge lako Tukufu ambayo ni Muswada uitwao *Constitution Review Commission* au Muswada wa Kuunda Tume ya Mabadiliko ya Katiba ya nchi au kwa lugha yangu binafsi naweza kusema kuwa ni unaopendekeza iundwe Tume itakayoiangalia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ya kuanzia Ibara ya (1) hata ile ya 152 pamoja na nyongeza zake kwa madhumuni ya kupendekeza mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, Katiba ya sasa imekwishafanyika mabadiliko zaidi ya mara kumi mathalani mara 13 au 14 kama sikosei na mara zote hizi Katiba ilikuwa inafanyiwa mabadiliko kwa madhumuni maalum ili kuziba mwanya fulani au kutatua tatizo fulani. Mfano, mwaka 1992 Katiba

ilifanyiwa mabadiliko ili kuruhusu mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa nchini na mwaka 1995 ukafanyika uchaguzi mkuu wa Vyama Vingi vya Siasa na kuzaa Bunge la Vyama Vingi vya Siasa (*Multiparty Parliament*).

Lakini kwa mapendekezo ya Serikali ambayo nyaunga mkono ni kuunda Tume itakayokusanya maoni kutoka kwa wananchi kama niliyoyasema hapo awali ni kuangalia Katiba mpya yote kuanzia Ibara ya (1) hata ile ya 152 na nyongeza zake. Hivyo kwa maoni yangu ni kwamba kiini cha Muswada huu ni kuundwa kwa Tume itakayokusanya maoni toka kwa wananchi kwisha, suala hili likieleweka hakuna ubishi, majibishano au malumbano yoyote. Tume hiyo itakapoundwa itakwenda kwa wananchi kupata maoni yao. Kwa mfano, Katiba hii ya sasa ina Sura kumi. Kazi itakayofanywa na Tume nadhani ni kuangalia sura baada ya sura kupata maoni hayo. Mfano, Sura ya Kwanza yenye ibara 32 inazungumzia kuhusu eneo hili.

Mheshimiwa Spika, Sura ya Pili yenye ibara 34, inazungumzia kuhusu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wetu watoe maoni yao kuhusu eneo hili. Sura ya tatu yenye ibara 40 inaelezea kuhusu chombo chetupi sisi, yaani Bunge la Jamhuri ya Muungano, watu watatoa maoni yao kuhus chombo hiki. Hivyo Tume itaendelea kufanya hivyo hadi ile Sura ya Kumi au *Chapter Ten*.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kusema kwamba ieleweke kuwa kilicholetwa mbele yetu Bunge na Serikali ambapo kwa usahihi, kilicholetwa kwetu kama "*National Assembly to be specific and not Parliament* ni uundwaji na Tume ya Kukusanya Maoni ya Katiba." Baada ya mchango huo na jumla sasa niingie kwenye vipengele vya Muswada, nikianza na *Long Title*.

Mheshimiwa Spika, niruhusu ninukuu sehemu ya eneo hili, mstari wa kwanza na wa pili: "*An Act to provide for the Establishment of the Constitutional Review Commission*." Mwisho wa kunukuu. Nukuu hii, kama niliyoyosema hapo awali, ndio msingi na mapendekezo ya Serikali kwetu Wabunge kuhusu Muswada huu kwamba, Serikali inapendekeza kuundwa kwa Tume ya Kukusanya na Kuratibu Maoni ya wananchi. Aidha, lugha hii inaonekana wazi kwenye Ibara ya (4) ya Muswada.

Mheshimiwa Spika, ili ibara ndogo ya (1) ya Ibara ya (1) ya Muswada iende sanjari na *Long Title* niliyosoma hivi punde napendekeza neno *Commission* lionezwe baada ya neno *Review* ili ibara ndogo hii isomeke kama ifuatavyo:-

"This Act may be listed as the Constitutional Review Commission Act, 2011".

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia mchango wangu niende ibara ya 20 ya Muswada inayoongelea kuhusu uundwaji wa Bunge la Katiba. Hapa natofautiana na mapendekezo ya Serikali, maoni yangu ni kwamba, badala ya chombo hicho kuundwa na Rais kazi hiyo ifanywe na Bunge kwa kujigeuza kuwa *Constituent Assembly*, kama ambavyo hujigeuza kuwa Kamati ya Matumizi au Kamati ya Bunge Zima. Sababu za maoni yangu haya ni *cost implication*. Sababu nyingine ni kwamba, watu wanaopendekezwa kwenye chombo hicho ni wengi sana na pengine wengi wao watakuwa tayari wametoa maoni yao kwenye Tume. Bahati mbaya hayakuafikiwa na Tume au hayakuingia kwenye taarifa ya Tume, basi wataanzisha mjadala mpya kwenye *Constitution Assembly* hivyo kuzua upya malumbano.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa Bunge kujigeuza kama *Constitution Assembly* wakati wa kutunga Katiba mpya ya nchi kama sikosei ulitumiwa na Afrika Kusini na hivyo kutungwa kwa Katiba ya sasa ya nchi hiyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, maoni nitakayoyatoa, yanaweza yasiwafurahishe baadhi ya watu, lakini ndio maoni yangu, kama ambavyo niliwahi kusema kuwa, kipindi cha maswali kwa Waziri Mkuu kifutwe kutokana na kupoteza lengo la kuanzishwa kwake. Yamekuwepo maneno mengi sana kutoka kwa watu mbalimbali, watu binafsi, baadhi ya Wabunge, vikundi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mapendekezo ya Serikali juu ya Muswada ulio mbele yetu. Muswada husika uliposomwa kwa mara ya kwanza, na majadiliano kufanyika ndani ya Bunge Serikali ambayo ndio *mover* ili kutilia maanani maoni ya Waheshimiwa Wabunge na wananchi

kwa ujumla wake waliutoa. Serikali imeuleta Muswada huu ili usomwe mara ya pili japokuwa watu wametaka usomwe mara ya kwanza sina hakika kama Kanuni za Bunge zinazo-cover eneo hili wanazifahamu vizuri kwa kutilia maanani maoni mbalimbala yaliyotolewa.

Mheshimiwa Spika, bado watu hawataki na kuendeleza malumbano ambao hayana tija, matokeo yake hatutafika kule tunakotaka kwenda.

Mheshimiwa Spika, maoni yangu, kama hali itaendelea kama ilivyo Serikali kama *mover* wa Muswada huu, *withdraw* na Rais Kikwete kwa kutumia mamlaka aliyonayo kisheria aunde Tume kama ile ya Jaji Mkuu Marehemu (Mungu ailaze roho yake mahali pema Peponi) Francis Nyalali maarufu kama Tume ya Nyalali, ambayo ilipendekeza mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa, ambapo matunda yake tunafaidi humu ndani na ile Kamati ya Kuratibu Maoni kuhusu Katiba ya Nchi, Taarifa ya mwaka 1999, maarufu Kamati ya Jaji Robert Kisanga, ambao pamoja na mapendekezo kadhaa ambayo Kamati hiyo ilipendekeza ni pamoja na pendekezo la kuongeza idadi ya Viti vya Wabunge Wanawake na kufikia asilimia 30% ya Wabunge wote. Pendekezo hilo, liko ukurasa wa nne, hoja ya nane (c) ya taarifa hiyo na illafikiwa na Serikali, ikaleta Muswada Bungeni na kupitishwa na Bunge na Rais kusaini Muswada huo na kuwa Sheria. Hii inaonekana wazi kwenye ibara ya 66(i) ya Katiba ya nchi ambapo baadhi yetu tumefaidi matunda ya Kambi hiyo.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema hapa ni kamba, Tume au Kamati ambazo ziliwhi kuteuliwa na Marais waliopita, zilifanya kazi nzuri ambazo matunda yake tunayaafaidi wengi wetu, hivyo, ikibidi basi Serikali i-*withdraw* au au iuondoe Muswada huu au ashauriwe Rais aunde Tume au Kamati.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono Muswada au hoja hii.

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Spika, sisi Wabunge tulimo ndani ya Bunge hili na wale wenzetu waliotoka mara baada ya Uchaguzi wa Oktoba 2010, tulikuwa tunaitwa Wabunge wateuliwa, ni pale tu tulipoapishwa ndipo tukawa Wabunge. Katika kiapo hicho tunatakiwa tulinde na kuitetea katika kiapo hicho, tunatakiwa tulinde na kuitetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Katiba hiyo inatambua uwepo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Baraza la Wawakilishi Kifungu 102-107 cha Katiba kinahusika. Iweje leo Mbunge aliyeapa kuilinda na kuitetea Katiba aweze kudharau Zanzibar kuwa ni sehemu ya mdau wa Muungano.

Mheshimiwa Spika, Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani alidhihirisha kuwa Zanzibar inapendelewa, sioni hilo kwani Muswada wa Marekebisho ya Katiba ulichokifanya ni kwenda kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ndani ya Muswada huo inadhihirika wazi uwepo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hakuna upendeleo wowote kama ilivyodaiwa na Kambi Rasmi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, nimependekeza Kifungu cha 13(3) kifanyiwe marekebisho, nionavyo mimi, Katibu wa Tume asiwe ni Mtumishi wa Serikali au si lazima awe Mtumishi wa Serikali, wako Majaji Wastaifu wengi ambaa wanaweza kushika nafasi hiyo.

Mheshimiwa Spika, ipo haja kuwepo Kifungu kitakachomtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aweze kukagua mahesabu ya matumizi ya Tume na Bunge Maalum la Katiba.

Mheshimiwa Spika, ndani ya Muswada huu hamna muda unaoeleweka ni lini kura ya maoni itafanyika, ni vema mchakato ueleze ni lini (*timeframe*) kura ya maoni itafanyika.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

MHE. HUSSEIN MUSSA MZEE: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Katiba pamoja na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kufanikisha Muswada huu ambao ni mzuri uliokidhi haja. Kwa Wazanzibari pamoja na Watanzania Bara, huu ni Muswada tu kwa ajili ya kuelekea huko kwenye Katiba mpya, sasa wale wanaoupinga Muswada huu hawaitakii mema Tanzania. Pia nafikiri hawajui historia ya Muungano wetu huu, kwani Tanzania imepatikana kwa Muungano wa nchi mbili kati ya Tanganyika na Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, sasa nachangia Sehemu ya Tano ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, Kuundwa Bunge la Katiba, 20(ii) naona haina haja ya Rais wa Tanzania na Zanzibar kushauriana na Wanasheria kwa vile Rais anao uwezo wa kushauriana na mtu yejote wakiwemo Wanasheria Wakuu, kwa hiyo, hakuna haja ya Rais kulazimisha.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 24(3) iko haja ya kukirekebisha, kimetumika kutokana na Katiba yetu ya mwaka 1977. Sasa Katiba hii ilikuwa imetumika wakati wa chama kimoja. Sasa theluthi mbili kwa Wazanzibar kwa wakati huo ilikuwa ni rahisi, lakini sasa Vyama Vingi theluthi mbili inakuwa vigumu kupata ushauri wangu. Kifungu hiki kibadilishwe kwani huenda isipatikane hiyo theluthi mbili ya Zanzibar, ningependekeza iwe nusu ya *majority* ili tusije tukakwama huko mbele, nia yetu tufanikiwe kuwa na Katiba mpya.

Mheshimiwa Spika, kipengele kinachohusu Muungano wetu kisiguswe, ni kizuri na nakipongeza.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. DKT. FENELLA E. MUKANGARA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono Muswada huu kusomwa kwa Mara ya Pili. Nampongeza Mheshimiwa Rais, Dokta Jakaya Mrisho Kikwete kwa uamuzi wa kuanzisha huu mchakato, ni uamuzi wa busara na ujasiri.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza pia Waziri, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Sheria na Wajumbe kwa kazi nzuri na yenye kuzingatia umuhimu wa kuratibu maoni mbalimbali yaliyojiteze katika kuboresha Muswada huu. Napongeza pia maoni mbalimbali yaliyotolewa ya kuunga mkono na kuboresha muonekano wa Muswada huu kwa jamii na kujenga msingi imara wa demokrasia katika nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 33, pale inapozungumziwa Sekretarieti, kifungu cha 13(3), sifa za kuwa Katibu wa Tume nashauri zibadilike kidogo. Kigezo cha kwamba Katibu Mkuu lazima awe Mwanasheria siyo sahihi na hakina maeleo ya kitaaluma kwa nini? Tukizingatia Tume kazi yake kubwa ni kukusanya maoni ya watu mbalimbali, hapa anahitajika Katibu ambaye ni mtafiti anayeelewa masuala ya kura za maoni (*opinion polling*). Akiwa ni Mwanasheria ni *added advantage*, siyo kigezo cha kwanza.

Mheshimiwa Spika, huyu Katibu anategemea kusimamia utengenezaji wa chombo (*tools*) mbalimbali za kukusanya hayo maoni, utekelezaji wake na kusimamia uchambuzi wake kitaalam ili yawekwe kisheria na kuona ni namna gani yanaingia katika Katiba. Mchakato huo wote wa kwanza, Katibu anasimamia a *social political process*.

Mheshimiwa Spika, nashauri tuwe makini tusimfunge Rais kwa kutoa Muswada unaotoa picha kwamba Katibu ni lazima awe Mwanasheria. Inafahamika kiutendaji suala la kuandika Katiba ni la kisheria lakini suala la kutafuta maoni, kiutendaji si la kisheria wapo watu wenye hiyo fani kwa jamii yenye kubeba masuala yanayoingia katika Katiba, wapewe hiyo nafasi bila kuweka vigezo vinavyombana Rais katika hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi ni makosa kuweka kigezo cha Katibu kuwa Mwanasheria, katika hili nashauri kiondolewe au kiongezwe: "Mtafiti wa masuala ya kura ya maoni". Hili nalisitiza tukizingatia kwamba tayari *Secretariat* itakuwa na Wanasheria wa kutosha, ni muhimu wapate Katibu mwenye uelewa wa masuala ya *social political* na pia mtafiti kuweza kutoa na kusimamia mchanganuo wa mawazo mbalimbali, mtafiti mwenye ujuzi wa sheria ni *added value*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu jina la Muswada, naona na kushauri kama wengine ni sahihi *Constitutional Review Act*, labda kuwafahamisha wananchi wafahamu tu kwamba sheria hii ikitungwa si kwa ajili ya zoezi la muda la mwaka 2011 tu, bali ni sheria ya kuweka utaratibu wa kurekebisha Katiba au kutunga Katiba mpya inayotegemewa kudumu kwa miongo mingi. Utaratibu huo haukuwepo katika Katiba na sheria za sasa. Hata kama ikipatikana Katiba mpya kwa mchakato wa sasa yawezekana kuwa huko mbele Katiba hiyo ikataka marekebisheso. Hivyo basi, jina linafaa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nafasi ya Rais katika mchakato wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba. Wapo wanaosema kuwa Rais asishiriki asilani katika mchakato wa mabadiliko ya Katiba, wengine wanasema ni kwa sababu yeze ni zao la Katiba iliyopo, wachangiaji wengi wameeleza vizuri sana na nategemea wananchi wameelewa vizuri kwa nini huu mchakato unaanza na Rais na kuishia na Rais.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria unatoa na unaonesha ni mchakato mrefu wenye vipengele vingi na Rais anashiriki mara chache sana kuliko wadau wengine wengi amba wana nafasi nyeti zaidi ya kuunda Katiba wakiwa wapo ndani au nje ya Tume ya Katiba mfano mzuri katika hili ni Wanasheria. Ushiriki wa Rais ulioainishwa katika Muswada ni wa kutangaza Bunge la Katiba, kutia saini Muswada ili iwe sheria, Katiba, kuchangia kuteua wajumbe 116 wa kuwa katika Bunge la Katiba, kutangaza kuvunja Tume, kuteua Tume, kuipa hadidu za rejea Tume. Lakini hata kutika hilo nguvu za Rais zimedhibitiwa kwa vigezo kadhaa vyta uteuzi vilivyomo katika Muswada ambavyo vinazingatia uwiano na upanuzi wa uwakilishi wa makundi katika Tume. Kama tulivyoona wengi wenye kulalamika na kusitiza makundi fulani yawepo, tayari yapo.

Mheshimiwa Spika, pia unaacha uwezekano wa Rais kuunda Bunge la Katiba kwa kulitangaza Bunge liliopo na kuongeza Wajumbe 116 kuwa Bunge la Katiba. Huu niupongeze ni utaratibu unaokubalika na hasa kwa kupunguza gharama za uchaguzi wa Bunge lingine la ziada kwa ajili ya Katiba tu.

Mheshimiwa Spika, pia faida nyingine ni kuvuna manufaa ya uzoefu wa Bunge liliopo hivi sasa na hasa kuzingatia tumetoka katika uchaguzi, napenda niseme tu heshima hiyo kutoka kwa Rais kwa wananchi wake na kwa demokrasia inaonekana vizuri zaidi katika Muswada huu kwa kuweka maamuzi ya wananchi juu ya Bunge na Rais kwa kutambua kuwa uhalalisho (*validation*) wa Katiba ni wao kupitia kura ya maoni (*referendum*) baada ya Bunge kupitisha Muswada na Rais kutia saini Sheria ya Katiba. Nafasi ya Rais ni mahali pake kuwa na Katiba. Nafasi ya Rais ni mahali pake kuwa na *powers* hizo zote.

MHE. ZAKIA H. MEGHJI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, inaonekana baadhi ya viongozi wamechoshwa na amani na hivyo wanataka kuondoa amani. Viongozi amba wamechaguliwa na wananchi wanapoamua kutofanya kile walichowaahidi wananchi wao na kujihusisha zaidi na vitendo vyta kuvunja amani. Amani ikitoweka wote watahusika hakuna wa chama hiki au kile, zaidi watakaoumia ni wanawake na watoto.

Mheshimiwa Spika, siku zote binadamu wana mawazo mbalimbali na huweza kutofautiana, ni muhimu kuwa wavumilivu na kusikiliza mawazo ya wenzako na kujaribu *ku-argue your case*, ukishindwa basi ni uungwana tu kukubali. Hiyo ndiyo demokrasia tunayozungumzia. Jambo linalonekana kufanya na chama cha CHADEMA kwa sababu zao wenyewe, kuwa wao hawakumtambua Rais tokea awali, hata pale Rais alipoapishwa walitoka nje. Ni kwa sababu hiyo ndiyo inayofanya CHADEMA kukataa madaraka yoyote ya Rais katika mchakato wa mabadiliko ya sheria hii.

Mheshimiwa Spika, Muswada umeweka vizuri juu ya mawasiliano kati ya uongozi wa Zanzibar na Tanzania Bara na pia utaratibu wa uwakilishi. Hii inatambua nafasi ya Zanzibar kihistoria na hivi sasa katika Muungano. Inasikitisha unapoona viongozi wanaobeza uongozi wa

Zanzibar, Rais wa Zanzibar na nafasi ya Zanzibar, nashauri wakasome tena historia ya Zanzibar, Muungano na Katiba yetu.

Mheshimiwa Spika, katika *Constituent Assembly* kutakuwa na Wabunge wote na wawakilishi pamoja na wengine watakoateuliwa, haielekezi watateuliwa vipi. Nashauri kipengele hiki kiangaliwe kwa kuwa Bunge hili na Baraza la Wawakilishi wamechaguliwa, basi kuwe na utaratibu na wale wengine nao pia wachaguliwe kama katika ngazi za Wilaya, Mkoa, kupitia Vyama vya Wafanyakazi, Ushirika na kadhalika, ili kuleta uwiano.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 14, Sehemu ya Tano (20)(2)(c) na (d) hapa wanatajwa Mawaziri wanaohusika na mambo ya Katiba na pia *Attorney General*. Hakuna haja ya vipengele hivi kwa kuwa hawa hawa pia ni Wabunge.

Mheshimiwa Spika, Katiba ya sasa ndiyo itakayofanya kazi mpaka Katiba inayokuja ipitishwe, kwa hiyo hakuna *vacuum* na kwa hiyo hayo yaliyopendekezwa ni muhimu yaende sambamba na Katiba yetu. Ni vizuri *terms of reference* za Tume sasa zikawekwa kwenye sheria hii. Ni muhimu pia kuweka vigezo vya Wajumbe wa Tume kwani hawa ndiyo wanapokea mawazo na kuyaandika katika Muswada na pia Tume kwanza hupeleka ripoti kwa Rais na baada ya *consultation* na Rais wa Zanzibar na kupeleka katika Bunge la Katiba. Ni kweli aliyetoa kazi siku zote anarudishiwa kazi, lakini kwa kuwa Rais ndiye anayeitisha Bunge la Katiba na baadaye kuwa chini ya Bunge la Katiba, basi ripoti ya Tume inaweza kwenda moja kwa moja kwenye Bunge la Katiba kwa kuwa ni yeze kama Kiongozi Mkuu wa Taifa anayesimamia mchakato mzima. Katibu wa Tume naye pia badala ya kuteuliwa nafasi hii inaweza kutangazwa na watu mbalimbali waka-*apply* katika kazi hii na yule atakayekidhi vigezo akapata kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wajumbe wa Tume isiwe zaidi ya thelathini, iwe si zaidi ya ishirini ili kupunguza Wajumbe wa Tume.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 8, kifungu cha 9(2)(1) kuhusu *Commission shall adhere to national values and ethos* (a) mpaka (i), suala la *gender equality* ni muhimu na lingepaswa liingizwe.

Mheshimiwa Spika, jina la Muswada pia u-reflect na kuanza mchakato.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono Muswada huu.

MHE. SHAFFIN A. SUMAR: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja. Awali ya yote natoa pole za dhati kwa wana-Tabora na wana-Mbeya kwa matatizo yaliyowakumba kiasi ambacho amani ilivunjika.

Mheshimiwa Spika, nilishangaa sana kusikia hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani iliyosomwa na Mheshimiwa Tundu Lissu, inaelekea kuwa CHADEMA wamechoka na amani tuliyonayo. Lakini nimejifunza mambo mawili ambayo ni kwamba, CHADEMA wana matatizo ambayo ni masuala mawili nayo ni Rais na Muungano. CHADEMA hawamtambui Rais wetu, tutakumbuka kwamba mnamo tarehe 18/11/2010 CHADEMA walisusia hotuba ya Rais ambapo Rais alihutubia Bunge jipya la Kumi, CHADEMA walisusia kwa maana ya kutokuntambua Rais wa Jamhuri, Rais ambaye anatokana na Katiba ya Nchi yetu. Katiba ambayo waliapa kiapo cha kuilinda na kuitetea siku chache tu kabla ya kususia hotuba ya Rais.

Mheshimiwa Spika, Rais wetu kwa nia njema ameamua kukubali kuwa Watanzania wapate Katiba mpya, lakini CHADEMA bado wanasusia mjadala, sisi Wabunge tumechaguliwa na wananchi na hapa Bungeni ni sehemu ambayo tunapata fursa ya kuwatetea wananchi wetu waliotuchagua, "hakika mbishi hatibiki".

Mheshimiwa Spika, lakini CHADEMA wanacheza mchezo huu kwamba Rais akikubali tutagoma, Rais akikataa pia tutagoma.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kuhusu Muungano. CHADEMA wanajitambua kuwa kule Zanzibar wao hawana kura za uhakika, hawana wanachama, ni njama nzito kwao, ndiyo maana hawataki Muungano lakini Watanzania waelewe kwamba kuvunja Muungano ni kosa ambalo halitasameheka wala kusahaulika athari yake itaendelea kuathiri miaka na miaka ijayo sababu kule Zanzibar kuna Wazanzibar na Wazanzibara, kuvunja Muungano ni kuanza kutenganisha familia hizo pia huku bara kuna Wazanzibar ambao wameoa au wameolewa, tusiwanyime haki zao za kuishi bara. Muungano ni jambo la kujivunia katika Bara zima la Afrika, hakuna nchi hata moja ambayo imeingia Muungano na nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, Katiba ni sisi sote, hali yetu, maisha yetu, furaha yetu na utamaduni wetu ndiyo maana ya Katiba. Tusinghaji Katiba ikishaandikwa ndiyo inaanza kujengwa, kuna fursa ya kutosha kabisa ya kurekebisha Katiba, mfano, Katiba ya Kenya iliandikwa 2010 na mwaka huu wanafanya marekebisco kwenye Katiba, ni jambo la kawaada. Katiba siyo Msahafu kwamba usifanyiwe mabadiliko hata kama Serikali ikiwachukua maprofesa walioTABAHARI katika masuala ya kuandika Katiba na wakaandika lakini bado Katiba hiyo itahitaji marekebisco.

Mheshimiwa Spika, jukwaa la Katiba walitoa mapendekezo mengi na hoja zingine zimechukuliwa na Serikali na kuingizwa kwenye Muswada huu ambayo imesema kumpunguzia madaraka Rais pia hadidu za rejea zimeelezwa ndani ya Muswada huu, sasa hofu inatokea wapi? Naomba Watanzania wakubali kuwaamini Wabunge wenu ambao tutawatendea haki na sisi tusipofanya hivyo uchaguzi ukija halali yenu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGWALLA: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuwapongeza nyote mlioshiriki kwa kazi hii nzuri. Watanzania waelewe kwamba Bunge sasa halijadili kuandika Katiba mpya, bali tunajadili Muswada kwa ajili ya kutunga Sheria ambayo itapelekeea kuanza mchakato wa kutunga au kuandika Katiba mpya; ambapo kunaelezwa utaratibu wa kuunda Tume itakayokusanya maoni ya Watanzania, lakini pia sheria hii imeweka hadidu za rejea.

Mheshimiwa Spika, Naipongeza Serikali kwa hili, wenye kulalamika kuhusu ubovu wa sheria hii wana matatizo yao ambayo mimi sina dawa ya kuwapa, maana Serikali imemtengenezea Rais masharti ya kufuatwa pia imeweka hadidu za rejea. Yote haya hayajawahi kuwepo huko nyuma. Hii inaonesha ni jinsi gani Serikali yetu imesikia mapendekezo ya wadau na kuamua kuweka uwazi zaidi kwenye hili suala na pia kupunguza kwa kiasi kikubwa kabisa *discretion* ya Rais wetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali iendelee mbele na jitihada hizi ili tupate Katiba mpya, msiwasikilize hao wenye malengo yao ya siasa za vurugu. Watanzania wakumbuke hatujawahi kuwa na matatizo ya kazi zilizofanywa na Tume huko nyuma, Tume nydingi zilileta maoni yao kama yalivyo na hayajawahi kuwa ya kumfurahisha Rais hata siku moja, kuanzia Tume ya Nyalali hata ile ya Kisanga.

Mheshimiwa Spika, pia niwapongeze sana kwa kuchukua njia ndefu na ngumu kufikia Katiba kwa maana ya kuanzia *Constituent Assembly* hadi hapo baadaye *referendum*, ni njia hatari na wengine duniani wamekuwa wakiikwepa lakini sisi kwa kuleta demokrasia na kuongeza ushiriki wa wananchi moja kwa moja tumeamua kuipendekeza, nadhani ipite kama ilivyo.

Mheshimiwa Spika, kazi ya kutunga sheria Kikatiba ni ya Bunge na nawapongeza Serikali na Kamati ya Sheria na Katiba kwa kuendesha zoezi hili vizuri. Endeleseni mshikamano huo na sisi tutaendelea kuwaunga mkono. Nashauri zoezi hili liharakishwe na iundwe *task force* ya muda ili kuwaelimisha wananchi wachache walipotoshwa na wanasiaya uchwara wenye uchu na tamaa ya kutawala kwa mabavu bila kupewa ridhaa na wananchi.

Mheshimiwa Spika, nchi hii ni huru na ina mifumo mizuri iliyotufikisha hapa kwa amani. Hii ni tunu ambayo tutailinda kwa kila hali. Tusikubali kuvurugwa na wapotoshaji hawa kwa maslahi yao binafsi. Nchi hii ina Rais na Bunge liliowekwa Kikatiba, ina Katiba ambayo inaongoza kila kitu,

ukitaka Rais asishiriki kuunda Tume au Wabunge wasishirikishwe, sasa unataka nani afanye hizi kazi, maana sisi tupo hapa Kisheria na Kikatiba.

Mheshimiwa Spika, natanguliza shukrani zangu za dhati na fanaka.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja iliyopo mbele yetu kwamba Muswada tajwa usomwe kwa mara ya pili ili hatimaye kutoa fursa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuunda Tume kwa ajili ya kukusanya maoni ya kuundwa kwa Katiba mpya na Bunge la Katiba.

Mheshimiwa Spika, kimsingi naipongeza Kamati ya Sheria na Katiba kwa kuweza kuunda Muswada tajwa kwa wakati, pia niipongeze Serikali kwa utayari wake wa kuridhia marekebisho mbalimbali yaliyopendekezwa na wadau pamoja na Kamati yenyewe. Aldha, naunga mkono Mheshimiwa Rais ambaye ndiye Mkuu wa nchi aunde Tume ya kukusanya maoni ya namna nzuri ya kuundwa kwa Katiba mpya ya nchi wakati huu tunapojiandaa kuadhimisha miaka hamsini ya uhuru wa Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, nchi yoyote duniani inaongozwa kwa mujibu wa Sheria Mama ya nchi ambayo ni katiba. Kwa msingi huo mgawanyo wa madaraka baina ya Taasisi mbalimbali katika dola hubainishwa ndani ya Katiba ya nchi husika.

Mheshimiwa Spika, mahusiano baina ya dola na wananchi wake yanawekwa na kuzingatiwa ndani ya Katiba. Katiba vilevile ndicho chombo kinachoundwa na kuweka misingi inayotawala mahusiano baina ya mtu na mtu.

Kwa mantiki hiyo basi, dola ambalo linagawanywa kwa mihimili mitatu ambayo ni Serikali, Bunge na Mahakama. Mgawanyo baina ya Mihimili hiyo mitatu unazingatiwa ndani ya Katiba ya nchi. Kuna kila sababu sasa kwa upande wa Serikali kuhakikisha kwamba taratibu zote za kisheria zinachukuliwa kuhakikisha kwamba mchakato mzima wa uundwaji wa Tume ya Kukusanya Maoni ya uundwaji wa Katiba mpya ya nchi kwa kuanzia na upitishwaji wa Muswada wenyewe tunaopitisha hii leo.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuhakikisha kwamba wale wote wanaojiandaa kukwamisha zoezi hili wakiwemo Jukwaa la Katiba, Wanaharakati wasiokuwa na nia njema pia wanasiaya wanadhibitiwa kwa nguvu zote ili wasiweze kusababisha uvunjifu wa amani wakati wote wa mchakato wa kupatikana kwa Tume na Bunge Maalum la uundwaji wa Katiba mpya.

Mheshimiwa Spika, kwa namna nyingine, naunga mkono Muswada huu kwa asilimia mia moja.

MHE. ALIKO N. KIBONA: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Rais kwa uamuzi wa kuleta mapendekezo ya kuitazama upya Katiba yetu. Nampongeza Waziri wa Katiba na Sheria kwa kufanya kazi nzuri ya kuchapisha *draft* nzuri ya kuonesha mchakato wa kuunda Tume ya kuratibu majadiliano ya Katiba. Nawapongeza sana Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria kwa kufanya kazi nzuri pia.

Mheshimiwa Spika, maoni yangu ni kwamba, Tume itakayoundwa na Rais, itakayokusanya maoni, iwe na mchanganyiko wa makundi yote ya kijamii madhehebu, wasomi, wafugaji, wakulima, wafanyabiashara na kadhalika. Kila kundi litoe maoni bila kutishwa au kushinikizwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Katiba ya zamani iliyorekebishwa tangu uhuru kwa nyakati tofauti. Katiba hiyo hiyo imeendelea kufanya kazi, lakini haikuwahi kusambazwa kwa watu wengi na kueleweka. Basi, kabla ya kupigwa kura ni vizuri watu wakasoma na kueleweka kwa watu wengi katika nyanja mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Muswada unasema Raisi atashauriana na ... Maoni yangu, Rais asipewe mipaka. Akitaka kupata ushauri aamue yeche, kamwe mtu katika kufanya jambo halazimishwi kwamba, ushauriwe na mtu fulani. Busara yake ndiyo iamue anapotaka ushauri, apime yeche mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, naunga mokono hoja.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumekwishafunga mjadala, sasa tunaanza kuwaita mtoa hoja na watu wake waanze kujibu hoja moja moja; ninadhani ataanza Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa Mwaka 2011. Nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Waziri Celina Kombani, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mwandishi Mkuu wa Sheria, Makatibu Muhtasi, Makarani na Madereva wa Ofisi yangu na Wizara ya Katiba na Sheria. Aidha, kwa aina ya pekee, ninawashukuru sana Viongozi wetu Wakuu; Rais wa Jamhuri ya Muungano, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete; Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal; Rais wa Zanzibar, Dkt. Ali Mohamed Shein; na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayaza Pinda. (*Makofii*)

Ninakushukuru sana Mheshimiwa Spika, kwa uongozi wako katika jambo ambalo liko mbele yako. Ninawashukuru sana Mheshimiwa Othuman Masoud, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Wasaidizi wake, kwa mchango na ushirikiano wao katika kuuboresha Muswada huu, bila kumsahau Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria wa Zanzibar. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umechapishwa upya, umetafsiriwa katika Lugha ya Kiswahili na lugha zote mbili zinatumika. Hata hivyo, Muswada ulio Bungeni ni ule unaosomeka kwa Lugha ya Kiingereza, kwa sababu huo ndiyo ambaa umefanyiwa rejea na ndiyo ulioletwa mwanzo. Muswada umefanyiwa marekebisho yatonakayo na Maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Maoni ya Wadau, Majukwaa, Makongamano na Barua za Wasomaji, kwa njia nyingine zozote ambazo tulipata lakini baadhi ya marekebisho yanatokana na michango mahiri ya Waheshimiwa Wabunge, ambaa ndiyo wawakilishi wa watu.

Muswada huu umechangiwa na Wabunge wasiopungua 64, wengine kati yao wameuliza maswali na kutaka ufanuzi wa mambo waliyoyaona hayaeleweki, majina ya Wabunge hao yatatajwa na Mheshimiwa Waziri. Wengine wamezungumzia utaratibu ambaa wao wanafikiria ungefuatwa katika kushughulikia Muswada huu; wengine wametoa mapendekezo ya kuuboresha Muswada; na wengine wametoa tahadhari kwa maoni yao. Mambo yote hayo yanazungumzika, ingawa muda wa kufanya hivyo hautoshi.

Jambo moja kubwa lillojitokeza ni madaraka ya Rais ya kuwateua Wajumbe ya Kuratibu Maoni ya Wananchi na Mamlaka yake kutengeneza hadidu za rejea, yaani *terms of reference*.

Mheshimiwa Spika, lakini kabla sijarudia hapo ni vizuri tuangalie madai mengine ambayo yametolewa badala ya utaratibu huu tuliuopendekeza. Yametolewa mapendekezo kuhusu kuanzisha Baraza la Katiba, yaani *Constitutional Conference*, hoja hii inadai kwamba yangefanyika mabadiliko kwenye ibara ya 98 ya Katiba ili kuweka utaratibu wa kuundwa kwa Mabaraza ya Katiba, ambayo yangetoa maoni na mapendekezo katika Rasimu ya Katiba. Rasimu ya Katiba, iwasilishwe kwenye Bunge Maalum la Katiba na Wajumbe wa Baraza la Katiba watokane na Vyama vya Siasa, Asasi za Kiraia na Uwakilishi wa Makundi Mbalimbali ya Kijamii.

Mheshimiwa Spika, utaratibu unaopendekezwa ni moja ya njia zinazotumika katika kupata Katiba Mpya katika mazingira ambayo pengine yanatofautiana na mazingira tuliyonayo. Katika nchi nyingine, Wajumbe wa Baraza la Katiba wanatokana na masharti ya sheria. Kwa mfano, hapa kwetu Rais angeweza kuitumia Sheria ya Uchunguzi, yaani *Commission of Inquiries Act*, Sura ya 32 ya Sheria zetu, kama iliyofanyiwa masahihisho mwaka 2002. Baada ya kutafakari, sisi tumeona kwamba kwa Mwongozo wa Katiba yetu iliyopo na Vyombo vya Kikatiba vilivyopo kama vile Bunge, tunaweka utaratibu huu tunaopendekeza sasa katika Muswada ili utufikishe kwenye Katiba Mpya. Utaratibu unaopendekezwa ni mzuri kwa kuwa unatoa fursa zifuatazo kwa Tume:-

- (i) Unaiwezesha Tume kutumia Wataalam Elekezi katika kutafiti na kutoa ushauri wao; na

- (ii) Kupata maoni na ushauri wa Makundi Mbalimbali ya Jamii, kama vile Asasi za Kijamii, Asasi za Kidini, Vyama vya Siasa, Taasisi za Elimu za Juu, Vyama vya Wafanyakazi, Makundi yenyé Mahitaji Maalum, Vyama vya Wakulima, Vyama vya Wafugaji na Vikundi vingine vya Watu Waliojiunga Pamoja kwa malengo yanayofanana.

Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Makundi hayo, ndio yatakayokuwepo kwenye Rasimu ya Katiba. Baada ya kupata Rasimu ya Katiba, Tume itachapisha Rasimu ya Muswada kwenye Gazeti la Serikali na Magazeti ya Kawaida ili Wananchi waelewe maudhui yake. Baada ya hatua hiyo, Tume itaunda Mabaraza ya Katiba ili kupata maoni zaidi ya Wananchi. Utaratibu huu unatoa uwakilishi kwa uwazi zaidi, tofauti na chombo kinachopendekezwa na Mheshimiwa Tundu Antiphas Lissu, Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu masuala ya Katiba na Sheria na Mheshimiwa Moses Machali, ambaye pia alikuwa na mawazo kama hayo.

Mheshimiwa Lissu, anapendekeza *Constitutional Conference* ya kuteua Wajumbe wa Tume na Mheshimiwa Machali, anapendekeza *Multiparty Commission*. Hata hivyo, suala la nani hatimaye atawateua Wajumbe wa Tume haliwezi kuwa la Vyama vya Siasa kama iliyotokea Nchini Kenya kama alivyoshauri Mheshimiwa Tundu Lissu. Kwa sababu ya tofauti za itikadi, itakuwa vigumu kufikia mwafaka baina ya Tume ya aina hiyo, jambo ambalo linaweza kuleta vurugu na matusi katika mikutano hiyo. Tumejifunza na tusikubali kufanya makosa yaliyofanywa na jirani zetu kwa kuzingatia ukweli kwamba, tunaanzisha mchakato huu bila kushurutishwa; ni vyema tuchukue tahadhari ya kutosha. Wanasiasa watapata fursa kutoa maoni kupidia Mabaraza na Makundi ya Vyama vya Siasa, lakini pia watakuwa Wajumbe wa Bunge Maalum. Vilevile watashiriki katika kuwaelimisha Wananchi kuiwigia kura ya maoni Katiba inayopendekezwa. Kutokana na maelezo, hatukubaliani na mantiki kuhusu ama *Constitutional Conference* ya aina iliyopendekezwa na Mheshimiwa Tundu Lissu au *Multiparty Commission* kama alivyopendekeza Mheshimiwa Machali. (*Makofii*)

Kwa kuwa uzoefu umeonesha kwamba, makundi ya asili ya aina hiyo yanaweza kuteka nyara mchakato wa Katiba na kuugeuza kuwa suala la kisiasa, kikabila au undugu.

Baada ya maelezo hayo, ninaomba sasa nieleze ni kwa nini tumefanya madaraka ya Rais kuwa kama yaliyvo katika Sheria na ningependa kwenda kwenye fungu linalohusika.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba iliyopo, Rais ndio Mkuu wa Nchi, ibara ya 33 ya Katiba yetu ipo wazi. Kwa hiyo, Rais amepewa mamlaka ya kuwateua Wajumbe wa Tume ya Kuratibu Maoni ya Wananchi kama inavyoonyeshwa katika ibara ya tano, baada ya kushauriana na Rais wa Zanzibar. Ibara hiyo pia imefanyiwa marekebisho ya kuwaondoa Wanasheria Wakuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Zanzibar kama tulivyo kuwa tumeweka mwanzo.

Mheshimiwa Rais atamteua pia Mwenyekiti wa Tume hiyo pamoja na Makamu wake na Wajumbe wengine wa Tume hiyo. Rais amewekekwa masharti ya kufuata katika ibara ndogo ya tatu, kwa kuzingatia maoni ya watu wengine kwamba Rais asiwe na madaraka makubwa zaidi. Masharti aliywokeweka Rais yapo matatu na katika ibara ya tatu, ningependa kuyasoma nayo ili twende pamoja.

Katika kufanya uteuzi wa Wajumbe wa Tume, Rais atazingatia masuala ya uzoefu katika kufanya mapitio ya Katiba na sifa za kitaalam za Wajumbe kwenye mambo ya Katiba, Sheria, Utawala, Uchumi, Fedha na Sayansi ya Jamii. Mheshimiwa Rais amebanwa pia kuzingatia jiografia na mtawanyiko wa watu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, atazingatia pia umri, jinsia, uwakilishi wa makundi mbalimbali ya kijamii na pia masharti ya watu amba sheria inasema wasiteuliwe kuwa kwenye hiyo Tume.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais pia amepewa mamlaka katika Muswada wa awali kutengeneza hadidu za rejea. Kutokana na maoni ya Waheshimiwa Wabunge, pamoja na maoni ya watu wengine nje ya Bunge, hadidu za rejea zitakuwa ni sehemu ya sheria katika kifungu cha

tisa na kifungu cha 16. Tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, ambao wametoa maoni yao kuhusu jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi wa mabadiliko haya, ibara ya nane, inaeleza pia majukumu ya Tume kama ni kuratibu na kukusanya maoni ya Wananchi kuititia na kutafiti usahihi na ulinganifu wa masharti ya Kikatiba yanayohusu Mamlaka ya Wananchi, Mifumo ya Kisiasa, Demokrasia, Utawala na Sheria na Utawala Bora. Pia kutoa mapendekozo kwa kila hadidu ya rejea na kuandaa na kuwasilisha Ripoti. Ripoti itakayowasilishwa na Tume, itawasilishwa kwa Mheshimiwa Rais na Rais amepewa mamlaka tena ya kuitangaza katika Gazeti la Serikali kusudi Wananchi wafahamu kitu kilichopelekwa kwake. Baadaye Ripoti hiyo itapelekwa kwenye Bunge Maalum la Katiba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo pia limepigiwa kelele ni hizi hadidu za rejea, lakini kutokana na maoni tuliyoyapata kwa Waheshimiwa Wabunge, tumeridhika kwamba mabadiliko tuliyofanya yanakidhi haja na tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa hili.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo lilitaka kuleta tatizo kidogo ni maoni kwamba, hatua tulioitumia kuleta Muswada huu haitendi haki. Niseme wazi kwamba, Bunge hili linaendeshwa kwa msingi wa Kanuni za Bunge; na vilevile Waheshimiwa Wabunge tuna jukumu kubwa sana la kuheshimu Kanuni za Bunge pamoja na Katiba tuliyotumia kuapa Bungeni. Hoja hii iliibuliwa na Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwamba, Muswada huu ungesomwa mara ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, kama ulivyofafanua na kama Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge kama Mheshimiwa George Simbachawene na Mheshimiwa Andrew Chenge walivyofafanua, Muswada huu ulikwishesomwa mara ya kwanza. Bunge lako linaongozwa na Kanuni; na Kamati ya Kudumu ya Katiba, Sheria na Utawala Bora, iliyojua ikishughulikia Muswada huu, ilitoa taarifa ya kumaliza kuujadili Muswada huu kwa mujibu wa Kanuni ya 85(1).

Baada ya taarifa hiyo, Muswada huu ulipangwa katika shughuli za Bunge na kwa kufuata masharti ya Kanuni ya 86(2), Waziri aliuwasilisha Bungeni. Maneno ya kukejeli yaliyotolewa dhidi ya Spika kwamba alilingilia kazi ya Kamati yanaskitisha, kwani Kamati haikulalamika kuhusu jambo hili. Nilipokwenda kwenye Kamati niliwaona na kuwashuhudia Wajumbe wa Kamati wa CHADEMA walioshiriki vizuri katika mchakato huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninakubaliana kabisa na angalizo la Mheshimiwa Profesa Anna Kajumulo Tibaijuka wakati alipokuwa akichangia alisema, tuache *propaganda* kwani Muswada umeboreshwa. Inashangaza ni Muswada huu tu ndiyo unaodaiwa kusomwa mara ya kwanza mara mbili, Muswada wa Sheria ya Ununuzi wa Umma uliopitishwa Jumatatu tarehe 14 Novemba, 2011 ni wa mwaka jana, Muswada wa Sheria ya Gharama za Uchaguzi, yote ilichapishwa tena lakini suala la kurudia kuisoma kwa mara ya kwanza halikujitokeza.

Muswada kusomwa mara ya kwanza ni kitendo kinachoashiria kuanza kwa hatua za Kibunge za kujadili na kuitisha au kuukataa Muswada wa Sheria. Muswada ukipelekwa kwa Spika, basi Spika huupeleka kwenye Kamati; mantiki ni kwamba, marekebisho yanayotarajiwa katika Muswada yamefanyika. Wingi au uchache wa marekebisho haubadili Kanuni za 83, 84 na 85 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2007. Ninapenda kuchukua nafasi hii, kuwaarifu Watanzania wenzangu kwamba, wasipotoshwe na baadhi ya Wabunge kuhusiana na utaratibu huu wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nitalisemea kwa kifupi ni masahihisho ambayo tumeyafanya kutokana na maombi ya Waheshimiwa Wabunge. Kwanza ni Kamati iliposema kwamba, Wanasheria Wakuu wa Serikali wasitajwe, hilo tumeshaliondoa kwamba iwepo Ibara ya 20(4) kuainisha utaratibu wa kuitisha Bunge Maalum ikieleza muda na mahali ambapo Bunge hilo litakutana. Ushauri huu umezingatiwa kwenye Jedwali la Marekebisho, aya ya pili.

Kuhusiana na Rasimu ya Kanuni za Bunge Maalum zitayarishwe mapema; ushauri huo utazingatiwa kwamba, kwenye Ibara ya 24(3) hilo litazungumzwa na Mheshimiwa Waziri na pia Ibara ya 32(5) ileze kuwa Bunge Maalum linaweza kuitishwa tena ili kurekebisha masharti yaliyomo kwenye Katiba na hivyo kusaidia kuondoa masuala ya migogoro katika Katiba inayopendekezwa kwa lengo la kuirekebisha ili ipate kuhalishwa tena na Wananchi kupitia kura ya maoni. Utaratibu wa kurekebisha masharti ya Katiba utawekwa katika Katiba yenyewe na Wananchi watapata fursa ya kujadili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Ibara ya 34 kwamba, itamke toleo litakalozingatiwa iwapo kutakuwa na migongano kati ya toleo la Kiingereza na la Kiswahili la Muswada, maelezo ni kwamba, mwongozo wa jambo hili upo katika tafsiri ya Sheria ambayo inaeleza kwamba, Lugha Rasmi ya Sheria ni Kiswahili na Kiingereza na kwamba pakitokea mgongano kati ya matoleo hayo, basi toleo la Lugha ya Kiingereza litakuwa ndiyo mwongozo katika tafsiri Mahakamani na mahali pengine. Hata hivyo, Katiba haifungwi na mwongozo huo kwa kuwa iliandikwa kwa Lugha ya Kiswahili na baadaye kutafsiriwa kwa Lugha ya Kiingereza. Kwa hiyo, lugha inayotawala katika Katiba ni Lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, suala kwamba Mamlaka ya Rais ni makubwa nimeshaeleza kwamba, hiyo inatokana na ukweli kwamba, Rais ni Mkuu wa Nchi lakini vilevile Katiba ya sasa inatumika na masharti yako kwenye Katiba.

Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa Ismail Rage, Mheshimiwa Capt. John Komba, Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi na Mheshimiwa Sara Msafiri Ally, walitoa angalizo kwamba, Wanasheria Wakuu wasiwe katika nafasi za uundwaji wa Bunge na Bunge Maalum kwa kuwa Rais ndiye Mkuu wa Nchi basi wabaki kuwa washauri; hilo limezingatiwa vizuri sana.

Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, ameshauri kwamba, Ibara ya 32(3) ioneshe muda ambaa Tume za Uchaguzi zitaitisha uchaguzi mwingine baada ya kura ya maoni ya Katiba inayopendekezwa kuwa pana. Hoja hii imezingatiwa katika Jedwall, lakini ninapenda kutoa tahadhalii kwamba, kwa upande wa Zanzibar daftari litakalotumika ni Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na siyo Daftari la Wakazi. Kwa upande wa Tanzania Bara pia ni Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Mheshimiwa Felister Bura, ninamshukuru sana; amesema kwamba, Muswada ueleze jinsi Watanzania watakavyopiga kura kuridhia Katiba kwa mujibu wa kifungu cha 16(9) na tumesema kwamba, Ibara ya 16(9) inazungumzia kuhusu ushiriki wa Watanzania pekee katika Mabaraza na si suala la kupiga kura tu; utaratibu wa kuwatambua Watanzania hao utazingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za nchi zilizopo, ikiwa ni pamoja na Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Aidha, Mheshimiwa Bura amesema kwamba, haionekani kama Wajumbe wa Bunge Maalum wataapa. Hoja hiyo imezingatiwa na kuna marekebisho.

Mheshimiwa Moses Machali, ingawa hayupo hapa lakini alitoa maoni kwamba, Muswada ukisomwa mara ya pili ni kukiuka Ibara za 8 na 9; maelezo hayo nimeshayatolea ufanuzi.

Kuhusiana na mamlaka ya Rais, majibu ni hayo hayo na kuhusiana na Wabunge na Wanasiisa wasizuiwe kushiriki katika mchakato huo kwani wana taaluma, tukasema kwamba hapana Wabunge watashiriki kwenye hatua ya pili ya Bunge la Katiba.

Mheshimiwa Saidi Mohamed Mtanda na Mheshimiwa Zarina Shamte Madabida, wamezungumzia kuhusu adhabu; tumezingatia na sasa kuna Jedwali lenye masahihisho.

Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, ameuliza vigezo vilivyotumika kupata Wajumbe wa Bunge Maalum; kwenye Ibara ya 20(2) kifungu cha sheria hiyo kinaonesha watakavyopatikana.

Mheshimiwa Richard Ndassa na Mheshimiwa Agripina Zaituni Buyogera, wamesema kwamba, Muswada ungeitwa Sheria ya Kuunda Tume ya Mabadiliko ya Katiba. Kwa kweli suala hili

tulishalieleza kwa kirefu na tunashauri kwamba, jina libaki kama liliyo. Aidha, kuna ushauri uliotolewa kwamba, Wajumbe kutoka Taasisi za Elimu ya Vyuo Vikuu iechezwe kama ni Walimu au ni Wanafunzi. Majibu ni kwamba, Mjumbe anaweza kuwa ni Mwanafunzi au Mwalimu ilimradi anakidhi kigezo hicho, lakini izingatiwe pia kwamba, Wanafunzi wajue kwamba wapo shulenii kwa ajili ya kusoma.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mapendekezo ni kwamba, Ibara ya 14 inataka malipo ya Wajumbe wa Sekretarieti walipwe kwa kadiri Waziri atakavyoona, kama ambavyo Mheshimiwa Gosbert Blandes alishauri na kwamba tayari tumeshafanya marekebisho kwenye eneo hilo.

Jambo lingine ambalo amelisema ni kuhusu hadidu za rejea zikae kwenye *schedule* au kwenye Jedwali na sisi maoni yetu ni kwamba, zikae kwenye Sheria yenewe kama watu wengi wanavyopendekeza.

Mheshimiwa Andrew Chenge, ameulizia kifungu cha 16(8) na kifungu cha 18 havioneshi mtiririko wa jinsi Mabaraza hayo yatakavyofanya kazi. Ninapenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, hilo limeshughulikiwa kama utakavyoona kwenye Jedwali la Mabadiliko. Mambo mengine ni kutoka kwa Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, ambaye amesema kwamba, Wajumbe hawa ni wachache na anapendekeza wawe wengi. Tumefanya marekebisho na kuutilia maanani ushauri wake.

Mheshimiwa Spika, ushauri mwagine ni kutoka kwa Mheshimiwa Sara Msafiri Ally, ambaye anauliza kwamba ni nini msingi wa kupiga kura? Hili ni swali zuri kwa kila upande wa Muungano wakati nchi ni moja; ni kweli lakini sababu ni kulinda maslahi ya kila nchi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema marekebisho hayo, mengine tutayaona tutakapokwenda kifungu kwa kifungu; ninapenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia Muswada huu. Ninaunga mkono kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makof!*)

SPIKA: Ahsante sana na sasa nimwite mtoa hoja. (*Makof!*)

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, kwa mara nyininge tena, ninachukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa nafasi ya kufanya majumuisho ya mjadala huu kuhusu Muswada wa Mabadiliko ya Katiba wa Mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ambaa uliwasilishwa Jumatatu, tarehe 14 Novemba, 2011 umejadiliwa sana na Waheshimiwa Wabunge wengi, bila kujali itikadi za kisiasa na umewavutia Waheshimiwa Wabunge wengi. Huu ni ushahidi kwamba, suala la mapitio ya Katiba kwa lengo la kupata Katiba Mpya ni ajenda ambayo kila Mtanzania amekuwa akiisubiri kwa hamu ili kutoa maoni yake. Sina shaka kwamba, baada ya kukamilisha tarehe za kutunga Sheria inayopendekezwa, taratibu za kuunda Tume, Watanzania watashiriki kikamilifu katika mchakato wa kutoa maoni baada ya kuundwa kwa Tume.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, ninapenda kukushukuru wewe binafsi, kwa kazi nzuri ambayo umefanya ya kutupa miongozo mbalimbali mahali ambapo uliona tumekwama. Kwa kweli tunakushukuru sana.

Pia ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa kutoa hotuba nzuri kwa niaba ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, pia ninakushukuru sana kwa kuwajumuisha Wajumbe katika Kamati hii, kwa kweli wametupa msaada mkubwa sana katika kuuboresha Muswada huu. Ushahidi wa kazi hii nzuri ya Kamati ni Jedwali la Marekebisho kwa Lugha ya Kiingereza na Kiswahili. Mtakumbuka vilevile kwamba, kuchapishwa tena kwa Muswada kilitokana na ushauri wa Kamati ambayo illiratibu Vikao vya Wadau Mjini Dodoma, Jiji Dar es Salaam na Mjini Zanzibar. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, wenzangu upande wa pili wa Muungano ameshawashukuru Mheshimiwa *Attorney General*, tumefanya kazi kwa pamoja na tumeshirikiana vizuri kuanzia mwanzo hadi mwisho.

Mheshimiwa Spika, sasa ninaomba nichukue nafasi hii, niwataje Wabunge waliochangia kwa maandishi na waliochangia kwa kuzungumza. Waliochangia kwa kuzungumza ni wafuatao:-

Mheshimiwa Pindi Chana, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Tundu Lissu, Waziri Kivuli wa Wizara ya Katiba na Sheria na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Anne Malecela, Mheshimiwa Dkt. Augustino Mrema, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Christopher Olonyokie Ole-Sendeka, Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mheshimiwa Moses Joseph Machali, Mheshimiwa Ismail Aden Rage, Mheshimiwa Felister Aloyce Bura, Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu, Mheshimiwa Angellah Kairuki, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Capt. John Komba, Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Mheshimiwa Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka, Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mheshimiwa Eng. Hamad Yussuf Masauni, Mheshimiwa Mussa Haji Kombo na Mheshimiwa Betty Eliezer Machangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Subira Khamis Mgusu, Mheshimiwa Dkt. Seif Seleman Rashidi, Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mheshimiwa Agripina Zaituni Buyogera, Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar, Mheshimiwa Mwigulu Mcchemba, Mheshimiwa Saidi Mohamed Mtanda, Mheshimiwa Andrew John Chenge, Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya, Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mheshimiwa Assumper Nshunju Mshama, Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Sara Msafiri Ally, Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, Mheshimiwa Mohamed Hamisi Missanga, Mheshimiwa Dkt. William Augustao Mgimwa, Mheshimiwa Eugen Elishininga Mwaiposa, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Mussa Zungu Azzan, Mheshimiwa Abdulkarim Esmail Hassan Shah, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde, Mheshimiwa Benardetha Kasabago Mushashu, Mheshimiwa Anna Margaret Abdallah, Mheshimiwa Mchungaji Luckson Ndaga Mwanjale, Mheshimiwa Jaddy Simai Jaddy, Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mheshimiwa Clara Diana Mwatuka, Mheshimiwa Sylvester Massele Mabumba na Mheshimiwa Zahra Ali Hamad. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hao ndio waliochangia kwa kuzungumza, lakini ninaomba niwatambue pia waliochangia kwa maandishi nao ni Mheshimiwa Catherine Valentine Magige, Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi, Mheshimiwa Zarina Shamte Madabida, Mheshimiwa Abia Muhamma Nyabakari, Mheshimiwa Mohamed Hamisi Missanga, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa Pereira Ame Silima, Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar, Mheshimiwa William Augustao Mgimwa na Mheshimiwa Benedict Ngalamu Ole-Nangoro, Mheshimiwa Athumani Rashid Mfutakamba, Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee, Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mheshimiwa Dkt. Maua Abeid Daftari, Mheshimiwa Faith Mohamed Mitambo, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mheshimiwa Rosweeter Faustin Kasikila, Mheshimiwa Abdul Rajab Mteketa, Mheshimiwa Kaika Saning'o Telele, Mheshimiwa Dkt. Christina Gabriel Ishengoma na Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Aina Mohamed Mwidau, Mheshimiwa Vita Rashid Mfaume Kawawa, Mheshimiwa Saidi Ramadhani Bwanamdogo, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla, Mheshimiwa Shaffin Ahmedali Sumar, Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji, Mheshimiwa Al-Shaymaa John Kwegyir, Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa, Mheshimiwa Ramadhani Haji Saleh, Mheshimiwa Abdallah Sharia Ameir, Mheshimiwa Innocent Kalogeris,

Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Neema Mgaya Hamid, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mheshimiwa Waride Bakari Jabu, Mheshimiwa Clara Diana Mwatuka, Mheshimiwa Brig. Gen. Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Stephen Ngonyani, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Deo Filikunjombe, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah na Mheshimiwa Modestus Kilufi.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Jasson Rweikiza, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Salome Mwambu, Mheshimiwa Sylvester Mabumba, Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mheshimiwa Amos Makalla, Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, Mheshimiwa Agness Hokororo, Mheshimiwa Haroub Muhammed Shamis, Mheshimiwa Aliko Kibona, Mheshimiwa Said Mussa Zubeir, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sita, Mheshimiwa Deogratias Ntukamazina, Mheshimiwa Nyambari C. M. Nyangwine, Mheshimiwa Shawana Bukheti Hassan, Mheshimiwa Dkt. Fenella Mukangara, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Mariam Nasoro Kisangi na Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi.

SPIKA: Muda huo hatuuhesabu, tunaanza kuhesabu sasa dakika hamsini.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, pia ninapenda kuwashukuru wadau mbalimbali ambao wametoa maoni ya kuuboresha Muswada huu.

Ninaomba niwatambue kama ifuatavyo: *Tanzania Centre for Democratic*, kwa barua yao ya tarehe 2 Juni, 2011 iliyosainiwa na Mheshimiwa Ibrahim Lipumba; maoni yao mengi yamezingatiwa. Chama cha Majaji Wastaafu, maoni yao yamezingatiwa kwa kiasi kikubwa. Jukwaa la Katiba wametoa maoni yao kwa maandishi, mengi yamezingatiwa.

Wananchi mmoja mmoja kupitia vipindi mbalimbali, maoni mengi yamezingatiwa. *Tanganyika Law Society*, maoni yao kwa ujumla yamezingatiwa. Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani, baadhi yamezingatiwa na wanazuoni wote walilotusaidia kwa njia moja au yingine katika kuuboresha Muswada huu, angalieni kwenye *Schedule of Amendments*.

Idadi kubwa ya Waheshimiwa Wabunge walichangia hoja hii na wadau mbalimballi. Kama nilivyosema ni ushahidi wa kutosha kwamba, Muswada huu umepata maoni mengi na ushahidi ni *Schedule of Amendment* ya kwanza na ya pili.

Kama nilivyosema awali, mjadala umevuka mipaka ya itikadi za vyama vya siasa. Vyama karibu vyote vilivyo na Wabunge ndani ya Bunge hili, ambavyo ni Chama cha Mapinduzi(CCM), Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Chama cha Wananchi CUF, Chama cha NCCR – Mageuzi na Chama cha TLP, vimeshiriki kujadili na kuuboresha Muswada huu. (*Makof*)

Kwa ujumla, michango ya Wabunge wengi ilikuwa ni kuipongeza Serikali kwa kuwasilisha Muswada huu ambao utaongoza katika safari ya kupata Katiba Mpya. Michango mingi ilirejea vifungu mbalimbali ambavyo tayari Serikali ilikuwa imeshavifanyia kazi kutokana na ushauri wao, hasa wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Pia kama alivyooleza Mwanasheria Mkuu, michango mingi ilikuwa na lengo la kuboresha.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na nyongeza ambazo zimetolewa na Wabunge mbalimbali kutoka kwa Mheshimiwa Zarina Madabida, Mheshimiwa Godfrey Zambia, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa Mohammed Habib Mnyaa, Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, Mheshimiwa Mussa Hassan Zungu, Mheshimiwa Jasson Rweikiza na Mheshimiwa Ali Khamis Seif; wameleta Jedwali la Nyongeza ambalo Waheshimiwa Wabunge wamegawiwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya jumla, ninapenda kutoa maelezo mahususi yaliyojadiliwa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nianze moja kwa moja kwa kujikita katika maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani. Kwa kuwa wameleta maoni yao kimaandishi na walisema yanukuliwe kwenye

Hansard, wajibu wangu ni kuyajibu na kuyatolea ufanuzi, kwa sababu aliyejatoa ni Waziri Kivuli wa Katiba na Sheria, ambaye yuko kwenye Kambi Rasmi ya Upinzani.

Mambo mahususi ambayo aliyejatoa ni kama ifuatavyo: Muswada huu ni mpya una tofauti kubwa ya kimsingi na Muswada wa zamani.

Mheshimiwa Spika, maudhui na muundo wa Muswada huu havina tofauti yoyote na Muswada wa mwanzo kama inavyodaiwa na Kambi Rasmi ya Upinzani. (*Makofî*)

Hebu tuyaaangalie maudhui ya Muswada huu na kama mna Muswada wa zamani angalieni kama kuna kuna tofauti yoyote. Maudhui hayo ni:-

- (a) kuunda Tume ya Mabadiliko ya Katiba Mpya ili iratibu na kukusanya maoni ya Wananchi juu ya Katiba;
- (b) Kuainisha na kuchambua maoni ya Wananchi;
- (c) kuainisha masharti kuhusu Mabaraza ya kuhalalisha masharti yaliyomo katika Rasimu ya Katiba;
- (d) kuweka masharti ya utayarishaji na uwasilishaji wa ripoti kuhusu maoni ya Wananchi;
- (e) kuweka utaratibu wa kuunda Bunge Maalum (Bunge la Katiba); na
- (f) kuweka masharti ya uendeshaji wa Kura ya Maoni.

Hivyo, ukiyaangalia maudhui kwa ujumla hayajabadilika.

Mheshimiwa Spika, aidha, Muswada huu una sehemu tano pamoja na majedwali. Maudhui na Muundo wa Muswada wa mwanzo viliboreshwa zaidi kutokana na maoni ya Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, pamoja na wadau niliowataja.

Waheshimiwa Wabunge wenzangu mmeupitia kwa undani na kwa umakini Muswada huu; je, ni kipengele gani kikubwa ambacho kimeubadilisha huo Muswada kuwa ni mpya?

Wabunge wenzangu, angalieni katika kichwa cha habari kirefu, angalieni ibara ya nne ya Maudhui na sehemu nyingine zote, tuone ni sehemu gani ambayo ilikuwa na mabadiliko makubwa. Kwa hiyo, kwa ujumla maudhui hayajabadilika katika Muswada huu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, la pili, mapendekezo ya Muswada kuhusu uteuzi wa Wajumbe, Watendaji na Watumishi wengine wa Tume, yana lengo la kuhakikisha kwamba, matokeo ya kazi ya Tume ni yale yale yanayotakiwa na Rais na Serikali yake na Chama chake. Hayo yalikuwa ni maoni mimi nayaita ya Waziri mwenzangu wa Katiba na Sheria.

Hoja hii haina msingi wowote. Uteuzi wa Wajumbe, Watendaji na Watumishi wengine wa Tume unafanywa kwa kuzingatia Katiba iliyopo sasa na Sheria za nchi. Hatujakwenda nje ya Katiba, hatujakwenda nje ya Sheria za Nchi. Mfumo wa Serikali tulionao, unampa madaraka Rais ya kuwa Kiongozi wa Serikali, Mkuu wa Nchi na Amiri Jeshi. Aidha, kwa kuwa Rais amechaguliwa na Wananchi wengi, anao uhalali wa kusimamia mchakato huu kwa kuteua Tume. (*Makofî*)

Izingatiwe hapa kwamba, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mojawapo ya mambo ya Muungano. Kwa mujibu wa Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, mamlaka yote ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano juu ya mambo ya Muungano yamo mikononi mwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofî*)

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, kwa namna yoyote ile hakuna namna ambayo mchakato wa kutunga Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, itamuweka pembedi Rais ambaye ni Mkuu wa Nchi. Kwa namna yoyote ile, mamlaka ya Rais yaliyomo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano, hayawezi kuondolewa kwa sheria ya kawaida kama hiyo ninayoiwasilisha Bungeni.

Mheshimiwa Spika, suala la badala ya Tume hiyo kuwa Tume ya Rais iwe Tume ya Vyama; Mwanasheria Mkuu amelieleza vizuri, kwa ufasaha na utaalami. Mimi ninalieleza kisiasa ninasema kwamba; hivi Tume hii ikiwa Tume ya Wanasiwa wa Vyama mbalimbali wenyewe Sera mbalimbali kweli tutaunda Katiba au itakuwa vurugu? (*Makof!*)

Wakati wa uchaguzi wote tulikuwa na Ilani za Vyama mbalimbali; Chama cha Mapinduzi ilani yao, CUF ilani yao, CHADEMA ilani yao, kila mtu ana malengo yake. Sasa uwaweke kwenye chungu kimoja uwaambie hao ndiyo waunde Tume! Ninafikiri matokeo yake mtayaona, hayatakuwa mazuri, hayatatupeleka tunapotaka kwenda. (*Makof!*)

Lingine amesema Tume ya Vyama itakuwa na uhalali wa kisiasa (*political legitimacy*) kubwa zaidi ya Tume ile ya Rais. Ninasema hoja hii haina msingi; Rais amechaguliwa na Wananchi na inabidi tumuamini. Ninamshukuru sana dada yangu, Mheshimiwa Clara Mwatuka, yeye anasema kwamba, jamani Rais tulyemchagua ni Jakaya Mrisho Kikwete, lazima tumheshimu na lazima tukubaliane naye. Tena amesema vizuri; "Mimi nilikuwa na Rais wangu wakati wa uchaguzi Mheshimiwa Lipumba aligombea, ameshindwa tumekubali yaishe sasa Rais ni huyu mmoja." Sasa kwa wale wasiomtambua ndiyo wanaoleta uchonganishi wa aina hiyo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Ibara ya 10 ya Muswada huu kuhusu uhuru wa Tume hayatoshelezi hata kidogo. Haya ni maoni na kwamba, Wajumbe wapewe ulinzi wa ajira zao na wapatiwe ulinzi kama walivyo Majaji wa Mahakama ya Tanzania ili kuzuia uwezekano wa Wajumbe kuondolewa kwa sababu zisizotokana na utendaji wao wa kitaalam au ukosefu wa maadili.

Ninasema mchakato huu ni wa muda, Tume hii ni ya muda siyo ya kudumu, kwa hiyo, lazima tutaendana na masharti ya kazi za muda na siyo za kudumu. Rais anawateua Wajumbe hao na akishawateua tumemuwekea vigezo vyta kuangalia. Kwa hiyo, hoja ya kusema kwamba, wawekewe ulinzi kama walivyo Majaji, wapewe ajira ya kudumu; hilo hatukubaliani nalo.

Mheshimiwa Spika, pia suala la Mamlaka ya Rais, nina-quote: "Mfumo wetu wa Kikatiba umejengwa juu ya nguzo kuu ya Urais wa Kifalme, kwa vile Rais katika mfumo huu ana mamlaka makubwa."

Waheshimiwa Wabunge, kwanza, ninawashukuru sana mmelisema hili kwa uzuri kabisa. Nikirudia nitakuwa nimeharibu, kwa sababu maoni yenu mliyoyatoa mmeulewesha Umma wa Tanzania kwamba, Urais wetu sisi siyo wa Kifalme; upo kwenye Katiba na kwenye Ibara ya 40(2) inasema wazi vipindi vyta Rais ni viwili.

Sasa huo Ufalme labda wenzetu wana kitabu kingine wanachokitumia, lakini kwa msomi wa Tanzania kusema nchi hii tunatawaliwa Kifalme, watoto tunaowazaa sasa hivi ikiwaingia akilini tunawapotosha vyta kutosha. Kwa hiyo, siyo vyema kuiptotosha jamii hasa ya vijana, kwa sababu sisi tunatumia Katiba na tunaiheshimu.

Wabunge wote pamoja na Wabunge wa Kambi Rasmi ya Upinzani, wameapa kwa kutumia Katiba iliyopo sasa hivi na si vinginevyo. Tumeapa hapa mbele ya Spika kwamba, tutaiheshimu na tutailinda. Sasa unataka uanze kuchakachua! Wanaochakachua hiyo Katiba wakati wake bado. Twende kwenye Katiba iliyopo, tufuate yaliyomo, baadaye huko tunakokwenda ndiko tutakakoichambua Katiba kwamba, aah, sasa tunataka Utawala wa Kifalme, sijui wa Kisultani, sijui wa Kiukoo. Maoni haya hayatatorewa na kichwa kimoja, yatatolewa na Watanzania wote. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, katika Bunge liliopita, nilitahadharisha; wenzangu waliona kama nilimshambulia Mheshimiwa Tundu Lissu; nilitahadharisha Kambi Rasmi ya Upinzani wawe wanapitia Rasimu au Maoni anayoyatao Waziri Kivuli wa Katiba na Sheria, yanaonekana kama ni maoni yake. Sidhani kama Wabunge wenyewe busara wa Kambi ya Upinzani wamepitia vizuri hiyo hotuba. Wangeipitia sidhani kama wale Wabunge wa Zanzibar wangekubali Zanzibar itukanwe, ina maana hawakushirikishwa. (*Makof*)

Mheshimiwa spika, pia alisema kwamba, Muswada huu unaendeleza kivuli kirefu cha Urais wa Kifalme katika mchakato wa upatikanaji wa Katiba. Sisi tunasema kwamba, aah, labda mwenzetu ana ajenda nyingine; lakini Mtanzania yeote kwa sasa, kwa elimu mliyoitoa Wabunge, anajua kabisa nchi hii haiendeshwi Kifalme na huu Muswada haujkwenda kinyume cha Katiba na pia haujkwenda kinyume na Kanuni za Bunge. Kwa hiyo, hicho kivuli cha Urais wa Kifalme mmekieleza vizuri na nisingependa tuendeleze mjadala kama huu.

Lingine, anasema kwamba, watakaoteuliwa na Rais kuunda Tume watakuwa tishio kwa *status quo* kwamba, watakuwa *royal* kwa Rais. Jamani; hivi *procedures* zote hizi tunazosimema kwamba, Rais anaunda Tume, Tume inakwenda kwa Wananchi kukusanya maoni, yaktoka kule yanarudi, wanaandikwa vizuri, baada ya kuandika wanarudi kwenye Mabaraza kuwaliza jamani hayo ndiyo mliyopendelekeza wanasesma ndiyo; tunapitia kwenye Bunge Maalum, tunapitia kwenye *referendum*; jamani *procedures* zote hizi tuna wasiwasiani? (*Makof*)

Muswada huu ninaona umetupa mamlaka makubwa sana na tumwombe Mwenyezi Mungu, hatua zote hizi ambazo tumezidhamiria kwa dhati kabisa, ziwe *transparent* na kuaminiana. Kuaminiana ndiyo kuwe zaidi. Muamini mwenzio kwa sababu usipomuamini na yeze hatakuamini.

Tukiishi maisha ya kutokuaminiana ina maana kwamba, Rais sasa hivi akichagua Mawaziri hamuwaamini, RCs hamtawaamini, sijui akina nani hamtawaamini; ninaomba tuishi maisha ya kuaminiana.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo amelizungumzia ni kwamba, Wateule wa Rais watapa shinikizo kutoka kwa Rais na Chama chake. Jamani nimewaeleza hiyo *procedure* itakuwa *transparent* na tunapitia katika hatua mbalimbali; kwa hiyo, hakuna namna yoyote ambayo huyo Rais atawenza kubadilisha maoni ya Wananchi, kwa sababu Katiba ni Wananchi na siyo Rais peke yake.

Mamlaka ya uteuzi wa Tume yaondolewe kutoka mikononi mwa Rais; hili nimeshalizungumza. Lingine, wamesema kwa kuzingatia marekebisho ya Ibara ya 9 ya Muswada, hajulikani Rais atatoa maelekezo gani kwa Tume au kule kutokuaminiana. Ninasema kwamba, *transparent* ni kubwa sana katika Muswada huu.

Kuhusu hadidu za rejea, Mheshimiwa mwenzangu kama angehudhuria Vikao vya Kamati ya Bunge, yote haya angeyapata. Mimi ninawaeleza ukweli Watanzania kwamba, tulipouwasilisha Muswada kwa mara ya pili kule Dar es Salaam mwezi Juni, Mheshimiwa Tundu Lissu, alikuwa Tarime. Wakati tuko kwenye vikao hapa Dodoma kuanzia siku ya kwanza, nina *attendance* ya Wabunge kwa sababu nilhudhuria mle, haku-*attend* hata kikao kimoja. Kwa hiyo, mawazo mengi na *schedule of amendment* ambayo Serikali tulishaifanyia kazi bado ameyaingiza kwenye *speech* yake. Kwa hiyo, unaona kabisa kwamba, ushiriki wake ni mdogo sana. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, ninasikitika sana labda Mawaziri wenzangu, Mawaziri wao Vivuli wanawasaidia; mimi Waziri Kivuli wangu kama hahudhuria vikao ananaisaidiaje kutoa mawazo? Kwa hiyo, kusema kweli mambo mengi ambayo ameyasema, kama angehudhuria vikao nina uhakika kwamba angeweza kuyapata na kuchangia vya kutosha, kwa sababu kwenye ile Kamati CHADEMA walikuwepo; Mheshimiwa Halima Mdee ametoa mawazo mazuri na mengi yamezingatiwa; Mheshimiwa Akunaay ametoa mawazo mazuri na mengi yamezingatiwa na mashahidi akina Mheshimiwa Hamad Rashid, Mheshimiwa Chenge, tulikuwa katika *dialogue* nzuri sana ndiyo maana tulikuballiana mambo mengi sana.

Mheshimiwa Spika, sitaki kuingilia sana kuhusu uwakilishi wa Zanzibar; jamani siyo jambo la busara; katika Bunge liliopita la Bajeti nilisema watu wengine ni wachochezo, yaani kila kitu ni

kuchochea chochea tu ili watu wagombane. Sasa ya Zanzibar sijui Rais amefanyaje; ana madaraka makubwa, ana kura ya turufu; kwa nini tuwe sawa? Ameeleza vizuri Mheshimiwa Mwanasheria Mkoo wa Serikali kuhusu masuala ya Muungano. Watu warudi kwenye *Articles of Union*, wasome vizuri; na Waheshimiwa Wabunge ninaomba msome vizuri ili unapochangia uonekane na wewe umechangia umesoma hicho kitu na ume-pursue vizuri. Maana unawenza ukasoma uka-pursue unavyojuu wewe. Jamani tuangalie vizuri, tusome hatua kwa hatua ili tusiwapotoshe na tusiwachonganishe Watanzania. Sasa hivi unawachonganisha Tanzania Zanzibar na Tanzania Bara; hivi unawaachanisha namna gani?

Mheshimiwa Spika, Wapemba wamejaa Dar es Salaam, Wasukuma wamejaa Zanzibar; hivi unawatenganisha namna gani? Kwa uchochezi huu, ninaomba Tanzania Zanzibar na Bara tusikubali mawazo ya mtu mmoja. Kwa ujumla yale ya Zanzibar nilishasema kwenye kikao kilichopita kwamba ni uchonganishi na kwa kuwa yamerudiwarudiwa ninazidi kusema kwamba ni uchonganishi na siyo mzuri na ninahisi kwamba ni mawazo ya mtu mmoja na siyo mawazo ya wengi, ndio maana ninawaasa Wabunge wenzangu wale wa Zanzibar wa CHADEMA, wangeweza hata kupitia tu ile Rasimu ili waone yale matukano; je, wao wanayakubali na kama hawayakubali wasingetoka Bungeni wangekuwa na Wazanzibari wenzao kwamba jamani kwa hayo matukano bora hata Ubunge wenyewe uende huko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mengi ameshajibu Mwanasheria Mkoo wa Serikali. Kuhusu hilo la hadidu za rejea kama nilivyosema na tumeshalingiza kwenye Sheria, Ibara ya 9 na 16, kwa hiyo, hilo ni zuri. Hapa unaona kabisa kwamba, walisema Rais tulimpa madaraka makubwa, lakini tumekaa na Kamati tunesikiliza maoni ya Wadau mbalimbali tukasema aah hili kwa nini tusiliweke kwenye Sheria. Kwa hiyo, tumeliweka kwenye Sheria, maoni ya wadau ina maana yamezingatiwa vilivyo.

Mheshimiwa Pindi Chana, kwa niaba ya Kamati alisema tuongeze baadhi ya makundi kama vile Wafanyakazi, Wakulima na kadhalika. Hilo Waheshimiwa tumelizingatia, lakini hatukuandika makundi yote kwenye Muswada huu kwa sababu siyo rahisi kuyamaliza makundi yote. Kwa hiyo, tulichofanya sisi kama Serikali, tukasema kutokana na maelezo yenu mmepanua wigo wa wawakilishi, kwa hiyo na sisi kama Serikali tumeamua kuongeza idadi ya Wajumbe ili ikidhi yale mahitaji ya makundi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Margaret Mkanga amechangia sana hilo, kwa upande wa Vijana kulikuwa wakereketwa akina Mheshimiwa Mama Bura, Mheshimiwa Amina Makilagi, wakereketwa wa Vijana, Wanawake na Wazee. Kwa hiyo, tukasema hatuwezi tukayaandika makundi yote, ila tulichofanya tumeongeza idadi ili kukidhi makundi hayo. Kwa hiyo, ushauri wa Kamati na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge tumeuchukua kama uliyyo. Kuhusu Kanuni za Bunge Maalum zitayarishwe mapema, Rasimu itatayarishwa mapema, lakini watakaopitisha hiyo Rasimu kuwa Kanuni za Bunge Maalum watakuwa ni Bunge Maalum wenyewe.

Mheshimiwa Spika, mengi yameshajibiwa na Mheshimiwa Anne Kilango, yaani alitutahdarisha tukasema jamani mjadala huu uwe wa amani na utulivu na Wabunge wengi tu wamechangia, samahani siwezi kuwataja wote kwamba kweli mchakato huu inabidi tuwe wavumilifu. Sisi wenzeni tumekuwa wavumilifu, mimi na Mwanasheria Mkoo wa Serikali kila siku tuko kwenye *front page*. Mimi pamoja na Spika kila siku tuko katika ukurasa wa mbele tunavumilia na tunaomba Watanzania tuvumiliane badala ya kutukanana, tujenge hoja tusitukanane, hatuna utamaduni huo. Kwa hiyo, kwa hilo ninasema kwamba, ametu-caution na baadhi ya watu kwenye vyombo vya habari wametu-caution sana, kama jana nilimwona mse maji mmoja kwenye *ITV* sijui anaitwa Humphrey Polepole, ameeleza vizuri jinsi Muswada huu ulivyo kuwa. Kwa hiyo, unaona kabisa kwamba, kuna watu wanaouelewa ila kuna watu hawataki kuuelewa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Betty Machangu na Mheshimiwa Mama Anne Kilango Malecela wamesema, Wanasiasa hawajazuwa kuwa Wajumbe wa Tume; sisi tumetaja *specific group* ya Wanasiasa, hakuna kipengele chochote kwenye Ibara ya 6 tuliposema kwamba, Wanasiasa hapana. Sisi tumetaja Makundi Maalum na Wanasiasa siyo Wabunge tu, siyo Wawakilishi tu na siyo Vlongozi wa Vyama vya Siasa tu, sisi tumetaja hilo kundi, lakini Wanasiasa hatukumkataza kabisa Rais kwamba hakuna Wanasiasa ye yote kuingia kwenye Tume.

Zitatumika busara tu kama kuna Mwanasiasa ambaye hayuko kwenye hayo makundi tuliyoyataja, kama tunamwona kwamba atatusaidia tutam-*accommodate*, Rais na Rais wa Zanzibar watatumia busara zao. Kwa hiyo, Wanasiasa hawajakatazwa kwenye Tume bali tunesema kwamba, makundi haya kama sisi Waheshimiwa Wabunge tutashiriki kule mbele sasa kwenye Bunge Maalum, tutakuwepo, tutatoa rai zetu na tutayaweka mambo vizuri, kwa hiyo, hili ninaomba Wananchi walielewe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kupotoshwa kwa Muswada, limechangiwa na Wabunge wengi; alianza Mheshimiwa Mrema, wakaja Mheshimiwa Mnyaa, Mheshimiwa Ummu Mwalimu, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Ester Bulaya, Mheshimiwa Zarina Madabida, Mheshimiwa Simbachawene na Mheshimiwa Chenge, akaeleza kwa undani kabisa kwamba jamani eeh ametusaidia sana. Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana ulivyowaingiza kwenye Kamati Mheshimiwa Chenge na Mheshimiwa Hamad Rashid na Mheshimiwa Kafulila na Mheshimiwa Ole-Sendeka, walitoa mchango mkubwa. Wametusaidia sana, Wanakamati ni mashahidi, ilikuwa tunabishana kwa hoja hatuendi kiholela. Mimi, Spika kwa hilo hata anayepiga dongo akupige tu, lakini Mwenyezi Mungu anajua nini ulichofanya katika kuurekebisha na kuuweka vizuri Muswada huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala lingine ingawa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali alijibu baadhi ya masuala ya Mheshimiwa Hamad Rashid, lakini moja alisema Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, ilipitia Muswada kwa kina kiasi cha kupunguza madaraka ya Rais kwa kuingiza hizo *terms of reference* ziwe sehemu ya Ripoti; jamani kweli walikuwa *serious*. Kwenye Kamati tulikuwa *serious* na tulikaa Serikali na Kamati vizuri na mengi yamezingatiwa na ndiyo hayo ambayo yameboresha Muswada. Mheshimiwa Hamad Rashid akatupa elimu kidogo kuhusu Muungano, nami nimekubaliana naye kwamba ametusaidia kwa kiasi kikubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Hamad Rashid naye akatu-*caution* akasema, tunatakiwa kujenga hali ya kuaminiana na kuheshimiana ili Taifa letu liendelee vizuri. Ushauri huu ni mzuri na tusipojenga misingi ya kuaminiana hatutafika mbali. Kwamba, yule ni mbaya akishatajwa Rais mtu ana *allergy*, akishatajwa Rais wa Zanzibar basi tena mtu roho inamuumma mpaka; sasa mnataka tuwe Marais wangapi, Rais ni mmoja tu. Rais wa Zanzibar na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nao wamechaguliwa na Watanzania, lazima tujenge uaminifu kwao. Sasa unaposema kwamba hao hawaaminiwi sijui na nini; ni mazingira ya kutoaminiana na tukianza na mazingira ya kutoaminiana hatutafika mbali.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mnyaa ye ye alisema kuwe na ratiba maalum ya kupatikana kwa Katiba Mpya itamkwe kuwa Uchaguzi wa Mwaka 2015 utafanywa kwa Katiba Mpya. Sisi tumejipangia, yaani tuna *road map* ambayo tumejipangia; sasa siyo vyema na siyo busara kuingiza kwenye Muswada huu, kwa sababu huwezi ukajua kwamba ukiweka kwenye Sheria hivi pengine muda fulani, mambo fulani yanatakiwa kurudishwa, kupelekwa kwa Wananchi na pengine muda wa kukusanya maoni ya Wananchi hautoshi, kwa hiyo, tunaomba mtuachie hapa ili tuweze kuendelea na kazi zetu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ismail Aden Rage, ye ye alisema wanaokataa Muswada wanatafuta nafasi ya kufanya vurugu. Watanzania wawe na imani na Wabunge wao na Rais wao ambao walimchagua wenye. Ninakubaliana na Mheshimiwa Rage kwamba, tujenge imani kwa sababu ni sisi wenye tuliyemchagua.

Mheshimiwa Felister Bura alisema tuongeze makundi hasa kundi la wafugaji, tumekubaliana naye. Mheshimiwa Felister Bura na Mheshimiwa Amina Makilagi kama nilivyowataja wakereketwa wa Wanawake, wamesema jinsia izingatiwe; hilo tunasema busara hizo zitatumika.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Felister Bura alitoa angalizo kwamba, Muswada haujaonesha kama Wajumbe wa Bunge Maalum wataapa. Tumesema hilo limezingatiwa kwenye *Schedule of Amendment*.

Mheshimiwa Moses Joseph Machali anasema Muswada Kusomwa kwa Mara ya Pili siyo halali. Mwanasheria Mkoo wa Serikali ameshalijibu vizuri sana. Suala lingine Mheshimiwa Machali amesema Wabunge na Wanasiasa wasizuiwe, hilo ninafikiri nimelitolea ufanuzi kwamba ni kundi tu la Wanasiasa ambalo tumeona kwamba kwa kuwa hii ni *fulltime job*, siyo vyema tukawaingiza katika Tume ili wafanye kazi zao na kama nilivyosema, kila mtu ana itikadi yake, sasa tukisema hiyo Tume iwe ya Wanasiasa itakuwa vurugu kweli maana kila mtu ana malengo yake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la Mheshimiwa Profesa Anna Tibajuka, amelijibu vizuri Mwanasheria Mkoo wa Serikali kwamba sasa hivi siyo wakati wa *propaganda*, sasa hivi ni wakati mzuri wa kupitisha huo Muswada na wawakilishi wapo ndani ya Bunge wamewasilisha kama ilivyo Miswada mingine. Kwa hiyo, ushiriki wa Wananchi watashiriki hapo baadaye, kazi ni kwetu Waheshimiwa Wabunge. Baada ya Muswada huu kupita, beba Muswada wako rudi kwenye Jimbo ukawaeleze Wananchi kwamba, jamani Muswada huu ulikuwa hivi ili wale wapotoshaji ambao watazunguka pengine na wao wakute wewe Mbunge tayari kwenye Jimbo lako umeshawaeleza Wananchi wako. Jamani tutumie vyombo vya habari viliyoko Majimboni kwetu; kwa mfano, kule Ulanga nina Radio Ulanga, Nachingwea kule wana Radio Nachingwea, kwenye Halmashauri nydingi sasa hivi kuna vyombo vya habari; kwa hiyo ni vyema tukatumia vyombo vya habari kueleza ukweli ulivyo kwa sababu siyo Watanzania wengi ambao wana televisheni walituangalia wakati tunachangia Muswada huu. Kwa hiyo ni vyema tukaenda sisi kueleza ni nini ambacho kimetokea katika Bunge hili na Muswada huu una maana gani.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kombo yeye amesema mchakato ushirikishe pande zote mbili za Muungano; ni kweli umezingatia na kwa kuwa tulikuwa naye kwenye Kamati, ametoa mawazo mazuri sana. Mheshimiwa Kapteni John Komba yeye amesema, Wazanzibari 116 kwenye Bunge Maalum wasiwe chini ya theluthi moja. Hilo tumelizingatia vizuri tu ndiyo hao ambao wana nia nzuri ya Muungano.

Mheshimiwa Simbachawene amesema, Wananchi watashirikishwa vizuri katika mchakato wa kupata Katiba Mpya. Hilo ni sawa, ndiyo hatua ambayo tutaifikia hapo baadaye.

Mheshimiwa Mama Zarina Madabida amesema Serikali itoe elimu kwa Wananchi ili kuelewa vizuri Sheria na Tume itakayokusanya maoni. Kama nilivyosema; tukitoka hapa na Muswada wetu twende tukatoe elimu na sisi upande wa Serikali tutajitahidi kutoa elimu zaidi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Betty Machangu alitupa angalizo kwamba, kuwe na angalizo kwa Wananchi watakaopewa elimu ya uraia ili wasipotoshwe. Hili ni angalizo zuri sana kwamba, kuna wengine kazi yao *by profession* wao ni wapotoshaji; kwa hiyo, angalizo hilo tumeliona na tumeliangalia katika Sheria hii. Kuhusu kigezo gani kilitumika kupata Wajumbe 116; hili lilelezwa vizuri sana na Waziri mwenzangu wa Katiba na Sheria wa Zanzibar. Alieleza vizuri tu akasema Zanzibar kuna Majimbo 50 na Tanzania Bara kuna Majimbo 239. Sasa amesema huo usawa tunaousema ni usawa wa uwakilishi na siyo usawa wa nusu kwa nusu, ndiyo maana ukipiga mahesabu vizuri utaona kwamba, Bara lazima tutazidi kwa namba kwa sababu tuna Majimbo mengi zaidi. Huo ndiyo uwakilishi ambao sisi tumeuongelea.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Andrew Chenge ametufafanulia mambo mengi, jamani yeye ni Mwanasheria, ametupa maangalizo mengi na mengi tumeyazingatia katika Jedwali la Pili. Tulitoa Muswada na Jedwali la Kwanza na Jedwali la Pili tumelitoa hivi karibuni. Kwa hiyo, tunaposoma Jedwali la Kwanza lile tulitolitoa pamoja na Muswada, tuangalie na Jedwali la Pili ambalo pia mmetoa maoni yenu na sisi wengine tumeyazingatia.

Mheshimiwa Mkono yeye aliuliza Watanzania walioko nje ya nchi watafikiriwaje katika mchakato wa kupata maoni ya Katiba. Wao watatoa maoni yao kutoka huko nje, lakini maoni hayo lazima yaingie kwenye Tume na siyo vinginevyo. Kwa hiyo, hawatatengwa wasitoe maoni yao, lakini maoni lazima waya-channel kwenye Tume. Pia ameuliza fedha za kutembelea nchi nzima kukusanya maoni ya Wananchi waishio Tanzania zitatoka wapi?

Jamani! Maadam tumeshaamua kwamba hili ni jambo la Kitaifa, fedha zitatoka kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na tumeiweka vizuri kwenye Jedwali la 14(1).

Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, ye ye alisema, kwa kweli Wajumbe wa Bunge Maalum ni wachache. Ndiyo maana tumeongeza idadi ya Wajumbe kwa kuzingatia maoni ya Waheshimiwa Wabunge, akina Mheshimiwa Laizer, wale walio taja makundi maalum akina Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Angella Kairuki anasema jamani msiache wafanyakazi na wa Elimu ya Juu. Kwa hiyo, tumeongeza namba ili kukidhi matakwa ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Laizer anasema kule kwa wafugaji msije mkakosa kufika, hapana. Tume itafika kila mahali ndiyo maana *roadmap* yetu tumewawekea kipindi kirefu sana ili waweze kukusanya maoni ya wananchi, sio yanayowakilishwa. Tunataka ya wananchi wenyewe na si kikundi cha watu kinasema hayo ndiyo mawazo ya wananchi, hapana. Tutawafikia kule kijiji ili watueleze maoni yao sio kakikundi kamoja tu kanakuja hapa kanasema hayo ndiyo maoni ya wananchi, hapana Tume haitakubali. Tutapokea mawazo ya vikundi mbalimbali lakini kule kwa mwananchi mmojammoja Tume itafika na kufanya mikutano na wananchi ili kuwaelimisha kwanza na pili kupata maoni yao. Kwa hiyo, tunaonya kabisa vile vikundi ambavyo vinakusanya maoni kwamba hayo ndiyo maoni ya wananchi, sio Mwakilishi popote, sio Mbunge, maana afadhalii Mbunge anasema kwamba nawakilisha Jimbo la Ulanga Mashariki, sasa mwiningine anasema haya ni maoni ya wananchi wakati ni mawazo yake ye ye binafsi. Kwa hiyo, lazima tutahadharishe sana.

Mheshimiwa Spika, maoni kwa kweli yalikuwa ni mengi na tumeyaweka kwenye mafungu na wale Wabunge ambao hatukuwataja, *issues* zao zinafananafanana na maoni ya wengine, kwa hiyo, ikiwa bahati mbaya umetoa maoni yako lakini hayakuwa *considered* katika *schedule of amendment*, kwa kweli uchukulie kwamba tumechukua maoni yako, tumeyathamini na tumeyaelewa.

Mheshimiwa Spika, kuna Mheshimiwa mmoja nimekosea jina lake ni Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, sasa unajua tena mimi ni Mpogoro, kwa hiyo, si rahisi kuyatamka maneno yote vizuri kutokana na uasilia wenyewe kila mtu na lugha yake.

Mheshimiwa Spika, nachukua tena nafasi hii, kwa kweli nakushukuru sana kwa kuundesha mchakato huu vizuri na Watanzania niwaambie kwamba isinge kwa Spika kuwa imara Serikali tungeyumba, Kamati inge yumba na tulikuwa tuna *m-consult* kwamba hivi hapa tunakwendaje? Anasema nendeni hivi na kweli mkienda mnaona mnafanikiwa. Kwa hiyo, Muswada huu umepitia katika *stage* zote, Kanuni za Bunge zime fuatwa vizuri na Mheshimiwa umetusaidia kwa kiasi kikubwa mpaka hapa tulipofika. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge ushahidi tosha kwamba Muswada huu maoni ya wananchi yameingizwa vilivyo, uko kwenye *Schedule of Amendment* ya kwanza na *Schedule of Amendment* ya Pili.

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru wewe, Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kweli alitufanya kazi ya ziada, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Rais mwenyewe, kwa kweli kulikuwa na *consultation* za hali ya juu na za umakini na kwa kweli katika mchakato huu wa mwanzo tumeshirkiana vizuri sana na pande zote mbili za Muungano. Ushahidi upo hapa Bungeni, tupo na Waziri wa Katiba na Sheria wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na yupo hapa wiki nzima, watendaji wake tuko nao hapa wiki mbili. Wiki yote ile ambayo tulikuwa kwenye Kamati, Katibu Mkuu kwa Wizara ya Katiba na Sheria alikuwepo, Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Zanzibar alikuwepo, kwa hiyo, tulikuwa na timu nzuri ambayo tuliweza kusaidiana ndiyo maana unakuta kwenye Kamati hatukuwa na matatizo. Nyie wa Bara kama swali limewashinda wenzeni Zanzibar wanajibu. Tulikuwa timu moja. Kwa hiyo, mimi naomba tuendeleze *sprit* hiyo ili tuweze kwenda vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, nawashukuru Wabunge wote kwa kunisikiliza na natambua sana mawazo ya wote ni mazuri, hii kazi mliyoifanya ni muhimu na ndiyo maana na mimi mnaona ninaongea kwa ku jiamini kwa sababu tumefanya kazi hii vizuri na Mheshimiwa Pindi Chana na Kamati yake, Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Uongozi wote wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja illitolewa iamuliwe*)
(*Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pilli*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Sasa napenda niwatambue walioko kwenye *Speaker's Gallery* nilikuwa sina majina yao. Ni Mheshimiwa Abubakary, Waziri wa Katiba na Sheria Zanzibar, yupo Ndugu Hassan Rashid, Katibu Mkuu, Waziri ya Katiba na Sheria Zanzibar, yupo Ndugu Said H. Said, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ahsanteni na karibuni sana.

Nitatumia Kanuni ya 28(2) ikifika saa saba tuongeze kama nusu saa kusudi tuweze kumaliza kazi tuliyonayo na tukitoka hapa tuna mgeni, Makamu wa Rais yupo pale nje kwa ajili ya uzinduzi wa *TAPAC*. Kwa hiyo, tunaendelea Katibu.

KAMATI YA BUNGE ZIMA

Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa Mwaka 2011 (*The Constitutional Review Act 2011*)

Ibara ya 1

MHE. JASSON S. RWEIKIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeondoa kusudio langu la kufanya marekebisho. (*Makofi*)

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 2

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 3

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 4

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekubaliana na marekebisho niliyoyafanya. Ahsante.

MHE. JASSON S. RWEIKIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nami nimeondoa kusudio langu la marekebisho katika Ibara hii. (*Makofi*)

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 5

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii ilikuwa na maneno yale yanayotaka Majaji wa sehemu zote wawe sehemu ya kumshauri Mheshimiwa Rais wakati wa kuunda Tume lakini nimekubaliana na mapendekezo hayo kwa hiyo sina sababu ya kuendelea.

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 6

MWENYEKITI: Unajua tunawaita kama walivyoleta. Kwa hiyo aliywahi kwanza ni Mheshimiwa Zambi.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 6 inahusu uteuzi wa Makamishna kwenye Tume ambayo itakwenda kuratibu zoezi la kura za maoni. Sasa ukisoma Muswada unasema kwamba kuna msingi wa idadi sawa kwa Wajumbe lakini ukienda kwenye kipengele cha (b) kinasema katika uteuzi huo Mamlaka ya Uteuzi atazingatia Jiografia pamoja na mtawanyiko wa watu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa nataka Serikali itoe maelezo hapa, unaposema msingi wa usawa halafu unakuja kusema kwamba atazingatia Jiografia na mtawanyiko wa watu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania maana yake nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nilikuwa nimetoa mapendekezo yangu ili kutoa kile ambacho nimeona kama mkanganyiko kwamba: "(2) subject to subsection (3), the Commission shall be comprised of such number of members from either part of the United Republic as may be appropriate for the effective performance of the functions and exercise of powers of the Commission." Sasa kama Serikali inakubaliana sawa. Kama haikubaliani basi naomba maelezo yale niliyoomba pale mwanzoni.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mheshimiwa Zambi kwa kuonyesha na kufanya kazi ya Mbunge na anatufanya tunasimama kila wakati. Shabaha ya kuweka Wajumbe sawa katika ile Ibara ya 6(2) ni kuzingatia hali yetu ya Muungano kwanza, kwa sababu hiyo ni *substantive condition*. Ile ya (b) nitasoma kwa kingereza; "the President shall have regard to geographical and the population diversity of the United Republic of Tanzania. Maana yake ni kwamba Mheshimiwa Rais atazingatia jiografia ya nchi yetu na mtawanyiko wa watu kwa maana ya kwamba tuna watu tofauti na wa kila hali. Kwa hiyo, atakapokuwa anachagua Wajumbe wa Tume azingatie hilo. Ahsante sana.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba niseme mimi ni mmoja wa watu ambao tunaheshimu Muungano uliopo. Naomba nitamke hilo na wenzangu Wabunge wanielewe hivyo. Lakini katika busara ya kawaida nadhani kwa baadaye na kwa sababu tuna chombo ambacho kinashughulikia Kero za Muungano basi kingeangalia na eneo hili. Tunapoteua watu katika vyombo vya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania basi wakazingatie hata Kanuni ya uwiano wa watu kati ya Tanzania Bara pamoja na Tanzania Zanzibar. Ahsante.

MHE. ZARINA S. MADABIDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Serikali imezingatia mapendekezo niliyyoyatoa na wameyafanya kazi. Nashukuru.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru imekuwa *covered* na Mheshimiwa Zambi.

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 7

MHE. ENG. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho ambayo nilihitaji kufanya katika Ibara ya 7, ni kwamba ile *sub-clause* (2) ifutwe na *sub-clause* (3) iwe ndiyo *sub-clause* (2) na iongezwe *clause* nyingine mpya ambayo inasema kwamba: "(3) the Chairman and the Vice Chairman of the Commission shall be elected by Members of the Commission from amongst themselves on the basis of the principle that where the Chairman hails from one part of the United Republic, the Vice Chairman shall be a person who hails from the other part of the United Republic" Nilifanya hivi kwa sababu ya kwamba hii Tume tayari imeshachaguliwa na Rais kwa ushirikiano na Rais wa Zanzibar na ni watu ambao wanajulikana, wana uzoefu. Sasa wenyewe wajichague Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti kwa kutegemea ushauri huo. Ahsante.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali tuliliangalia hilo lakini tukajiuliza watu mmeteuliwa leo, kesho mmchague Mwenyekiti, je, mtafahamiana? Halafu pili, kazi ya Uenyejekiti ni ngumu. Mkumbuke kwamba huko mbele Mwenyekiti huyo atakuwa na kazi

ya ziada ya kuwasilisha Muswada na kufanya mambo mengine. Kwa hiyo, anatakiwa mtu ambaye ni *competent*, mwenye uzoefu wa muda mrefu na ambaye anaweza aka-manage kuiongoza vizuri Tume hiyo. Ni kwa nia nzuri tu.

MHE. ENG. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu maelezo ya Mheshimiwa Waziri lakini nilifanya hivi kwa kuelewa kwamba Tume hii kwanza ni ya watu wenye sifa maalum kubwa na heshima kubwa Tanzania na wenye elimu ya kutosha. Sasa kwa vile wameshachaguliwa na Marais, wao wenyeewe wanajijua uzoefu wao. Kwa hiyo, ili kuondosha ile kwamba kila kitu Rais sasa hawa watakuwa wamejichagua wenyeewe na ingekuwa na nguvu fulani.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa juu maneno haya yanaweza yakawa na mantiki.

MWENYEKITI: Kwa juujuu, sio kwa juu tu.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Kwa juujuu, lakini hili jambo ni jambo kubwa sana na tuamini kwamba yale madaraka ambayo anayo Rais kwa mujibu wa Ibara ya 33 ya Katiba na dhamana ya Rais kama Mkuu wa Nchi, mimi napendekeza kwamba kifungu hicho kibaki kama kilivyo kwa sababu Mheshimiwa Rais ana njia zake nzuri zaidi za kuwapata hao watu na anawafahamu Watanzania karibu wote akitaka.

MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na wazo hilo. (*Makofii*)

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 8
Ibara ya 9

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 10
Ibara ya 11

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 12

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 13

MHE. DKT. WILLIAM A. MGIMWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo mazuri ya Mheshimiwa Waziri pamoja na Mwanasheria Mkuu, naondoa kusudio langu la *ku-move schedule of amendment*. (*Makofii*)

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia, niliomba Waziri anipe maelezo kwenye Ibara ya 13(3) kuhusu Katibu wa Tume kwamba lazima awe Mwanasheria. Moja ya sababu ambazo nilisema mimi nilidhani sio vizuri kumfunga Mheshimiwa Rais kwamba Katibu wa Tume hii awe Mwanasheria. Mimi naamini uongozi ni pamoja na uzoefu, lakini tunahitaji mtu ambaye anajua historia ya nchi yetu, ana uelewa halisi wa hali ya siasa ya nchi yetu, ana uelewa wa mfumo wa kijamii wa nchi yetu, anaelewa elimu ya mchakato wa kuunda Katiba lakini pia ana elimu ya utafiti wa maoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kuamini kwamba wanaoweza haya yote ni Wanasheria peke yao. Nilikuwa nadhani ni muhimu tubadilishe Ibara hii ili tumwachie Rais uwanja mpana,

aamue nani wa kuteua, siyo lazima awe Mwanasheria. Lakini kwenye Sekretarieti kuwepo na Wanasheria wa kutosha kadri watakavyoona inafaa, lakini siyo kwa Katibu wa Tume. (*Makofi*)

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati fulani mambo haya yanaonekana kama ni ya kujipendelea lakini uzoefu wetu ndiyo unaotufanya tuweke sharti hilo la kutaja *profession* ya Uanasheria. Kwa sababu gani, kwa sababu mambo haya, ni mambo ya Katiba na Sheria na itakuwa rahisi zaidi na kwa ufanisi zaidi kama Katibu atakuwa ni Mwanasheria na kwenye Sekretarieti, tunathamini sana *profession* za watu wengine, tunathamini sana. Kwa hiyo, kwenye Sekretarieti pia kutakuwa *profession* nyingine, lakini Katibu, tulikuwa tunashauri kwamba ibakie kama ilivyo hivyo. Tunafanya hivyo kwa sababu ya uzoefu tulionao.

MWENYEKITI: Mheshimiwa, wewe hukutoa hoja, kwa hiyo sikupi nafasi ya pili.

(*Ibara iliyojajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 14

MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekubaliana na maelezo yaliyotolewa na Serikali kuhusu Waziri.

(*Ibara iliyojajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara Mpya ya 15

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri hii Tume kutokana na kazi zake itakuwa na gharama kubwa. Sasa, sikuona katika Muswada kuwa limo suala zima la ukaguzi wa fedha ambazo watazitumia. Kwa hiyo, nimependekeza tupate Ibara mpya ya 15 ambayo itakuwa na sehemu mbili; sehemu ya kwanza ni kumtaka Katibu atayariske taarifa za fedha ndani ya miezi mitatu baada ya kumalizika mwaka wa fedha lakini sehemu ya pili; nikapendekeza kuwa hesabu hizo aziwasilishe kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, huo ndiyo msingi wa kusema Ibara hiyo iongezwe. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mwanasheria Mkuu au nani, lengo la kuongeza Ibara nyingine!

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Ali Khamis Seif. Tunakubaliana na pendeleko lake kwa heshima kabisa. Tutaweka Ibara hiyo, haitaitwa Ibara ya 15, bali tunaomba iwe Ibara ya 16. Hiyo, tutafanya kwenye uandishi, lakini tunaikubali kama ilivyo bila mabadiliko. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Kwa hiyo, katika uchapishaji wa baadaye itakuwa Ibara ya 16, kwa sasa hivi tutaendelea na namba hizi, lakini wata-*reallocate numbers* hizi, kwa sasa ni Ibara ya 16, Ibara ya 17 ndiyo itakuwa Ibara ya 16 sasa lakini tukubali kwamba hicho kitakaa nafasi ya 16. Kwa hiyo, *re-numbering* itafanyika.

(*Ibara Mpya iliyojajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya Awali ya 15

(*Ibara iliyojajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 16

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna marekebisho ambayo nadhani yatafafanuliwa vizuri kisheria na Mwanasheria Mkuu kuhusu Ibara hii ilivyoandikwa, *interpretation* yake, kwa sababu 16(a) inataka *amendment* inayoonyesha kwamba Waheshimiwa Wabunge na viongozi wana uhuru wa kutoa elimu ya uraia kuhusu

mchakato wa Katiba. Kwa hiyo, ni *amendment* ambayo nadhani *Attorney General* ndiye anaweza akai-move vizuri kisheria lakini, kuna *amendment* inatakiwa hapa.

MWENYEKITI: AG, tusaidie sisi ambao hatukuwa pamoja na ninyi.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba twende kwenye *further schedule of amendment*. Hii anayosema Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ni *amendment*, nafikiri ni ukurasa wa 3 pale ambayo inasema kwamba, *actually inazungumzia Ibara ya 19*. Sasa hatujafika huko nafikiri Waziri ungesubiri tufikie Ibara ya 19.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Sawa!

MWENYEKITI: Kuna Ibara mpya ya 16A kwenye *amendment* ya Serikali!

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 17

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 18

MHE. JASSON S. RWEKIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na maelezo ya Mheshimiwa Waziri na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo, naondoa hoja yangu. (*Makofii*)

MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi pia naafikiana na mapendekezo kwa sababu yale niliyokuwa nayahitaji yamezingatiwa, naondoa mapendekezo yangu. (*Makofii*)

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Ibara ya 18 kama tulivyofanya marekebisho kwenye *further schedule of amendment*, ukurasa wa 2, eneo la (G), kile kifungu cha (4) ambacho kinasomeka "...for the purpose of subsection (3), the Chairman of the Commission shall not be a member of the Constituent Assembly and shall retire from the Constituent Assembly after presentation of the Draft Constitution"

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunapendekeza kufanya marekebisho ili Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Tume wabaki kwenye ukumbi wa *Constituent Assembly* kwa ajili ya kutoa ufanuzi inapobidi. Kwa ajili hiyo, tunaomba sasa kifungu hicho kisomeke kama ifuatavyo:-

"For the purpose of subsection (3), the Chairman and members of the Commission may give clarifications which may be necessary during deliberations or during debates by the Constituent Assembly".

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kurudia kwa ruhusa yako!

MWENYEKITI: Rudia! Uende pole pole kidogo!

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Inasema:-

"For the purpose of subsection (3), the Chairman and members of the Commission may give clarifications which may be necessary during the debate by the Constituent Assembly".

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Kwa hiyo, tuna-amend kifungu cha 18(4) kama kilivyoletwa kama *amendment*.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hii *further schedule of amendment* ya Serikali, hiyo hiyo Ibara ya 18 (4)...

MWENYEKITI: Kama kilivyokuwa *re-amended*.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Kama ilivyoandikwa hapa.

MWENYEKITI: Kama kilivyokuwa *re-amended* aliyosoma hapa?

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Ndiyo!

MWENYEKITI: Kama ilivyoikuwa *re-amended*!

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Ndiyo!

MWENYEKITI: Haya!

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Sasa, huku chini najaribu kusoma hapa kifungu kidogo kinasema kwamba, "For the purposes of subsection (3), the Chairman of the Commission shall not be a member of the Constituent Assembly..."

MWENYEKITI: Hiyo imekuwa *amended*, hiyo imefutwa!

MHE. GEORGE S. SIMBACHAWENE: Imefutwa hii?

MWENYEKITI: Imefutwa, ndijo haya aliyokuwa anasoma hapa. Inasema:-

"For the purpose of subsection (3), the Chairman and members of the Commission may give clarifications which may be necessary during the debate by the Constituent Assembly". Hiyo ndijo *amendment* mpya inaondoa hii.

MHE. DKT. WILLIAM A. MGIMWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nina wazo tofauti kidogo. Kwa sababu, tukisema "For the purpose of subsection hiyo, the Chairman and members of Commission may give clarification which may be necessary...". Sasa mimi nafikiri iwe "which may be required" kwa sababu *necessary we may not be able to determine whether this is necessary*. Kwa hiyo, hali halisi itakuwa "when it is required".

MWENYEKITI: Haya, Kiingereza tu!

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: *We have no problem with that amendment!*

MWENYEKITI: Sasa, badala ya *necessary iwe required*. Haya!

(Ibara iliyo tajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 19

MHE. ZARINA S. MADABIDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ibara hii ilikuwa inazungumzia kuhusu makosa na adhabu ambayo ilikuwa inahusu Tume na Sekretarieti, lakini mwananchi hawi *covered* lakini naona Serikali imekubaliana na mapendekezo hayo na wamekiboresha vizuri sana. Kwa hiyo, nakubaliana nao.

MHE. ANDREW J. CHENG: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona. Nilitegemea kwamba AG ange-pickup kile ambacho Mheshimiwa Prof. Tibajuka alipaswa kukisema mwanzoni kuhusiana na Ibara ya 19(2) (a) inayosema: "any person who- (a) carries on an activity of coordinating and collecting public opinions;" Sasa, ukiachia hivyo, unawenza ukawafunga wengi tu. Sasa, tunataka tu ufute ile semi-colon baada ya *opinions*, useme *contrary to this Act commits an offence*, zishabihiane na (b) na (c). Kwa hiyo narudia:- "Any person who-

(a) carries on an activity of coordinating and collecting public opinions contrary to this Act, commits an offence". Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofii*)

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, namshukuru sana Mheshimiwa Andrew John Chenge, Mbunge wa Bariadi Magharibi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa zamani kwa mabadiliko haya aliyosema na mimi sina matatizo nayo. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Kwa hiyo, tunaongeza tu kwenye kifungu cha 2(a) tu.

MHE. SAIDI M. MTANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Mheshimiwa Chenge amenifilisi, isipokuwa wakati wa mchango wangu nilizungumzia juu ya adhabu kali ambayo imewekwa katika kifungu hiki cha 19 kwamba "...isipungue mwaka mmoja kwa yule mtu ambaye atakuwa ametenda makosa haya au faini isiyozidi milioni tano". Nilombwa Serikali iliangalie hili vizuri, lakini sasa hivi wameleta marekebisho yanayosema, faini kuanzia milioni tano hadi milioni 15 au jela miaka mitatu. Sasa nilitaka njue kwa nini Serikali hajakubaliana na mawazo yetu na badala yake imeongeza adhabu kali zaidi?

MWENYEKITI: Sasa wewe ulikuwa unazungumza tu, uliyozungumza siyo *amendment*. Maelezo Mheshimiwa!

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliyapa uzito mkubwa sana maoni ya Mheshimiwa Mbunge, lakini kwa kuzingatia pia hii tabia ambayo sasa inaonekana kama, Wamasai wanasema inaenea kama "*lomonii*". *Lomonii* ni moto wa porini ambaa wakati fulani usipoangalia unaweza kuunguza nyumba nyingi sana na pia ni njia ya kusalimiana kwa Wamasai kwamba ukimkuta njiani na mwingine anamwambia mpaka wa mwisho anajua kuna matatizo gani katika jamii. Kwa hiyo, matatizo haya tuliyonayo sasa ambayo yanababishwa na watu ambaa hawataki kufuata utaratibu katika mambo ya siasa, inatakiwa kutoa elimu ya kisiasa katika jambo hili la Katiba kwamba wapewe adhabu kali, ndio maana yake. (*Makofii*)

(*Ibara iliyo tajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 20

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho niliyoyafanya, Serikali ilishayafanya tayari. Kwa hiyo, nakubaliana nayo. (*Makofii*)

MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara hii nilitaka kuwepo na wigo mpana zaidi wa uwakilishi lakini, naona suala hilo limezingatiwa na Serikali na mimi naondoa hoja yangu. (*Makofii*)

MHE. MUSSA Z. AZZAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi hiki, kulikuwa hakuna muda wa kuanzisha Bunge la Katiba. Serikali imekubali, nimeridhika.

MHE. JASSON S. RWEKIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nilikuwa napendekeza kufuta Bunge Maalum la Katiba, lakini baada ya kupata maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mheshimiwa Waziri, nimeridhika na maelezo yao. Kwa hiyo, naondoa hoja yangu. (*Makofii*)

(*Ibara iliyo tajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 21

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara hiyo, Serikali imeleta mabadiliko kwamba kuna matumizi ya neno "Mwenyekiti", lakini kwa *version* ya Kiingereza yanatumika kama *Chairman and Vice Chairman*. Nilikuwa napendekeza kwamba yatumike maneno *Chairperson and Vice Chairperson*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siyo Mwanasheria. Naomba Serikali ieleteze kwa nini mnataka kutumia maneno *Chairman* na *Vice Chairman* ukizingatia kwamba yeyote, awe mwanamke au mwanaume anaweza kuwa Mwenyekiti? (Makof)

MWENYEKITI: Haya, afadhalii! Mheshimiwa AG!

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, iko sera ya matumizi ya uandishi wa sheria ambayo inazuia matumizi ya maneno ambayo yana-*genderize* kwamba uwe *gender sensitive*. Kwa hiyo, *Chairperson* ni sawasawa. Lakini kwa mujibu wa Sheria yetu, Sura ya Kwanza ya Tafsiri ya Sheria zetu, unapotumia neno *person* ambayo ni *masculine*, linamaanisha pia kwamba ni *feminine*, kwa hiyo, ndiyo Sheria inasema hivyo lakini Sera yetu ya Sheria ndivyo ilivyo lakini tunawaita hivyo. Kama unachukua neno *chairman*, hata kwenye *chairperson* kuna *son* kule mwisho. Kwa hiyo, siyo hoja, ni kwamba Sheria ina-regulate jambo hilo.

MWENYEKITI: Sheria bado siyo *gender sensitive*, Mheshimiwa Zambi.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru AG kwa tafsiri yake, lakini neno letu la Kiswahili Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti hayana ubaguzi kabisa, hivi kwa nini tunang'ang'ania maneno ya Kiingereza ambayo yanaonesha ubaguzi, kwa nini Serikali isitafute maneno ambayo hayataonesha ubaguzi katika matumizi hata kama Sheria ndivyo inavyosema? (Makof)

MWENYEKITI: Naona kwenye Kiswahili si ndiyo tumesema Mwenyekiti na Makamu na *amendment* ya Muswada huu ndiyo unasema hivyo. Hilo neno tulishabishana miaka yote ikabakia kisheria *the Chairman includes female and male*.

(Ibara iliyotajwa hapo Juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge zima pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 22

MHE. ESTHER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupata maelezo ya kina kutoka Serikalini nimeamua ni-withdraw.

(Ibara iliyotajwa hapo Juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge zima Pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 23

(Ibara iliyotajwa hapo Juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara Mpya ya 24

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza Ibara ya 24 inayohusiana na mambo ya gharama za mchakato huu wa kupata Katiba, 24(1) inasema kuwa gharama hizi za Tume zitoke katika Mfuko Mkuu wa Serikali, lakini 24(2) kuwa Wajumbe wa Tume na Katibu pamoja na Wafanyakazi wao mishahara yao pamoja na marupurupu mengine mwamuzi awe Rais kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kwa mara nyininge kumshukuru Mheshimiwa Ali Khamis Seif, kwamba ile Ibara sasa, kwanza tunakubali kwamba kuwe na Ibara ambayo itasomeka Ibara ya 24 inayohusika na *expense of the Constituent Assembly* na tunakubali mapendekezo yake yote bila kuondoa hata neno moja. (Makof)

(Ibara mpya iliyotajwa hapo Juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya Awali ya 24

MWENYEKITI: Sasa Ibara hizi zote zitakuwa *renumbered* lakini sasa tutatumia namba zilizopo kwa hizi *reference*.

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 24 ukiangalia marekebisho ya Serikali wamekubali kusahihisha Ibara ndogo ya (1) na kuiondoa Ibara ndogo ya (2) lakini wao wanabakiza Ibara ndogo ya (3) kuipandisha iwe ndiyo Ibara ndogo ya (2).

Mimi rai na pendelezo langu ni kwamba, Ibara nzima ya 24 ifutwe na kuandika upya Ibara ndogo ya (1) kwa maana kwamba, ninachopendekeza ni kuondoa ile ya (3) ambayo inapandishwa kuwa ya (2) inayosema, *the provision of the Constitution Bill shall require passing by the Constituent Assembly on the basis of support of two third majority of total number of members hailing from mainland Tanzania and two third majority of the total number of members hailing from Tanzania Zanzibar*. Nilichokuwa naona, sina tatizo sana la theluthi mbili kwenye Bunge Maalum, tatizo langu ni kwamba Bunge hilo Maalum kama marekebisho ya Serikali yalivyoletwa hapa, yanasema Bunge Maalum litatunga Kanuni kwa ajili ya kuendesha shughuli zake na hilo nakubaliana nalo. Nikawa nafikiri kwamba sisi tukiwa Bunge la Jamhuri ya Muungano kuwawekea sharti hili la namna ya kuendesha shughuli zao, nilikuwa napendekeza hili liende kwenye Bunge Maalum la Jamhuri ya Muungano katika uundaji wa Kanuni zake ili wenyeve wakajivekee Kanuni zao. Nilikuwa nataka kuishauri Serikali kama inaweza ikakubaliana na mimi katika pendelezo hili.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumshukuru sana Mheshimiwa Ole Sendeka kwa maoni yake. Ni kweli kwamba katika hali ya kawaida ingekuwa hivyo lakini hili suala la *two third* ni suala zito kwa msingi kwamba Kiswahili sijui nini, lakini ni *substantive provision* ya Sheria na Katiba na kama ndivyo huwezi kuipeleka kwenye Kanuni. Kwa hiyo, tukafikiri kwamba pengine ni vizuri itamkwe kwenye Sheria kwa sababu msingi wake ni lazima utoke kwenye Sheria na haiwezi kuwa chini ya Sheria ukaweka kwenye Kanuni. Kwa hiyo, maeleo yetu ni hayo tu na tunaomba utuunge mkono kwamba ibaki kama ilivyo.

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Mwenyekiti pamoja na ukweli kwamba Bunge Maalum la Katiba litakuwa juu ya Katiba ya sasa, linafanya kazi kwa niaba ya Watanzania, lakini kwa kuwa ni rai ya Serikali yangu kwamba pengine hili lishughulikiwe hapa badala ya kwenda kushughulikiwa na Bunge Maalum, basi naomba nikubaliane na *Attorney General (Makofî)*

(*Ibara iliyotajwa hapo Juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara Mpya ya 25

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo haya ni yaleyale ambayo nimeyapendekeza katika Ibara ya 15 kuwa Karani aweke mahesabu ya matumizi miezi mitatu baada ya kumalizika mwaka wa fedha. Vilevile kuwe na ukaguzi wa fedha hizo au matumizi hayo amba unatafanywa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo, hayo ndiyo marekebisho ambayo ninayataka.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kukubali yale ya Kifungu cha 24 inafuatia pia kwamba haya aliyoyapendekeza tunayakubali. (*Makofî*)

(*Ibara mpya iliyotajwa hapo Juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya Awali ya 25

Ibara ya 26

(*Ibara zilizotajwa hapo Juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara 27

MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Katika Ibara ya 27 nilitoa pendelezo kwamba badala ya Tume ya Uchaguzi Tanzania Bara na Zanzibar

kusimamia zoezi hili, kwa sababu tupo katika mchakato maalum wa kuandaa Katiba Mpya, nilipendekeza kwamba iundwe Tume Maalum ambayo itasimamia na kuratibu zoezi zima la kura za maoni.

MWENYEKITI: Umependekeza, hujatoa sababu gani unatofautiana na hii iliyopo hapa.

MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE: Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu kwamba zoezi hili ni kubwa na la msingi ili kuondoa dhana ambayo imo miongoni mwa baadhi ya watu kwa kusema kwamba Tume hizi za Uchaguzi Bara na Zanzibar haziko huru, basi tuunde Tume Maalum ambayo itasimamia zoezi hili mahsusi.

MWENYEKITI: Kwa hiyo, uhuru utakuwepo, haya Mwanasheria Mkoo wa Serikali.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba nimewahi kusikia watu wanasema Tume hizi zilizopo siyo huru, lakini katika hukumu nilizosoma zote ambazo zinatolewa baada ya Uchaguzi Mkoo sijawahi kupata mahali ambapo Mahakama Kuu au Mahakama ya Rufaa imesema kwamba Tume ilifanya mambo ambayo yanaonesha kwamba haiko huru. Kwa hiyo, hii ni *perception* ambayo kwa kweli haina msingi wa Sheria wala Kikatiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tunalo Daftari la Kudumu la Wapigakura ambalo linasimamiwa na Tume zetu za uchaguzi, *NEC* na *ZEC*. Madaftari hayo huwezi ukayaomba *NEC* au *ZEC* ikakupa, ni madaftari yao, kwa hiyo itabidi utayariske Daftari lingine la kufanya shughuli hii.

Tatu, *issue* hii tunayoanzisha ili upate uhalali wa kuwa hiyo *Special Commission*, ni lazima uende kwenye Katiba ili kuipa uhalali Tume hiyo. Kwa kweli sisi hatuoni sababu kubwa ya kufanya hivyo.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nilikuwa nashauri kwamba ni vizuri tutumie vyombo vyetu vilivyopo kwa ajili ya kufanya shughuli hii ambayo pia ni muhimu. Hiyo *perception* ya kutokuwa huru kwa kweli ni *perception* ambayo haina msingi na Waheshimiwa Wabunge nafikiri ninyi ni mashahidi, ndiyo mnajua uhuru au kutokuwa huru kwa Tume hizo, mimi sina ushahidi wa Tume hizo kutokuwa huru. Nashauri mapendeleko yaliyowekwa na Serikali yabakie kama yalivyo.

MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mwanasheria Mkoo wa Serikali kwa maelezo hayo, ameongelea mambo mazuri na kwa kina, *as long as anatu-assure kwamba Madaftari yataboreshwa* lakini vilevile Tume yenye nayo itaboreshwa basi mimi naafikiana na pendekezo hilo na ninafuta *amendment* yangu.

(Ibara iliyotajwa hapo Juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge zima pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 28

(Ibara iliyotajwa hapo Juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 29

(Ibara iliyotajwa hapo Juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 30

(Ibara iliyotajwa hapo Juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 31

MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ilikuwa ni palepale kwamba zoezi hili liratibiwe namna gani. Nadhani katika hili tumekubaliana na Mwanasheria Mkoo kwamba Daftari lile litafanyiwa maboresho na Tume yenye we itafanyiwa maboresho. Baada ya hapo, nadhani suala hili halina hoja tena, naliondoa.

(Ibara iliyotajwa hapo Juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 32

MHE. ENG. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, haya marekebisho ya Serikali ambayo ni *paragraph ten* katika marekebisho ya Serikali ambayo mimi nataka kufanya marekebisho, inahusiana na baada ya kura za maoni, matokeo ya kura za maoni ikiwa upande mmoja wa Jamhuri ukisema hapana au pande zote za Jamhuri zikisema hapana, kwa mujibu wa marekebisho ya Serikali ni kwamba itaitishwa tena kura ya maoni *within thirty days*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku thelathini baada ya kukataliwa kuitisha tena kura ya maoni ni siku chache sana, kwa sababu tunaelewa kisiasa hapo zinahitajika kampeni na *ku-convince* watu. Kwa hiyo, siku thelathini ni kidogo na mimi nimependekeza siku tisini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, katika marekebisho ya Serikali ilikuwa hajasemwa kwamba kura ya maoni ya mara ya pili kama hiyo Katiba imekataliwa tena Serikali ifanye nini. Tunajua Katiba ya mwaka 1977 iliyopo ndiyo itatumika, lakini sasa Muswada hauelezi patafanyika nini tena. Sasa ikiwa kura ya maoni upande mmoja au pande zote utakataliwa tena kwa mara ya pili tufanye nini, Katiba ya mwaka 1977 itumike lakini baada ya kipindi cha mwaka mmoja basi iitishwe tena kura ya maoni baada ya watu kuelimishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo marekebisho yangu, ahsante.

MWENYEKITI: Mara tatu? Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili la Mheshimiwa Mnyaa la kuongeza siku na kwamba siku thelathini ni kidogo, unajua hili zoezi ukishalimaliza kutakuwa na *tension* na kwenye *statecraft*, hiyo *tension* utaimaliza tu kwa kutangaza kwamba kwa siku thelathini kama tulivyopendekeza basi utarudiwa, kwamba baada ya kushauriana na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar mnapanga siku nyingine. *You point another day within thirty days*, kwa hiyo ita-reduce ile *tension* kwa upande mmoja. Unasema umemaliza shughuli lakini *within thirty days* unasema tutakuwa na mchakato mwagine tarehe fulani *and then* wanasiisa mnaangukia njiani kufanya *political runwork*, tatarudia, ikashindikana tena, tutaendelea mpaka hapo tutakapopata Katiba Mpya na nafikiri kwamba hatuna haja ya kuandika hilo kwenye sheria. Ndiyo maoni yetu na tunafikiri kwamba tumefikiria vyema, lakini kama mna mawazo mengine Sheria inaishi ikifika wakati huo tutababilisha Sheria, ahsante.

MHE. ENG. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, anazo hoja, basi kama haikubaliki hivyo basi *at least two within 90 days*.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba twende kwenye *schedule of amendment*, ukiangalia *section 32 (4)* kwenye (X) tunasema, *Notwithstanding subsection (3)*, hii ambayo anaizungumzia Mheshimiwa Mnyaa, *the National Electoral Commission may, where circumstances so require, afford*:

(a) sufficient time for sensitization and public awareness on the referendum on the proposed constitution; or

(b) necessary time for the President in agreement with the President of Zanzibar to reconvene the Constituent Assembly in order to consider the provisions of the proposed constitution."

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kwamba hiyo inachukua hayo mambo ambayo yanaweza kutokea na ni vizuri kujua kwamba mambo yanaweza kutokea na tunafikiri tumeya-cover vizuri. Ukiangalia kwenye jedwali la Kiswahili ile (4), bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (3), Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kukubaliana na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar inaweza pale ambapo mazingira yataruhusu:-

(a) kutoa muda unaotosha kwa ajili ya uhamasishaji wa wananchi juu ya upigaji kura ya maoni ya Katiba inayopendekezwa; au

(b) kutoa muda utakaonekana unafaa kwa Rais kwa kukubaliana na Rais wa Zanzibar kuitisha upya Bunge Maalum kwa madhumuni ya kuboresha masharti ya Katiba inayopendekezwa.

MHE. ENG. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sahihi nakubaliana na Serikali, nafuta pendeleko langu. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Bulaya, ngoja kwanza, kuna watu wanasema niongeze muda, nilishaongeza muda, kabla sijakaa niliwaambia nitaongeza muda baada ya saa saba. Kwa hiyo, tupo kwenye kipindi cha muda wa nyongeza.

MHE. ESTHER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi baada ya kupata maelezo ya kina kuhusiana na siku thelathini, lakini pia baada ya Serikali kufanya marekebisho na kueleza kwa kina nini kitafanyika baada ya kura za maoni kupigwa na upande mwingine wa Muungano kutofikia asilimia hamsini na mimi naunga mkono mapendekezo hayo. Ahsante.

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 33

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

MWENYEKITI: Samahani sijakuona ulikuwa unasema wapi?

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka ufanuzi kwenye Ibara ya 32 pale alipoweka (c) mwishoni, kwamba kwa kubadilisha Ibara ndogo ya (4) kuwa ya (5).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ndogo ya (4) inasema endapo wingi wa kura ya maoni utakuwa ni "Hapana" Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977 itaendelea kutumika. Nilitaka kujua kama, kwa sababu huku ilsemekana Ibara ya (4) nayo inafutwa, nilitaka kujua ndiyo amemaanisha kwa kusema Ibara ndogo ya 4 itakuwa ndiyo ya (5)?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kupata *clarity* kwenye eneo hilo.

MWENYEKITI: Sawa, Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunai-renumber Ibara ndogo ya (4) kama Ibara ya (5).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuongeza, Katiba yetu ya mwaka 1977 itakuja kuondoka baada ya kuwa tumepata Katiba Mpya. Katiba Mpya ndio itakayoondoa Katiba yetu. Katiba yetu itaendelea mpaka hapo tutakapomaliza mchakato huu. (*Makof*)

MWENYEKITI: Nilishahoji Ibara ya 32, Ibara ya 33 nimeshahoji. Karibu Mheshimiwa Mnyaa.

Ibara Mpya 34

MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara hii, mimi nilitaka iongozwe Ibara mpya ya 34 ili tutamke wazi kwamba mchakato huu mzima wa Katiba Mpya utamalizika ikifika tarehe 31 Desemba, 2014.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni wazo zuri sana lakini ni la kiutendaji na mimi maagizo niliyonayo ambayo hayajaingia kwenye Sheria hii ni kwamba

itakapofika tarehe 26 mwezi wa nne, 2014 wakati tunaadhimisha miaka 50 ya Muungano *inshallah* kutakuwa na Katiba Mpya. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Kwa hiyo, hakuna haja ya kuingiza ndani ya Sheria.

MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Nakubaliana na uamuzi huu.

(*Ibara Mpya iliyotajwa hapo juu ilikataliwa na Kamati ya Bunge Zima*)

Ibara ya 34

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote*)

Jedwali la kwanza

(*Jedwali liliilotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Jedwali la Pili

(*Jedwali liliilotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote*)

Jedwali la Tatu

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekubaliana na masahihisho niliyoyafanya kwa hiyo, nakubaliana.

(*Jedwali liliilotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Jedwali Jipya la Nne

(*Jedwali liliotwajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote*)

(*Bunge lilitrudia*)

T A A R I F A

Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa Mwaka 2011 (*The Constitutional Review Act 2011*)

(*Kusomwa Mara ya Tatu*)

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwa mujibu wa Kanuni ya 89 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2007 kuwa Kamati ya Bunge Zima umeupitia Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa Mwaka 2011 yaani (*The Constitutional Review Act, 2011*), Ibara kwa Ibara na imekubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika. Hivyo basi naomba kutoa hoja kwamba Muswada ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa Mwaka 2011, (*The Constitutional Review Act, 2011*) kama ulivyorekebishwa au kubadilishwa katika Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja illiamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa*)

SPIKA: Muswada huu umepita hatua zake zote isipokuwa tu moja ambayo imebakia ni ya Mheshimiwa Rais kuweka mkono katika Muswada wetu huu ili uwe sheria. (*Makofii/Vigelegele*)

Waheshimiwa Wabunge, kwanza kabisa lazima niseme kama ifuatavyo:-

Jana nilipata nafasi ya kuongea na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani mimi mwenyewe na Makatibu wangu hawa Mezani. Nilichopenda kuongea, mimi nilimwambia niambiwe ukweli tatizo liko wapi? Kwa sababu mimi mpaka wenzetu wanatoka nje sikuwa naelewa tatizo hasa ni nini? Kwa hiyo, nikasema kwa jina la Mungu nataka niambiwe kwa sababu mimi binafsi nimejicheki mwenyewe kwamba nimekosea Kanuni, nimesoma na kurudia Kanuni nikakuta kwenye Kanuni sijakosea. Nikaita watalaaam wangu hawa labda mnisaidie kusoma na wameandika makala kabisa jinsi tulivyofuata Kanuni hatukukosea mahali. Nikasema naomba nielezwe wapi nimekosea mimi kama Kiongozi wenu na Kiongozi wa Taasisi kama nimekosea nina wajibu wa kusema hapa tarehe fulani nimesema sivyo. Ni lazima niseme hivyo kwa sababu tunajenga *precedent*. Kwa hiyo, nasema kama nimekosea niko radhi kuja hapa Bungeni kusema tarehe fulani nilisema hivi nimekosea. Kwa hiyo, hakuweza kunithibitishia hili. (*Makofii*)

Lakini nikasema kwa upande wa pili, kwamba huu Muswada haukuufuata *procedures* zote si kweli, *public hearing* imefanywa vizuri sana na tunao ushahidi wote. Lakini tukaeleza pia huu Muswada ni *technical*, ukimpelekea mama yangu kule kijijini umwambie habari ya kuwa kuna kuundwa Tume atanilewa? Lakini tukimaliza huu Muswada na ukawekwa saini, Tume ikaundwa ikaenda mpaka kule kijijini kwangu kabisa atakayekwenda kumuuliza mwanamke wa kijijini yeye atasema mimi mbolea hajji kwa wakati ama haitoshi, ndivyo atakavyosema. Mwingine atasema mimi nachota maji kilomita mia moja, ndivyo atakavyosema. Hili zoezi nawaambia litachukua pengine miaka miwili mpaka kupata wananchi wote watoe maoni yao. Hilo linaleweka, lakini *technically* kabisa tuanze kuuliza kila mtu nikawaambia si *realistic* na wala si ukweli.

Lakini kosa walilofanya wenzetu ni kuondoka na kutokuchangia hapa mawazo yao hata yawe makali, mategemeo yangu mimi yalikuwa huu Muswada usingeisha leo nilitegemea *amendments* zilizojaa hapa labda tungefika mpaka wiki ijayo kwa sababu kuna *amendment* za Wabunge. Lakini kitendo cha wao kutoka hawajatimiza wajibu wao wa Kikatiba. Hawajatimiza wajibu wao wa Kutunga Sheria kwa niaba ya wananchi. (*Makofii*)

Sasa hatua yoyote inayofanywa, bahati mbaya mtu anayesema ukweli hapendi kusikilizwa, uongo unaonekana mtamu zaidi kuliko ukweli. Ukweli unabakia pale, *Bill* hii imefuata hatua zake zote na tumetunga kwa mujibu wa Sheria, tatizo letu ni wenzetu walilotoka bila kuwashirikisha Watanzania maoni yao. Watanzania wanaoandamana hawajui wanaandamana kwa sababu gani lakini wangekupeko hapa wangejua kwa nini wanaandamana kwamba maneno yao hayakusikilizwa na kwa mujibu wa Mabunge ya Vyama Vingi wanasema hata wale wachache wape nafasi ya kusikika. Kwa hiyo, wangekuwepo hapa wangesikika, wananchi wangejua wanachama wetu walikuwa wanasema hivi, sasa hawakusema kitu, ukiacha maoni ya Mheshimiwa Tundu Lissu. Kwa hiyo, hapa wananchi hawakutendewa haki ya kutowasikia Wabunge wao wanalamikia nini. Kwa hiyo, walio wengi wanachukua nafasi kwa sababu ndio walikuwa wengi. Lakini wao wangekuwepo hapa wangesikika, wanapokwenda kuandamana huko ndio wangekuwa wanasema si mlisikia nilikuwa nasema hivi, wenyewe hawakusikika. Lakini sasa kitu gani tunachobishana? Kwa hiyo, tulikubaliana kutokukubaliana kwamba hawakuwatendea haki Watanzania. Kwa hiyo, wananchi tumepitisha Muswada huu wala msiwe na wasiwasi tumeupitisha kwa mujibu wa Sheria, taratibu na Kanuni za Bunge zote. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa kama nilivyosema hatua imebakia moja ya Mheshimiwa Rais kukubali au kukataa na wanamshawishi akatae sjui hii ina mantiki gani.

Kwa hiyo, baada ya kusema hayo, napenda pia kutoa taarifa kwamba natumia Kanuni ya 30 (6) kwamba Shughuli za Bunge katika kila Kikao zitatekelezwa kwa kufuata orodha za shughuli za siku hiyo au kufuata utaratibu mwininge amba Spika ataagiza ufuatwe kwa ajili ya uendeshaji bora wa Shughuli za Bunge. Sasa huu utaratibu mwininge kwa leo, halafu nitamwomba pia na Kiongozi wa Serikali atoe hoja kwamba kesho tukae kama Bunge.

Sasa hii ya leo ni kwamba mkiangalia *Order Paper* yetu baada ya Muswada kilichokuwa kinaendelea hapa ilikuwa ni Mwenyekiti wa Kamati Teule ya Bunge awasilishe taarifa, sasa tumebadilisha ili Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini aanze kusudi kesho atakavyotoa hoja ya kwamba kesho tukae kama Bunge tuwe na muda wa kuzungumzia Kamati Teule. Kwa hiyo, jioni saa 11.00, naomba tuanze na Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini. Kwa hiyo, hilo ndio badiliko tu kwamba tumebadilisha badala ya kuanza na Kamati Teule tunaanza na Kamati ya Nishati na Madini. Lakini pia tutaomba itolewe hoja jioni kwa sababu muda umekwisha kabisa. Kwa hiyo, kwa leo tutakaporudi saa 11.00 tutashughulikia Kamati ya Nishati na Madini.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kueleza hayo, nawaombeni tukitoka tu tum-join Makamu wa Rais, ni mgeni wetu katika shughuli ya TAPAC. TAPAC imetimiza miaka 10 toka ianzishwe kwa hiyo, nawaombeni wote tushiriki pale, ni muda mfupi halafu tutaendelea na shughuli zingine. Kwa hiyo, nasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

(*Saa 7.15 mchana Bunge lilitishwa mpaka saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilitrudia*)

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Sylvester Masele Mabumba) Alikalia Kiti

Taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini juu ya Uendeshaji wa Sekta Ndogo ya Gesi Nchini

MHE. SELEMANI J. ZEDI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA NISHATI NA MADINI): Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba kuchukua fursa hii kwa niaba ya Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kukushukuru wewe binafsi kwa kutoa kibali ili Kamati ya Nishati na Madini kupitia Kamati yake Ndogo kufanya kazi kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Kikatiba ya Bunge katika kuisimamia na kuishauri Serikali na vyombo vyake kwa niaba ya wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 115, Nyongeza ya Nane, kifungu cha 9(1)(d) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, naomba kutoa taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini iliyochunguza uendeshaji na uendelezaji wa sekta ndogo ya gesi hususan ushiriki, ufanisi na uadilifu wa Kampuni ya Pan African Energy Tanzania Limited (PAT) katika mchakato wa uendelezaji wa sekta ya gesi nchini kwa maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chimbuko la Kamati Ndogo ni hoja zilizojiteza wakati Kamati ilipokuwa inajadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012. Wakati wa mchakato huo Kamati ilipata taarifa kutoka kwa wadau mbalimbali kuhusu mapungufu mbalimbali yanayolenga sekta ya gesi katika mahusiano ya wadau wa gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo tarehe 15 Julai, 2011 wakati Kamati ya Nishati na Madini inawasilisha taarifa yake ya Bajeti ya Mwaka 2011/2012, Bungeni katika sehemu ya Maoni na Ushauri wa Sekta ya Gesi, Kamati ilitoa hoja ya kuunda Kamati Ndogo kufuatilia suala hili. Wabunge waliunga mkono hoja hii na Mheshimiwa Spika alikubaliana na ushauri huo wa Kamati. Aidha, Katika kuhakikisha kazi hiyo inafanyika kwa ufasha, Kamati Ndogo ilipewa Hadidu za Rejea (*Terms of Reference*) na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe tisa wa Kamati waliteuliwa kuunda Kamati Ndogo ya Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 114(18) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, Wajumbe hao ni:-

Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mwenyekiti; Mheshimiwa Charles John Paul Mwijage, Mjumbe; Mheshimiwa Nassir Abdallah Yusuph, Mjumbe; Mheshimiwa Christopher Olonyokie Ole-Sendeka, Mjumbe; Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mjumbe; Mheshimiwa Mwanamrisho Taratibu Abama, Mjumbe; Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mjumbe; Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, Mjumbe na Mheshimiwa Sarah Ally Msafiri, Mjumbe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha kazi hiyo inafanyika kwa ufasaha, Kamati Ndogo ilipewa Hadidu za Rejea (*Terms of Reference*) zifuatazo:-

- (1) Kubainisha kama Mikataba, taratibu na Kanuni zinazotawala shughuli za gesi zinazozingatia maslahi ya Taifa na hazitiliwi shaka na wadau.
- (2) Kubainisha mahusiano ya wadau wakuu wa gesi.
- (3) Kubainisha kama maamuzi yanayoendesha shughuli za gesi kama vile gharama za ujenzi, uendeshaji na mambo mengine yanayoweza kuathiri gharama na usalama wa shughuli yanafikiwa kwa ufanisi na yanazingatia maslahi ya Taifa.
- (4) Kubainisha kama kuna hali ya kuviza, kuficha na uhamasishaji hasi wa shughuli za maendeleo ya gesi mionganoni mwa wadau. Pia kubaini kama mfumo wa uendeshaji shughuli unaleta ukiritimba (*Monopoly*) ambao unawenza kuzuia ushiriki wa wadau wengi kwa tija na maslahi ya Taifa.
- (5) Kuandaa Ripoti na kuishauri Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ili imshauri Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Kamati Ndogo. Kamati ilipewa muda wa wiki tatu kukamilisha kazi hii ambayo ilianza rasmi tarehe 4 Septemba, 2011, lakini kutokana na ukubwa wa kazi, Kamati iliongezewa wiki mbili ili kuweza kuikamilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa majukumu yake Kamati ndogo ilikutana na baadhi ya wadau wakuu wa Sekta ya gesi kama ifutavyo:-

- (a) Wizara ya Nishati na Madini;
- (b) Shirika la Maendeleo ya Petroli (*TPDC*);
- (c) Shirika la Ugavi la Umeme (*TANESCO*);
- (d) Kampuni ya *SONGAS*;
- (e) Kampuni ya *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)*;
- (f) Kampuni ya *Ndovu Resources*;
- (g) Kampuni ya *Wentworth Resources*;
- (h) Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (*EWURA*);
- (i) Kampuni ya Twiga Cement; na
- (j) Baadhi ya wadau wa gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipanga ratiba na kufanya kazi zake kama ifuatavyo:-

- (1) Kupata maelezo yanayohusu sekta ya gesi kutoka:
 - (i) Timu ya wataalam wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (*TPDC*).
 - (ii) Mwanasheria wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (*TPDC*).
 - (iii) Mkaguzi Mkuu wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (*TPDC*).

(iv) Wahandisi wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (*TPDC*) kuhusu uzalishaji, usafirishaji, usambazaji wa gesi pamoja na utunzaji wa visima na mitambo ya gesi.

- (2) Kupata maelezo ya kisheria kutoka kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.
- (3) Kupata maelezo kutoka Wizara ya Nishati na Madini na Kitengo cha Songo Songo *Project Monitoring Unit (PMU)* kilichopo chini ya Wizara hiyo.
- (4) Kupata maelezo mbalimbali kutoka kwa wataalam wa *TANESCO* kuhusu uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa gesi.
- (5) Kupata maelezo mbalimbali kutoka kwa wadau wa gesi nchini kuhusu hali halisi ya sekta ya gesi nchini na mahusiano ya wadau.
- (6) Kupata taarifa zinazohusu sekta ya gesi kutoka kwa Kampuni ya SONGAS, Pan African Energy Tanzania Tanzania Limited (PAT), Wentworth Resources, Ndovu Resources na Twiga Cement.
- (7) Kufanya ziara katika mradi wa gesi ya Songosongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya gesi nchini. Ugunduzi wa gesi nchini; Gesi ya Songosongo iligunduliwa na Kampuni ya *Agip Spa* Mwaka 1974. Aidha, tathmini ya awali iliyofanywa na Kampuni ya *Agip Spa* ilionesa kuwa gesi hii haina manufaa ya kiuchumi na hivyo wakaamua kuliacha eneo hilo. Mnamo Mwaka 1975 Serikali kupitia *TPDC* ilitathmini upya taarifa za kina na kuchimba visima vya gesi namba tatum, nne, tano, saba na tisa. Matokeo ya tathmini yalionesha kuwa gesi hiyo inafaa kiuchumi. Visima hivi vilitunzwa na *TPDC* kwa kutumia mapato yaliyokuwa yanatokana na biashara waliyokuwa wanafanya ya kuagiza na kusambaza mafuta, jukumu hili liliendelea mpaka mwaka 1997 walipovikabidhi kwa Songas.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu rasilimali ya gesi na mahali zilipo. Kiasi kikubwa cha rasilimali ya gesi inapatikana eneo la Kusini mwa nchi yetu, hususan maeneo ya mwambao wa Kusini mwa Tanzania (Songosongo, Mnazi Bay na bahari ya kina kirefu). Eneo la Songosongo linakadirwa kuwa na akiba ya gesi yenye futi za ujazo trillioni mbili (27cf) na kati ya hizo, futi za ujazo zilizothibitishwa ni bilioni 880; wakati eneo la Mnazi bay linakadirwa kuwa na akiba ya gesi yenye futi za ujazo Trillioni tano (5cf) na kati ya hizo, futi za ujazo zilizothibitishwa ni bilioni 262.

Gesi ya Songosongo inapatikana katika eneo ambalo katika mikataba inayohusika na mradi huo na linajulikana kama Songosongo *Gas Field* au *Contract Area* au *Development License Area*. Eneo hili limegawanyika katika sehemu kuu mbili yaani *Discovery Block* mbili na kuna visima vitano vinavyozalisha gesi; *Adjoining Blocks* zipo saba na hakuna kisima. Katika *Discovery Block* kuna sehemu ambapo gesi imethibitika kuwepo (*proven section*) na kuna sehemu ambayo inabidi kufanyiwa kazi kuizalisha gesi iliyoko ardhini (*unproven section*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa undelezaji wa gesi asili nchini umegawanyika katika sehemu kuu mbili zinazojulikana kama:- Utafutaji na uzalishaji wa gesi (*Upstream*), usafishaji, usambazaji na utumiaji wa mafuta na gesi (*midstream and downstream*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utafutaji na uzalishaji wa mafuta na gesi (*upstream*). Shughuli zote za utafutaji wa mafuta na gesi nchini unatawaliwa na Sheria ya Utafutaji na Uzalishaji Mafuta ya mwaka 1980 (*The Exploration Act, 1980*) na mikataba husika imeundwa katika mfumo wa *Model Production Sharing Agreement (MPSA)* pamoja na Sera ya Nishati ya Taifa. Katika mfumo huu, mwekezaji analipia gharama zote za utafutaji. *TPDC* huwajibika kuchangia gharama baada ya ugunduzi kufanyika. Uhai wa mkataba unategemeana na utekelezaji wa mpango kazi uliokubalika kati ya Serikali, *TPDC* na mwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango kazi huo hujadiliwa kila mwaka kati ya pande zote tatu za mkataba. Pale endapo mpango kazi uliokubalika haukutekelezwa inavyotakiwa, mikataba inaipatia Serikali na *TPDC* nafasi ya kufuta mkataba kwa misingi ya kisheria. Pale ambapo

ugunduzi wa mafuta na au gesi umefanyika, mikataba inaipa nafasi *TPDC* kuchangia gharama za uendelezaji kuitia *Joint Operating Agreement (JOA)* kati ya *TPDC* na mwekezaji. Aidha, pale ambapo mwekezaji anaposhindwa kuendeleza mradi kama ilivyokubalika (kimkataba) basi *TPDC* ina nafasi ama kuchukua uendeshaji wa mradi wote ama sehemu ya mradi. *TPDC* inaweza kuwa na nafasi kubwa zaidi ya maamuzi katika mikataba hii endapo itawekeza inavyostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa usafirishaji, usambazaji na utumiaji wa mafuta na gesi (*midstream and downstream*) shughuli hii hutawaliwa na Sheria ya *EWURA Cap 414* kwa kuwa kwa sasa Sheria ya Gesi nchini haipo. Hivyo basi, makubaliano katika mkataba baina ya wadau hutakiwa kuwasilishwa *EWURA* kwa mapitio na baada ya kujiridhisha hupanga bei za gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wadau wakuu katika sekta ya gesi na mahusiano yaliyopo kwenye Kampuni za gesi nchini. Wadau wakuu kwa sasa katika Sekta ya Gesi ni pamoja na:-

- (a) Serikali kuitia Wizara ya Nishati na Madini hasa katika masuala ya Sera.
- (b) Watafutaji na wazalishaji wa gesi asili na mafuta kama *TPDC, Pan African Energy, Wentworth Resources* na Ndovu Resources.
- (c) Wawekezaji katika miundombinu mfano *SONGAS*.
- (d) Watumiaji wa gesi asili ambao ni pamoja na *TANESCO, Viwanda, Majumbani* na Idara au Taasisi mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahusiano ya wadau katika sekta yoyote ni jambo la muhimu sana, hapa nchini kwetu hakuna mfumo wowote au maalum uliowekwa kisheria unaosimamia mahusiano ya wadau katika sekta ya gesi. Watafutaji na wazalishaji wa gesi na petroli nchini wameunda umoja wao ambao unaitwa *OGAT (Oil and Gas Association in Tanzania)*. Serikali na *TPDC* huwa ina utaratibu wa kukutana kujadili maendeleo na changamoto zinazopatikana katika kutafuta na kuzalisha petro/na gesi. Hata hivyo, taasisi hii haina nguvu sana.

Aidha, mradi wa *Songsongo Gas to Electricity Project* pamoja na wadau wengine wana mfumo wa kukutana kila mara kwa mkuuso unaoitwa *GWG (Gas Working Group)* kujadili masuala anuai ya gesi na kutolewa maamuzi ya mwisho ya utekelezaji ambayo hupelekwa kwenye bodi zao husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya sekta ya gesi nchini; Tanzania ya leo inaendelea kujionea mabadiliko makubwa katika sekta ya gesi, Kamati Ndogo imejiridhisha kwa hili baada ya kukutana na wadau mbalimbali wenye leseni na wasio na leseni. Aidha, sekta hii ndiyo mzalishaji mkubwa wa nishati ya umeme tunayoitumia sasa na mchango wake umedhihirika. Serikali imeweza kuokoa jumla ya dola bilioni 2.5 kwa kutumia gesi kuzalisha umeme katika mradi wa Songsongo kwa kipindi cha miaka sita ambazo zingetumika kuagiza mafuta ya kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na visima vya gesi vilivyopo na miundombinu ya kusafishia na kusafirishia gesi kwa watumiaji, gesi yenye ujazo wa futi za ujazo milioni 105 husafirishwa kwa siku. Kati ya hizo futi za ujazo 105 milioni zinazosafishwa na kusafirishwa, futi za ujazo 80 milioni hutumika kuzalishia umeme na futi za ujazo 25 milioni hutumiwa na viwanda vipatavyo 36 kama nishati ya kuendeshea mitambo kikiwemo Kiwanda cha Twiga Cement (*Wazo Hill*) ambacho kinatumia futi za ujazo milioni 15 kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kampuni zinazojihusisha katika uchimbaji wa gesi. Idadi ya Kampuni zinazojihusisha na uchimbaji wa gesi nchini ni 15 zikiwa na mikataba 22. Kampuni hizo ni pamoja na Ndovu Resources, Petrobras, Statoil, BG Ophir Energy, Dominion Oil and Gas, Tullow Oil, Songas, Pan African Energy Tanzania Ltd, Mauriel ET Prom, Heritage, HydroTanz, Beach Petroleum, Doudsal Resource, Shell International na Key Petroleum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa visima ambavyo tayari vimechimbwa nchini ni 52. Kati ya hivyo, visima 15 ndiyo vimegundulika kuwa na gesi. Aidha, kati ya hivyo 15, visima saba vipo Songosongo, visima vinne vipo Mnazi Bay, kisima kimoja kipo Mkuranga na visima vitatu vipo kwenye bahari ya kina kirefu (*Deep Sea*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na ongezeko la Mradi na mahitaji ya gesi; mahitaji ya gesi nchini yamekuwa yakiongezeka siku hadi siku hasa kutokana na ukweli kwamba nishati hii ni nafuu kwa maana ya kuzalisha umeme, kuendesha mitambo, kutumia majumbani na pia ni rafiki wa mazingira. Kwa mujibu wa mipango ya uzalishaji umeme nchini, inaonesha kuna miradi mitatu ya uzalishaji umeme inayotarajiwa kukamilika katika kipindi cha miaka miwili ijayo. Kuna mradi wa Kinyerezi wa MW 240 utakaohitaji gesi kiasi cha futi za ujazo milioni 50 kwa siku, Mradi wa Somangafungu wa MW 230 utakaohitaji gesi kiasi cha futi za ujazo milioni 50 na Mradi wa Jacobsen wa MW 100 utakaohitaji gesi kiasi cha futi za ujazo milioni 20 kwa siku. Aidha, viwanda vingi vilivyopo eneo la Mikocheni, Dar es Salaam vimeomba kuunganishwa na mfumo wa gesi na TPDC inategemea kuanza Mradi wa Ujenzi wa Bomba la gesi kwenda Mikocheni. Hata hivyo, kwa sasa bomba lilolopo la Mradi wa Songas ni dogo na halikidhi mahitaji na hivyo kuwepo haja ya ujenzi wa bomba kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuchukua maamuzi ya kukopa fedha kutoka Serikali ya China ili kujenga Bomba kubwa litakaloanzia Mtwara – Somangafungu - Dar es Salaam – Tanga ambalo gharama yake inakadiriwa kuwa dola za Kimarekani milioni 778.

Bomba hilo ambalo kutoka Mtwara hadi Somangafungu litakuwa na kipenyo cha inchi 24 na uwezo wa kupitisha gesi kiasi cha futi za ujazo milioni 520 na kuanzia Somangafungu hadi Dar es Salaam bomba hili litakuwa na kipenyo cha inchi 36 na uwezo wa kupitisha gesi kiasi cha futi za ujazo milioni 784 kwa siku. Pia ujenzi wa bomba hilo unakwenda sambamba na ujenzi wa mtambo wa kusafishia gesi wenye uwezo wa kusafisha gesi kiasi cha futi za ujazo milioni 210 kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni neema kwa Taifa letu na Kamati inaanini bomba hili litaleta manufaa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu taarifa zilizowasilishwa mbele ya Kamati. Wadau mbalimbali walitwa mbele ya Kamati kwa lengo la kuwahoji na kuleta taarifa za kimaandishi zinazohusiana na masuala ya Sekta ya Gesi. Wadau hao walitoka Wizarani, Taasisi za Serikali, Kampuni za gesi pamoja na watu binafsi. Kamati iliwahoji na kuomba taarifa mbalimbali pamoja na vielelezo ambavyo vililenga kusaidia Kamati katika kukamilisha kazi yake na kujiridhisha na ushauri itakaoutoa. Baadhi ya Taarifa za msingi zilizowasilishwa mbele ya Kamati ni pamoja na:-

Taarifa kutoka Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) (Kiambatisho Na. 1) kwa nyakati tofauti, Kamati Ndogo ya Nishati na Madini ilikutana na kuwahoji watendaji mbalimbali kutoka Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC); Utawala, Mwanasheria, Mkaguzi wa Ndani na Wahandisi. Wakati wa mahojiano taarifa mbalimbali zilitolewa na vielelezo viliwasilishwa mbele ya Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mradi wa Songa. Taarifa ilitolewa kuwa Mikataba ya mradi wa gesi iliyojadiliwa, kukubaliwa na kusainiwa na Serikali pamoja na SONGAS ilikuwa kumi na nane. Katika majadiliano hayo, upande wa Serikali uliwakilishwa na: Kamishna wa Nishati, Maafisa Waandamizi wa Wizara ya Nishati na Madini, Hazina, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, iliyokuwa Wizara ya Mipango, TANESCO na TPDC. Aidha, Serikali ilishirikisha wataalam waelekezi kutoka Marekani, Canada na Norway. Majadiliano ya Mkataba yalianza mwaka 1993 na mwisho Mkataba ulisainiwa tarehe 11 Oktoba 2001. Ili kufanikisha Mradi huu, Serikali ilikopa fedha kutoka Benki ya Dunia, European Investment Bank (EIB) na Swedish International Development Agency (SIDA) jumla ya dola za Kimarekani milioni 216 na kuikopesha Kampuni ya Songas kwa mujibu wa masharti ya Mkataba ili kuzalisha umeme na kuiuzia TANESCO.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TPDC walieleza kuwa Mikataba kumi na nane iliyoingiwa ilikuwa katika makundi mawili nayo ni:-

Kundi la kwanza, lilihusu mikataba tisa ya msingi (*Basic Agreements*) ambayo inaainisha haki na majukumu ya pande zilizotazamiwa kuhusika katika kutekeleza mradi. Mikataba hii ni:-

- *Mikataba wa Utekelezaji (Implementation Agreement (IA));*
- *Mikataba wa wabia (Shareholders Agreement (SA));*
- *Mikataba wa uzalishaji na ugawanaji (Production Sharing Agreement (PSA));*
- *Mikataba wa Gesi (Gas Agreement (GA));*
- *Mikataba wa Uendeshaji (Operational Agreement (OA));*
- *Mikataba wa Uhamishaji Mali za Songosongo (Songosongo Facilities Transfer Agreement (SFTA));*
- *Mikataba wa Ununuzi wa Umeme (Power Purchase Agreement (PPA));*
- *Mikataba wa Kuhamisha Eneo la Ubungo(Ubungo Complex Transfer Agreement (UCTA)); na*
- *Mikataba wa Kusafisha na Kusafirisha gesi (Gas Processing and Transportation Agreement (GPTA)).*

Kundi la pili, lilihusu mikataba tisa inayohusu masuala ya fedha za kugharania Mradi (*Financial Agreement*). Mikataba hii inaainisha pesa zitakazopatiana , wahusika wa kuzilipa pamoja na uhakika wa ulipaji wa madeni ya umeme, uhakika wa upatikanaji wa faida kwa wawekezaji, kinga dhidi ya kushuka kwa shilingi ya Tanzania na kadhalika. Mikataba hii ni:-

- *Mikataba wa Maendelezo ya Mkopo (Development credit Agreement (DCA));*
- *Mikataba wa Fedha wa EIB (EIB Finance Contract);*
- *Mikataba wa Mkopo wa EIB (EIB On-Lending Agreement);*
- *Mikataba wa Escrow (Escrow Agreement);*
- *Mikataba wa Pesa za Kigeni (Hard Currency Agreement);*
- *Mikataba wa Liquidity Facility (Liquidity Facility Agreement);*
- *Mikataba wa kupokea Mkopo (Loan Assumption Agreement);*
- *Mikataba wa Hati ya Fedha (Debenture Agreement); na*
- *Mikataba wa Ongezeko la Mkopo (Subsidiary Loan Agreement).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umiliki wa visima nya gesi. TPDC walieleza kuwa kwa mujibu wa kifungu 4(1) cha Sheria ya Utafutaji na Uzalishaji Mafuta, Sura ya 328 (*The Petroleum Exploration and Production Act, Chapter 328 of the Revised Edition of Laws of Tanzania*), Mikataba ya Uzalishaji na Ugawanaji (*Production Sharing Agreement – PSA*) inatambua kuwa maliasili za mafuta na gesi ni mali ya Serikali. Mwekezaji anapata haki ya kushiriki katika mapato au mgao wa rasilimali ya mafuta na gesi pale anapowekeza ili kuizalisha rasilimali hii.

Mwekezaji hupata sehemu tu ya rasilimali kulingana na kiwango alichokitumia kuwekeza na kiasi fulani cha faida, kinachobaki ni mali ya Serikali. Kwa misingi hiyo ya PSA, kiasi ambacho Serikali itastahili kupata inategemea sana na usahihi na uhalali wa gharama za mwekezaji. Mgao wa Serikali unaweza kupunjwa na mwekezaji iwapo atatoa gharama zisizo sahihi au zisizo halali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kuwa, Mkataba uliingiwa baina ya Serikali, *TPDC, SONGAS* na *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* kuhusu umiliki na uendeshaji wa visima vya gesi. Mkataba wa uzalishaji na ugawanaji (*PSA*) umeonesha kifungu ambacho kinaruhusu Kampuni ya *SONGAS* kumpa mamlaka *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* kuvitumia visima vya gesi. Aidha, kupitia *Gas Agreement* ambayo ni mojawapo ya mikataba iliyoingiwa katika kufikia azma ya utekelezaji wa mradi wa Songosongo, kuna kifungu 2.1 na 2.2 kinaonesha namna *SONGAS* alivyopewa umiliki wa visima vitano na *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* alivyopewa kazi na *SONGAS* kuvitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu katika Mikataba. Kamati ilifahamishwa kuwa, Mkataba wa *PSA* ndio mwongozo mkuu wa mahusiano yote yanayohusu uzalishaji na ugawanaji wa mapato ya gesi baina ya *TPDC* na mbia yejote. Kwa mujibu wa kifungu cha 5.1 cha *PSA*, kimeeleza wazi kuwa *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* walipewa majukumu ya kufanya shughuli za utafiti, kutumia kiasi cha dola za Kimarekani millioni mbili ili kutafuta *data* za mtetemo (*seismic*) katika *unproven section* (sehemu ambayo inabidi kufanyiwa kazi kuizalisha gesi iliyoko ardhini) au katika *Adjoining Block*, kuchimba angalau kisima kimoja cha utafiti katika *Adjoining block* na kutafuta masoko ya gesi ya ziada. Haya yalitakiwa yafanywe katika kipindi cha awali cha miaka mitano ya *PSA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali ya masikitiko *TPDC* walieleza Kamati kuwa, kifungu cha 5.3 kiliondoa ulazima wa *Pan African Energy-Tanzania Limited (PAT)* kuwekeza katika *Adjoining block*. Kifungu hiki kinawapa uhuru wa kuwekeza au kutowekeza katika *Adjoining Block*, Kimsingi katika *PSA* ya kawaida kipengele 5.1 ndio uti wa mgongo wa *PSA* na ambako wanetakiwa waweke mkazo kwa sababu hakujafanyiwa kazi. Kifungu hicho kinaendelea kuwaachia haki zote katika *Discovery Block* ambako hakukuhitajika kufanyiwa kazi bali kuzalisha na kuuza gesi tu. Haki hiyo inatolewa na kifungu cha 4.2 na 4.3 cha *PSA* ambacho kinazipa *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* na *TPDC* haki zote za kuuza *Additional Gas*. Kiwango cha hatarisho la kuwekezaji (*risk*) inayotakiwa katika *PSA* kwao haipo au ni kidogo sana. *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* walizembea kuendeleza *Adjoining Blocks* baada ya kugundua kuwa wangeweza kupata mapato katika *Discovery Block* pasipo kutumia gharama zaidi hali iliyopelekea muda wake wa uendelezaji kwisha na hivyo kuwalazimu kuachia *Adjoining Block*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko Kamati ilifahamishwa kuwa kwa makusudi kabisa *Pan African Energy Tanzania (PAT)* waliamua kutowekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa upungufu mwininge wa Mkataba huu ni kuwa Mkataba hauruhusu mabadiliko ya haraka ya mahitaji ya kiwango cha gesi (*Gas demand*) inayotumika pale nchi inapopata dharura ya upungufu au ukosefu wa umeme kwa sababu ya ufinyu wa bomba la gesi. Maelekezo ya awali ya Serikali kwa wawekezaji illkuwa ni kupanua bomba la gesi na kiwanda cha kusafisha gesi ili isafirishwe kwa wingi zaidi kukidhi mahitaji ya kuondoa au kupunguza mgawo wa umeme. Maelekezo haya yamekutana na pingamizi mbalimbali kutoka kwa wadau wa gesi kwa kuwa wanataka kupata mapato ya juu. Aidha, hali hii ilijionesha kwa Kampuni ya *Pan African Energy-Tanzania Limited (PAT)* na *Songas* kutoa pingamizi kubwa kuiruhusu Kampuni ya Ndovu Resources inayochimba gesi huko Kiliwani kuunganisha kisima chao kwenye bomba la *Songas*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kuwa Mkataba wa uzalishaji na ugawanaji (*PSA*) wa *TPDC* na *Pan African Energy Tanzania Ltd (PAT)* una vipengele tata na vya makusudi vyenye maana zaidi ya moja ambavyo vingine vinatafsiriwa tofauti na *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* kuhusu haki ya *TPDC* kuwekeza katika uzalishaji (*Participation in Development*) kwa mfano, Kifungu cha 8.1 cha *PSA* kinampa haki *TPDC* kuwekeza katika uzalishaji ambako kutaongeza mgawo wake kufikia asilimia ishirini, lakini kwa makusudi na tafsiri potofu *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* wamekuwa wakikataa maombi ya *TPDC* ya kutaka kushiriki katika kuwekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ilijidhihirisha wazi wakati wa mchakato wa kuchimba kisima namba kumi (*SS10*) na *TPDC* walipotaka kushiriki lakini *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* walikuwa wagumu kuwakubalia ili wapate kujirudishia gharama za uchimbaji. (Kiambatisho Na.

2(a) barua ya *TPDC* kutaka kushiriki). Kiambatisho Na. 2(b) *minutes* za kikao ambazo *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* iliwa inataka mazungumzo zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu shughuli za ugavi. Kamati ilielezwa kuwa Kampuni ya *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* mara kwa mara imekuwa ikifanya shughuli za ugavi bila kumshirikisha mbia wake *TPDC* kinyume na Mkataba wa uzalishaji na ugawanaji (*PSA*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kuwa Kifungu cha 15 cha *PSA* kinamtaka *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* kutoa upendeleo kwa bidhaa za Tanzania na wakandarasi wa Kitanzania kwa masharti ya kuflikia viwango vya Kimataifa na kumudu ushindani. Aidha, taratibu za zabuni za Kitanzania zenyenye kuzingatia hali halisi ya Tanzania zinatakiwa zitumike ili kuwapa fursa Watanzania kufanya ugavi. *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* imekuwa ikikiuka taratibu za manunzi za Tanzania na Mkataba wa uzalishaji na ugawanaji (*PSA*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kuwa Mkataba wa Soko na Mauzo (*Marketing and Sale Agreement*) unaitaka *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* kufanya shughuli za ugavi kwa kushindanisha. Hata hivyo, *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* kwa muda mrefu imekuwa ikitumia Kampuni moja tu ya *LOOTAH BC* kufanya shughuli za ugavi bila kuishindanisha na kampuni nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kuwa, Mkataba wa uzalishaji na ugawanaji (*PSA*) na Mkataba wa Soko na Mauzo (*Marketing and Sale Agreement*) unamtaka *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* kumshirikisha *TPDC* wakati anapojadili masuala ya mauzo ya gesi na wateja wao. Kampuni ya *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* imekuwa ikiipuuzia na kutomwalika *TPDC* katika majadiliano na wateja wake na badala yake imekuwa ikiwasilisha makabrasha kwa *TPDC* kwa ajili ya kusainiwa mapatano yao baada ya majadiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuharibika kwa visima vitatu vya gesi. Kamati ilifahamishwa kuwa, visima vitatu vya gesi vilivyopo *Songosongo* viligundulika kuwa vimeharibika na havifai kutoa gesi mwezi Oktoba 2010. Visima hivyo ni kisima namba tano (*SS5*) ambacho kilikuwa kimeharibika sana kikifuatia kisima namba tisa (*SS9*). Aidha, kisima namba saba (*SS7*) kimeathirika kidogo na pia kisima namba tatu (*SS3*) na kisima namba nne (*SS4*) vimeathirika kidogo zaidi. Tarehe 27 Novemba 2010, kisima cha gesi namba tano (*SS5*) kilifungwa na kisima namba tisa (*SS9*) kimepunguza kiwango cha gesi kinachozalishwa na kitafungwa Aprili, 2012. Aidha, Mkataba wa Gesi (*Gas Agreement*) kati ya Serikali, *TPDC* na *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* chini ya kifungu cha 7.6(e) kinaonesha wajibu wa *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* kusimamia uendeshaji, usimamizi na ukarabati wake kwa kufuata mkataba pamoja na taratibu za utafutaji na uchimbaji wa sekta ya mafuta na gesi duniani *production logging* kwa kutumia vifaa vinavyokubalika kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uharibifu huo, Kamati ilielezwa kuwa Mpango wa gesi (*Gas Master Plan*) unamtaka *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* katika kipindi cha miaka miwili hadi mitatu kufanya ukaguzi na ukarabati wa visima pamoja na mitambo ili kuhakikisha hali nzuri ya mitambo pamoja na visima kama njia mojawapo ya kuhakikisha usalama na ubora wa uendeshaji wake. Ilisisitizwa kuwa *PAT* ilizembea kwa kukaa zaidi ya miaka sita bila kufanya ukaguzi huo hali ambayo ilipelekeea uharibifu wa visima hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TPDC* walijulisha Kamati kuwa, baada ya kugundulika uharibifu kwenye visima (*corrosion*) walifanya mawasiliano na *Songas* kwa barua yenye Kumb Na. *TPDC* – C/P50/126 ya tarehe 15 Aprili, 2011 ili ukarabati uweze kufanyika. Hata hivyo, jithihada hizo ziligonga ukuta baada ya *Songas* kuandika barua ya tarehe 28 Aprili na 28 Julai, 2011. (Kiambatisho Na. 4 barua za *Songas*) ikipinga wao kuwajibika na uharibifu huo. Aidha, gharama zilizotumika na *Pan African Energy Tanzania (PAT)* kufanya utafiti na ukaguzi wa uharibifu (*corrosion logging* na *corrosion log interpretation*) mpaka sasa zimefikia jumla ya dola za Kimarekani 1,176,624.91.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukaguzi wa hesabu za *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)*. Kamati ilielezwa kuwa, Idara ya ukaguzi ya *TPDC* imefanya ukaguzi wa hesabu za *Pan*

African Energy Tanzania (PAT) kwa mujibu wa Kifungu 21.2 cha *PSA* na imegundua upungufu na ukiukwaji ufuatao:-

(a) Udanganyifu unaofikia jumla ya kiasi cha dola za Kimarekani milioni 64 ambazo ni sawa na fedha za Kitanzania Shilingi Bilioni 110 ambazo *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* imejirudishia isivyo halali kama gharama walizotumia kuzalisha gesi kutoka Mwaka 2004 hadi 2009. Kati ya hizo, *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* wamekiri kwamba walijirudishia isivyo halali kiasi cha dola za Kimarekani milioni 28.1 na kwamba dola za Kimarekani milioni 36 zilizobaki wanaandaa vielelezo vya kuthibitisha uhalali wa kujirudishia gharama hizo. Kwa mujibu wa *TPDC* na Wizara, ifikapo tarehe 30 Septemba 2011, *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* walitakiwa wawe wamewasilisha vielelezo hivyo, vinginevyo wakamilishe ulipaji wa fedha zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya vitendo vya udanganyifu wa kimahesabu uliofanywa na Kampuni ya *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* ni pale ambapo Mwekezaji huyu alipokuwa akitumia fedha za Watanzania Kulipia gharama za kutafuta mafuta na gesi katika nchi za Gabon, Uganda na Nigeria. Aidha, amekuwa akilipwa gharama za kusafirisha gesi kutoka kwa Makampuni mawili tofauti ya *Songas* na *TPDC* kwa kusafirisha kiasi hicho hicho cha gesi. Kamati inaona udanganyifu huu ni wa makusudi kwa kuwa umekuwa ukijirudia kwa namna ile ile kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2004 hadi 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka Kamati inakamilisha taarifa hii ilielezwa kwa barua yenye kumb. Na *CDA.90/159/01* ya tarehe 20 Oktoba, 2011 kutoka *TPDC* kuwa *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* walikuwa wamewasilisha vielelezo vya kiasi cha dola za Kimarekani 1,042,516. Katika kiasi hicho wamethibitisha kuwa dola za Kimarekani 746,153 ni gharama sahihi za mradi na kiasi kingine cha dola za Kimarekani 296,363 zimegundulika na wamekubali kuwa ziliingizwa kwenye gharama za mradi kimakosa na kinyume cha Mkataba.

(b) *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* wamekiuka taratibu za kisheria za kodi kama vile kutokata kodi ya zuio (*with holding tax*) kwa mapato ya Kampuni ya nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pamoja na uthibitisho wa ukaguzi wa *TPDC* uliounesha Kampuni zaidi ya nne ambazo malipo yao hayakukatwa kodi ya zuio, Kumbukumbu za *TRA* zimemuunesha *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* kama mlipaji wa kodi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa za taasisi hizi mbili zinaonesha kuwa kuna uwezekano wa Kampuni kuonekana inalipa kodi wakati kuna baadhi ya kodi haizilipi kwa makusudi au kwa kutokujua.

(c) Maofisa Wakuu wa *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* walajiriwa kama wataalam elekezi kwa nyakati tofauti na kulipwa ujira wa shughuli wanazofanya wakati pia wanalipwa mishahara mikubwa kwa kufanya kazi zao za kawaida (*double payment*).

(d) *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* wamekuwa na utaratibu wa kuchanganya mahesabu ya masuala ya *upstream* na *downstream* pamoja ili waweze kurejeshewa gharama zao katika utaratibu wa *PSA* kwa upande wa *upstream*.

(e) *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* wamekuwa na tabia ya kutotunza taarifa au nyaraka za mahesabu yake ya uhasibu kinyume na taratibu za Mkataba wa *PSA* (Ibara 21.1).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ulipaji wa kodi ya mapato na mrabaha. Kamati ilielezwa kuwa, jukumu la kulipa kodi na mrabaha lipo chini ya *TPDC* na analipa kutoka katika faida yake ya mgawo wa mapato ya gesi (*profit gas*) kulingana na kiwango kilichowekwa na Serikali. Sheria ya kodi nchini inataka kila upande ambaao ni wabia kulipa kodi yake yenye, hali hii ni tofauti kwa *TPDC* na *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)*. Mfumo wa mkataba uliopo, *TPDC* analipia kodi ya mapato *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)*. Mfumo huu uliwekwa toka awali ili kusaidia makampuni ya kigeni yasikwepe kodi na hivyo Serikali kuwa na uhakika wa mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ilitolewa kuwa *PSA* kati ya *TPDC* na *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* ni tofauti na *PSA* nyingine kwa kuwa *TPDC* mgawo wake (*profit gas*) unashuka kadiri uzalishaji unavyoongeza. Kamati ilielezwa kuwa mrabaha na kodi za *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* hulipwa na *TPDC* kutoka katika sehemu ya mapato ya *TPDC*. Ni dhahiri kuwa kwa utaratibu huu kuna kipindi *TPDC* na kwa maana hiyo Serikali ya Tanzania itakuwa haipati chochote katika gesi inayozalishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipokea mapendekezo kutoka *TPDC* kuwa kiwango cha mrabaha kilipwe kutockana na mapato ya jumla kabla mgawo haujafanyika kwani kwa ilivyo sasa, mrabaha huu unatolewa katika mgawo wa *TPDC* na hivyo kulikosesha Taifa mrabaha stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TPDC* kuomba kuongezewa watumishi (Kiambatisho Na.8). Kamati ilifahamishwa kuwa *TPDC* kwa vipindi tofauti ilituma barua kwenda Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kuomba kuongezewa idadi ya watumishi wa kada tofauti tofauti ili kuongeza nguvu ya ufanyaji kazi hasa katika ufuatilaji na usimamizi wa utafutaji na uzalishaji wa mafuta na gesi. Serikali kupitia Menejimenti ya Utumishi wa Umma mara kwa mara ilikataa kutoa kibali cha ajira kwa *TPDC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imedhihirishiwa kuwa Serikali haikuzingatia kuwa *TPDC* inahitaji kuongezewa wafanyakazi kwa kuwa shughuli za utafutaji wa mafuta zilliongezeka na pia Shirika lina mikataba ya *PSA* zaidi ya 20, ugunduzi wa gesi asili katika maeneo mengi tofauti; yote haya yanahitaji watu wa kutosha katika kutekeleza majukumu yake. Maombi ya ajira kwa mwaka 2008/2009 yalikuwa ya watu 29, kibali kilichopatikana au kutolewa ni ajira ya watu sita tu. Aidha, ilielezwa kuwa Serikali haikutilia maanani maombi ya awali ya *TPDC* kupewa kibali cha kuajiri pamoja na kwamba walielezwu kuwa katika kipindi cha miaka mitano ijayo kwa wakati huo, wafanyakazi wataalam zaidi ya 20 watakuwa wamestaifu na hili litakuwa janga kubwa kwa Shirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu msimamo wa *TPDC* kuhusu gharama zisizo halali iliyojirudishia *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* (Kiambatisho Na. 9). Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (*TPDC*) ndiye msimamizi mkuu wa Sekta ya Gesi kwa niaba ya Serikali. Kutokana na kitendo cha *Pan African energy Tanzania Limited (PAT)* kuinyima Serikali gawiwo lake inalostahili kwa kujirudishia gharama za uzalishaji gesi ambazo hakustahili kinyume na taratibu za mkataba, *TPDC* imetoea msimamo ufuatao:-

(a) Mahusiano kati ya *TPDC* na *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* ni ya kimkataba na kwa msingi huu kila upande unao wajibu na haki ya Mkataba (*PSA*). *PAT* chini ya Ibara 24.4 anapaswa kufuata sheria zote za Tanzania.

(b) Kitendo cha *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* kujirejeshea au kuchukua gharama ambazo hakustahili na hatimaye kuisababishia Serikali na *TPDC* hasara ni uzembe wa hali ya juu (*gross negligence*) na ni uvunjifu wa sheria za nchi.

(c) Kitendo cha *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* kutotunza taarifa au nyaraka za mahesabu yake ya uhasibu ni uvunjifu wa Ibara ya 21.12 ya *PSA*.

(d) Kama Serikali ikikubali kusubiri nyongeza ya mgao wake miaka ijayo kama wanavyotaka *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* na sio kuongezewa mgao wake kila mwaka kosa lilipofanyika, basi msimamo huo utakuwa kichocheo kwa wawekezaji kuwa wazembe au walegevu katika kudhibiti gharama. Pia wanaweza kubambikiza gharama za makusudi. Hapa ifahamike kuwa Serikali kupitia msimamizi wake *TPDC* haitagundua gharama zisizokubalika na mwekezaji atanufaika isivyostahili na Serikali itapunjika katika kipindi chote cha Mkataba.

(e) *TPDC* inataka kuhakikisha kuwa njia au namna ya kurekebisha gharama zilizokataliwa isiwe tegemezi au isitegemee kiasi cha gharama za mwaka ule ambako kosa lilitokea na ufumbuzi na namna ya kurekebisha usibadilike mwaka hadi mwaka kama ambavyo *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* wanataka.

(f) Marekebisho ya kurudisha fedha iliyojirejeshea *Pan African energy Tanzania Limited (PAT)* yasivunje na kukiuka misingi inayofanya *PSA*. Hii ina maana kuwa:-

(i) *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* wanasema kuna gharama zisizokubalika mwaka wowote ule ambako tayari mgao wa mapato umefanyika, basi marekebisho yafanywe kwenye gharama zilizobaki ambazo zitarudishwa miaka ifuatayo. Kwa mfano, wanataka gharama zilizokataliwa mwaka 2005, zirekebishwe mwaka 2011. Hata hivyo, gharama zisizorudishwa kwa kipindi chote mpaka 2011 ni kubwa kuliko mapato ya mwaka 2011, kwa mantiki hii Serikali haitaambulia kitu na *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* ataendelea kunufaika mpaka hapo mapato yatakapokuwa mengi kuliko gharama.

(ii) *TPDC* inasema kuwa kama kuna gharama zilizokataliwa mwaka wowote ule, basi marekebisho yafanywe mwaka ule ule kwenye gharama za mwekezaji *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* alizodai kurudishwa na akarudishiwa. Hii itapunguza kiasi cha gharama zilizorudishwa mwaka ule na kuongeza mgao wa gesi (*profit gas*) kwa mwaka husika.

(g) Misingi ya *PSA* ni kuwa mwekezaji atumie fedha zake kwanza kabla ya kurudishiwa, kwa hoja ya *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* wanajijengea misingi ya kuwa na hali ya kurudishiwa gharama kabla ya kutumia au kuwekeza hivyo watakiuka misingi ya Mkataba wa *PSA* walioingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa kutoka katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, (Kiambatisho Na. 10). Katika kutekeleza kazi hii kwa umakini mkubwa, Kamati Ndogo ya Nishati na Madini iliomba kupatiwa Mtaalam wa masuala ya sheria kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ili kuititia na kuangalia maudhui ya Mkataba ya Mradi wa Songosongo iliyofungwa kati ya *TPDC* kwa niaba ya Serikali, Songosongo Tanzania Limited na *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* na kutoa maoni yake kuhusu mikataba hiyo. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliwasilisha maoni yake mbele ya Kamati kwa Barua yenye Kumb. Na. JC/N.10/1/83. Hata hivyo, Kamati imeelewa nafasi ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu katika kuwasilisha maoni yao mbele ya Kamati kwa kutoa utangulizi wa KANUSHO (*Disclaimer*) kuwa, nanukuu:-

"Maoni haya yametolewa yakiwa na dhumuni moja tu la kuisaidia Kamati Ndogo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini iliyoundwa kwa dhumuni la kuititia na kufuatilia uendeshaji wa sekta Ndogo ya Gesi na mchakato wa uendelezaji wa Gesi nchini kutathmini Mikataba ya Mradi wa songosongo. Maoni haya yasichukuliwe kuwa ni ushauri au msimamo wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania'

Maoni haya yametolewa yakizingatia kwamba pande zote zilizohusika zikiwakilishwa katika kujadili Mikataba na pia wakati wa mazungumzo ya Mikataba ya Mradi huu wa Songosongo.

Kwa ufahamu tulionao, tunaelewa kuwa Mikataba hii ilikuwa ni Mikataba ya kwanza kujadiliwa na kufungwa katika nchi yetu na kwamba katika majadiliano hayo ya Mikataba kila upande ulijadili kwa nia njema wakiwa na imani kuwa kila upande uliohusika kwenye majadiliano haukuwa na nia ya kudanganya upande mwingine.

'Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali haitowajibika na ukamilifu, ukweli au uhakika wa habari au maoni yoyote yaliyotolewa humu". Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msimamo huu uliotolewa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, ambayo kimsingi ndiyo kimbilio la Serikali pale masuala ya kisheria yenye utata yanapojoitokeza yanayoathiri maslahi ya Taifa. Kamati hii haijaandika maoni yoyote kama taarifa kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuwa Ofisi hii ni mdau Mkuu katika uandaaji wa Mikataba na ni dhahiri kuwa katika hitimisho la suala hili na yeze atatoa taarifa kama mhusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu taarifa kutoka kwa wadau mbalimbali wa gesi. Kamati ilipata fursa ya kukutana na wadau mbalimbali wa gesi. Mdaa mmojawapo aliwahi kufanya kazi

na Kampuni ya *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* ambaye alieleza kuhusu shughuli kuu za gesi ambazo ni utafutaji na usambazaji kama ambavyo zimeshaelezwa awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mdau huyo alieleza kuwa katika kipindi ambacho alikuwa mtumishi wa *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* aliona upungufu mwingu wa kiutendaji ambao ulikuwa unafanywa na Kampuni hiyo kinyume cha taratibu na alijaribu mara kwa mara kushauri ili taratibu zifuatwe na kueleza kuwa matendo hayo ambayo ni kinyume na taratibu siyo mazuri na yanawenza kuifikisha Kampuni pabaya lakini hakusikilizwa na alionekana mbaya hali iliyopelekea aache kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mdau alieleza Kamati kuwa, akiwa mwajiriwa wa *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* iliunda timu ya wataalam (*Technical Team*) ili kuweza kufuatilia upungufu mbalimbali unaojitokeza kati ya *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* na *TPDC* hasa katika maeneo yafuatayo:-

(a) Utaratibu wa kutoa zabuni ambao haukuwa wazi na shindani kwani mara zote *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* imekuwa ikitoa zabuni kwa Kampuni moja ijlukanayo kama Lootah BC Gas kinyume na taratibu.

(b) Kinyume na matakwa ya Mkataba, gharama za vifaa vya ujenzi vilikuwa vinanunuliwa na *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* bila kuwajulisha *TPDC* ili kujiridhisha kama gharama hizo zipo sawa.

(c) Kinyume na matakwa ya mkataba, *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* wamekuwa na tabia ya kuzidisha (*inflate*) gharama za uendeshaji ili kujrudishia zaidi na kupunguza gawiwo kwa Serikali au *TPDC*.

(d) Katika kuhakikisha nchi inanufaika na rasilimali tuliyonayo, *TPDC* katika miradi ya gesi kama ule wa kuhamasisha matumizi ya gesi, iliona kipaumbele kiwe kwa taasisi za umma kama JKT, Magereza na taasisi nyingine, lakini *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* walikataa na hivyo kwenda kinyume na Mipango ya nchi ya kunufaika na rasilimali hii.

(e) *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* wamekuwa wakijilipa gharama za kutafuta masoko wakati masoko hayo yalikuwa tayari yapo na yalikwisha tafutwa na *TPDC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mdau alieleza kuwa upungufu hayo wote umekuwa ukifanywa na *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* kwa makusudi kwani walikuwa wanajua wanachofanya. Aidha, alieleza mahusiano ya wadau wa sekti ya gesi hususan *TPDC* na *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* kuwa siyo mazuri kwani *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* siyo mwekezaji mwaminifu na hivyo ipo haja kwa Serikali kufanya tathmini ya kina (*Due Diligence*) kabla ya kuingia mkataba na wawekezaji. Pia alisitiza ipo haja ya kupitia upya Mikataba yetu ili kuhakikisha nchi inanufaika zaidi tofauti na ilivyo sasa kwani Mkataba wa Songsongo una upungufu mwingu ambao unahitaji kuangaliwa na vilevile mkataba huo haupo wazi pale mwekezaji anaporudisha gharama zake za uwekezaji nani atamiliiki rasilimali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu taarifa kutoka kwa *SONGAS*. *Songas* ni mionganoni mwa wadau wakuu katika mradi wa Songsongo kwa maana ndiyo wallingia Mkataba na Serikali au *TPDC* ili kuzalisha umeme kwa kutumia gesi ya Songsongo mnamo mwaka 2001 na uzalishaji ulianza rasmi mwaka 2004. Kazi kubwa ya *Songas* ni kuzalisha umeme kiasi cha MW 180 ambacho wanamuuzia *TANESCO*, kuwekeza na kuendesha miundombinu ya Songsongo ili kuwezesha usafirishaji wa gesi na kuza kwa watumiaji wengine Dar es Salaam.

Miundombinu ambayo *Songas* anamiliiki inajumuisha visima vitano (vilivyokuwa vya Serikali au *TPDC*), mtambo wa kusafisha gesi wenye uwezo wa kusafisha futi za ujazo milioni 105 kwa siku ambao unaendeshwa na *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* na bomba la kusafirisha gesi lenye uwezo wa kusafirisha gesi kiasi cha futi za ujazo milioni 105 kwa siku lenye urefu wa Kilomita 225 kutoka Songsongo hadi Dar es Salaam ambalo linamiliikiwa na kuendeshwa na *Songas*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Songas* walieleza kuwa mahitaji ya gesi nchini yamekuwa yakiongezeka kutokana na ukweli kwamba nishati hii ni nafuu na pia ni rafiki wa mazingira na hivyo kufanya kiasi cha gesi kinachofika Dar es Salaam kutotosheleza mahitaji. Kutokana na hali hii *Songas* imeona haja ya kuboresha miundombinu kwa maana ya mitambo ya kusafisha na bomba la kusafirisha na ndio maana mara kwa mara imekuwa ikifanya upanuzi ili kuongeza uwezo (*re-rating*) ambao kwa sasa umefikia kikomo na hivyo kuwepo kwa ulazima wa kujenga bomba lingine na mtambo wa kusafisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Songas* walieleza kuwa mahusiano yao na wadau wengine ni mazuri na wamekuwa wakishirikiana vizuri. Aidha, Kamati ilipotaka kujua kuhusu nani anahusika na uzembe uliosababisha visima kuharabika (*corrosion*) kwa maana ya kutofanya ukaguzi kwa mujibu wa *Gas Agreement*. *Songas* walieleza kuwa kwanza jukumu hilo sio masharti ya kimkataba bali ni ushauri tu, lakini pia kwa kuwa anayeendesha (*operate*) visima hivyo ni *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* na *TPDC* basi hao ndio wanapaswa kuhusika na kubeba gharama za ukarabati wa visima hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Songas* walipouliwza wanasemaje kuwa *Additional Gas production inaweza* kuwa ni mojawapo ya sababu iliyosababisha visima kuharibika kutokana na visima kuzalisha zaidi ya uwezo wake wa kawaida, wadau hawa walisema kuwa hiyo pia inawezekana kuwa moja ya sababu kuu za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kuona kuwa kinyume cha taratibu na tamaduni za mikataba mtu ambaye tumempa dhamana kubwa ya kusimamia rasilimali hii muhimu anakataa kubeba jukumu lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ziara ya Songosongo. Kamati ilipata fursa ya kutembelea Mradi wa Songosongo. Katika ziara hiyo Kamati iliona visima vitano vya gesi ambavyo imekabidhiwa Kampuni ya *Songas* pamoja na mtambo unaotumika kusafisha gesi. Aidha, Kamati iliona kisima kipyä kilichochimbwa *SS10* ambacho gesi yake inapitishwa kwenye bomba la kisima namba nne ili kuweza kufika katika mtambo wa kusafisha gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia iliona mtambo wa kuzalisha umeme wenye jumla ya mashine tatu ambao unazalisha umeme kiasi cha *MW 0.6* kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya mradi na wananchi wa Songosongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ililezwa kuwa wafanyakazi wa mradi ambao wameajiriwa na Kampuni ya *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* kwa kazi za kitaalam wapo 34 na wanasihamiwa na wazungu wawili. Wafanyakazi hawa wamejigawa katika makundi mawili na wanafanya kazi kwa wiki nne na kupumzika wiki nne kwa kubadilishana. Aidha, kuna wafanyakazi wengine wapatao 90 ambao wanatoka katika Kijiji cha Songosongo wengi wao wakiwa wapishi na walini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ilipata nafasi ya kuongea na watendaji wa Kijiji cha Songosongo ambao walieleza mahusiano yao na wawekezaji siyo mabaya isipokuwa hali ya usalama siyo ya kuridhisha kutokana na kukosekana kwa Kituo cha Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ilipata fursa ya kuona kisima cha Kampuni ya Ndovu Resources ambacho kinategemewa kuunganishwa katika mtambo wa kusafisha gesi wa *Songas* ifikapo Machi, 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu taarifa kutoka *TANESCO*. *TANESCO* ambalo ni Shirika la Ugavi wa Umeme nchini lina Mkataba na wadau mbalimbali wa gesi nchini wakiwemo *SONGAS*, *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* na *TPDC*. *TANESCO* na *Songas* wana Mkataba wa Ununuzi wa Umeme (*Power Purchase Agreement*) kiasi cha *MW 178* ambao unatokana na gesi asili ya Songosongo. Katika Mkataba huo, *TANESCO* anawajibika kumlipa *Songas* kutokana na umeme anaoupata. Hata hivyo, *TANESCO* ilieleza kuwepo kwa changamoto za kimkataba ambazo wanakabiliana nazo:-

(a) Muda wa kufanya matengenezo ya kinga (*Service*) kwenye mitambo kuwa ni mrefu sana na hivyo kutoa mwanya mkubwa kwa *Songas* kutowajibishwa hasa pale mitambo inaposhindwa kufanya kazi.

(b) Gharama anazoingia *Songas* za kuwekeza na kuendesha mitambo hupitishwa moja kwa moja kwenye *tarif* hivyo *Songas* hana changamoto ya kupunguza gharama zake.

(c) Bei ya umeme ambayo *TANESCO* ananunua kwa *Songas* ni Tsh 111/Kwh wakati *TANESCO* anauza kwa Tsh.141/Kwh, faida ya Tsh 30/Kwh haikidhi gharama za usafirishaji, usambazaji na upotetu wa umeme na hivyo *TANESCO* kushindwa kujidoresha.

(d) Pamoja na *Songas* kuhakikishiwa kulipwa gharama zote, baada ya miaka 20 mitambo hiyo inabaki kwake. Hakuna mkataba wa *Build and Operate Transfer*.

(e) *Songas* amepewa nafasi ya kupitia upya gharama anazotumia na ikionekana zimezidi asilimia kumi kulinganisha na gharama zilizokadiriwa kimkataba, *Songas* anaruhusiwa kupandisha bei na hivyo kuongeza gharama kwa *TANESCO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)*, *TANESCO* walieleza kuwa mahusiano baina yao siyo ya kuridhisha kwani kuna changamoto za kimkataba kama ilivyokuwa kwa *Songas*, changamoto zilizoanishwa ni:-

(a) *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* anashindwa kutoa ushirikiano na kukwepa adhabu pale inapotokea hitilafu na hivyo kutupiana mpira na *Songas*. Hii inatokana na ukweli kwamba *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* ni mwendeshaji na siyo mmiliki.

(b) *TANESCO* akiwa ndiye mtumiaji mkubwa wa gesi, hana nafasi ya kujua mfumo wa usafirishaji (kiasi na kasi ya gesi) hasa pale linapotokea tatizo la upatikanaji wa gesi ya kutosha kwani inawezekana *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)/SONGAS* wakawa wanauzu gesi nyingi kwa viwanda na hivyo kusababisha wao kupata kiasi kidogo ikilinganishwa na mahitaji.

(c) *TANESCO* ilichangia kiasi cha dola laki nne (\$400, 000) ili kuongeza uwezo wa mitambo ya kusafisha gesi kutoka futi za ujazo milioni 70 kwa siku hadi 110, lakini mategemeo ya *TANESCO* kupata gesi ya kutosha hayajafikiwa kutokana na kiwango kidogo kilichoongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa kutoka *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)*. *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* ni Kampuni ambayo kwa mujibu wa Mkataba wa gesi Kifungu cha 2.2 (a) imepewa jukumu la kufanya shughuli za utafiti, uendelezaji kwenye eneo la gesi ya Songsongo na kwa kushirikiana na *TPDC* kuuza gesi ya ziada na kufanya operesheni na kazi nyinginezo kwenye eneo la gesi ya Songsongo kulingana na matakwa ya vipengele vya Mkataba wa gesi na *PSA*. Kwa sasa *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* ndiye msafirishaji na msambazaji mkuu wa gesi nchini. Kwa kushirikiana na *TPDC* wanauzu gesi ya ziada (*Additional gas*) na wanagawana gawio mara baada ya *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* kutoa gharama zake za uzalishaji ambazo ameingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* katika maeleo yao walidai kwamba katika kipindi chote ambacho wamefanya kazi na *TPDC* wamekuwa wakiwasilisha kila mwezi nyaraka zinazoonesha gharama walizotumia na hivyo wamekuwa wazi katika kufanya kazi na *TPDC*. Pamoja na *PSA* kumpa haki *TPDC* kukagua hesabu za kila mwaka za *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* ndani ya miaka miili baada ya mwaka husika, pamoja na *TPDC* kukaa muda mrefu bila kufanya ukaguzi huo, *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* walitoa ushirikiano na kuhakikisha ukaguzi huo unafanyika. Aidha, tangu awali wamekuwa tayari kufanya marekebisho pale inapojoitokeza wahasibu wao kuchanganya gharama na kuandaa ripoti ya gharama za uendeshaji. Pamoja na hayo, *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* wamekuwa wakiwahimiza *TPDC* kuhakikisha wanafanya ukaguzi kama inavyotakiwa na *PSA* kwani ndiyo msingi wa kuhakikisha kunakuwepo uwazi na kujenga imani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa maelezo ya *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* walieleza kuwa, kiasi cha dola za Kimarekani 28,053,680 walizilingiza kimakosa kwenye gharama za uendeshaji. Aidha, walieleza kuwa kama *TPDC* wangefanya ukaguzi mapema kama inavyopaswa kwenye *PSA* basi kuna uwezekano gharama hizi zilizorudishwa kimakosa zingekuwa kidogo kwani zingegundulika mapema. *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* walikubali kuziondoa gharama hizo kwenye *Cost Pool* baada ya ukaguzi wa *TPDC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa maelezo ya wataalam wa *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)*, wanasma kwamba, *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* haidaiwi na *TPDC* fedha zozote kwani katika gharama za uendeshaji ambazo *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* imeingia kiasi cha dola za Kimarekani milioni 133, *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* tayari imeshajirudisha dola za Kimarekani milioni 80, hivyo bado bakaa ya dola za Kimarekani milioni 53. Aidha, *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* inakubali dola za Kimarekani milioni 28 ambazo zimeingizwa kimakosa zitolewe kwenye *cost pool* na wabaki wanadai dola za Kimarekani milioni 25.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* walieleza kuwa gharama hizo zinazofikia dola za Kimarekani milioni 28.1 ziliingizwa kimakosa kwenye mkataba wa uzalishaji na ugawanaji mapato (*PSA*) na hawakuwa na nia yoyote mbaya. Aidha, kiasi cha dola za Kimarekani milioni 36 ambazo *TPDC* wanadai kuwa nazo zimeingizwa kimakosa kwenye *PSA*, *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* inaendelea kufanya kazi ikiwemo kutoa ufanuzi na kuwasilisha nyaraka kwa wakaguzi wa *TPDC* ila *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* inaamini gharama hizo ni halali kuingia kwenye *PSA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha makosa yaliyojiteza hayatokei tena, *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* walieleza baadhi ya hatua ambazo wameanza kuchukua kuwa ni pamoja na:-

- (a) Kuimarisha Idara ya Uhasibu kwa kuajiri Meneja wa Fedha na Mhasibu Mwandamizi na watumishi wengine wenye uwezo na uzoefu.
- (b) Kuomba kupatiwa ankara za manunuzi ya huduma na bidhaa (*Invoice*) zenye maelezo ya kina kutoka kwa wakandarasi wanaofanya nao kazi.
- (c) *Logistic team* imeboreshwa ili kuweza kutoa huduma bora na kutunza kumbukumbu.
- (d) Mfanyakazi Mtanzania amechaguliwa kuwa Meneja Mkuu Msaidizi na moja ya jukumu lake ni kuhakikisha *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* inakuwa na mahusiano mazuri na wadau kwa kutimiza wajibu wake kwa mujibu wa *PSA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipotaka kujua *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* anaionaje *PSA* baina yake na Serikali au *TPDC*, jibu lilikuwa la kustaajabisha kwani walisema *PSA* wanaifurahia na ni sawa na Biblia, hivyo haiwezi kubadilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaamini kwamba *PSA* hii haizingatii maslahi ya Taifa. Aidha, *TPDC* imenesha wazi kutoridhishwa na Mkataba huu na hivyo ipo haja ya kuufanya marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu taarifa kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (*EWURA*) (Kiambatisho Na. 13). Tarehe 28 Septemba 2011, Watendaji wa *EWURA* walikutana na Kamati Ndogo ya Bunge ya Nishati na Madini kutoa ufanuzi kuhusu masuala mbalimbali katika tasnia ya gesi asilia nchini. Tarehe 30 Septemba, 2011, ufanuzi na nyaraka mbalimbali (katika vitabu kumi) ziliwasilishwa kwenye Kamati. Ufuatao ni muhtasari wa yaliyowasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upanuzi wa Bomba. *EWURA* akiwa Mdhibiti wa Nishati na Maji, moja ya jukumu lake ni kukokotoa bei ya gesi nchini. Kwa mujibu wa Taarifa ya *EWURA*, mahitaji ya kupanua miundombinu ya gesi yalijulikana na Serikali tangu mwaka 2000 hata kabla majadiliano

yake na *Songas* kuhusu Mradi wa Songosongo hayajakamilika. Serikali ilipendekeza Bomba la gesi kutoka Songosongo hadi Somanga fungu liwe la kipenyo cha inchi 18 badala ya 10 na kutoka Somangafungu hadi Dar es Salaam liwe la kipenyo cha inchi 16 badala ya 12 kama ilivyopendekezwa na *Songas*. Nia ya Serikali ilikuwa kutumia mtaji wa mkopo ambao ulikuwa ni asilimia 75 na masharti nafuu lakini pia kutokufanya upanuzi wa mara kwa mara na hivyo kupunguza usumbuwa wa viumbe vyaa bahari ambao wapo sehemu ya Hifadhi ya Bahari (*Marine Park*) na wanalindwa na Mikataba ya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *EWURA* walieleza kuwa *Songas* na *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* waliamua kipenyo kidogo kwa makusudi ili baadaye wakati wa upanuzi wa bomba wawekeze kwa kutumia mtaji wa mmoja wa wawekezaji binafsi katika *Songas au GlobeEq* kwa asilimia mia moja ili waje walipwe kwa riba ya asilimia 22 ikilinganishwa na ile ambayo Serikali imepata kutoka Benki ya Dunia ya asilimia 0.75. Mkakati wa *GlobeEq* umekuwa ni kuongeza uwekezaji katika *Songas* kwa kutumia utaratibu wa kupanua miundombinu kwa kutumia fedha za *GlobeEq* pekee jambo ambalo halina maslahi kwa Taifa. Hata hivyo, baada ya mabishano ya kina *Songas* na *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* waliamriwa na Benki ya Dunia kuwa kipenyo cha bomba la baharini kuwa inchi 12 na inchi 16 nchi kavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa *Songas* na *Artumas Group*. *EWURA* ilikanusha habari zilizosambazwa na baadhi ya wadau wa sekta ya Gesi ikiwemo Wizara ya Nishati na Madini kuwa kuchelewa kutekelezwa kwa Mradi wa Miundombinu ya Gesi Asili (Mradi), uliopangwa kutekelezwa na Kampuni ya *Songas* tangu mwaka 2006 ulisababishwa na urasimu wa *EWURA*. Kwa mujibu wa kumbukumbu zilizowasilishwa kwenye Kamati *EWURA* ilieleza kuwa:-

(a) Katika kipindi chote, *EWURA* ilitoa ushirikiano wa dhati kwa Kampuni ya *Songas*, kwa kutambua kwamba gesi asili ni mkombozi wa haraka wa uchumi wa Tanzania endapo itatumika kuzalisha umeme. Kwa kawaida (*industry best practices*) maamuzi ya kudumu miaka mingi (zaidi ya mitano) na fedha nyingi za kigeni huchukua takriban siku 180. Mwaka 2007, *EWURA* ilitumia siku 120 kutoa uamuzi, mwaka 2009 ilitumia siku 84 na mwaka 2011 ilitumia siku 105. Kwa nyakati zote hizo, *Songas* iliomba *EWURA* iongeze muda wa mchakato ili maamuzi ya *EWURA* yazingatia matakwa yao;

(b) Kila mara, Kampuni ya *Songas* imekuwa ikibadili kauli zake kuhusu gharama, upeo na faida inayotarajiwa kutoka kwenye Mradi. Gharama za kununulia mitambo (*gas processing plant*) haikuongezeka sana zaidi ya kutoka Can \$ 7.5 milioni hadi Can\$ 10 milioni katika kipindi hicho. Gharama za usimamizi hazikutarajiwa kubadilikabadi, bali gharama za mkataba wa ujenzi (*Engineering, Procurement and Construction (EPC) Contract*) zilongezeka kutoka US\$ 16 milioni (mwezi Desemba 2006) hadi US\$ 36 millioni (mwezi Aprili 2007) baada ya *EWURA* kutoa uamuzi. Taratibu za manunuzi nazo zilitia mashaka makubwa kwani hazikuwa za ushindani wa wazi;

(c) Kampuni ya *Songas* ilitaka kutumia fedha zake (*equity funding*) badala ya mikopo ya benki kwa riba na faida kubwa kwenye mitaji kati ya 16% na 22% ikilinganishwa na 10% hadi 15% kwa miradi inayofanana na hiyo barani Afrika. Huko Ulaya, Asia na Australia, riba na faida kwenye mitaji ni 4.5% hadi 9.5%. Katika mazingira ya vita (*DRC, Somalia, Sudan Kusini, Afghanistan*) riba na faida kubwa zaidi ya 25% hutolewa. Kwa kawaida, mikopo yenye masharti nafuu kwenye miradi ya miundombinu ya muda mrefu haipungui asilimia 60 ya mtaji wote;

(d) Kampuni ya *Songas* ilihaha na kutapatapa kukwepa udhibiti kwa kujaribu kubadili mikataba ya mradi iliyoingiwa kabla *EWURA* hajaanzishwa. Kama haitoshi, *Songas* walijaribu kufungua shauri kwenye Baraza la Ushindani Huru (*Fair Competition Tribunal*) na kurubuni Wizara na *TANESCO* waitetee *Songas* dhidi ya maamuzi ya *EWURA*. Haikuishia hapo, Kampuni ya *Songas* ilijaribu kumtumia Waziri wa Nishati na Madini hata Waziri Mkuu kutengua maamuzi ya *EWURA*. Hata hivyo, Waziri mwenye dhamana juu ya *EWURA* (Waziri wa Maji) (Kiambatisho Na. 14) alipinga vikali njama za Kampuni ya *Songas*. Njama za Kampuni ya *Songas* kujaribu kukwepa udhibiti zilikemewa na kuzimwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu (Kiambatisho Na. 15) mwezi Mei 2009;

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapongeza msimamo wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji na Waziri Mkuu katika kusimamia maslahi ya Taifa.

(e) Ni jambo la kawaida kabisa, Asasi mpya ya Kiserikali inapoanzishwa kwa malengo maalum au kutungwa kwa sheria mpya kudhibiti jambo fulani, wazoefu wa mifumo ya zamani hutunisha misuli kwa kukaidi au kujaribu kuona kitakachotendeka kama mifumo na mamlaka zipo. Sheria mpya na taratibu mpya sharti zijaribiwe ili kuona kama zinafanya kazi. Aidha, kwa wafanyabiashara wasio waaminifu, ni jambo la kawaida kutengeneza mazingira ya upungufu wa mali au huduma (*demand and supply*) ili kupandisha bei za vitu au huduma. Wakati mwiningine ni kutokuwa na elimu ya udhibiti au kudharau mifumo na taratibu zilizopo. Kampuni ya *Songas* inaweza kuwa ilisukumwa na mojawapo kati ya yaliyotajwa; na

(f) Pamoja na kujaribu kuyumbisha Serikali na *EWURA*, uamuzi wa *EWURA* wa mwezi Aprili 2011 (unaokubalika leo kwa Kampuni ya *Songas*) haukuiongezea hata chembe ya maslahi Kampuni ya *Songas*. Badala yake, uamuzi wa *EWURA* unaibana zaidi *Songas* kuliko ilivyokuwa katika maamuzi ya mwaka 2007 na mwaka 2009. Kwa maneno mengine, Kampuni ya *Songas* illipotezea muda Taifa kiasi cha kujikuta linashuhudia upungufu katika ugavi wa gesi asili kwa mahitaji ya kuzalisha umeme kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *EWURA* walieleza kwamba, uvumi uliotajwa kuhusu kuchelewa kwa Mradi wa *Songas* ulisambazwa tena na wadau wa sekta ya Gesi ndani ya Serikali kuwa msaada wa *ORET* (€22 milioni) wa kutekeleza Mradi wa Umeme Vijijiini kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara ulifutwa kutoana na *EWURA* kuchelewa kutoa leseni na uamuzi kuhusu bei za umeme. Kumbukumbu zilizohifadhiwa *EWURA* kutoka *FMO* na *ORET* (za mwezi Februari na Juni 2010) zinathibitisha kuwa, *EWURA* ilitimiza wajibu wake kwa wakati, bali ahadi za Serikali na Kampuni ya *Artumas Group* hazikutekelezwa kwa wakati. Yafuatayo ni mazingira yaliyosababisha msaada wa *ORET* kufutwa:-

(a) Serikali illingia Mikataba na Kampuni ya *Artumas Group* tarehe 12 Desemba 2008, miezi mitatu na nusu kabla Sheria ya Umeme 2008 haijaanza kutumika tarehe 1 Aprili 2009. Sheria hiyo (kifungu cha 41(7) cha Sheria ya Umeme, 2008) ilizua yeyote aliyeingia mikataba na Serikali kabla ya Sheria ya Umeme 2008 haijaanza kutumika asipewe leseni. Kwa hili, Serikali ilitenda kosa hilo ikijua kwani ndiyo iliyokuwa na dhamana ya kutangaza tarehe ya Sheria hiyo kuanza kutumika. Vifungu kadhaa vilifutwa na Bunge la Tisa mwaka 2010;

(b) Kampuni ya *Artumas Group* ilikumbwa na m dororo wa uchumi duniani kuanzia mwezi Oktoba 2008, hali iliyodumu hadi mwezi Oktoba 2010, kampuni hiyo ilifilisika rasmi na kununuliwa na Kampuni ya *Wentworth*. Kwa sababu hiyo, Kampuni ya *Artumas Group* ilikosa sifa ya kukopeshwa na *FMO* fedha (US\$ 35 millioni) za kutekeleza Mradi wa Umeme Vijijiini. Ili msaada wa *ORET* utolewe, sharti mojawapo ilikuwa kwamba taratibu za kupata fedha za mkopo kwa Kampuni ya *Artumas Group* zikamilike;

(c) Miundombinu ya umeme iliyomilikiwa na *TANESCO* katika Mikoa ya Lindi na Mtwara ilibidi ihamishiwe na kuendeshwa na Kampuni ya *Artumas Group*, jambo ambalo ililoishinda Kampuni ya *Artumas Group* licha ya *TANESCO* kuwa tayari kujiondoa katika Mikoa ya Lindi na Mtwara kwa dhati kabisa;

(d) Kama ilivyo kwa Kampuni ya *Songas*, Kampuni ya *Artumas Group* illiamini kuwa kwa kuwa Mikataba ilifungwa na Serikali, hivyo pasinetokea asasi yoyote kuhoji uhalali wa masuala yaliyofungwa na mikataba. Licha ya kutokubali kurekebisha dosari kwa hiari tangu mwezi Agosti 2008 hadi Mei 2010, Kampuni ya *Artumas Group* ilidharau pia taratibu zilizokuwepo. Leo hii mikataba iliyofungwa na misaada ya leseni iliyotolewa imekufa na haitumiki; na

(e) Kwa upande wa *EWURA*, msamaha wa leseni (*exemptions*) kwa makampuni ya *Artumas Group* na Umoja *Light* zilitolewa mwezi Februari 2010 baada ya kukamilisha mchakato uliodumu kwa siku 75 tu. Mchakato wa bei za umeme ulikamilika mwezi Mei 2010 baada ya *EWURA* kulazimisha kufunga mjadala. Kuchelewa kutoa maamuzi ya bei kulitokana na Kampuni za

Artumas Group na *Umoja Light* kushindwa kuwasilisha ushahidi wa gharama za mradi na Kumbukumbu za *ORET* na *FMO* zilizopo *EWURA* zinazeleza kuwa sababu kuu ya kukosa msaada wa *ORET* ni ahadi za Serikali za kukamilisha masharti ya msaada wa *ORET* kushindwa kutimizwa kwa zaidi ya mara tatu kwa miaka mitatu, licha ya *ORET* kuongeza muda, jambo ambalo halikuwa la kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu zabuni na gharama za ujenzi. Taarifa ilitolewa kuwa, baada ya mradi kukubaliwa ilifanyika *Zabuni* ya *Kimataifa* na kwa kuwa *Songas* ilikuwa inaipendelea Kampuni ya *Webster* ilitaka ichukuliwe kwa gharama ya dola milioni 156 kwa ujenzi wa kipenyo cha awali cha inchi 10 na 12 na kwa kipenyo cha inchi 16 kilichoongezeka walikubali watatoza dola milioni 15 zaidi. Hata hivyo, walipofanya zabuni huru na shindani, Kampuni ya *Lasern & Turbo* ilishinda kwa gharama za dola milioni 100 na kukubali gharama za nyongeza ya kipenyo cha inchi 12 na 16 kuwa ni dola milioni nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ilitolewa kuwa, ukame wa mwaka 2005 ulisababisha kuwepo na miradi mingine ya dharura ambayo ilihitaji kutumia gesi ambayo isingetosha kwa kutumia bomba liliopo. Aidha, *EWURA* iliundwa kwa wakati huo na kupitia maombi ya *Songas* ya ujenzi wa bomba ambayo gharama yake ilikuwa ni dola milioni 29.8 na walipewa kibali cha kujenga tarehe 12 April 2007. Aidha, wiki mbili baadaye *Songas* waliomba kubadilisha gharama ya ujenzi kutoka dola milioni 29.8 hadi kufikia dola milioni 60 kwa madai kwamba gharama za awali hazikuwa sawa kitu ambacho *EWURA* walikataa na kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati na Madini na Mwanasheria Mkuu wa Serikali *Songas* aliamriwa atangaze zabuni tena. Kwa ujumla mashine za kusafisha gesi hazina gharama kubwa kwani zinauzwa takribani dola milioni 7. 5, gharama kubwa ipo kwenye kuanganisha hizo mashine, lakini hazifikii kiasi ambacho *Songas* alitaka cha dola milioni 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *EWURA* waliendelea kueleza kuwa *Songas* baada ya kuamriwa walileta maombi mengine tena ambayo *EWURA* waliyafanya kazi na kama zilivyo taratibu kabla *EWURA* hajapitisha bei hizo alilitisha mkutano na wadau na ili kupitia Rasimu ya Maamuzi, wadau wote waliridhika isipokuwa *Songas* ambaye alitaka apewe riba ya asilimia 17.2. Hata hivyo, *EWURA* ilitoa angalizo kwa *Songas* kwamba maeneo yafuatayo wayaangalie tena:-

- (a) Kusifanyike utaratibu ambao hauna ushindani; na
- (b) Kusifanyike vitu ambavyo vitawafanya *Songas* wafanye biashara hiyo wao peke yao millele (*monopoly*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada wa Sheria ya gesi asili nchini. *EWURA* walieleza kuwa, Sera ya Nishati ya Mwaka 2003 imesheheni kauli nzuri kuhusu misingi ya kutoa huduma za nishati (umeme, mafuta, gesi asili na nishati mbadala) pamoja na kuundwa kwa mamlaka huru ya udhibiti. Hata hivyo, Sera hii haitoi mwelekeo bayana wa kuendeleza tasnia ya gesi asili. Kwa hali hiyo basi, kuna haja ya kudurusu Sera ya Nishati, kuandaa Muswada wa gesi asili wenye kutoa majibu ya maswali magumu ya Watanzania wa leo na wa miaka 50 ijayo. Majukumu kati ya asasi moja na asasi nyingine yaainishwe bayana na kutenganishwa kwa lengo la kuleta ufanisi na kuongeza tija. Aidha, mipango mkakati na kabambe iandaliwe ili kuibua miradi ya miundombinu na mahitaji ya rasilimali. Taifa likichelewa kuweka nyenzo hizi muhimu, likaruhusu majadiliano na mikataba kuchukuwa nafasi, kipindi si kirefu yatashuhudia manun'guniko kuwa nchi imeuzwa na mivutano kati ya wananchi na wawekezaji na ya wananchi na Serikali yao itajitokeza kwa nguvu sana jambo ambalo ni vyema likaepukwa mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *EWURA* walieleza kuwa kukosekana kwa Sheria ya Gesi kumesababisha kila kitu kiwe kwenye mkataba kitu ambacho si kizuri na hivyo ipo haja ya Serikali kuharakisha mchakato wa utungwaji wa sheria ili hata utaratibu wa kupanga bei uainishwe humo. Pamoja na hayo, kutokana na tatizo liliojitokeza la *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* kujiongezea gharama za uzalishaji, *EWURA* ilisitiza wakati umefika sasa kuwa gharama anazoingia *Pan African Energy Tanzania Ltd (PAT)* zisimamiwe vyema na *TPDC* na kama *Pan African Energy Limited (PAT)* atajirudishia gharama zake zote basi miundombinu aliowekeza ibaki kuwa mali ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa maelezo ya *EWURA*, maeneo mapya yanaweza kuongezwa kwenye Muswada wa Gesi Asili na kuupatia sura pana. Hii ni pamoja na kuongeza kauli mahsus ikuhusu uwekezaji katika miundombinu ya gesi asili (*Greenfield Infrastructure Incentive Package*). Jambo hili ni muhimu kuvutia wavekezaji katika maeneo ambayo si rahisi kuyafikia katika kipindi cha miaka 20 ijayo. Tunaweza kuazima maneno mazuri kutoka kwenye Sheria ya Australia Kusini (Sura ya Tano ya Kitabu cha VIII) ili kuona kama miundombinu ya kupeleka gesi asili inajengwa kuelekea Zanzibar, Morogoro, Mbeya, Dodoma, Shinyanga, Kigoma, Mwanza na Arusha katika miaka 50 ijayo. Vile vile, viongezwe vifungu vitakavyohimiza matumizi bora ya gesi asilia (*promotion of the efficient use by consumers of gas*) na malengo ya jumla ya ufanisi wa watoa huduma (*overall energy efficiency targets*) kama ilivyo Sheria ya Miundombinu ya Gesi na Umeme (*Utilities Act 2000*) ya Uingereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu shauri la *Songas* kwenye Baraza la Ushindani wa haki. Kamati ilielezwa kuwa mwenendo wa shauri lilliofunguliwa na Kampuni ya *Songas* dhidi ya maamuzi ya *EWURA*. Kufungua shauri ni haki ya msingi ya Kampuni ya *Songas* kama hairidhiki na uamuzi. Tathmini ya jambo linalokatiwa shauri na mwenendo wa shauri ndiyo mambo ya kuzingatia katika maelezo ya *EWURA*. Baada ya *EWURA* kuyashtukia mabadiliko yaliyoandalila kufanywa kwenye Mikataba ya Mradi (11) iliyointiwa mwaka 2001, uhusiano wa kikazi kati ya watendaji wa *EWURA* na Wizara ya Nishati na Madini uliingia dosari. Kwa ufupi, masuala ambayo *EWURA* iliyasimamia ni kuona kuwa:-

(a) Mikataba haibadilishwi kuzuia udhibiti kwa Kampuni ya *Songas* au kuzuia ushindani wa wazi wa kibiashara kwa washiriki wengine. Maamuzi ya *EWURA* ambayo hayakupendwa na Kampuni ya *Songas* yalichukuliwa kuwa ni mabadiliko ya sheria (*Change in Law*) na hivyo kuishawishi kudai fidia;

(b) Mikataba haitoi haki kwa Kampuni ya *Songas* kulipwa na Serikali endapo kwa maoni ya *EWURA*, malipo hayo yamekataliwa kwa misingi ya kiudhibiti. Waziri alipewa siku kumi kupinga na kusitisha utekelezaji wa maamuzi ya *EWURA* au Serikali kulipa tofauti kati ya matarajio ya Kampuni ya *Songas* na kiasi kitakachopitishwa na *EWURA*;

(c) Mikataba haitoi mwanya kwa Kampuni ya *Songas* kukimbilia kwenye Mabaraza ya Usuluhishi nje ya nchi (*ICC* au *ICSID*) kabla juhud za ndani (kama vile Baraza la Ushindani wa Haki) hazijashindwa; na

(d) Mikataba haiorangezi maana au kuongeza orodha ya masuala yasiyotarajiwa (*Force Majeure Events*) zaidi ya orodha na hatua zilizokubalika mwezi Oktoba 2001. Kitendo cha Kampuni ya *Songas* kutaka malipo kutoka kwa mpokea huduma ambaye hakupokea huduma wakati wa kipindi kigumu kilipingwa na *EWURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *EWURA* ilieleza kuwa mazingira ya kushangaza ni pale ambapo kwa makusudi, watendaji wa Wizara ya Nishati na Madini pamoja na *TANESCO* waliamua kuisadia Kampuni ya *Songas* kushinda shauri. *TANESCO* iliomba Baraza la Ushindani Huru likubali ombi la kuunganishwa kwenye shauri kama mlalamikaji. Ombi lilitupiliwa mbali na Baraza la Ushindani Huru kwani siku za kukubaliwa kuunganishwa kwenye shauri zilikuwa zimepita. Wizara iliandika barua kupinga baadhi ya maamuzi ya *EWURA* na kuipatia Kampuni ya *Songas* nakala ya wazi ili itumike kama kielelezo kwenye shauri dhidi ya *EWURA*. Baada ya kutafakari hatma ya shauri, Mwezi Desemba 2009, Kampuni ya *Songas* ilifuta shauri kabla halijasikilizwa. Januari 2010, Kampuni ya *Songas* iliomba ushauri kutoka *EWURA* kuhusu hatua za kuchukua kurekebisha mikataba, jambo ambalo lilitkelezwa na *EWURA* kwa dhati na *EWURA* ilitoa maelekezo mwezi Mei 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeshangazwa na kitendo cha Wizara ya Nishati na Madini kushindwa kutetea maslahi ya nchi hii na kuikandamiza *EWURA* kwa kuitetea *Songas* hasa kwa kuipatia nakala ya barua ambayo ilimwandikia *EWURA* ambayo naye *Songas* aliitumia kama kielelezo cha kuongeza nguvu mashtaka yake kwenye Baraza la Ushindani Huru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii imedhihirisha wazi kuwa ni kwa kiwango gani Wizara hii imeshindwa kulinda na kusimamia maslahi ya Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwenye kikao cha kuihoji Wizara kuhusiana na kitendo chao cha kuishurutisha *EWURA* kupitisha maombi ya *Songas* ya upanuzi wa miundombinu ya gesi isiyo na tija, lakini bado Wizara iliendelea na msimamo ule ule kuwa mazingira yaliyokuwepo ya tatizo la upatikanaji wa gesi yaliilazimu Serikali kuhakikisha mchakato wa upanuzi wa miundombinu ya gesi unafanya haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hairidhiki na utetezi huo kwani kimsingi *EWURA* alikuwa anaona gharama za *Songas* zilikuwa hazilindi maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uamuvi wa kubadili mitaji binafsi kuwa mikopo, kwa mujibu wa maelezo, *EWURA* haikuwa na mamlaka ya kuamua kubadili mitaji binafsi (*preferred equity shares*) kuwa mikopo (*loan notes*), suala hili lilikuwa chini ya Serikali, Msajili wa Makampuni (*BRELA*) na Benki Kuu ya Tanzania. Serikali ilitishwa kuwa mikataba (hususan *Power Purchase Agreement*) unatoa fursa kwa Kampuni ya *Songas* kuongeza madai ya gharama mtambuka (*miscellaneous charge*) ili kuonesha faida na kuwa na sifa ya kutoa gawio. Kifungu cha 3.10.3 cha *Power Purchase Agreement* kinatoa mwanya huo, lakini kifungu cha 4.14(b) cha Mkataba wa Wabia (*Shareholders' Agreement*) kinaelekeza kuwa Kampuni ya *Songas* ikopeshwe fedha kwa riba ya *LIBOR+2%* ili itimize wajibu wake kwa wabia wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *EWURA* walieleza kuwa hii ndiyo ilikuwa njia safi. Hata hivyo, walieleza kuwa Sheria ya Makampuni haiko wazi kuhusu hatua za kuchukua, hivyo ni vizuri Sheria hiyo iangaliwe ili suala hili lisitokee kwani Benki Kuu haikuwa ikiangalia jambo moja tu kama taratibu za kupeleka nje ya nchi gawio kwenye mtaji uliotoka nje ya nchi na kusajiliwa katika mabenki yaliyopo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji katika miradi hutegemea zaidi mikopo (50% hadi 80%) na mitaji binafsi (20% hadi 50%) au misaada ya hisani (*grants*) au michango (*contributions*). Uwiano mzuri wa fedha za mitaji (*Weighted Average Cost of Capital*) hupunguza makali ya maisha. Si jambo bayo kubadili mitaji binafsi kuwa mikopo endapo riba kwenye mikopo itapunguzwa kutoka kati ya 18% na 22% za sasa hadi kati ya 8% na 12%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kushangaza ni taarifa kuwa, mabadiliko ya mitaji binafsi kuwa mikopo iliyofanya katika uwekezaji wa *Songas*, Serikali haikupata chochote. Aidha, uwiano wa mikopo kwa mitaji binafsi (*debt or equity ratio*) baada ya mabadiliko hayo ni 96:4 badala ya kusudio la awali la 75:25.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasisitiza wakati umefika sasa Serikali kupitia upya mikataba ambayo ina upungufu ukiwemo wa *Liquidity Facility Agreement*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu taarifa kutoka kampuni ya *Twiga Cement*. *Twiga Cement* ni mmoja wa watumiaji wa gesi asili kwa ajili ya kuendesha mitambo ya kuzalisha saruji. Kampuni hii illanza kutumia gesi ya Songosongo mwaka 2004 kiasi futi za ujazo milioni 5.4 kwa siku. Hata hivyo, mwaka 2009 mahitaji yaliongezeka hivyo walisaini mkataba na Kampuni ya *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* ili kuweza kupokea kiasi cha gesi futi za ujazo milioni 13 kwa siku. Kutokana na mahitaji ya saruji kuongezeka na kutokuwepo na gesi ya kutosha nchini kunakosababishwa na kufikia ukomo wa mitambo ya kusafisha na bomba la kusafirisha. Kwa hali hiyo *Twiga cement* itakumbana na uhaba wa gesi kwa ajili ya kuendesha mitambo yao kuanzia mwaka 2012. Aidha, *Twiga Cement* illieleza Kamati kuwa imepanga kuwekeza mtambo wa MW 30 endapo gesi ya kutosha itapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Twiga cement* walieleza kuwa, pamoja na kutumia gesi asili lakini kuna nishati mbadala ya makaa ya mawe ambayo ni rahisi ikilinganishwa na gesi. Lakini upatikanaji wa gesi ni rahisi zaidi ikilinganishwa na makaa ya mawe kwani usafirishaji wa makaa ya mawe unagharama zaidi na hivyo kuendelea kutumia nishati ya gesi asili. Kwa sasa *Twiga Cement* wanatumia gesi kiasi cha futi za ujazo milioni 15 kwa siku na kati ya hizo, futi za ujazo milioni sita wanununa kutoka kwa *Songas* na futi za ujazo milioni tisa wanununa kwa Kampuni ya *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)*. Aidha, walieleza Kamati kuwa Kampuni hizi mbili huwauzia gesi kwa bei tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya Twiga *Cement* ilishauri kuwa sekta ya gesi inabidi iendelezwe na kuvutia wawekezaji. Kwa mujibu wa maelezo yao hakuna juhudzi zozote za kutosha zilizofanyika kuboresha sekta hii na kwamba Serikali lazima ijipange vizuri kwani rasilimali hii itasogezza uchumi wa Taifa mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya Twiga *Cement* ilieleza kuwa ipo tayari kuongeza uzalishaji kwa kutumia gesi hata kwa kusaini mkataba wa miaka kumi ijayo. Walieleza zaidi kuwa gesi inaweza kutumika kwenye viwanda vingi nchini kwani nishati hii ni rahisi ikilinganishwa na nishati nyingine kama mafuta mazito (*Heavy Fuel Oil*), lakini pia gesi ni rafiki wa mazingira hivyo ikitangazwa na matumizi yake kuhamashishwa kutabadilisha sura ya nchi na maisha ya Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya Twiga *Cement* walieleza kuwa sekta ya gesi inakumbana na changamoto zifuatazo:-

- (a) Kutokuwepo ushindani wa kibashara kutokana na kuwepo kwa Kampuni moja tu ya *Pan African Energy Tanzania Ltd (PAT)* kama msambazaji wa gesi nchini.
- (b) Kutokuwepo kwa Sheria ya Gesi kunaifanya sekta ikose mwongozo.
- (c) Serikali kutoipa umuhimu unaostahili sekta hii muhimu na adhimu ya gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa kutoka kampuni ya *Wentworth Resources*, Kamati ilieleza kuwa Kampuni ya *Wentworth Resources* inashughulika na kazi ya utafutaji na uzalishaji wa gesi na mafuta. Pamoja na hayo, Kampuni inaiuzia *TANESCO* umeme ambao unasambazwa kwenye Mikoa ya Lindi na Mtwara isipokuwa kwa Wilaya ya Kilwa na Liwale. Aidha, walieleza kuwa Mradi wa Umeme Mtwara una uwezo wa kufua umeme kiasi cha *MW12*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya *Wentworth Resources* yenyе hisa (25.4%) ikishirikiana na *TPDC* yenyе hisa (20%), *Maurel & Prom* yenyе hisa (38%) na *Cove Energy* yenyе hisa (16.6%) wamefanikiwa kufanya utafiti na kuchimba gesi eneo la Mnazi Bay na wanaendelea na utafiti mwingine. Kampuni pamoja na wabia wake inaendelea na mazungumzo na *TANESCO* kwa ajili ya kujenga kituo cha kufua umeme wa gesi kiasi cha *MW300* ambacho kitajengwa Mtwara Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya *Wentworth Resources* walieleza kuhusu sekta ya gesi na mafuta na kusema kuwa nchi yetu ina gesi nyangi lakini bado hajagundua mafuta ingawa dalili zipo katika maeneo ya Lindi, Mtwara, Tunduru, Pemba na Tanga. Aidha, walieleza kuwa kutokana na wingi wa gesi tuliyonayo nchi haipaswi kuwa maskini na wakatoa mfano wa nchi kama Qatar kuwa hapo awali iliikuwa ni moja ya nchi maskini lakini baada ya kugunduliwa kwa gesi nchi hii ni moja ya nchi tajiri. *Wentworth* walieleza kuwa Kampuni yao ndiyo ilijenga Sekta ya gesi Dubai na Qatar na wanataka kuona Tanzania nayo inabadilika inakuwa kama nchi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya *Wentworth Resources* waliomba Serikali isaidie ili msaada wa dola za Kimarekani milioni 30 uliositishwa na Serikali ya Uhlanzi kuitia *ORET* urudishwe. Kiasi hicho cha fedha kililenga kutoa nafuu ya gharama za kuunganisha umeme kwa wananchi 45,000 katika Mikoa ya Lindi na Mtwara. Aidha, walipendekeza kuundwe Kitengo ndani ya Serikali ambacho kitakuwa kinashughulikia masuala ya uwekezaji mkubwa ambacho pia kitakuwa kinashauri Makatibu wakuu na Mawaziri na walisisitiza ni vyema kitengo hiki kiwe chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu taarifa kutoka Kampuni ya Ndovu *Resources*. Kamati ilifanya kikao na Kampuni ya Ndovu *Resources*. Katika kikao hicho Kamati ilieleza kuwa Kampuni ya Ndovu *Resources* imesajiliwa nchini na inashirikina na Kampuni mama iitwayo *AMINEX* iliyopo Uingereza. Mwaka 1999 ilianza kazi na kupata Kitalu kiiwachoo Nyuni eneo la Kiliwani kisiliani Songosongo. Mnamo mwaka 2008 waligundua gesi Kiliwani *North* ambayo ni kiasi cha futi za ujazo milioni 45 kwa siku. Kiasi hiki kinawenza kuzalisha umeme *MW 200*. Kwa sasa wapo kwenye mchakato wa kuunganisha kisima hicho na mtambo wa kusafisha gesi wa *Songas* umbali wa takribani Kilomita tatu na nusu. Kulingana na mipango yao inatarajiwa ifikapo mwezi Machi, 2012

gesi itakuwa imefika kwenye mitambo tayari kwa kusafishwa. Aidha, wamekubaliana kwa kuanzia watapeleka gesi kiasi cha futi za ujazo milioni 14 na zitaongezeka itakapobidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya *Wentworth* ilieleza kuwa mahusiano kati yao na wadau wengine siyo mabaya sana ingawa kuna changamoto kadhaa wanazokumbana nazo ikiwa ni pamoja na:-

(i) Hapo awali walipata ugumu kuunganisha Kisima chao kwenye mtambo wa kusafisha gesi wa *Songas*.

(ii) Ugumu wa kupata *PSA* baina yake na *TPDC* na Wizara ya Nishati na Madini kwani wameelezwa kuwa imekwama kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

(iii) Usalama katika bahari kwani maharamia ni wengi pamoja na ulinzi uliopo lakini bado hautoshi.

(iv) *EWURA* pamoja na kufanya vizuri, lakini inaonekana hawana mahusiano mazuri na Wizara ya Nishati na Madini na hii inatokana na *EWURA* kusimamiwa chini ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Aidha, *EWURA* inadhibiti gharama za *downstream* na kuacha za *upstream*, hivyo kukosekana udhibiti ulio sahihi.

(v) Wizara ya Fedha na *TRA* kuchelewesha *Refunds* zao, hii itafukuza wawekezaji.

(vi) *TANESCO* imekuwa ikiwavunja moyo kwani tangu mwaka 2006 wametuma maombi ya kuwauzia gesi bila majibu. Aidha, mpaka wakati wanahudhuria kikao cha Kamati walikuwa na wiki saba tangu wawasilishe Waraka wa Maelewano (*MoU*) ya kuwauzia gesi bila majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu taarifa kutoka Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Nishati na Madini ambayo ni msimamizi wa Sekta ya Gesi, ilihudhuria vikao vya Kamati kwa nyakati tofauti na ilitoa maeleo mbalimbali na ufanuzi wa hoja zilizojitekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu muundo wa Mtaji wa *Songas*, Wizara ilieleza kuwa wakati *Songas* inaudwa 2001, uwiano wa mkopo na mtaji binafsi wa *Songas*, ulikuwa 75:25 (Dola za Kimarekani milioni 216: dola za Kimarekani milioni 61). Aidha, ilielezwa kuwa dola za Kimarekani 216 ziliikuwa ni jumla ya mkopo ambaa Serikali ilikopa kutoka taasisi mbalimbali za kifedha na Serikali nayo ikaikopesha *Songas*. Taasisi hizo ambazo ziliikopesha Serikali ni; Benki ya Dunia (*IDA*) dola za Kimarekani milioni 140.8, Benki ya Rasilimali ya Ulaya (*EIB*) dola za Kimarekani milioni 53.1, Shirika la Maendeleo la Sweden (*SIDA*) Dola za Kimarekani milioni 15.179. Fedha hizo zilikopwa kwa viwango tofauti tofauti vya riba na vipindi tofauti vya kuanza kulipa mkopo na riba (*grace period*) (Kiambatisho na 18).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilijulishwa kuwa mmoja kati ya wanahisa wa *Songas* (*CDC GlobeEq*) aliyeokuwa anamiliki hisa za upendeleo (*Preference shares*) aliamua kuzibadili hisa zake na kuzifanya kuwa mkopo (*Loan notes*). Kamati ilielezwa kuwa lengo la kufanya mabadiliko haya ni kumwezesha *CDC GlobeEq* kulipwa riba kila mwezi bila kujali kuwa *Songas* imepata hasara au imepata faida. Aidha, baada ya mabadiliko haya muundo wa mtaji wa *Songas* (*Capital Structure*) ulibadilika na kuwa na uwiano wa mkopo kwa mtaji binafsi wa 96:4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwiano uliotajwa hapo juu ni wa ajabu na haukulaliki kwa mujibu wa taaluma za kifedha na kiuchumi. Kamati haikubaliani na muundo huu wa mtaji na inashauri taratibu za kifedha za kubadili muundo huu zifanyike ili kulinda maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu fedha za mafunzo, Wizara pia ilihojiwa kuhusu fedha za mafunzo ambazo *TPDC* hupokea kutoka kwa wabia wanafanya shughuli za utafutaji na uzalishaji wa mafuta na gesi. Kutoptana na taarifa zilizowasilishwa kwa Kamati, *TPDC* kwa mwaka 2010/2011, ilikuwa imepokea jumla ya dola za Kimarekani milioni 1.75 ambazo ni sawa na bilioni tatu za Kitanzania kwa ajili ya mafunzo na nusu yake zikaelekezwa Wizarani. Katika hali ya kushangaza

taarifa iliyowasilishwa na *TPDC* inaonesha dhahiri kuwa fedha hizi hazitumiwi kwa malengo yaliyokusudiwa. Mathalani kwa mujibu wa vielelezo kutoka *TPDC* inaonekana kuwa shilingi milioni 20 zilitumika kama mchango wa maandalizi ya bajeti kwa mwaka 2010/2011 na fedha nyingine nyingi zitemumika kulipia tiketi za ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mfuko wa kufidia makali ya gharama za umeme (*National Tariff Equalization Fund*). Wizara ilieleza Kamati kuwa, Serikali ilikubali kuanzishwa kwa Mfuko wa kufidia makali ya gharama za umeme (*National Tariff Equalization Fund - NTEF*) ili kutoa fidia ya bei ya umeme utakaozalishwa na Mradi wa Umeme Mtwara (*MEP*). Fidia hiyo ililenga kuleta uwiano wa bei katika kipindi cha miaka mitatu ya mwanzo ya mradi wakati idadi ya wateja ikiwa bado ni ndogo. Katika makuballiano hayo, ilikadiriwa kuwa kiasi cha dola za marekani milioni 14.5 zitawekezwa katika Mfuko wa *NTEF* katika kipindi cha miaka mitatu mara tu mikataba itakaposainiwa. Wizara ilianza kutenga fedha hizo kuanzia bajeti ya mwaka 2008/2009 na hadi kufikia 2010/2011 jumla ya shilingi bilioni 18.1 sawa na dola za marekani milioni 12.1 zimebekwa katika Mfuko huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kuwa katika kukabiliana na changamoto za upatikanaji wa umeme katika Wilaya zilizokuwa zinahudumiwa na kituo cha kuzalisha umeme cha Masasi, ukarabati na ujenzi na miundombinu ulifanyika. Iliamuliwa chini ya Mikataba ya *Masasi Interconnection Construction and Reimbursement Agreement (MICRA)* fedha za *NTEF* zitumike kuunganisha umeme kutoka Mtwara hadi Masasi. Aidha, ilielezwa bayana kuwa baada ya mikataba kusainiwa, fedha za *NTEF* zitarudishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilijulishwa kuwa Septemba 2007, Serikali ilisaini Mikataba wa kupatiwa msada wa fedha na Serikali ya Uholanzi kiasi cha dola za Marekani milioni 28.8 kuititia taasisi ya *ORET* kwa lengo la kuimarisha miundombinu ya kusambaza umeme pamoja na kupunguza gharama za kuunganisha wateja wapya. Aidha, Disemba 2008 mikataba mitano kwa ajili ya utekelezaji wa mradi ilisainiwa kati ya Serikali na *Artumas*. Serikali iliwalishwa na (Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Fedha na Uchumi, *TANESCO* na *TPDC*). Mikataba hiyo ilitarajiwaa kusihi (*effective date*) miezi 12 baada ya kusainiwa kutokana na kuwepo kwa masharti ya utekelezaji (*condition precedent*) kabla ya kuanza rasmi utekelezaji wa mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kuwa wakati ikisubiriwa kusihi kwa mikataba, mambo kadhaa yalijitokeza hali iliyopelekea msaada wa *ORET* wa dola za Marekani milioni 28.8 usitishwe. Sababu hizo ni pamoja na:-

(a) Mwekezaji kushindwa kuthibitisha kuwa na fedha (*matching fund/non grant fund*) kwa ajili ya kuwekeza kwenye mradi.

(b) Hali ya kifedha ya *Artumas* kuwa duni kutokana na kudorora kwa hali ya uchumi duniani mwaka 2009. Hali hiyo ilipelekeea Kampuni ya *Artumas* kuuza sehemu ya hisa zake ambapo kwa sasa imehamishiwa kwa Kampuni ya *Wentworth Resources Limited* ya Canada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeshtushwa kuona Wizara imekuwa ikiomba fedha za Mfuko wa kufidia makali ya gharama za umeme (*National Tariff Equalization Fund*) kwa takriban miaka minne mfululizo bila kutoa taarifa ya mabadiliko ya matumizi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Kamati imeelezwa kuwa fedha za Mfuko wa kufidia makali ya gharama za umeme (*National Tariff Equalization Fund*) zilizotengwa kwenye bajeti ya 2011/2012, zimebadilishwa matumizi yake na sasa zitatumika kununulia mafuta mazito kwa ajili ya Mtambo wa *IPTL*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fedha za Kitengo cha Usimamizi na Utaribu wa Mradi wa Songsongo (*PMU*) Kamati ilipokea taarifa kutoka Kitengo cha Usimamizi na Utaratibu wa Mradi wa Songsongo (*PMU*) ambayo ilieleza kuwa kitengo kilanzishwa mnamo Mwaka 2002 na Serikali na kupewa jukumu la kusimamia utekelezaji wa Mradi wa Songsongo. Kitengo kiliundwa na wataalam toka *TPDC* (1), *TANESCO* (1), *NEMC* (2), Wizara ya Wanawake na Watoto (1), *OSHA* (1), Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira (1) na kutoka Wizara ya Nishati na Madini (3) pamoja wasaidizi wa Ofisi (8). Mradi huu wa Songsongo umegawanyika katika makundi makuu matatu yaani

Mradi wa Umeme uliotekelizwa na *Songas*, Mradi uliohusiana na huduma za kijamii na mazingira, pamoja na kuimarisha uwezo wa watendaji (*capacity building*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilielezwa kuwa, Miradi mikubwa ya kijamii ni Mradi wa Umeme Vijijini (*The Wayleave Village Electrification (WVES)* na *Resettlement Infrastructure Development Scheme (RIDS)*). Katika Mradi wa *WVES*, *PMU* ilisimamia usambazaji wa umeme na maji kwa wananchi wote ambao mradi huu umewapitia. Kwa upande wa *RIDS*, *PMU* ilisimamia ujenzi wa barabara, mabomba ya maji na umeme. Baada ya kukamilika kwa miradi hii, *PMU* imeendelea na jukumu la kusimamia utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam ambao unatarajija kuanza mwishoni mwa mwaka huu 2011. *PMU* wameeleza kuendelea kusimamia utekelezaji wa Mradi wa Uendelezaji wa gesi asili ya Mnazi Bay hususan Mtwara *Energy Project* na Mradi mkubwa wa kuzalisha *MW* 300 za umeme Mtwara; kushauri masuala ya kisera, mapendekezo ya Sheria ya Gesi Asili, Maandalizi ya Mpango Kabambe wa Matumizi ya Gesi Asili na Mapendekezo ya Kanuni zitakazotumika chini ya Sheria Mpya ya Gesi Asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu dhamana ya mikopo. Kamati ilijulishwa kuwa wakati wa m dororo wa uchumi, Wizara kupitia HAZINA ilimpa fedha *ARTUMAS (stimulus package)* ya shilingi za Kitanzania bilioni kumi kwa lengo la kuwasaidia ili waendelee na mradi. Fedha hii ilitolewa kama mkopo na *Artumas* waliweka dhamana ya asilimia mia moja ya hisa zake na pia walikubaliana mauzo yote ya gesi yapitie kwenye Benki ya *TIB*. Aidha Wizara imeieleza Kamati kuwa Kampuni ya *Artumas* ilibadilisha jina na kuwa *Wentworth Resources* na kwamba mkopo huo wote na dhamana zake umerithiwa na Kampuni ya *Wentworth Resources*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kujiridhisha Kamati iliomba maelezo ya ziada na vielelezo vinavyoonesha mabadiliko ya umiliki kutoka *Artumas* kwenda *Wentworth* na uthibitisho kuwa mmiliki mpya anakubali deni hilo. Kamati imeridhika kwa maelezo na vielelezo kuwa deni letu liko salama na dhamana iliyowekwa inakubalika benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utendaji wa Wizara, Kamati hairidhiki na utendaji wa Wizara hasa pale iliposhindwa kusimamia suala la upatikanaji wa watumishi walioombwa na *TPDC*. Kama ilivyoolezwa awali na ushahidi wa vielelezo viliviyowasilishwa kwenye Kamati, *TPDC* walieleza umuhimu wa kuajiri wataalam ili waweze kuyakabili majukumu yaliyokuwa mbele yao, hii ni pamoja na kusimamia na kukagua utendaji wa wabia wanaoshiriki katika utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi ikiwemo Kampuni ya *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* kwa mujibu wa Mikataba yao (*PSA*). Ni imani ya Kamati hii kuwa Wizara yenye dhamana ingeweza kueleza kwa mamlaka husika hatarisho linalokabili maslahi ya Taifa na hizo mamlaka zingeruhusu *TPDC* iajiri kama ilivyoombwa. Kwa mtazamo wa Kamati, upotevu wa dola milioni 64 zinazozungumziwa, Wizara haiwezi kukwepa lawama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imeonekana dhahiri kuwa Wizara ya Nishati na Madini haikuwa makini tangu mwanzoni wakati wa hatua ya kuingia Mikataba ya *Songas* na Mikataba wa *PSA* wa *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* na *TPDC* kutokana na udhaifu ulivyojonesha. Aidha, upungufu kwenye Mikataba iliyopo ni matokeo ya Wizara kutokuwa na utayari, utashi, umakini na uzalendo katika kusimamia rasilimali ya gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Nishati na Madini imeonesha kushindwa kuingilia kati pale ambapo wawekezaji *Songas* na *Pan African energy Tanzania Limited (PAT)* wanapokwenda kinyume cha kimkataba. Mfano ni pale *Songas* walipozembea na kufanya kisima namba tano, saba na tisa kuharibika (*Corrosion*). Ni jambo la kusikitisha pamoja na mkataba kuainisha wajibu wa mwekezaji katika kusimamia visima, wawekezaji wamegoma kuvirekebisha au kuvitengeneza na Wizara haijachukua hatua ya maana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bomba jipyä la gesi, Kamati inatambua na kupongeza juhudi za Serikali kuharakisha mchakato wa ujenzi wa bomba jipyä la gesi kutoka Mnazi Bay (Mtwara) hadi Dar es Salaam na hatimaye Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaunga mkono mradi huu baada ya kupata taarifa kutoka Wizara ya Nishati na Madini kuwa Mradi huu utajengwa kwa Mkopo wenge gharama nafuu sana kwa riba ya takriban asilimia mbili tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bomba hili ambalo litakuwa na uwezo wa kupidisha gesi kiasi cha futi za ujazo milioni 784, litafikisha gesi ya kutosha kwenye miradi mipyga ya uzalishaji umeme ya Kinyerezi (*MW* 240), Somangafungu (*MW* 230) na *Jacobsen* (*MW* 100) na kukidhi mahitaji mengine ya gesi ya viwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imepokea taarifa za kushangaza kuhusu jitihada zinazofanywa na Kampuni ya *Songas* kutaka kupinga ujenzi wa mradi wa bomba hili jipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Kampuni ya *Songas* kupinga ujenzi wa bomba hili ni kuwa, akiba ya gesi iliyopo Mtwara (Mnazi Bay) ni kidogo mno kulinganisha na ukubwa wa bomba linalojengwa na hivyo mradi utakuwa na hasara na hautakuwa na manufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kushangaza hapa ni pale ambapo Kampuni ya *Songas* inafanya jitihada za ziada ili kupata kibali cha kufanya upanuzi wa miundombinu ya kusafisha na kusafirisha gesi ya Songsongo hadi kufikia futi za ujazo milioni 140 kutoka milioni 105 kwa siku za sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upanuzi huu ambaao *Songas* wanaomba kufanya utaongeza upatikanaji wa gesi kwa kiasi cha futi za ujazo milioni 35 kwa siku, ongezeko ambalo linaweza kutosha kuzalisha *MW* 170 za umeme, wakati ongezeko hili *Songas* wanakadiria kulifanya kwa gharama ya dola za Kimarekani milioni 120 ambazo ni 40% ya fedha hizo itakuwa ni mtaji binafsi wa *Songas* ambaao utalipwa riba ya 22%, jambo ambalo litafanya mradi huu kuwa wa gharama sana kulinganisha na manufaa yatakayopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapinga kwa nguvu zote utekelezaji wa mradi huu wa upanuzi wa miundombinu ya *Songas* kwa kuwa hautakuwa na maslahi kwa Taifa bali atakayefaidika ni *Songas*, badala yake Kamati inapendekeza Serikali kutoyumbishwa na yeoyote katika jitihada za kutekeleza mradi wa bomba jipya la gesi kutoka Mnazi Bay Mtwara hadi Dar es Salaam na Tanga. Bomba hili linatakiwa likamilike haraka iwezekanavyo ili nchi iwe na usalama na uhakika wa upatikanaji wa gesi kwa maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kujibu hoja ya *Songas* kisayansi tunaishauri Serikali kupidia *TPDC* ihamasishie shughuli za uchimbaji gesi katika maeneo ya Songsongo, Mkuranga na Mnazi Bay maeneo ambako bomba linapita. Taarifa zilizowasilishwa mbele ya Kamati na wadau mbalimbali zinaonesha kuwa kuna hazina kubwa ya gesi katika maeneo hayo hivyo hakuna haja ya kuwa na wasiwasi wa upatikanaji wa gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni kuhusu maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndio mmiliki halali (kisheria) wa ardhi yote iliyoko nchini kwa maana ya nchi kavu na baharini. Hivyo kila rasilimali iliyoko chini ya ardhi ni mali ya Serikali. Utafutaji, ugunduzi na uuzaaji wa rasilimali hizo huongozwa na sheria mbalimbali zinazotungwa na Bunge letu Tukufu kuhusiana na rasilimali hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya rasilimali ya gesi asili iliyoko nchini mwetu hajatungiwa Sheria yoyote mahsusii inayosimamia utafiti, uzalishaji na uuzaaji wake kwa ukamilifu. Hili ndio chimbuko kubwa linalosababisha ukiukwaji wa mikataba karibu yote iliyofungwa baina ya Serikali ya Tanzania na wabia wengine wa gesi kwa kuwa hakuna sheria mahsusii inayolinda rasilimali hii kwa maslahi ya Taifa. Kutokana na ukosefu wa Sheria ya Gesi nchini wadau na Taasisi mbali mbali za Serikali wamekuwa wakitumia Sheria ya Utafutaji na Uzalishaji Mafuta ya Mwaka 1980 (*The Petroleum Exploration and Production Act, Cap 328*) kama sheria mbadala katika kusimamia masuala ya gesi, sheria ambayo kwa ujumla wake ni kudhibiti utafutaji, uzalishaji na usambazaji wa mafuta ya petrol nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, pamoja na matumizi ya Sheria ya Utafutaji na Uzalishaji Mafuta bado watendaji wanaohusika na usimamizi wa sekta ya gesi nchini siyo makini katika kutekeleza majukumu yao ya kusimamia utekelezaji wa sheria panapotokea ukiukwaji wa vipengele katika mikataba iliyofungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ndogo imepitia kwa kina Sekta ya Gesi na hususan ushiriki wa Kampuni ya *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)*. Kamati inatambua kwamba Sekta hii ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi na hifadhi ya mazingira na kama itasimamiwa kikamilifu hasa kwenye Mikataba, basi mchango wake kwenye maendeleo ya Taifa hili ni mkubwa sana. Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo yafuatayo ambayo inaomba Bunge iyapokee, iyaridhie na kuyaazimia:-

(1) Serikali hususan Wizara ya Nishati na Madini itambue kuwa pamoja na *TPDC* kuwa msimamizi wa Sekta ya Gesi kwa niaba ya Serikali, lakini Wizara ya Nishati na Madini ndiye mdau mkuu katika Mikataba hii yenye utata kwa niaba ya Taifa na hivyo anapaswa kusimama sambamba na *TPDC* kutetea maslahi ya Taifa kwani Wizara ilikuwa haifanyi hivyo.

(2) Kamati imejiridhisha bila shaka kwamba kwa kipindi cha 2004 hadi 2009, Kampuni ya *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* imejirudishia isivyo halali gharama zinazofikia jumla ya dola za Kimarekani milioni 28.1 sawa na fedha za Kitanzania bilioni 46.3. Kutohakana na kujirudishia fedha hizo isivyo halali kumefanya Serikali kukosa gawio lake linalofikia dola za Kimarekani milioni 20.1. Aidha, mpaka wakati Kamati inaandaa ripoti hii, Kampuni ya *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* imeshindwa kuwasilisha uthibitisho wa uhalali wa kujirudishia gharama nyingine zinazofikia jumla ya dola za Kimarekani milioni 36. Hali hii inaonesha mashaka makubwa katika uendeshaji wa sekta hii muhimu ya gesi.

(3) Kwa kuzingatia kuwa *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)*. *PAT* walifanya udanganyifu wa makusudi kwa kipindi cha 2004 hadi 2009 na kusababisha Serikali kukosa gawio lake inalostahili, Kamati inashauri mapunjo hayo ya Serikali yanayofikia dola za Kimarekani milioni 20.1 yarejeshwe mara moja na kwa kuwa mapunjo hayo ni ya muda mrefu, marejesho yake yaambatanishwe na riba kwa viwango vya benki (*Time Value for Money*). Aidha, upelelezi ufanyike katika hesabu za *PAT* kwa mujibu wa Sheria ya Kanuni za Adhabu, vifungu vifuatavyo: (i) kifungu 350 kwa kosa la kuweka mahesabu yasiyo sahihi katika kitabu cha mahesabu; (ii) kifungu 315 kwa kosa la kughushi; (iii) kifungu 316 kwa kutoa taarifa za uongo; na (iv) kifungu 317 kwa kutoa taarifa za mahesabu za kughushi na ushahidi ukipatikana Kampuni ya *Pan African Energy Tanzania Limited* Wafanyakazi wote waliohusika katika udanganyifu huu washtakiwe kwa mujibu wa Sheria.

(4) Kutohakana na *Pan African Energy Tanzania (PAT)* kukosa sifa za uaminifu, Kamati inashauri Mkataba wa *Pan African Energy Tanzania (PAT)* usitishwe. Aidha, utekelezaji wa kuvunja mkataba huu uende sambamba na kuhakikisha kuwa taratibu za kisheria na za kimkataba zinazingatiwa, uwepo wa usalama wa visima na mitambo na uwepo wa uhakika wa huduma ya upatikanaji wa gesi nchini.

(5) Kamati inashauri utaratibu wa *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* kujirejeshea gharama za usambazaji chini ya muundo wa *PSA* usitishwe mara moja. Aidha, kutoka na mahitaji makubwa ya gesi asili katika matumizi ya viwandani na majumbani, jitihada za uhamishaji wa matumizi hayo zlongezeko na gharama za usambazaji zirejeshwe kwa kutumia *tarrif* za bei.

(6) Serikali kama msimamizi wa mikataba inayo haki ya kukagua gharama za mwekezaji. Mikataba yote ya *PSA* ina vipengele vinavyoipa uwezo huo Serikali au msimamizi wa Mkataba kwa kutambua uwiano wa mgao wa Serikali na usahihi au uhalali wa gharama za mwekezaji. Katika *PSA* ya Songosongo haki hiyo ya kukagua gharama za *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* imepewa *TPDC* kwa mujibu wa kifungu 21.2. Hata hivyo, Kamati imegundua kuwa Serikali imezembea kusimamia suala hili na hivyo kutoa fursa kwa mwekezaji kudanganya na kujilipa fedha nyingi za walipa kodi wa Tanzania kinyume na taratibu za Mkataba. Kamati inapendekeza mapungufu haya yarekebishwe mara moja.

(7) Kwa mujibu wa mkataba wa gesi: "Katika kipindi ambacho gesi itakuwa imekwisha (*depleted*), basi mapato yatokanayo na mauzo ya mabaki ya mitambo ya gesi yatatumika kulla pia gharama za kurejesha au kutunza mazingira ya eneo la uchimbaji wa gesi katika hali iliyosalama". Kamati haipendezwi na utaratibu huo na inaishauri Serikali kuititia TPDC kutafuta utaratibu mzuri utakaokubalika kisheria ambapo Kampuni ya SONGAS itawabidi watenge fungu la pesa la kugharamia urejeshaji au utunzaji wa mazingira wa maeneo ya uchimbaji wa gesi pindi gesi itakapokuwa inakaribia kwisha. Aidha, Serikali isikubaliane na vipengele kama hivi, mara nyingi wawekezaji hawa huondoka kama sio kutoroka baada ya kumaliza uchimbaji wa migodi au vitalu.

(8) Mkataba wa PSA, kifungu cha 10.4 na 10.5 vimetoa utaratibu wa namna ya kugawana mgao unaotokana na faida ya gesi iliyopatikana kutoka eneo lenye gesi iliyothibitishwa (*proven gas*) na gesi isiyothibitishwa (*unproven gas*). Mgao huu utabadilika kwa mujibu wa ushiriki (*participation*) wa TPDC. Aidha, kwa kuwa gesi ya ziada inaweza kuzalishwa kutoka katika eneo ambalo gesi imethibitishwa au ambalo gesi haijathibitishwa na Pan African Energy Tanzania Limited (PAT) wana haki ya kupata sehemu ya mapato yatokanayo na mauzo ya gesi ya ziada (*additional gas*).

Kamati inaona kuwa siyo sahihi kuendelea na utaratibu huu kwani kwa kufanya hivyo ni kumlipa Pan African Energy Tanzania Limited (PAT) mara mbili (*double payment*) ya kile anachostahili kwa kuwa Pan African Energy Tanzania Limited (PAT) inanufaika kwanza na marejesho ya utafutaji wa gesi kwenye visima ambavyo tayari vilikuwa vimekwishathibitishwa na TPDC kuwa na gesi na pili anagawana mapato na TPDC. Kamati inasisitiza utaratibu huu wa ugawanaji wa mapato katika mazingira haya unahitaji kuangaliwa upya kwa kuwa hapo awali Pan African Energy Tanzania Limited (PAT) alipewa unaifuu huu kwa kutegemea kuwa angetafuta na kuendeleza vitalu tisa vya gesi na si viwili kama ilivyo sasa kwenye eneo lile lile la uzalishaji tofauti na alivyotakiwa kufanya kwa mujibu wa PSA. Kamati inashauri mkataba kufanyiwa marejeo.

(9) Kamati imegundua kuwa, kwa sasa masuala ya sekta ya gesi nchini yanasmamiwa na Sheria ya Utafutaji na Uzalishaji wa Mafuta ya Mwaka 1980 (*The Petroleum Exploration and Production Act, 1980*) na mikataba ya uzalishaji na ugawanaji (PSA) ambayo inatoa mwanya kwa wawekezaji kujipatia faida kubwa kuliko anavyostahili. Kamati imebaini kwamba, kutokuwepo kwa Sheria ya Gesi kumefanya sekta ya gesi ikose mwongozo na usimamizi wa kutosha na hivyo wadau kutoja mwelekeo na imeathiri mahusiano ya wadau kwa jinsi yanavyopaswa kuwa. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kukamilisha haraka mchakato wa Sheria ya Gesi ili kuhakikisha rasilimali hii muhimu inatumika kwa maslahi ya Taifa.

(10) Utaratibu wa umiliki wa mitambo na mali nyingine baada ya muda wa Mkataba kwisha umefafanuliwa vizuri katika kipengele cha 17 cha PSA ikiwemo mali zisizohamishika na zinazohamishika. Aidha, Kamati haikubaliani na kifungu cha 17.3 cha PSA: "TPDC wanahaki ya kununua chochote kilichoagizwa na PAT kutoka nje ya nchi na ambacho hakijalipiwa kodi kwa bei ya kibashara, isipokuwa kwa vifaa vilivyoainishwa kwenye vipengele 17.1 (a) na 17.1 (b) vya PSA". Kwa kawaida, katika PSA yoyote ile, mitambo na mashine zote (ikiwa ni pamoja na mitambo na mabomba ya gesi) zilizounuliwa kwa ajili ya shughuli za kutafuta na kuendeleza gesi au mafuta chini ya PSA, zinatakiwa kuwa mali ya Serikali au Shirika la Mafuta na kwa sababu hii ndio maana huwa hailipwi kodi. Uhamishaji wa haki za umiliki wa mali hufanyika aidha baada ya Kampuni ya Kimataifa kurejesha gharama zake za kununulia mitambo na kuifunga au mwisho wa uzalishaji. Kwa mantiki hii, Kamati haioni sababu ya kuwepo kwa kifungu hiki cha 17.3 cha PSA.

(11) Msingi mkuu wa Mkataba wa Uzalishaji na Ugawanaji (PSA) ni kwamba, mwekezaji anaingia kwanza kuzalisha na baadaye kugawana na Serikali kulingana na mapato yaliyopatikana. Lakini mkataba huu mwekezaji amekuta uwekezaji umeshafanyika kwa maana ya visima tayari vimechimbwa na hivyo kukosekana uhalali wa mwekezaji kuwa mbia katika mikataba ya gesi. Pamoja na hoja za utetezi zinazoegemea mazingira ya wakati huo, Kamati inashauri kipengele hiki kiangaliwe upya.

(12) Mikataba ya mradi wa gesi ilijojadiliwa na kukubaliwa na kusainiwa na Serikali pamoja na SONGAS ilikuwa kumi na nane. Mikataba hii ina vipengele tata na nya makusudi vyenye maana zaidi ya moja ambavyo vingine vinatasiriwa tofauti na wadau husika. Ipo haja kwa Serikali yetu kufanya tathmini ya kina (*Due Diligence*) kabla ya kuingia mkataba na wawekezaji. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeonesha kutokuwa makini katika kupitia, kujadili na kusimamia mikataba kama hii inayoingia kwa niaba ya Serikali na hatimaye Serikali imekuwa ikiingia hasara kubwa katika sekta hii ya nishati na wawekezaji wamekuwa wakineemeka kwa kunyonya rasilimali ya Watanzania ambao wengi wao ni maskini. Hali hii inaashiria kuwa imefika wakati kwa Serikali kuwachukulia hatua kali watendaji wote wanaochangia hasara kubwa kwa Serikali.

(13) Kamati imejiridhisha kwamba, kuna upungufu mkubwa wa watumishi wenye utaalam wa kiseka kuanzia ngazi ya Wizara, Taasisi zake na hata kwenye jamii na hakuna mfumo endelevu unaohakikisha nchi inakuwa na wataalam wanaohitajika (*Succession plan*) katika Sekta za nishati na gesi. Serikali kama msimamizi wa kutoa vibali nya ajira nchini kupitia Ofisi yake ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma inapaswa kuwa mstari wa mbele katika kufanya utafiti na tathimini ya ajira zinazoombwu ambazo vibali vyake vinatakiwa kutoka haraka ili maslahi ya Taifa yalindwe. Mathalani wataalam wa kijiolojia ya miamba. Kamati inaamini kuwa dola za Kimarekani 64 zilizoripotiwa kwenye ukaguzi wa TPDC kusingetokea kama kibali cha kuajiri wakaguzi wa ndani wa mahesabu wa TPDC kingetolewa mapema.

(14) Kamati imeridhika kuwa kuna uhusiano mbaya kati ya TPDC na *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* ukizingatia kuwa mahusiano yao ni ya kimkataba na kila upande unao wajibu na haki ndani ya mkataba (PSA). Mfano mzuri ni kuwa, *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* amekuwa akikiuka baadhi ya vipengele nya mkataba wa uzalishaji na ugawanaji (PSA). *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* chini ya Ibara ya XXIV (24.4) anapaswa kufuata sheria zote za Tanzania; *Pan African Energy Tanzania (PAT)* amevunja Ibara ya 21.1 ya PSA kwa kitendo chake cha kutotunza taarifa au nyaraka za mahesabu yake ya uhasibu kwa mujibu wa taratibu za kihasibu zilizokubaliwa Tanzania. Aidha, *Pan African Energy Tanzania Limited* imekuwa haiishirikishi TPDC katika kufanya manunuzi kinyume na taratibu. Mifano hii michache inaashiria uwepo wa uhusiano mbaya unaofanywa na *Pan African energy Tanzania Ltd (PAT)*.

(15) TANESCO amelalamika kuwa *Pan African energy Tanzania Limited (PAT)* amekuwa akikwepa adhabu pale inapotokea hitilafu kwenye visima nya gesi na mitambo ya kusafisha gesi na hivyo kutupiana mpira na Songas na hii inatokana na *Pan African energy Tanzania Limited (PAT)*. PAT kuwa mwendeshaji tu wa visima na mitambo hiyo na siyo mmiliki. Kamati imeridhika kuwa mahusiano ya mbia huyu siyo mazuri na hivyo Serikali iangalie Mkataba wao.

(16) Katika Sekta ya Gesi lipo tatizo kubwa la baadhi ya visima kuharibika (SS 5, 7 na 9). Hata hivyo, Kamati inashangazwa na ucharaka wa Kampuni ya *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* kukimbilia kuchimba kisima kingine SSA badala ya kuokoa visima nya awali ambavyo tunahakika vina gesi nyingi, zaidi ya hapo zipo taarifa kuwa *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* wanalenja kuchimba kisima kipyra SSA ambacho watatumia mtambo wa kuchimbria (*drill rig CARROL 6*) ambao umeaminika kuwa ni wa gharama kubwa na haufai kutumika kwa mazingira ya nchi yetu. Kamati inaishauri Serikali kufanya jitihada za ziada kuhakikisha visima vilivyo haribika vinaokolewa ili viendelee kuzalisha kama ilivyo kawaada. Aidha, Serikali iihakikishe kuwa mitambo inayotumika katika kuchimba gesi na mafuta haitaingiza Taifa katika gharama kubwa na ambayo ni rafiki wa mazingira.

(17) Misingi ya Hoja walizokuwa wanatoa *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* za kurudisha gharama walizotumia isivyo halali yafanyike kwenye gharama zilizobaki na ambazo zitadaiwa na kurudishwa miaka inayofuata ni batili na ni sawa na kufanya marekebisho kwenye cost pool. Hoja hii ikikubaliwa na Serikali itakiuka misingi ya PSA ya kuwa mwekezaji atumie fedha zake kwanza kabla ya kurudishiwa gharama zake. Kamati inasilitiza *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* izilipe fedha hizi haraka iwezekanavyo.

(18) Katika hali ya kusikitisha na kuvunja moyo, Kamati imejiridhisha kuwa Wizara ya Nishati na Madini imekuwa haitoi ushirikiano wa kutosha kwa *TPDC* na *EWURA* hasa katika kusimamia masuala ya sekta ya gesi nchini. Vitendo vya ukiukwaji wa taratibu, udanganyifu na uhalifu vinavyofanywa na *SONGAS* na *PAT* kwa lengo la kuibia nchi vinaendelea kulelewa na havijakemewa na Wizara ya Nishati na Madini ipasavyo. Imedhihirika kuwa mara kwa mara Wizara imekuwa ikiwasaidia wawekezaji hawa katika mipango yao ya kufanya udanganyifu mfano, ni pale Wizara ilipofanya jitihada za makusudi kuilazimisha *EWURA* kuitisha maombi ya bei (*tarrif*) ya *Songas* ambayo hapo awali *EWURA* waliyakataa kwa kuwa yalikuwa na upungufu uliokinzana na maslahi ya nchi, zaidi ya hilo Wizara ya Nishati na Madini iliandikia *EWURA* barua ikielezea kuwa *EWURA* wamevunja sheria.

Jambo la kusikitisha Wizara ilitoa nakala ya barua hiyo kwa *SONGAS* ambaao nao waliiutumia barua hiyo kama kielelezo katika shauri lao walilofunga kwenye Baraza la Ushindani huru (*Fair Competition Tribunal*) dhidi ya *EWURA*. Kutokana na mwenendo wa Wizara katika kusimamia Sekta ya Gesi kama ilivyolezwa hapo juu, Kamati inashauri Serikali kuititia upya mfumo wa utendaji wa Wizara utakaohakikisha maslahi ya Taifa yanazingatiwa. Ni dhahiri uzoefu wa mgongano wa *EWURA* na Wizara unaonesha hatari inayokabilii sekta ya gesi. Aidha, kutokana na udhaifu mkubwa wa kiutendaji ambayo yameelezwa hapo awali, Kamati inashauri Serikali kuwawajibisha viongozi wakuu na watendaji waliohusika na uzembe huu na kuteua wengine wenye uwezo haraka iwezekanavyo.

(19) Pamoja na jukumu la kufuatilia rasilimali za Taifa (dola milioni 64) Kamati imebaini kuwa ulikuwepo uzembe uliopelekea visima namba tano na tisa, kuharibika (*Corrosion*). Matatizo ya kuharibika kwa visima yangeweza kutambulika mapema na kurekebishiwa kama *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* angezingatia maelekezo ya mkataba (*Gas Agreement* kifungu cha 7.6 (e)) kitendo ambacho hakufanya. Mbali ya hasara ya kupoteza visima hivyo, uendeshaji shughuli wa aina hii unaliweka Taifa katika hatari ya kukosa nishati hii muhimu katika kipindi ambacho gesi asili inategemewa katika kuzalisha umeme. Hivyo basi Kamati inapendekeza:-

(a) Vipengele vya utunzaji wa visima vilivyopo kwenye mkataba vizingatiwe na Kampuni inayohusika kuharibika kwa visima hivyo iwajibike kwa kuvikarabati visima hivyo kwa gharama zake.

(b) Serikali na wasimamizi wa sekta ya gesi wahakikishe kuwa utunzaji, ukaguzi na matengenezo ya mara kwa mara ya visima yanafuatwa ili isije kutokea visima hivi vinaharibika ghafla na kuhatarisha usalama wa Taifa.

(20) Kamati imeona kuwa uwepo wa Kampuni moja ya *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* ya usambazaji wa gesi kutoka maeneo ya uzalishaji kunawanyima fursa wawekezaji wengine na hivyo kusababisha migongano ya kibiashara pamoja na bei ya gesi kutokuwa na uwiano sahihi kwa watumiaji. Kamati imepata malalamiko kutoka wadau wa matumizi ya gesi kuwa hali hii inazuia ushindani wa kibiashara na kunyima fursa kwa viwanda vya uzalishaji wa bidhaa mbalimbali vinavyotumia nishati ya gesi kukua na kutanuka na pia kudumaza uchumi wa nchi. Kamati inatoa ushauri kuwa sasa umefikia wakati kwa wadau wa sekta ya gesi kupewa fursa ilio wazi katika kutafuta, kuzalisha, kusafirisha na kusambaza gesi. Kamati inapendekeza kwa Serikali kuwa, katika Sheria ya gesi itakayotungwa ni lazima iainishe ugatuaji (*Unbundling*) kwa upande wa utafutaji, usafirishaji na usambazaji. Hii itasaldia kukuza sekta ya gesi nchini kwa kuwa kampuni nyingi za gesi zitahusika kikamilifu na gharama kwa watumiaji kupungua kutokana na ushindani.

(21) *TPDC* akiwa ndiye msimamizi wa Sekta ya gesi kwa niaba ya Serikali Kamati inashauri shughuli zote za uwekezaji katika Sekta ya Gesi zisifanyike bila ya kuihusisha *TPDC*. Aidha, *TPDC* ihakakishe gharama zinazoingiwa kwenye mradi wanazihakiki ipasavyo. Pamoja na hayo Kamati inasisitiza shughuli zozote za uchimbaji zisiendelee bila ya kurekebisha visima ambavyo vimeharibika.

(22) Kamati imebaini kuwa fedha zinazotolewa na wabia wa *TPDC* katika utafutaji wa mafuta na gesi kwa lengo la kutoa mafunzo ya wataalam mbalimbali katika Sekta ya gesi

hazitumiki kwa malengo yaliyokusudiwa. Kamati imebaini kuwa fedha zinazofikia dola za Kimarekani milioni 1.75 kwa mwaka zinazotolewa na wabia hao hazitumiki kwa malengo yaliyokusudiwa. Aidha, Kamati imebaini kuwa sehemu kubwa ya fedha hizi zimekuwa zikitumika kulipia safari zisizo za mafunzo kwa Viongozi na Maafisa Waandamizi wa Wizara. Kamati inaona kuwa kitendo hiki ni ubadhilifu mkubwa wa fedha za umma na hivyo uchunguzi ufanywe kwa ajili ya hatua zaidi kuchukuliwa.

(23) Kufuatia kitendo cha Serikali kutumia fedha zilizokuwa zimepangwa kuondoa utofauti wa bei (*National Tariff Equalization Fund*) kinyume na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge, Kamati inaishauri Serikali kuanzia sasa kutumia fedha kwa ajili ya malengo yaliyokusudiwa na kuidhinishwa na Bunge. Aidha, inapoonekana kuna ulazima wa kubadili matumizi ya fedha hizo zilizoidhinishwa na Bunge, ni vizuri taratibu zinazotawala Sheria za Fedha zikazingatiwa na bila kuathiri Mamlaka ya Bunge.

(24) Kamati imejiridhisha kuwa hakuna mpango mahsus wenyewe kuonesha kalenda ya ulipaji wa mkopo wa dola za Kimarekani milioni 216 na kwamba kiasi gani kitalipwa na lini. Ni mapendekezo ya Kamati kuwa pamoja na manufaa ya mradi huu Mamlaka zinazohusika zinapaswa kuijandaa kwa kupanga ni lini na kwa namna gani watalipa deni hilo pamoja na riba yake kwa wakati.

(25) Kamati imebaini kuwepo kwa kasoro katika ulipaji wa kodi mionganoni mwa Makampuni. Kamati inaishauri Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) iongeze udhibiti katika ukusanyaji wa kodi katika sekta ndogo ya gesi kwa kushirkiana na Mamlaka na Taasisi nyingine za Kiserikali na sekta husika.

(26) Ili kulinda misitu na kupunguza gharama kwa wananchi, Kamati inaishauri *TPDC* iwezeshwe ili kuweza kutekeleza miradi ya gesi nchini kwa matumizi ya viwandani, majumbani na kwenye magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, Kamati inatambua kabisa umuhimu wa uwekezaji hasa uwekezaji unaohusisha sekta ya nishati, Kamati itaendelea kuheshimu, kushawishi na kuunga mkono juhudhi za Serikali na wadau mbalimbali katika uwekezaji wa sekta hii. Lakini kamwe haitakaa kimya, haitokubali wala kuunga mkono ubadhilifu katika sekta hii. Aidha, ielewewe kwamba Kamati inakemea moja kwa moja vitendo vya hila, ghirba na hujuma za kimahesabu zillizofanywa na Kampuni ya *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwa hakuna usimamizi thabiti na makini katika sekta ya gesi ambao kwa kiwango kikubwa unasababishwa na kutokuwepo kwa Sheria ya Gesi na hivyo kufanya sekta ikose mwongozo. Kamati imeridhika kuwa pasipo sheria ya gesi huwezi kuendeleza, kusimamia na kulinda maslahi ya nchi katika sekta hii. Kutokana na hali hiyo Kamati inaishauri Serikali kuharakisha haraka iwezekanavyo mchakato wa kutunga Sheria ya Gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kuwepo kwa maeneo mengi yenye utata ndani ya mikataba hii yanayosabisha migogoro na kuhatarisha maslahi ya nchi, Kamati inaishauri Serikali kuagiza wadau wote wanaohusika na mikataba hii kukaa na kurekebisha vipengele vyenye utata ili kuleta ustawi wa sekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasilitiza kuwa, Serikali iiamuru Kampuni ya *Pan African Energy Tanzania Limited* ilipe mara moja kiasi cha dola za Kimarekani milioni 20.1 ambazo ni gawiwo la Serikali ililopunjwa kutokana na *Pan African Energy Tanzania Limited* kukiri kujirejeshea isivyo halali dola za Kimarekani milioni 28.1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kutokana na kitendo cha Kampuni ya *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)* kuandaa na kuwasilisha mahesabu yasiyo sahihi. Kamati inaishauri Serikali ichukue hatua za kuchunguza kama kuna ukiukwaji wa Sheria za nchi na ianze mchakato wa kuwashtaki wahusika na pia kusitisha Mkataba na *Pan African Energy Tanzania Limited (PAT)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kurudia kukushukuru wewe binafsi na Bunge lako Tukufu kwa kukubali ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini wa kuunda Kamati Ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani za dhati ziende kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa kujitoa kwao na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika. Napenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa majina kama ifuatavyo:

Mheshimiwa January Y. Makamba, Mwenyekiti; Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mjumbe; Mhe Mariam Nassoro Kisangi, Mjumbe; Mheshimiwa Catherine Valentine Magige, Mjumbe; Mheshimiwa Amos Gabriel Makala, Mjumbe; Mheshimiwa Khalfan Hilaly Aesh, Mjumbe; Mheshimiwa Abia Muhamma Nyabakari, Mjumbe; Mheshimiwa Charles John Poul Mwijage, Mjumbe; Mheshimiwa Yusuph Abdallah Nassir, Mjumbe; Mheshimiwa Christopher Olonyokie Ole-Sendeka, Mjumbe; Mheshimiwa Dkt. Festus Bulugu Limbu, Mjumbe; Mheshimiwa Shafin Amedal Sumar, Mjumbe; Mheshimiwa Selemanni Jumanne Zedi, Mjumbe; Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga, Mjumbe; Mheshimiwa Josephine Tabitha Chagulla, Mjumbe; Mheshimiwa Mwanamirisho Taratibu Abama, Mjumbe; Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mjumbe; Mheshimiwa Suleiman Masoud Nchambis Suleiman, Mjumbe; Mheshimiwa Kisyeri Werema Chambiri, Mjumbe; Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, Mjumbe; Mheshimiwa Sarah Msafiri, Mjumbe; Mheshimiwa Munde Abdallah Tambwe, Mjumbe; Mheshimiwa Vicky Kamata, Mjumbe na Mheshimiwa John J. Mnyika, Mjumbe. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani za pekee kwa Wajumbe tisa wa Kamati ndogo chini ya uenyekiti wa Mhe. Diana Mkumbo Chilolo, ambao walijitoa kwa hali na mali na kufanya kazi bila kuchoka, kwa hakika wamefanya kazi kubwa sana na wanastahili pongezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile shukrani zetu ziende kwa wadau wote wa Sekta ya Gesi waliofika mbele ya Kamati na kutoa maelezo na ufanuzi wa hoja mbalimbali zilizojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dokta Thomas D. Kashilillah kwa kuisadia Kamati hii kufanya kazi vizuri. Aidha, nawashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano walioipa Kamati katika kutekeleza jukumu hili kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, nawashukuru Makatibu wa Kamati hii Ndugu Pamela Pallangyo na Ndugu Michael Kadebe kwa kuisadia Kamati na kufanikisha kumaliza kazi hii kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (Makof)

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Nashukuru hoja imetolewa na imepokelewa. (Makof)

Nakupongeza sana kwa taarifa ambayo umeiwasilisha hapa jioni hii ya leo na pia niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa mahudhurio ambayo mmeonesha kwamba mmeliwekea uzito suala hili. Sasa tunaanza majadiliano. Lakini naomba tu muelewe kwamba walioomba kuchangia hoja hii au taarifa hii ni wengi sana na taarifa hii inapaswa kwa vyovyote vile tuikamilishe leo. Kwa hiyo, naomba wale ambao kwa bahati mbaya mmeleta maombi yenu na hamtakuwa mmebahatika kuchangia basi tuwaamini wale ambao watachangia kwa niaba yetu.

Baada ya kusema hayo, naomba sasa niwataje ambao nitaanza nao sasa hivi; Mheshimiwa Murtaza Mangungu, atafuata Mheshimiwa Nassir Abdallah na Mhweshimiwa Engineer Mohamed Mnyaa, ajiandae.

Mheshimiwa Mangungu!

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya mwanzo ili niwe mchangiaji katika hoja hii iliyo mbele yetu. Kwanza kabisa namshukuru Mheshimiwa Spika, kwa kukubali kuunda Tume hii, lakini pia nampongeza sana Mheshimiwa Januari Makamba, pamoja na kuwa gesi haitoki katika eneo ambalo yeye lina nasaba naye, lakini naamini kabisa kwa uzalendo wake aliona ni jambo muhimu sana kuweza kufanyika uchunguzi huu. Binafsi ninazo kila sababu kuwapongeza Wajumbe wote walioshiriki katika kufanikisha Kamati hii na najua uzito wa kazi ambayo wamefanya, wamefanya kazi katika mazingira magumu, pamoja na hayo yote wamekubali kulitumikia Taifa hili katika hali ya uzalendo kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Bunge lako lifahamu na nilikumbushe sisi watu wa Kilwa, ndio tuliokuwa wa kwanza kabisa kupigana vita ya uhuru wa Mwfrika katika ukanda mzima wa Jangwa la Sahara na Baba wa Taifa alivyokwenda *UNO* alisema, nimekuja kudai uhuru wa Wamatumbi hawa, Wamatumbi amba walikuwa wanazungumzwa ndio sisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti hii pamoja na kuwa imesomwa katika hali ya uharaka, lakini imejawa na mambo mengi sana ya masikitiko. Kwa kweli, ingekuwa inaruhusiwa ningependa nitumie dakika zangu zote ntile, ili kuonesha kilio cha watu wa Kilwa na Tanzania nzima. Mradi huu wa gesi katika Visiwa vya Songsongo una historia ndefu sana, toka kabla sijazaliwa, mpaka napata akili yangu na mpaka hii leo nimekuwa Mbunge katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianzie pafupi, mwaka 1996 wananchi wa Kilwa walifungua kesi Mahakama Kuu kupinga mradi huu wa gesi usihamishwe kutoka Kilwa kuletwa Dar-es-Salaam na mradi huu ubakie palepale Kilwa ili wananchi wa Kilwa, wanufaikie na gesi hii. Nitazungumzia matatu tu kati ya mengi ambayo yanawaathiri, watu wa Kilwa.

La kwanza, umeme amba tunautumia hata ndani ya Bunge hili leo hii, inawezekana kabisa unatokana na gesi ya Songsongo. Lakini maeneo ambayo gesi inatolewa na maeneo yanayozunguka, mpaka hii leo hayana umeme! Ni jambo la kusikitisha sana! Maeneo ya Somanga, Tingi, Miteja, Nangurukuru na Matandu wakati ilitakiwa kabisa wananchi wote wa Mingundi, Kipatimu na Chumo, wanufaikie na umeme huu, mpaka hii leo, hatunufaiki! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1996 kama nilivyo sema kwenye kesi ile, uliingiwa Mkataba baina ya Ofisi ya Waziri Mkuu na wakazi wa Kilwa ili wafute ile kesi. Ni jambo la kusikitisha mwaka huu mwezi Oktoba, wananchi amba walikuwa wanafanya kazi ya ulinzi kwenye kituo cha gesi ya Songsongo pale *Songas*, wamefukuzwa kazi bila malipo na bila hali yoyote ya kiutu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifuata ripoti hii Kamati imependekeza, ipo haja kabisa ya Sheria ya Gesi itungwe kwa haraka ili na sisi tuweze kunufaika na kupata *royalty*. Nikizingatia ripoti ya Kamati hii, dola milioni 10.6 zimepatikana kwenye mwezi wa Agosti peke yake! Hapo na sisi tungeweza kupata *royalty* ya 3% tu! Ina maana kabisa 3% ingekuwa kwa hesabu za haraka haraka, zaidi ya milioni 530, ingeweza kutunufaisha sana. Lakini kwa mujibu wa ripoti hii, kumekuwa na udanganyifu uliopindukia. Sasa pamoja na mambo mengine yote naomba Bunge lako liridhie na liunge mkono jitihada za Kamati hii na mapendekezo ambayo yametolewa na Kamati hii. Bunge hili liyarihidhie na Serikali tunaamini kabisa kutokana na usikiu wake, wayazingatie na mkataba huu uvunjwe na ikiwezekana hawa watu waondolewe mara moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaonesha kabisa kwa kiasi gani na kwa namna gani, hawa wenzenetu amba tunawaita ni wawekezaji wamekuwa ni wababaishaji na hawana nia ya kutuendeleza sisi na kunufaika na rasilimali zetu kama Watanzania. Binafsi, kama ningekuwa kwenye mamlaka ya kushtaki nisingesubiri Kamati hii na Bunge hili liridhie! Hawa watu walitakiwa washtakiwe mara moja kwa sababu wame-commit criminal offence. Leo hii ikiwa gharama za uzalishaji wa gesi kutoka Kilwa, zinakwenda kujumlishwa na gharama za uendeshaji wa visima vingine vya gesi na utafiti mwingine katika nchi nyingine tofauti kama ilivyotamkwa hapa Guinea, Nigeria, Ghana na Uganda! Hili ni jambo la kusikitisha sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kabisa na maoni ya Kamati, lakini pia ningeomba na ningeshauri, mapendekezo haya ya Kamati kwa pamoja yalenge kutunufaisha sisi kama

Watanzania; lakini pia yalenge kuwanufaisha wananchi wa Kilwa, ambao wamesumbuka na wanasumbuka sana. Sasa hivi, Serikali imeingia Mkataba mpya na *China Exim Bank* kwa ajili, ya ujenzi wa Bomba la gesi kutoka Mtwara mpaka Somangafungu, ambalo litaendelea hadi Dar-es-Salaam mpaka kufika Tanga. Lakini ni kwa nini, haya mapendekezo ambayo Kamati imeyatoa, hayazingatiwi kwanza kabla mkataba ule haujaanza kufanya kazi na kujenga bomba jipya; kwa sababu, wasiwasi wangu isije ikawa tunawapa nafasi hawa watu kuendelea kutunyonya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi hasa nina mambo mengi sana ya kuchangia, lakini kwa kweli nachangia nikiwa na hasira sana. Ni jambo ambalo linanisikitisha, taarifa hii nimeipata wakati huu na sijaweza kuipitia yote na kubaini upungufu uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naomba niunge mkono hoja hii. Naliomba Bunge hili liridhie na liidhinishe mapendekezo haya yaliyotolewa na Kamati, tuiunge mkono Wizara katika utendaji wake na tuwaunge mkono wenzetu wa *TPDC* ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi kabisa na kuweza kuliletea tija Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MHE. YUSUPH A. NASSIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Lakini kabla sijaendelea, niwaulize Waheshimiwa Wabunge kwamba, watu tulio wapa dhamana hii wanatosha? Watu tulio wapa dhamana kama wabia wetu, wanatosha? Watu tulio wapa dhamana kama viongozi na watendaji wakuu, wanatosha? Basi kama hawatoshi, tuisome ripoti kwa kina na ikiwezekana tukapitie hata vile vielelezo au ushahidi uliotoka kwenye maeneo mbalimbali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa tangulizo hilo, ni ukweli usiopingika kwamba, Mkataba wa *Production Sharing Agreement* kati ya *Pan Africa* au hata uliomo wa *Songas* na Serikali yetu, kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli ni lazima uangaliwe upya, ama kwa kutengua vifungu au kwa kuufuta kabisa! Kwa sababu, hauna maslahi huko tuendako kwa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yale yaliyosemwa na Msomaji wa Taarifa yetu. Kuna baadhi ya maeneo aliyaruka na kwa sababu, alishatoa tangulizo la kwamba *Hansard* ipokee, tunachoweza kusema ni kwamba kuna upungufu mkubwa katika mkataba huu tulio kuwa nao ukilenga maeneo ya manunuzi, usiri katika uwekezaji na hata kutumia ubabe pale ambapo taasisi ya Serikali inapoamua kwa dhati kutaka kuwekeza ili angalau tuweze kuongeza *share* zetu kama Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ikakatazwa! Waheshimiwa Wabunge, umaskini ni kitu kibaya! Mkopo huu ulikuwa ni wa Serikali, ukaomba kutoka taasisi mbalimbali dola milioni mia mbili na kitu, leo hii tukakopessa *consortium* tukiamini fika. Matokeo yake tunakuja kunyimwa! Tunanyimwa haki ya kuwekeza na hatimaye pia tunaibiwa! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu upungufu huo uliozungumzwa wa kimahesabu au wa kiukaguzi, utupe picha halisi. Haiwezekani kwa kipindi *consecutively* cha miaka sita uwe unarejea kosa hilo hilo! Jamani huu ni wizi wa kukusudia! Haikuwa hivyo tu, tumejifunza mengi kutokana na kauli mbalimbali za watendaji kutoka Taasisi mbalimbali zinazowekeza kule; kwamba, kampuni ya *Pan Africa*, sijui ni nani aliyweweza na hata uongozi wa *Songas*, sijui ni nani anayeweza kuwapa kiburi cha kuweza kutuambia maneno mengine mazito. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa mahojiano yetu walisema Mkataba ulioingiwa pale ni *Biblical, we can not change the word*. Haya yalisemwa bayana! Sasa tukae leo tutafakari tutaendelea kufungwa mikono na mikataba hii? Au sisi kama kizazi na Taifa letu kufika miaka 50, tutaangalia kwa kina na kuangalia maeneo yenye udhaifu? Lakini haikuwa hivyo tu, kumekuwa na *message* nyngi za kutumia majina! Niseme tu, nimpe pole hata rafiki yangu sana Kiongozi mwenye dhamana, kwa maana ya Waziri Ngelleja. Hata kwenye *document* waliyotutumia juzi, wamemtaja wazi kwamba yeeye kawashauri kwamba, Kamati haina meno! Kamati ya Nishati na Madini itatoa tu ushauri! Hii ni *document* kutoka kwao na wametutumia *e-mail* ya kutuambia Waheshimiwa Wabunge, mtakachosema hakina maana! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niseme tu, sijui tunawezaje kutoa siri za hapa zikawafikia wawekezaji, halafu hatimaye sisi tudharaulike! Lakini kama ushauri tunaoutoa kwa Serikali hii...

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ridhaa yako naweza nikasoma *the last note*.

WABUNGE: Soma!

MHE. YUSUPH A. NASSIR: ... "Pan African Tanzania, understands the Parliament Committee can advise Parliament and that the Ministry can act or not on that advice. And that the recommendations have to be passed into law, before they can be enforced."

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yametokea wakati wa kikao walichosema hapa, "Minister Ngeleja, November 15th Meetings na kuna a lot humu ndani. Si hivyo tu, wametumia hata nafasi ya usiri wa kuhamisha mamlaka tofauti; mazungumzo yaliyofanyika kwenye nyumba nyeupe, unakwenda kuyaweka kwenye karatasi kama hii halafu unaya-circulate! Leo hii kila mtu anayo! Ya kwamba, aah! Sijui nisemeje, lakini ni kwamba..."

WABUNGE: Sema!

MWENYEKITI: Naomba msiongee. Tafadhalii naomba msiongee, msikilizeni zamu yenu ikifika mtachangia.

MHE. YUSUPH A. NASSIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba tumepewa uhakika, Rais wetu amepewa uhakika kwamba, mkataba huu hautaguswa. Kwa maana ya Rais wa *Pan Africa*, amekuwa assured kwamba, mkataba huu hautaguswa! Sisi tumeona mapungufu na *Penal Codes*, taarifa imezileza vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema kama itawezekana taarifa hii isomwe na ijadiliwe kwa kina sana na sio kwa masaa mawili, matatu. Ningependa twende hatua kwa hatua! Tuangalie kipengele na hata *correspondence* zilizomo. Haya tulioyatoa, kwanza tu labda, naomba *declare interest*, mimi ni Mjumbe kwenye Kamati ile ndogo. Sasa haya ambayo tumeweza kuyashauri na kuyaona yamedhihirishwa; hakuna mahusiano mazuri kati ya Taasisi moja na Taasisi nyingine, kati ya Wizara moja na Wizara nyingine! Ilifikia mahali, kama sio *intervention* ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, basi leo hii tungekuwa tunazungumza vitu vingine hapa! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Pan Africa* anaweza akaja na gharama zake za miradi ambazo anafanya *single sourcing*, akaja akatafuta Mkandarasi kwa maana ya *EPC*, akaja ye ye aka-put tu cost zake and eventually *TPDC* akawa coerced kuzikubali! Wakati *EWURA* anapofanya intervention, kukaja mtazamo mwingine! Nasema sisi tulikuwa ni wajukuu na naweza nikakiri inawezekana mimi ni mijukuu wa mama Anna Abdallah, ambaye wakati nchi hii inapata uhuru alikuwa na miaka 21. Sasa baada ya sisi kufikia umri huu mkubwa na Taifa kufikia miaka 50, sijui kama tutaendelea kuyatazama haya mambo kwa mtazamo usio sahihi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, nirudie tena; ipo haja ya kuichambua kwa kina taarifa hii. Tuangalie kila kipengele, tuangalie kila upande na tuone kule ambako tutaweza kutoka kwa mustakabali, sio wa kizazi changu tu lakini kwa kizazi cha watoto wetu. Tulisema tutajifunza kwa kadiri ya uwezo wetu na kutumia elimu tulioipata kwa manufaa ya wote. Tuone basi taarifa hii iwe ni sehemu ya elimu watakayoipata wale watakaokuja kukaa kwenye viti hivi baada ya miaka 10, 15, 20 au 30. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna upungufu mkubwa sana! Kuna attitude problem kati ya Kampuni hii na Taasisi inazohusiana nazo. Upungufu huu umeelezwa kwa kina ndani ya ripoti yetu hii na ripoti kubwa. Haikuwa hivyo tu, circulation ya e-mail hii imelenga kutuvunja makali! Kwa maana ya mtakachosema Wizara au Serikali inaweza ikakichukua au ikakiacha! Lakini sio hivyo tu ni kwamba, sisi tuna uwezo wa kuagiza Rais wetu, akaja akaongea na Kiongozi kwenye nyumba fulani na hatimaye sisi mambo yetu yakaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sio hivyo tu kuna mahali wakasema kwamba, mtakapoijidai ku-temper na *PSA*, kwa context ile ile kwamba ni *Biblical*, basi sisi tuta-defend integrity yetu na kadhalika tutaweza kui-sue Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa huyu ni mtu ambaye tuliingia naye mikataba out of good faith; tukiamini kabisa hata matumizi ya maneno

yale *shall or will*, tuliona tu kwa maana ya Kiingereza chetu sisi cha shule za Kata, basi yanatosha kwa sababu mkataba wetu tunaingia kwa nia njema. Matokeo yake ni hiki ambacho tumekipata sasa! Tunanyimwa haki ya uwekezaji, tunabambikiwa gharama kutoka kwenye maeneo mengine na tunasimama mahali ambapo si sawa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Tanzania yetu inaweza ikashindana na Quatar kwa *reserves zilizopo* na huu ni mkataba mmoja tu. Tuna leseni 24 kule, je, Wizara imeweza kufanya mpango gani wa *succession plan*? Lakini wapo watu mahiri waliosema kwamba, *reforms, reforms, reforms*, tukaacha kuangalia sekta ya nishati kwa umakini wake. Nikiangalia Wizara ambayo inaongozwa na rafiki yangu mpenzi William, walibakia wote pale juu umri wao ni mkubwa.

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

MWENYEKITI: Nakushukuru Mheshimiwa.

MHE. YUSUPH A. NASSIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja na nashukuru kwa muda. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kutokana na umuhimu wa taarifa hii, namwomba Mwanasheria Mkuu wa Serikali atoe hoja ya kutengua Kanuni ya 62(a) ambayo inasema tujadiliane kwa mchangiaji kuchangia kwa dakika 15 ili tupunguze iwe dakika kumi tupate wachangiaji wengi zaidi ili hoja hii tuitendee haki.

MWANASHERIA MKUU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutumia Kanuni ya 150(1) na kwa madhumuni uliyosema, naomba Bunge lako Tukufu litengue Kanuni ya 62 ambayo inatoa masharti ya Mbunge anayejadili hoja kuruhusiwa kuzungumza kwa muda usiozidi dakika 15, Kanuni hii itenguliwe iwe dakika 10 ili kuwawezesha Wabunge wengi zaidi kuchangia hoja hii mahsus na muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki!

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, ambao hawakuafiki ni wengi, hivyo, tutaendelea na utaratibu wetu wa dakika 15. (*Makofî*)

(*Hoja iliamuliwa na Kukataliwa*)
(*Bunge ililikataa kutengua Kanuni iliyopendekezwa*)

MWENYEKITI: Lakini Waheshimiwa Wabunge mlioomba ni wengi sana, mngekubali wengi mngepata nafasi ya kuchangia hoja hii.

(*Hapa Wabunge walipiga makelele*)

MWENYEKITI: Orodha ni kubwa, lakini basi naomba tuendelee mpaka saa mbili kasororobo tutakapomaliza mjadala wetu ambapo nitamwita mtoa taarifa. Naomba tuendelee, namwita Mheshimiwa Habib Mohammed Mnyaa.

MHE. ENG. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kabla ya kuchangia, ni lazima Wabunge tuoneshe masikitiko yetu na utendaji huu wa kazi. Ikiwa Kamati imeweza kutoa taarifa muhimu namna hii, pamoja na kwamba imewasilishwa Mezani asubuhi lakini tumegaiwa nakala hii sasa hivi. Sisi wengine siyo Wajumbe wa hii Kamati, naomba Serikali isitubane kwa siku, ikiwa leo haitatosha ziongezwe siku, taarifa hii ijadiliwe kwa kina. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja taarifa hii iendelee kujadiliwa na Serikali iongeze muda.

(*Hapa Wabunge wengi walismama kuunga mkono hoja ya
Mheshimiwa Engineer. Mohammed Habib Juma Mnyaa*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

MWENYEKITI: Naomba mkae! Naomba mkae! Naomba mkae! Kutokana na utaratibu ambao tulishawatangazieni na ratiba tukawapa, tunasikitika sana, tunasikitika sana.

WABUNGE FULANI: Aaaah!

(*Hapa kulikuwa na minong'ono kutoka kwa Wabunge*)

MWENYEKITI: Naomba tusikilizane! Hoja imetolewa, mmeiunga mkono lakini naomba mnisikilize, naomba mnisikilize. Waheshimiwa Wabunge!

(*Hapa Wabunge waliendelea kunung'unika na kupiga makofi na vigelele*)

MWENYEKITI: Naomba tusikilizane! Naomba tusikilizane! Naomba tusikilizane! Nitatoa maelekezo baadaye, lakini sasa naomba kumwita mchangiaji anayefuatia Mheshimiwa Charles Mwijage.

MHE. CHARLES P. MWIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. ENG. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sijachangia!

MWENYEKITI: Sorry, sorry! Samahani, samahani, samahani, naomba kwanza kaa chini. Umetoa hoja inaonesha kwamba, wewe uliishamaliza kwa sababu ultaka uongee zaidi siku zijazo.

(*Hapa Wabunge walizomea*)

MWENYEKITI: Kwanza kuzomea siyo ustaarabu. Naomba tuwe watu wazima, tusikilizane. Sisi sote ni watu wazima Waheshimiwa, tunajua wajibu wetu, tunapozomea tunapeleka *message gani kwa Watanzania?* Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mnyaa uendelee, uwe focused kwenye points zako halafu muda wa kumaliza ni saa mbili kasorobo kwa sababu bajeti hairuhusu kuongeza siku hata moja, kesho tutaahirisha Bunge. Naomba Mheshimiwa Mnyaa uendelee. (*Makofi*)

MHE. ENG. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniruhusu niendelee kwa sababu pale nilisema kabla sijachangia. Sasa naanza kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza natoa angalizo la jumla kwa Serikali. Kuna wale watu wanaoitwa *Economic Hit Man* ambao kama mtu hawajui aende kwenye website, amuangalie kiongozi imoja anaitwa John Perkins, atapata taarifa muhimu za hawa *Economic Hit Man* ambao wanajihusisha na miradi mikubwa ya umeme, gesi na madini. Serikali nyingi duniani hupokea madeni makubwa kwa Serikali hizo ili tuwaabudu watu hawa. Tanzania kwa bahati mbaya tumeangukia pia katika kundi hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2007, Februari, iliposomwa hapa ripoti ya Richmond ilipendekeza mambo mengi, mionganoni mwa hayo ni kupitiwa mikataba, lakini hilo halikutiliwa maanani. Haya ni matokeo yake; tumekuwa na mgawo wa umeme ambao hauishi na kila siku tuna dharura. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja katika sababu kubwa nataka niwaelezeni leo hapa na Serikali itakiri udhaifu huo ambao inaufanya kutokana na mikataba. Tarehe 14 Februari, 2006, Waziri wa Nishati wa wakati huo alitutangazia hapa Bungeni kwamba, mradi wa umeme wa

Kinyerezi *uta-take off* kwa muda wa miezi kama kumi na mbili na tutakuwa na umeme wa kutosha na mgawo wa umeme utakuwa historia. Lakini wakati anatangaza hivyo alisahau kwamba, miundombinu ya gesi, bomba kubwa la gesi kutoka Songsong mpaka upande huu wa nchi kavu Kilwa unamilikiwa na Songas na ilikuwa halitoshi kwa uwezo wake. Wakati tunapanga miradi ya gesi ikawa haitekelezeki ndiyo mpaka na miaka mingine mitano inafika bado tuna matatizo ya umeme. Chimbuko la haya ni mikataba mibovu ambayo inatokana na Serikali na Serikali imekataa kuipitia mikataba hiyo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Serikali itupatia maelezo, hivi mkataba utakuwa mzuri kiasi gani ikiwa *PanAfrica, TANESCO* na Serikali yenye we wanatumia *Law Firm* moja hiyo hiyo ya *Hunton Williams* wakati sisi tuna maslahi yetu, *PanAfrica* wana maslahi yao, Songas wana maslahi yao, sisi tutatendewa haki? Serikali ije itoe maelezo hapa, itakuwaje itumiwe *Law Firm* moja kwa watu wote hawa ambao tunafanya kazi nao, ili baadaye tupate maslahi? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na mapendekezo yaliyotolewa na taarifa hii, lakini Waswahili wanasema ukiumwa na nyoka ukiona ukuti unashtuka. Mimi nashtuka kwa misimamo ya Serikali. Pendeleko hili la nne la kuvunja mkataba ndiyo wasiwasi wangu. Nataka tukumbuke mwaka 1999 kampuni ya Addax ambayo ilikuwa ina-supply crude oil tulivunja mkataba nayo na *TPDC*, matokeo yake tukashindwa kesi na Serikali ikalazimika kulipa dola milioni 10. Baadaye tayari kesi ya *Dowans* na *TANESCO* ambayo inajulikana vizuri uhalali wa mkataba ule wa Richmond kwamba haupo lakini baada ya kuvunja mkataba, Serikali hiyo hiyo inailambia Dowans wa-supply umeme na ndiyo matokeo leo Mahakamani tukiambiwa kulipa watu wanapinga lakini ukweli ni matatizo ya Serikali yenye we ili yotusababisha kufika hapa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii ambayo imesababishwa na *PanAfrica* haivumiliki. Mimi ningeshauri badala ya kuvunja mkataba kama vipengele vingine vinavyozungumza washtakiwe, wahojive na walipe madeni yetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya madeni ni makubwa na kwa upande mwingine tunaweza tukasema madeni ya gesi ambayo ni shilingi bilioni 110 au zile walizokidhi dola milioni 28 na Zanzibar ina haki yake. Gesi ni ya Muungano na tangia mwaka 2004 haijapatikana share ikapelekwa kule Zanzibar. Kwa hiyo, wizi huu wameiibia Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yote na hizi fedha na Zanzibar na sisi tusimame kidete tuzipate. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna wizi wa usafirishaji tu wa dola za Kimarekani milioni 20 nazo pia ni haki yetu. Kwa maana hiyo, hii mkataba mibovu tuliyopendekeza, Serikali ione hali halisi sasa tulipofikia na kwa mkataba hii tunayoendelea nayo hatuwezi kufanikiwa na siku zote tutakuwa na matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tusomeni, miundombinu mikubwa ya gesi tuchukue mfano jirani zetu tu wa Kenya. Jirani zetu wa Kenya ile miradi ya *geothermal*, visima vyote vinachimbwa na Serikali lakini leo Tanzania pamoja na mikataba mibovu hii ambayo inasababisha hata *TPDC* ule uwezo wa kuwekeza na sisi tukawa na *dividend* kubwa umeshindikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe masuala haya yote ambayo yanaifikisha Tanzania katika hali kama hii yasivumiliwe tena. Kwa maana hiyo, lile ombi la kuwa muda uongezwe ili tupate muda wa kutosha wa kusoma ripoti hii ili wenzangu Wabunge wengine ambao hawajachangia waweze kuja na hoja nzito, muhimu na kuweza kuiboresha ripoti hii. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naomba nitoe huo muda kwa wenzangu lakini hayo niliyosema naomba yazingatiwe. Nashukuru. (*Makof!*)

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo.

MWENYEKITI: Naamu Mheshimiwa Machali.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 55 (3) (b) juu ya hoja ya kuahirisha Bunge au mjadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kutoa hoja hii; moja ni kwa sababu ya uzito wa jambo liliopo mbele yetu. Sababu ya pili taarifa hii ilivyo nzito na muda tulio nao kwa kuwa ni kidogo either... (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa samahani...

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, sijamaliza!

MWENYEKITI: Samahani basi, tusibishane! Hebu samahani, kaa utaendelea...

(*Hapa Waheshimiwa Wabunge waliguna kuonesha kutokulaliana na Mwenyekiti kumkatisha mzungumzaji*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa, pamoja na hii hoja ambayo unaelekea kutoa lakini pia tuzingatia ule uhalisia kwamba, kwa vyovytote vile kwa sababu mambo haya yana budget implication vileyile, tunaposema tu-extend lakini hali halisi hairuhusu tulizingatia hilo. Sasa endelea Mheshimiwa Machali.

(*Hapa Waheshimiwa Wabunge waliendelea kuguna*)

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, either hii hoja tuiongezee muda kwa kipindi hiki ambacho bado tunaendelea na Bunge, badala ya kumaliza kesho tuiongeze muda next week au kama haiwezekani kuongeza muda kwa sababu ya ukata wa fedha, natoa hoja tuiahirishe hoja hii mpaka hapo mwakani tutakapokutana mwezi Februari tupate muda wa kujadili kwa kina. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja.

(*Hapa Wabunge wengi wallsimama kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Moses J. Machali*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

KUHUSU UTARATIBU

MHE. CHRISTOPHER O. OLE- SENDEKA: Kuhusu utaratibu!

MBUNGE FULANI: Anza na wewe.

MBUNGE MWINGINE: Utaratibu wa nini?

MBUNGE FULANI: Nataka kuwaunga mkono ninyi.

MWENYEKITI: Naomba mkae.

MWENYEKITI: Naomba mkae! Mwanasheria Mkuu!

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaona kama kuna mtafaruku ambao tunaweza kuumaliza kwa kutumia busara na Kanuni zetu. Kanuni ambayo Mheshimiwa Mbunge Machali ameitumia inakupa nafasi kuamua kama jambo analozungumza ni la dharura.

Lakini pili muda ambao umebakira tungeweza kuutumia kujadili hoja hii na kama kutakuwa na watu wengine ambao wamebakira tunaweza kuamua tukachukua ushauri wake huo kwamba, hoja hii kama italala basi tutajadili kwenye Bunge la mwezi wa pili. (Makofi)

Ili kuwapa Waheshimiwa Wabunge nafasi ya kusema na kutushauri kwa sababu kwa upande huu wa Serikali hakuna anayefunika chochote katika hili. Ni vizuri Wabunge kama washauri na wasisimazi wa Serikali kama wanaona kwamba, nafasi haitoshi basi utumie ridhaa yako kama utaona inafaa wakati huo tutakapokuwa tumefika saa mbili kasorobo kufanya maamuzi kama Kanuni ya 55 inavyokutaka ufanye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninarudia kusema kwamba, ni wewe, hii ridhaa ni yako na Kanuni zinasema Kiti kiheshimiwe lakini pia kuna hoja nzito ya kuwa wazi katika jambo hili. (*Makofi*)

TAARIFA

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

KUHUSU UTARATIBU

MBUNGE MWINGINE: Kuhusu utaratibu!

MWENYEKITI: Naomba mkae chini. Waheshimiwa Wabunge, mimi nadhani hoja ambazo zimetolewa hapa zote ni *genuine* kwa manufaa ya nchi yetu, lakini nakuombeni tuendeleee baadaye nitatoa utaratibu ambao tutaufuata kwa sababu huko mbele nitawahoji kuona ni wangapi wanaafiki hoja hii ya kuupeleka mjadala huu kwa Bunge la mwakani. Tutaona wangapi wataafiki na wangapi hawataafiki. Kwa hiyo, sasa hivi naomba tuendeleee kujadiliana.

KUHUSU UTARATIBU

MBUNGE FULANI: Kuhusu utaratibu!

MWENYEKITI: Huu utamaduni, Mheshimiwa naomba ukae chini. Kwanza utaratibu wetu haumruhusu Mbunge kuanza kuongea kabla ya kuruhusiwa na Meza Kuu. Naomba tizingatie Kanuni zetu, tumejiwekea wenyewe hapa, tizingatie, naomba muamini baadaye nitawahoji. Kwa sasa hivi naomba tuendeleee kujadiliana. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mwijage aendelee na baadaye Mheshimiwa Mkosamali na Mheshimiwa Saidi Mtanda wajiandae.

MHE. CHARLES P. J. MWIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nisingekuwa Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini na kama nisingekuwa nimeshiriki katika kazi hii ningesema hii ripoti ni *scientific*, ni *objective* na ni *future focused*. (*Makofi*)

Hii taarifa inatoa mwangaza wa nchi yetu, naiambia Serikali yangu kwamba ipo haja ya kujitazama na kuijangalia kwamba hizi jitihada za kutafuta rasilimali na hasa gesi na mafuta tumejiandaa andaaje? Afadhalii ukaenda kwenye shamba la bibi ukachuma ukaondoka lakini huu ni utamaduni wa kula mali ya Marehemu na unakula mali ya yatima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna Sheria ya Gesi wala hatuna Sheria inayotawala mchezo, unaleta timu kubwa za *Manchester City* na *Manchester United* lakini Simba na Yanga unawaambia ingia uwanjani mcheze bila Sheria bila *referee*. Nchi hii Wabunge wenzangu muelewe shughuli zinaendelea lakini hakuna Sheria inayodhibiti gesi, kwa nini tusilet Sheria ya Gesi kwa dharura? Hapo ndipo tulipopotelea, watachukuliwa watu watorelewe kafara na watalaumiwa watu lakini hatuna Sheria ya Gesi, kwa nini?

Kwa nini unaacha mlango wazi kisha unamlamu mwizi amekuibia, kwa nini uliacha mlango wazi? Ni bahati mbaya au ni makusudi? Kuna kasoro katika utayari wa kuchuma rasilimali, nisingependa kugeuka fisadi lakini hata wakija wanaharakati hakuna Sheria ya Gesi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaeleze jambo lingine ambalo nimeshiriki sana, hawa wawekezaji, bahati mbaya sisi hatupingi uwekezaji, tunawahitaji wawekezaji na tunatambua

gharama kubwa za kuchimba mafuta kwa teknolojia ambayo hatuna. Jambo linalonisikitisha mimi Mwijage ni kwamba hawa watu wana vitisho, wana vitisho na ninadhani hata Waziri wa Nishati na Madini anatishiwa, wana vitisho vya ajabu! Wanasema kwamba kama tutafanya lolote kwenye *message* aliyotoa rafiki yangu kwamba kila mtu aliyepo kwenye sekta hii atajuta, wamesema kwa Kiingereza na imeandikwa hapa. Wanatutishia na ninawashukuru wenzangu nimewaambia wote kwamba msiogope kama ni kufa tufe lakini nikifa naitetea nchi yangu najua nitaitwa mwenyeheri. (*Makof!*)

Ndugu zangu, tatizo ni kwamba hatuna utayari na mfano mmoja niliotha kwamba Serikali ilishindwa kutoa kibali cha kuajiri wataalamu, madhara yake tumepoteza maelfu ya pesa. Ni kwamba hatuna utayari lakini uwezo wa kusomesha watu tunao na utsalamu uliotakiwa siyo wa kutisha. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo inahusu *management* ya shughuli nzima ambayo ipo hovyo. Kuhusu mikataba sisi hatusemi kwamba tuvunje mkataba lakini hata vile vipengele vya mkataba ambayo rafiki yangu anaviita *will and shall*, unajua mtoto aliyesoma shule ya Kata hawezu kutofautisha maana ya *will* na *shall* lakini maneno haya kwa wanasheria yana *impact* kubwa, hata vile vifungu ambavyo tunavikubali ambavyo watetezi wa mikataba hii wanasema ni matakwa ya wakati kwamba wakati ule ilibidi twende vile, hata vifungu vile hawa wabia wamevikiuka. Linakuja tatizo na niliposema kwamba hawa wawekezaji wanaitishia hata Wizara, Wizara inashindwa kuwakemea. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekwenda China kukopa, Serikali yetu tumeipongeza, mkopo wa China ni 22% lakini hawa wawekezaji sasa hivi wanahangaika, wanatembea nyumba kwa nyumba, jana niliwaambia rafiki zangu niliokuwa nao wakati nimevaa shati la kijani. Wapo hata Dodoma hapa wanataka kuja kuwekeza nchini kwa kukopa 22%, ndiyo nasema Serikali yangu msikubali mikopo ya 22% twende kwa rafiki zetu wa China hata ukimfufua Kambarage atakwambia rafiki yetu ni Mchini twende tukakope China tujenge wenywewe. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bajeti iliyopita baada ya suala ya *Pan African* kuleta utata Waziri Kivuli alitaka iundwe Tume, mimi nilisimama nikakataa nikasema hata kama binti yako ananyanyaswa si busara kwenda kuvunja ndoa, tuma watu wakapeleleze. Wapelelezi tumekwenda tumepeleleza tunawaambia kuna mashaka. Sasa naliambia Bunge kwamba kuna haja ya kuunda Tume kuangalia namna tunavyoendesha rasilimali hizi, Tume Teule ya Bunge iangalie mambo haya kwa upana kwani hatutakubali kubaki na mashimo na mimi binafsi nisingependa wajukuu wangu wanihesabu kwenye kundi la shemeji yangu Marehemu *Chief Mangungu* aliyeuza nchi kwa shanga, siwezi kukubali. (*Kicheko/Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumefanya kazi kwa hadidu za rejea, washiriki katika *industry* moja wanapaswa wawe na uhusiano. Napenda niwaambie kwamba uhusiano katika sekta ile si mzuri. *EWURA* inabishana na Waziri, Waziri anatoa *documents* yaani nyaraka ambazo mwekezaji anazitumia kwenye Mahakamani kuishitaki *EWURA* hakuna kinachoeleweka. Ndiyo maana ilifika mahali tukasema basi *EWURA* na yenyewe igatuliwe ili Waziri apewe watoto wanaoweza kumsikia, hakueleweki kule kwani uhusiano ni mabovu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa mahusiano *TANESCO* analia, *TANESCO* katika bili anazotuletea analazimika kupokea gharama zote kama zinavyoletwa na *Songo gas*, yeye hawezu kuhakiki kwa hiyo kila gharama inayoletwa inakwenda moja kwa moja, someni ripoti mtaona, *TANESCO* naye analia na *TPDC* analia hao ndiyo mimi nawaita wa Marehemu, watoto wa Marehemu lakini mtoto wa kufikia anakula chakula kizuri. Haiwezekani! (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *terms of reference* tuliopewa tuliulizwa kama kuna hali ya kuviza yaani hali ya kuzuia uhamashaji wa *gas*, ndiyo! *Songo gas* amekuwa akizunguka, tumeiandika. Analambia eti Serikali isijenge bomba iache yeye atafanya, mradi anaotaka kuufanya una gharama za ajabu na Wizara haijasema na Serikali haijasema. Kwa hiyo, kuna hali ya kuviza ndiyo mliyotutuma tumeyaona na tunawaambia haya songa mbele. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiyi, mlitutuma tukaangalie kama kuna ukiritimba katika sekta, ndiyo, ukiritimba upo katika sekta. *Songo gas* na *Pan African* hawaruhusu mtu mwingine aingie, tumewashauri na tumewaaambia na walipojua sisi tumekuwa makini, unajua *handsome boy* nikiwa nahoji mtu usiombee! Walipoona tumekuwa makini tumewahoji kwa nini visima vilivyoharibika vilivyokuwa vinatengeneza gesi kwa nini visikarabatiwe? Wamekimbia wamekwenda kutafuta mtambo mwingine na jana wamenitumia *email* kwamba mashine imeshafika, wanantumia *email* mimi ni nani? *Wana-post* kwenye ma- *internet* ya duniani kama imekuja. Kwa nini visima nya kwanza vilivyokuwa na gesi visikarabatiwe? Kama *PSA* inavyosema msidhani tunataka kuvunja mikataba, hapana iheshimu *PSA* mkarabati visima nya kwanza halafu tuje tuendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sipo kwenye hali nzuri kwani naona mali ya Marehemu inaliwa, siko kwenye hali nzuri naililia nchi yangu. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ole-Sendeka!

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeomba kusimamia kupitia Kanuni ya 68(1) na Kanuni ya 5. Kanuni ya 5 inaongoza na kubainisha mamlaka ya kiti chako na kwamba Spika atafanya kazi kwa kuzingatia Katiba na Sheria nyingine za nchi na Kanuni nyingine zilizopo, maamuzi ya awali ya Maspika wa Bunge pamoja na mila na desturi za Mabunge. Nataka kusitiza maamuzi ya awali ya Maspika wa Bunge. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo hoja nzito ambayo ndiyo nilikuwa nasema, najua utaelekeza kutuhoji lakini nilitaka utumie mamlaka yako, mimi ni Mjumbe wa Kamati hiyo ambayo imewasilisha taarifa hii. Rai yangu ambayo nilitaka kuomba utumie mamlaka yako kwamba upo uzoefu amba Bunge hili liliweza kuendeleza lakini Kamati ya Uongozi ilitwa kwenye chumba kilichopo nyuma ya hapo ulipokaa na ikashuriana na Serikali wakati wa hoja ya Mheshimiwa Kabwe Zitto na ikaja na rai ambayo ilipelekea baadaye kuundwa kwa Kamati Teule ambayo mimi nilitoa hoja. (*Makof*)

Ombi langu ambalo limetolewa baada ya Wabunge wengi kuzungumza umuhimu wa hoja inayojadiliwa ni kukuomba usituhoji mwishoni bali mjadala uendelee, usiku Serikali ikae na Kamati ya Uongozi iweze kuongeza muda ili hoja hii iweze kutendewa haki badala ya kuamuliwa kwa uamuzi wowote utakaoutoa ila mnaweza mkatafakari usiku wa leo na kesho mkatoa uamuzi baada ya kipindi cha maswali na majibu ili hoja hii iweze kutendelewa haki wakati Spika pia yupo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikuwa ni ushauri wangu kwa kutumia mamlaka ya Kanuni ya 5 ambayo yapo mikononi mwako. (*Makof*)

MWENYEKITI: Nakushukuru Mheshimiwa Ole-Sendeka, nimepokea na nitazingatia na nitatoa maelekezo. Naomba tuendelee na sasa nitamuita Mheshimiwa Mkosamali.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii ili na mimi niweze kuchangia hoja hii ilio mbele yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimekuwa na masikitiko makubwa na mimi niseme nazungumza na nipo tayari kuifia nchi yetu kwa sababu ni Watanzania wengi ambao wanakwenda kugombea Ubunge na kukosa nafasi hizo, sasa mimi nimekuja hapa ni lazima niseme kile ambacho naamini kwamba ninaifia nchi yangu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na watu wengi wanasmama kuomba hoja hii ipewe muda mrefu kwa ajili ya kujadiliwa na nikawa najiuliza ni kwa sababu gani mnataka kuminya ili tusijadili hoja hii? Sasa kumekuwa na nyaraka ambazo zimesambaa na moja ni nyaraka hii ambayo ameisoma mmoja wa Wajumbe na mimi ninayo. Inaonyesha kabisa kwamba hawa watu yaani *Pan African*, *Songas* na wengine wameshadharau Bunge hili yaani kwamba hata tukitoa recommendation yoyote haitafanyiwa kitu chocote kile cha msingi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikawa naijuliza kwamba hiki kiburi cha namna hii cha watu mpaka wanadharau Bunge kinatoka wapi? Wakati nasoma hii *document* nikagundua nikakuta kuna sehemu imeandikwa kwamba *President Kikwete insured ORCA and the Board of Directors of PSA would not be touched* yaani kwamba Rais Kikwete ameshawahakikishia kwamba mkataba huu hautavunjwa. Ni ujisadi hakuna kinachofanyika hapa tunapoteza muda kwani ameshawaambia ukweli kwamba mkataba huu hauvunji hata maoni ya Kamati waliyoyaleta leo hayatafanyiwa kitu chochote. Kwa hiyo, nchi hii ilishafikia mwisho, imeshauzwa na tunachojadili hapa ndiyo maana nikajuliza kwa nini ratiba ya Bunge imekuwa inachakachuliwa kiasi hiki? Imechakachuliwa sana na jana mmeahirisha baada ya saa saba hamkutani tujadili ili tujadili kwa muda mfupi halafu mtuzuie kuendelea kujadili suala hili ambalo mmeshatoa maelekezo mikataba hii ya kifisadi na wizi haitavunjwa. Hatukubali na tutaendelea *ku-pressurise* Watanzania tuandamane! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikataba hii imekuwa ni mingi sana na tumejua kwamba kuna watu wazito ambao wanaisimamia na tumekuwa tunatumia pesa nyigi bure kuunda Kamati ambazo zinatumia muda na pesa za Watanzania lakini hakuna kinachofanyika. Kwa hiyo, hoja hii ni nzito sana na mimi sikutaka kabisa kuingiza ndani na kuchambua hoja hii kwa sababu nimeona hata nikichangia watu wameshatoa *directives*, nitakuwa napoteza muda. Kwa hiyo, tunaomba tuendelee kujadili hii hoja lakini wale walioingia mkataba huu wanapaswa kuwajibika kwani mkataba umeonekana ni mbovu lazima tuwajue na wawajibishwe. *TPDC* ambao hawakufanya ukaguzi wamefanya ukaguzi kuanzia mwaka 2004 wawajibishwe na Mawaziri husika wawajibishwe walikuwa hawayajui haya? Kwa nini wasiyajue wakati ni Wizara zao, mpaka tuunde Tume na tutanunda Tume ngapi ndani ya Bunge hili? Tunaomba wawajibike, tunaomba sana kwani nchi hii sasa hivi ina wawakilishi humu ndani hatuvezi tukakaa kimya tukavumilia mambo haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba niishie hapo na wenzangu wachangie. (*Makofii*)

MHE. SAID M. MTANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nitumie nafasi hii kuwapongeza sana Wajumbe...Haisikiki?

MWENYEKITI: Naomba uendelee!

MHE. SAID M. MTANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nitumie fursa hii kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati hii ndogo ambao wamewasilisha taarifa yao hapa lakini pia nitumie fursa hii kuungana na Wabunge wenzangu kwamba jambo hili ni kubwa na ni muhimu sana kwa manufaa na mustakabali wa nchi yetu kwa hiyo, muda ambao umetengwa kwa ajili ya mjadala huu kwa hakika kabisa hauwezi kutosha kukidhi kiu ya Waheshimiwa Wabunge wenzangu. (*Makofii*)

Lakini pia niungane na ushauri wa Mheshimiwa Ole-Sendeka kwamba iko haja ya ninyi wakubwa wa Kamati ya Uongozi kuka na kutafakari na kuona ni namna gani mjadala huu upate muda wa kutosha ili Waheshimiwa Wabunge waweze kuutendea haki kwa kuujadili kwa kina na hatimaye tuweze kufikia mahali ambapo Taifa hili litaweza kupata nusura kupitia sisi Waheshimiwa Wabunge na wadau wengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mdogo wangu Mkosamali amesema tunapoteza muda katika Bunge, lakini nataka nimhakikishie kwamba ni wajibu wetu sisi Wabunge na ninaamini kabisa kwamba ushauri na mapendekezo tutakayoyatoa hapa yanaweza kusaidia sana kujenga na kuimarisha na kuondoa matatizo haya ambayo yapo mbele yetu. Kwa hiyo, ninaamini kabisa kwamba hapa hatupotezi muda, ipo haja ya kuendelea kutoa mawazo yetu kwa nguvu zetu zote kwa sababu hii ndiyo kazi yetu iliyoleta hapa Bungeni hatuvezi kuikwepa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo ya utangulizi ninaomba kwanza kusema kwamba tunajadili gesi na *report* hii inasema waziwazi kwamba rasilimali hii ya gesi katika nchi yetu inatoka Mkoa wa Lindi na Mkoa wa Mtwara kwa kutaja maeneo ya Songosongo na Mnazi Bay iliyopo Mtwara. Kwa hiyo, sisi Wabunge wa Mkoa wa Lindi na Mtwara kwanza tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa rasilimali hii lakini pili tunacho kilio kikubwa kabisa

kwamba mikataba hii tunayojadili haionyeshi dalili wala matumaini kwa wananchi wa Mkoa wa Lindi na Mtwara kabla hatujazungumzia maslahi ya wananchi wa Taifa hili kwa ujumla. (*Makof*)

Sisi Lindi na Mtwara madini yetu ndiyo hii gesi tunayoizungumza hapa, lakini mikataba haulezi. Mikataba hii ambayo tunailalamikia hapa haina maslahi yoyote yale kwa wananchi wa mkoa wa Lindi wala Mtwara.

Kwa hiyo, nitumie fursa hii kuiomba Serikali kwanza, Kamati imesema tuvunje mikataba, lakini nasema ni lazima tuwe waangalifu sana kwa sababu mikataba mingi tulioivunja tumekwenda Mahakamani na hiyo Wizara ambayo ndiyo inapewa jukumu la kusimamia tumeona namna ambavyo mikataba ambayo tumewahi kuivunja ilivyoliingiza hasara kubwa Taifa hili. Ni lazima tuwe makini, ninashauri tuiptie upya, tutoe mapendekezo yatakayowezesha mikataba isiweze kutuathiri kwa siku za baadaye kutokana na kuivunja kwa hasira zetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo rai yangu ya kwanza. Hii ripoti inaeleza sana hapa kuhusu *Pan Africa! Pan Africa! Pan Africa!* Lakini ninajuliza toka mwaka 2004 hadi mwaka 2009 tunao hao wadau waliokabidhiwa dhamana hii na Serikali kwa niaba ya Watanzania *TPDC*, Wizara yenye, lakini ripoti inasema watu hawa hawaelewani na hawana mahusiano mazuri. (*Kicheko*)

Sasa ninajuliza kama *TPDC*, wenzetu wa Wizara, hawana mahusiano mazuri, hawana maelewano mazuri, ni namna gani wanaweza kushikamana kusimamia rasilimali hii ya gesi ya Watanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapata hofu kubwa sana. Lakini katika mapendekezo yote yaliyotolewa na Kamati, sioni pendekezo ambalo linaonesha kabisa kwamba hawa wenzetu wa *TPDC*, lakini pia Wizara, haiwezekani hawa watu waweze kuiba mamilioni ya fedha imetajwa hapa bilioni 46, Serikali yetu inapoteza bilioni 36 lakini Wizara iko kimya, *TPDC* iko kimya, toka mwaka 2004 mpaka leo walikuwa wapi na wao ndiyo wenye dhamana? (*Makof*)

Kwa hiyo, ninadhani ipo haja ya ripoti hii kuwaangalia na hawa, kuwamulikia macho, kumulika ili tuone kama wao nao wanahusika au hawahusiki ili hatua ziweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana na rafiki yangu, mtani wangu Mheshimiwa Mwijage pale, *in fact* ni rafiki sana. Ninakubaliana naye kwa sababu hatuna sheria nzuri na engineer alikuwa ananinong'oneza hapa kwamba iliwahi kufikia mahali ilishawahidi kuletwa rasimu ya kuangalia hiyo Sheria ya Gesi, lakini imepigwa chenga, dana dana, hadi leo hatujui rasimu hiyo imeishia wapi.

Kwa hiyo, natoa wito na changamoto kwa Serikali kwamba sasa tunahitaji rasilimali ya gesi iweze kuwanufaisha Watanzania na iweze kutumika kama kichchoeo kikubwa cha maendeleo ndani ya nchi yetu. Tuleteeni sheria hiyo tuiptishe hapa kwa haraka ili gesi yetu kabla hajaanza kutoweka, maana taarifa nilyonayo pale Mtwara, gesi ile inao uwezo wa kuchimbwa kwa miaka 99. (*Makof*)

Lakini ukisoma hapa vipengele vyta vinasema eti kwamba baada ya gesi kuchimbwa hatimaye ile mitambo iliyotumika kuchimbia gesi itauzwa baada ya shughuli za uchimbaji kukoma eneo lile na fedha ile itatumika kuhifadhi mazingira ya eneo. Miaka 99 ni leo? Yaani watu wachimbe gesi waondoke pale Mtwara baada ya miaka 99 halafu ile mitambo iuzwe ndipo ipatikane fedha ya kuhifadhi mazingira pale Mtwara, inawezekana! Kwa hiyo, ninaomba sana Serikali iletu sheria haraka ili tuweze kunufaika na gesi hii kwa kadri inavyowezekana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo jambo lingine hivi visima vyta mafuta ambavyo vimeharibika, badala ya wenzetu hawa *Pan Africa* kukarabati visima vile saba ili viweze kuendelea kutoa huduma, wanafikiria kuchimba kisima kingine kwa gharama kubwa. Najiuliza kwa kuwa gesi ile ni muhimu sana taarifa hii inasema hapa kwa maendeleo ya viwanda kule Dar es Salaam na maeneo mengine, kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, hivi hawa watu siku moja wakiamua kufanya hujuma tu baada ya kuona sasa tunawashambulia kwa namna hii, kwa namna

tunavyoona wanatumia na wanakuja kuchukua rasilimali zetu katika nchi yetu, wakiamua kufanya hujuma tu viwanda nya Dar es Salaam vitazalisha? Haviwezi kuzalisha tena. Kwa hivyo, nadhani eneo muhimu na nyeti kama hili iko haja ya Serikali kukabidhi mradi huu au visima hivi kwa TANESCO kwa sababu wao ni sehemu ya Serikali na inaweza kutusaidia sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kurudia tena kwamba watu wa Lindi na Mtwara gesi ndiyo madini yetu. Tusingefurahi hapa tunasema China wametoa fedha kujenga bomba kubwa lisafirisha gesi kutoka Mtwara ifike Dar es Salaam na iende mpaka Tanga, sisi hii hatuafiki. Tutiafiki endapo tutakubaliana kimsingi kwamba katika mikataba hiyo mipya ni lazima kiwanda hicho kiwe Mtwara, *production* ifanyike Mtwara na usafirishaji wa gesi kwenda maeneo mengine ndipo unaweza kufuata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivi! Kwa sababu rasilimali hiyo ni lazima iwaneemeshe wananchi wa Mtwara na Lindi kwa sababu hiyo ndiyo rasilimali yetu. Kama madini wenzetu wanapata mirahaba au nini, sisi kwa nini hatuingizwi ili gesi hiyo iweze kutuneemesha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Mchinga hakuna umeme, Kilwa hakuna umeme, lakini gesi inatoka Songo Songo pale Lindi inakuja Dar es Salaam. Mnazibay pale, Kwanjao pale Tandahimba hakuna umeme muda mrefu sana, lakini gesi inazalishwa ipelekwe Dar es Salaam. Haiwezekani! Hatuwezi kuvumilia kuona gesi hiyo inakwenda huko wakati watu wa Kusini mnaishia kutusifu tu ndani ya Bunge kwamba, gesi inazilishwa Kusini, hatufurahi sisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni jambo ambalo ni lazima lizingatiwe. Sina lingine hapa vifungu vingine vitachangiwa na wengine, hoja yangu ya msingi ni kwamba kiwanda cha gesi lazima kiwe Mtwara, vijana wa Mtwara na Lindi wapate ajira kule, lakini tunakubaliana kimsingi kwamba baada ya *production* kufanya Mtwara ndipo sasa mtandao huo wa kupeleka gesi Dar es Salaam na Tanga uweze kuendelea. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana. Waheshimiwa Wabunge, naomba kwa mujibu wa Kanuni ya 65(3), Mheshimiwa Machali alitoa hoja ya kwamba mjadala huu kutokana na uzito wake na kutokana na muda, uendelee ama upelekwe mbele. Sasa ili kuitendea haki hoja yake ninaomba niwahoji. Wangapi amba wanaafiki hoja ya kuupeleka mbele...

MBUNGE FULANI: Mnyika kwanza.

MWENYEKITI: Mjadala huu yaani kwa Bunge la mwakani...

MBUNGE FULANI: Naomba tumalize na Mnyika kwanza.

MWENYEKITI: Wangapi amba wanahisi kwamba mjadala huu tuendelee nao ili leo hoja hii tuihitimishe? Naomba kuhoji amba wanaoafiki kusogezwa mbele mjadala huu waseme...

(*Hapa Waheshimiwa Wabunge walipiga kelele*)

MWENYEKITI: Wangapi wanaafiki mjadala huu usogezwe mbele kwa hoja ya Mheshimiwa Machali, waseme usogezwe mbele mpaka...

(*Hapa Waheshimiwa Wabunge walipiga kelele*)

MWENYEKITI: Mpaka Bunge la Januari?

MBUNGE FULANI: Mpaka saa mbili kasoro robo.

(*Hapa Waheshimiwa Wabunge walipiga makelele*)

MBUNGE FULANI: Yaani mjadala uendelee mpaka tumalize.

MWENYEKITI: Naomba tusikilizane, *order in the house! Order in the house!* Tusogeze mpaka Mkutano wa Sita, wangapi wanaafiki?

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

MWENYEKITI: Hakuna taarifa, hoja hii tuitendee haki kwanza.

(*Hapa Waheshimiwa Wabunge walinung'unika kipinga wazo la Mwenyekiti*)

MBUNGE FULANI: Mnyika kwanza.

MWENYEKITI: *Order in the house!* Hoja ilipotolewa nilisema nitatoa maelekezo baadaye, nitawahoji. Niliwahidi kwamba nitawahoji baadaye. Sasa ninaomba tumtendee haki aliyetoa hoja hii. Wangapi wanasema tusogeze mpaka Mkutano wa Sita yaani Januari, 2012?

WABUNGE FULANI: Muda bado.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

MWENYEKITI: Ambao wanaafiki isogezwe mbele waseme ndiyo!

WABUNGE FULANI: Muda bado, muda bado!

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

MWENYEKITI: *Order in the house! Order in the house!* Mheshimiwa Ole-Sendeka naomba ukae kwanza. Naomba tukae. Waheshimiwa Wabunge, nilipendelea tuendelee kujadiliana mpaka saa mbili kasoro robo, lakini...

(*Hapa minong'ono iliendelea mionganoni mwa Waheshimiwa Wabunge wakiendelea kipinga wazo la Mwenyekiti*)

MWENYEKITI: Tusikilizane. Sasa tusikilizane, tusikilizane, tusikilizane. Ningependa kupata maoni yenu wenye, kwa sababu kila mmoja aliyesimama hapa anasema mjadala huu haujatendewa haki, hoja ni nzito, sasa kupata baraka za Bunge zima ni vema tungeamua isitokezee kusema kwamba tumeburuza Bunge. Kwa hiyo, ili kutenda haki naomba ambao wanasema mjadala huu usogezwe mpaka Mkutano wa Sita waseme ndiyo...

WABUNGE FULANI: Ndiyoooooooo!

MWENYEKITI: Wangapi wanahisi mjadala huu tuendelee hadi leo saa mbili kasoro robo tuhitimishe waseme siyo...

WABUNGE FULANI: Siyoooo!

MBUNGE FULANI: Hatujaelewa.

MWENYEKITI: Naomba mnisikilize, Waheshimiwa Wabunge ninasema hivi, naomba mnisikilize.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ufanuzi tafadhalii tunaomba utusaidie utusikilize.

MWENYEKITI: Haya naomba maoni yako Mheshimiwa *Engineer Stella Manyanya*.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Samahani kidogo pengine unakuwa hutupati vizuri. Kuna wakati Mheshimiwa Ole-Sendeka alitoa ombi kwamba kwa hali hii iliyopo na kwa sababu jambo hili ni zito na wewe uko peke yako, pengine ni vyema

ukashauriana na wenzako. Hivyo ni vema tuache mpaka kesho ndipo utupe jibu, ili uweze pia kuwasiliana na wenzako kwa sababu jambo lenyewe ni zito. (*Makof*)

MWENYEKITI: Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Lukovi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Mwenyekezi, napendekeza kwamba kwa sababu muda tunao na kesho tunashughuli ambayo Bunge linaendelea tumalize hoja hii mpaka saa mbili kasoro robo kwa busara zake Mheshimiwa Spika ataitisha Kamati ya Uongozi ndio yenyenye mamlaka ya kupanga ratiba, tutapitia hii ratiba halafu itapanga ratiba ya kesho. (*Makof*)

Kwa hiyo, nilikuwa napendekeza tungemaliza ratiba ya hoja hii mpaka saa mbili kasoro robo, hata bila kuhitimisha, tusihitimishe. Kamati ya Uongozi ambayo ina uwakilishi wa Wenyeviti wote pamoja na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, tukae na Spika ili tuweze kupendekeza jambo hili na tuweze kufikiria ratiba ya kesho. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekezi, kwa heshima kubwa naomba kutoa hoja hiyo. (*Makof*)

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekezi, naafiki. (*Makof*)

(*Hoja ilitolewa ili iamuliwe*)

MWENYEKITI: Hoja imetolewa na imeungwa mkono, sasa naomba tuendelee na utaratibu wetu wa kuchangia mpaka hapo saa mbili kasoro robo. Naomba kumwita Mheshimiwa *Engineer Stella Manyanya...*

WABUNGE FULANI: Ulisema Mheshimiwa Mnyika.

MWENYEKITI: Aah Mheshimiwa Mnyika, na baadaye Mheshimiwa *Engineer Stella Manyanya* ajiandae na Mheshimiwa Dokta Hamisi Kigwangalla ajiandae.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekezi, nakushukuru...

MWENYEKITI: Mheshimiwa naomba ukae kidogo samahani. Labda naomba nihoji hii hoja ambayo imetolewa na Waziri wa Nchi, anayeshughulikia Bunge Mheshimiwa Lukovi,

(*Hapa kulikuwa na minong'ono mionganini wa Wabunge*)

MWENYEKITI: Hapana! Makubaliano yetu humu ndani hoja ikitolewa inaungwa mkono, lakini tunahoji. Sasa naomba niwahoji, wangapi wanaafiki hoja iliyotolewa na Waziri wa Nchi, anayeshughulikia Bunge?

(*Hoja kuhusu kuendelea kujadili Taarifa ya Kamati Ndogo ya Nishati na Madini kuhusu Gesi iliamuliwa na Kuafikiwa*)

MWENYEKITI: Sasa tutaendelea mpaka saa mbili kasoro robo...

(*Hapa Wabunge walipiga makelele*)

MWENYEKITI: Wasioafiki ni wangapi?

WABUNGE FULANI: Siyoooo!

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwa sauti ambazo zimetoka hapa *definitely* wote mliafiki kwa sababu tunaangalia uzito wa zile sauti zenyewe. Kwa hiyo, naomba tuendelee, Mheshimiwa Mnyika tafadhali.

MBUNGE FULANI: Huyu wakati mwingine anajichanganya mwenyewe kwa kuendelea kusema kusema tu. Sasa tunapoteza muda, ye ye alikuwa atoe taarifa tu.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza niseme kwamba, ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini, na naunga mkono mapendekezo yote 26 ya Maazimio ambayo tunaomba Bunge hili liyapitishe. (*Makofii*)

Lakini la pili Mbunge wa Jimbo la Ubungo, ambapo pamoja na kuwa gesi inachimbwa Kusini kwa sehemu kubwa biashara hii ya gesi inafanyikia kwenye Jimbo la Ubungo ambapo kampuni ya *Songas* ina kitovu chake. Sikuwa na dhamira ya kuchangia mjadala wa leo kwa sababu mengi ya maoni yangu mengine nimeyatoa kwenye Kamati, lakini kuna mambo yametokea siku hizi mbili, tatu, mpaka leo ambayo yamenifanya nisimame kuchangia. (*Makofii*)

Kwanza, niseme kwamba taarifa hii ni muhtasari, muhtasari wa mambo mengi sana, muhtasari wa ujisadi mwingi sana, ni muhtasari wa mambo ambayo ingebidi yasemwe yote kwa ujumla wake tungehitaji kuwa na *volume* kubwa kweli kweli. (*Makofii*)

Sasa kilichonishangaza ni uamuzi wa kampuni ya *Orca exploration* ambayo ni kampuni tanzu ya kampuni ya *Pan African Energy Tanzania (PAT)* ambayo imetajwa sana kwenye taarifa hii ya Bunge, kuanza kupita pita kushawishi kwa maneno ya uongo wakijaribu kujenga uhalali wa kutaka pendekezo namba nne la azimio kutokana na *Pan Africa Energy Tanzania* kukosa sifa za uaminifu, Kamati inashauri mkataba wa *Pan African Energy Tanzania* usitishwe. Kufuatia pendekezo hili wanazunguka wakishawishi, wanazunguka wakitishia kwamba pendekezo hili lionirolewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika kwamba nikisikiliza lugha sasa hivi kutoka kwenye lugha ya kuvunja mkataba na kusitisha, naona kama sasa na sisi tumeanza kupata hofu. Nimesimama kusema naunga mkono kwamba pendekezo hili la kusitisha mkataba liendelee. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtakumbuka tarehe 15 mwezi wa saba, nilipotoa maoni ya Kambi ya Upinzani kama Msemaji wa Wizara ya Nishati na Madini, nilisema wakati ule tulikuwa tunazungumza Kampuni ya *Pan Africa Energy* nikaitaja na ilikuwa inatajwa kwa mara ya kwanza wakati ule, kampuni ya *Orca exploration* na nikasema wakati ule tuna nakala za mawasiliano baina ya watendaji wa kampuni ya *Orca* na maofisa wa Ofisi ya Rais Ikulu wakishawishi mambo mbalimbali. Tukataka Serikali ichukue hatua wakati ule, tarehe 15 mwezi wa saba, naamini hatua hazikuchukuliwa ndiyo maana mpaka leo tarehe 15 Novemba, 16, 17, 18 wanaendelea kushawishi. (*Makofii*)

Sasa ninasema kuna taarifa ya Kamati yetu hapa, lakini kuna taarifa vilevile ya nchi zao wenye, taarifa ya Shirika la Sweden, linaitwa *Action Aid of Sweden*, wametoa taarifa. Hii kampuni *Songas* ina *interest* ya *SIDA* kwa maana ya Sweden na Serikali ya nchi yao ime-*invest* kwenye kampuni ya *Pan African Energy Tanzania*. Wao wenye kwenye taarifa yao ukiondoa hii ya mambo haya yaliyomo, nayasema haya kwa sababu wenye wameanza kutlisha na sisi tunasema yaliyopo kwao wenye, kama wanapinga taarifa ya Bunge la nchi yetu, watujibu taarifa ya Shirika la nchi yao, *Action Aid of Sweden*. Inasema kwamba kampuni hii ukiondoa huu uozo wote wa ujisadi tuliosema hapa, kampuni hii toka mwaka 2004 imekwepa kodi kwa kiwango cha dola milioni 65 sawasawa na bilioni 95.7 za Kitanzania, wamekwepa kodi kwa ripoti zao wenye. (*Makofii*)

Sasa kama hawa wanatuibia kwenye mapato yetu na wanakwepa kulipa kodi kwa taarifa zetu na kwa taarifa zao wenye, tunaogopa nini kujadili/kusitisha mkataba? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja zote za Kamati na ndio maana wakati ule tulipendekeza kuundwa kwa Kamati Teule kwa sababu Kamati za Bunge zinafanya kazi kwa njia za kawaida sana na Kamati Ndogo zinafanya kazi kwa njia ya kawaida sana. Lakini Kamati Teule ya Bunge kwa mujibu wa Sheria za Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge ina mamlaka makubwa sana ya kuitisha nyaraka, kuitisha mashahidi na mashahidi wakafanya kazi kwa kiapo cha kutenda yale wanayoyatenda na kusema yale wanayoyasema. Sasa kama bado wanaendelea kulitisha

Bunge letu na kuwatisha Wabunge waelewe tu kwamba bado fursa ipo hata Kamati Teule inaweza kwenda mbele zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nilitaka kulisema hapa kwamba jambo hili limejitokeza kwenye pendelezo la Kamati, pendelezo hili Azimio mojawapo la Kamati ni Azimio namba 5. Nitasa sehemu ya mwisho tu ya pendelezo namba 18. Inazungumza baada ya kueleza uozo huo wote; "Kamati inashauri Serikali kuwajibisha viongozi wakuu na watendaji walohusika na uzembe na kuteua wengine wenyewe uwezo haraka iwezekanavyo." (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu naunga mkono Azimio hili la kuwajibisha viongozi wa Wizara. Kwa kweli nilitarajia Waziri Ngeleja kwa sababu alikuwa anayajua haya kiubinadamu, kiustaraabu ningetarajia ajizulu. Lakini kwa sababu hajajizulu naomba niwe mkweli hapa nina *Hansard* ya Bunge ya Kikao cha Bunge cha Februari, 2010 na nina *Hansard* ya mwaka 2008. Ndugu zangu tuzungumze hapa kwa maslahi ya Taifa. Wakati ule Bunge liliazimia ni Azimio la Bunge namba 8 na namba 14. Wakati ule viliazimia kuhusu uwajibikaji wa viongozi wenyewe dhamana ya kisiasa, wakati ule walikuwa ni Mawaziri wawili, alikuwepo Waziri wa Nishati na Madini Bwana Ibrahim Msabaha na Waziri Karamagi, hizi ni kumbukumbu rasmi za Bunge. Sasa utekelezaji wa yale maazimio na nitarudi kwenye hili kwamba; "utekelezaji wa Serikali kwa sasa ni kwamba vyombo vyaya dola vimekamilisha uchunguzi wake wa ndani na nje kuhusu suala hili, zoezi linaendelea ili kufanya uchunguzi wa nje kwa kushirikiana na vyombo vyaya dola na vyaya Kimataifa." Sasa hao wanachunguzwa toka wakati ule mwaka 2008 kwa sababu ya mikataba na kuisababishia hasara Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu hapa ni nini? Waziri Ngeleja, Waziri wa Nishati na Madini anapaswa kuwajibika kisiasa, pamoja na kuwa mambo haya yametokea kati ya mwaka 2004 mpaka 2009 wakati kimsingi kuna wakati ambapo ye ye hakuwa Waziri, anapaswa kuwajibika kisiasa kwa sababu Kamati ya Bunge na Bunge na namalizia hapa kwenye hili na nitahamia kwenye suala lingine. Kuna Azimio lingine la muhimu sana la Bunge Azimio namba 3 naomba nilisome. Azimio namba 3 la Bunge lilikuwa linasema wakati huo; "Mkataba kati ya TANESCO na RICHMOND,LLC na DOWANS na kadhalika sitaki kuingia huko, lakini niende mbele kidogo na ile ya TANESCO na IPTL, SONGAS, AGGREKO, Alstom Power Rentals ipitiwe upya mapema iwezekanavyo kama ambavyo mikataba ya madini imepitiwa." (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili Azimio liliababishwa Serikali kuanguka wakati huo. Kwa maazimio haya, Baraza la Mawaziri likavunjika likaundwa Baraza lingine, liliopoingia Baraza jipya instrument mojawapo ambayo Baraza ilipewa kufanya kazi ilikuwa ni maazimio 23 ya Bunge. Kwa hiyo, leo Taifa lisengepoteza muda sasa hivi kwa kujadili Mikataba ya Songas na Pan African Energy Tanzania, na mikataba yote iliyotokana na hayo, kama toka wakati ule Waziri aliyekabidhiwa Ofisi, aliyekabidhiwa dhamana angesimamia kuchukua hatua zinazostahili. (*Makof*)

Ndugu zangu, tunaweza tukawa tunapendana sana na Waziri Ngeleja ni rafiki yangu sana, lakini hili ni suala la uwajibikaji. Lakini pamoja na kuchukua hatua za kisiasa za uwajibikaji za Waziri aliyopo sasa, mimi nataka kuju Mawaziri wote waliokuwepo ofisini kati ya mwaka 2004 mpaka 2009 sijui Karamagi, sijui Msabaha na nani tunaelewa kuna viongozi wako Mahakamani hivi sasa kwa kesi za uzembe na kuisababishwa hasara Serikali walioingia mikataba hii waliyoyafanya mambo haya kwa nini mpaka sasa wako mtaani? Hapa ndipo unapokuja msingi wa kisheria tutavunja sana mikataba na tutashtakiwa sana, lakini hatuonyeshi kama mikataba iliingia kwa nia mbaya tutaendelea kushindwa Mahakamani. Tukichukua hatua sisi dhidi ya mikataba mibovu iwe kwenye gesi au kwenye mafuta tutajenga msingi wa kisheria wa kulinda maslahi ya Taifa kwa yoyote yule anayetutisha kwenda Mahakamani. (*Makof*)

Ndugu zangu najua wengine wakati nasema haya walikuwa wanaumia na kuzomea na kuguna, lakini nillsema na narudia kusema tena leo mbele hapa. Taifa letu linafika hapa liliopofika ambapo bei ya umeme inakuwa juu wakati nchi yetu ina gesi ingeweza kufanya Mtanzania apate umeme bei rahisi. Gharama za maisha zinapanda wakati tungeweza kwa gesi yetu kutumia gesi majumbani, kwenye magari, viwanda na tungeongeza uzalishaji, tungepunguza utegemezi wa mafuta kutoka nje na kupunguza gharama za maisha kwa sababu si ya kutokuwa na sheria. Kwa sababu sheria kubwa kuliko zote haiandikwi inakuwa kwenye nafsi ya mtu ya uadilifu kwamba hili

nataka kulifanya, hili halina maslahi ya Taifa na sheria kubwa pamoja na kuwa hakuna Sheria ya Gesi lakini Katiba ya nchi yetu pamoja na ubovu wake ina vifungu vya kulinda rasilimali za nchi. Kiongozi yejote akikubali kuingia mkataba mbovu, akikubali mianya ya ujisadi kwenye ofisi ya umma aliyopewa kuitumikia anakiuka Katiba na ukiondoa makosa ya jinai ya uvunjaji wa sheria kukiuka Katiba ni kosa kubwa zaidi la kiuongozi. (*Makof!*)

Kwa hiyo, ndugu zangu nasema kuitakasa Serikali ili Serikali iaminike kwa Watanzania, ili Rais aaminike kwa Watanzania ni lazima timu inayomzunguka iaminike kwa Watanzania. Mimi ningekuwa Rais Kikwete leo kwa hali hii ya mwelekeo wa nchi ningevunja Baraza la Mawaziri. Kwa sababu tunalumbana leo, tunalumbana ya Katiba haya tutayazungumza tutaendelea kueleza msimamo wetu tulitoka kwa kuwatetea Watanzania, tutaendelea kueleza msimamo wetu na tutaupelea msimamo wetu kwa umma hatukuwepo kujibu, lakini tutajibu hoja moja baada ya nyingine, niliwhi kujuliza huu Muswada ulipita kwenye Baraza la Mawaziri kweli? Sasa yote haya, mikataba yote hii unaweza kujuliza haya yalipita kwenye Baraza la Mawaziri. Sasa tukubali kama Watanzania kufungua ukurasa mpya. Tufungue ukurasa mpya na mwanzo wa kufungua ukurasa huo ni huu. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Nashukuru Mheshimiwa. Namwita sasa Mheshimiwa *Engineer Stella Manyanya* na Mheshimiwa Dokta Hamisi Kigwangalla ajiandae na Mheshimiwa Magale Shibuda ajiandae. (*Makof!*)

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia japo nimeona kuna wazungumzaji wazuri wamechangia maneno mazito, lakini nami kwa kuwa inanikumbusha historia nimependa kuchangia. Pia nikushukuru sana kwa nafasi uliyoitoa kwamba kesho baada ya kutafakari utatujibu vizuri. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa hii iliyosomwa, kufuatia michango iliyotolewa, kufuatia mambo yaliyojitekeza huko nyuma na kufuatia utendaji wa Kamati ya Nishati na Madini iliyopita na hii ya leo, nina haya ya kujuliza. Hivi katika mambo haya yaliyopo hapa pamoja na kwamba wote tunachangia kwa uchungu kwa kusikiliza sana ukweli wa ujumla wetu sisi kufanya kazi hizi kwa pamoja upo, nauliza hivyo kweli upo? Ninazo sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya kwanza kama nilivyosema hayo mambo yameshawahi kujitekeza, lakini baada ya kufanya maamuzi katika hili Bunge letu wangapi wanasmama pamoja mpaka mwisho. Nasema hivyo kwa sababu nikianzia upande wangu wa Chama cha Mapinduzi, nikianzia upande wangu ambaa upo huku kulia, yaliyojitekeza yale masuala ya nyuma ya *RICHMOND* tulishirikiana lakini kufikia mahali tuliachana njia kwamba huyu labda muongo huyu mkweli. Tukafikiria wenzetu wa Upinzani labda wanasmama kwa dhati kwamba wako *serious* kwamba wao wanaona sisi tuko mafisadi, lakini niwaambie leo siri moja. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ule tunaleta taarifa ya *RICHMOND*, taarifa ya awali haikuwa na neno la kuvunja Mkataba, lile lilijitekeza wakati tumekaa kama Kamati Ndogo kwa kushauriana kabla ya kuletwu huku na baada ya kuletwu ikaonekana kwa hali hiyo Mkataba uvunjwe. Kwa kweli ushauri ule kwa Wajumbe wale alioutoa alikuwa ni kutoka Kambi ya Upinzani ni Mheshimiwa Zitto nakumbuka. Lakini baada ya Serikali kufuatilia Mkataba ule na ikaja kujiridhisha ikasema ivunje nani alikuwa wa kwanza kusema hapana, lazima ile mitambo inunuliwe tena kama sio Mheshimiwa Zitto, kwa sababu magazeti yatakumbuka na vyombo vitakumbuka. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyombo vya habari vimkuwa bega kwa bega katika kupinga ujisadi. Mwezi Oktoba au Novemba mwanzoni kama sikosei gazeti la Mwanahalisi liliandika kwamba "Mwakyembe na Manyanya walaumiwe kwa kuingiza nchi gizani," sikumuuliza, nilinyamaza. Leo tulifanya vile kwa nia ya kuona hali halisi iliyokuwepo. Mimi sikujibu kwa sababu nimekuwa nayajua mengi.

Leo hii tunaposema kwamba tuvunje huu Mkataba baada ya hapo atalaumiwa nani, ndio swali langu kwa sababu hatusimami wote mpaka mwisho. Lakini ukweli utabakia palepale hata kwenye mchango wangu wa juzi nimesema wakati tunaizungumzia Katiba, tatizo letu kubwa

Watanzania mpaka sasa hata sisi viongozi tuliope humu hatujasimama kama kitu kimoja, hatujajulikana ajenda yetu ya msingi ni ipi, tunasimamia lipi? Sasa hivi tunasema hivyo wawili wanasema lingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili ninalolisema tunatamani kupata *solution* ya haraka, *solution* ya haraka sasa hivi kwa sababu hili limejitokeza basi Mheshimiwa Ngeleja wewe utoke. Lakini mimi narudi nyuma sipendi kuchukua majibu napenda kuanza nyuma hivi Mkataba wa *Pan African* umeanza kipindi cha Ngeleja, kwa nini tunamwonea peke yake Ngeleja? Ndio swali langu. Kuna mtu sijui ameandika barua ya kusema mimi nimeambiwa kwamba na fulani basi hakuna atakayenigusa nilitegemea ndio imesema kwamba hamtaguswa na sahihi yake. Sasa mtu ameamua kujisemea hivyo anarusha kwenye *internet* basi tupate hiyo ambayo aliambiwa kwamba hataguswa. (*Makofii*)

Kwa hiyo, mtazamo wangu unabakia pale pale, kinachotutesa cha kwanza na nilikisema toka siku nilipowasilisha taarifa kwamba wataalam tuliomo katika sekta mbalimbali za kiutendaji hatutimizi vyema wajibu wetu. Aidha, kwa kutokuelewa tunachokifanya au kwa makusudi, hilo ndio suala ambalo lime-*conclude* sasa hivi. Lakini la pili ninalojisikitia nchi yangu Tanzania bado tutaendelea kuliwa na mikataba kama hiyo. Tutaendelea kuliwa kwa sababu ya umaskini wetu wa ufahamu, tutaendelea kuliwa kwa sababu tunapoletewa hizi taarifa unakuta kampuni inayoleta imo, unakuta Balozi inayohusika na kampuni kama hizo zimo. Kwa mfano, wakati tunatunga Sheria ya Umeme, Mabalozi wangapi walikuwa wanazunguka hapa na kutupa *dinner*, tuseme ukweli na ndiyo maana hata juzi nilisema kwamba hatuna haki ya kulaumiwa peke yetu au ku-*support* maandamano ya ujisadi bila ya kuwahusisha na wao, kwa sababu wanajua kinachoendelea katika nchi zetu. (*Makofii*)

Kwa hiyo, nasema hivi kama kweli tuna nia ya kujitoa hapa tulipo kwanza Watanzania wote tuwe kitu kimoja, tujue tatizo letu la msingi ni nini. Lazima tutofautishe kati ya kupambana kati ya Chama cha Mapinduzi na Vyama vya Upinzani kwa ajili ya mambo yetu ya kisiasa ya madaraka na kati ya kuzungumzia masuala halisi ambayo ni ujisadi huu uliopo katika mikataba yetu na tukitofautisha mambo haya mawili tutaweza kupata jibu. Lakini kwa sasa hivi hatuwezi kukaa pamoja kwa sababu huyu akileta ajenda hii, mwingine anafikiria ni kwa sababu fulani. Huyu akileta ajenda hii huyu anafikiria ni kwa sababu anataka kum-*support* fulani, matokeo yake hatupati jibu, matokeo yake hatutoi nguvu hata kwa yule mwenye kuweza kufanya maamuzi. Hivi mniambie kwa mfano katika kipindi kile hata kama Mheshimiwa Rais angependa kutoa maamuzi huku mwininge anasema hawa waongo, huyu mwininge anasema unajua kuna hili, huyu mwininge anasema hapana, hivi hizo nguvu za kufanya maamuzi anazipata wapi? Kwa sababu sisi wenyewe tunatoa *inputs* za aina tofauti tofauti. (*Makofii*)

Kwa hiyo, ushauri wangu wa dhati kutoka rohoni pamoja na mapendekezo yaliyotolewa humu kwanza nakubaliana kabisa isiwe taarifa hii kama ilivyo na bahati nzuri isiwe ya Kamati Teule iangaliwe kwa kina, Wanasheria ambao tunawaamini na wamebobebea watusaidie zaidi. Lakini si hivyo tu na hata hao Wanasheria na wenyewe wawe wazalendo, itakuwaje Mwanasheria mmoja huku unasema hiki kinafaa vunja, upande wa pili unaenda unasimama unasema huyu hana haki lipa, huu uzalendo wa Wanasheria wetu uko wapi au Mawakili wetu uko wapi? Ndiyo maana najiona sisi tumezungukwa na tatizo. Kwa hiyo, ninachoshauri kwa kina kabisa na kwa dhati ya moyo wangu na naamini hilo ndilo tatizo letu sote tutafikia hapo tutaangaliana usoni matokeo yake kila siku tutakuwa tunaletewa mikataba kama hiyo mmojawapo atakuwa anasogezwa anafyekwa kichwa, kesho kinatokea hicho hicho anafyekwa kichwa, lakini majibu ya msingi bado hatujapata. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo kubwa na hayo sio ya leo kama alivyosema Mheshimiwa Mnyaa suala la *Pan African* ni kwamba *pipe* haitoshi, kwenye ripoti yetu imejaa mle kibao, lakini watu walikuwa hawataki hata kuisikia wanasema hawa wazushi, leo ripoti hii ndiyo itakuwa tofauti na ile iliyopita, kwa sababu hatukushirikiana inavyostahili. Kwa hiyo, nizidi tu kuomba kwa sababu wote ni Watanzania, Serikali ni yetu, Bunge ni letu, Mahakama ni yetu, tukae wote katika kitu kimoja katika kuona ukweli ili tuweze kuisaidia nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu ni hiyo na sitakuwa na jibu la kusema naunga mkono Maazimio haya ninachosema kuna hoja za msingi za kuzijadili kwa muda ili kupata majibu sahihi. Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Manyanya. Sasa namwita Mheshimiwa Dokta Hamisi Kigwangalla.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, *asalaam alyekum*. Nimeanza kwa kuomba amani ya Mwenyezi Mungu iwe mbele yako na ninaamini pia tunapoongea hapa sisi watoto wa nchi hii tuna Mungu ndani yetu na kwa kada ambaye nimezaliwa na kulelewa katika itikadi na imani ya Chama cha Mapinduzi na kufundishwa uongozi thabiti na maandiko mazuri yaliyojaa hekima na busara ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ninaamini katika kusema ukweli. Nasema ninaamini katika kusema ukweli kwa sababu katika imani ya Chama cha Mapinduzi imeandikwa; "nitasemwa kweli daima fitina kwangu mwiko." (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme ukweli. Nimepata fursa ya kuipitia hii hotuba, hii taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini na nimeridhika kwamba wamefanya kazi nzuri na kabla sijasahau naomba iingie katika kumbukumbu kwamba ninayaunga mkono mapendekezo yao kwa asilimia mia kwa mia. Lakini pia naomba iingie katika kumbukumbu na iwe ni mojawapo ya maboresho ambayo nitayatoa hapa sasa hivi kwamba tuweke *deadline* katika mapendekezo yaliyotolewa na Kamati hii ya Kudumu ya Bunge. (*Makofii*)

Naomba tuweke *deadline* kwa maana ifuatayo; kwamba hawa watu wamekiri kwa kauli yao na nafsi zao na wakatamka kwa ndimi zao kwamba wamefanya makosa ambayo ni *honest* ya kuiba shilingi bilioni 46. Kwa kuwa wao wenyewe wamekiri na wakatamka kwa ndimi zao kwamba wameiba shilingi bilioni 46, mimi naomba Bunge lako Tukufu liweke kwanza *deadline* ya kuwataka warejeshe hizi shilingi bilioni 46 haraka iwezekanavyo. Ili niwe *objective* naomba nipayendekeze kwamba hizi shilingi bilioni 46 zilipwe ndani ya siku kumi zijazo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia wamekiri na kutamka kwamba watatoa taarifa nyiningine ya zaidi ya shilingi bilioni 36, lakini pia tofuti kati ya jumla ya shilingi bilioni 110 na zile shilingi 46 ambazo wamekiri kuiba nayo walisema wangeleta vielelezo lakini mpaka tunapoongea hapa bado hawajaleta vielelezo. Kwa hiyo, ukweli uko wazi kwamba kampuni ya *Pan African Energy* imeiba kwa kughushi, kwa hila, kwa ghiliba jumla ya shilingi bilioni 110. Hizi ni pesa ambazo kwa mujibu wa taarifa ya *Action Aid* zingewenza kusomesha watoto wa nchi hii zaidi ya 150,000 kwa mwaka mzima. Taarifa hii ya *Action Aid* niliweka mezani hapa Bungeni katika Bunge la Bajeti. Nimeisoma na nillisoma vizuri na nikaiilewa na nillisema hapa Bungeni. Ningetegemea Serikali toka kipindi kile mpaka leo hii wangkuwa wamechukua hatua madhubuti za kudai hizi pesa za Watanzania na kuzirejesha nchini kwetu. Nilisema mfumo wa wizi walioutumia ni mfumo wa *tax havens* kwa maana ya kufungua *off show account* kwenye nchi ambazo zina masharti rahisi ya wizi, zina masharti rahisi ya *accounting* ambayo yanahalalisha wizi wa fedha kutoka nchi nyiningine na kupelekwa katika nchi hizo na njia ni ya kuanzisha mikopo yao ya ndani ya kampuni yaani *PFI's* ambayo inawawezesha wao kujitengenezea mahesbu kwenye *account* yao kwamba wamejikopesha wao wenyewe na badala ya *ku-declare equity* wana-declare *loans* matoeko yake kila siku wanakuwa wanaonekana hawafanyi faida, wanakwepa malipo halali ya *cooperate tax* wanakwepa malipo ya *dividend* kwa nchi yetu lakini pia wanaiba pesa halali ambazo wangezilipa kama *withholding tax*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania ni watu wenyewe uelewa mkubwa sana na mfumo wetu wa elimu umetuelemisha vizuri kiasi kwamba mambo kama haya yahapaswi kututenga. Lakini nashindwa kuelewa, watendaji na watu tuliwapa dhamana ya kulinda rasilimali ya nchi yetu wameshindwa kuyaona haya mpaka wananchi wa Sweden wanayaona kabla yetu. Lakini hata baada ya sisi kuyasema hapa Bungeni kwenye Bunge la Julai, mpaka leo hii hakuna hatua zilizochukuwa zaidi ya hatua zilizochukuliwa na Bunge. Hivi nchi hii wazalendo waliobaki ni hawa Wabungeni tu, kwenye Serikali hakuna wazalendo? Ninauhakika kwa haya yanayosemwa hapa rafiki yangu, ndugu yangu Mheshimiwa William Ngeleja, Waziri wa Nishati na Madini anatamani kuficha kichwa chake kama mbuni kwenye mchanga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina uhakika huo na kama ningekuwa mimi nimekaa kwenye kitichake, kwa maneno haya yanayosemwa hapa kwa kusukumwa na uzalendo, kwa kusukumwa na ukweli na uhalisia kwamba yeze hakuwepo, maamuzi haya mengine ya kipuuzi yanafanya ningeweza kumwomba Mheshimiwa Rais nimirudishie nafasi yake ya Uwaziri, njiuzulu na hatimaye nikafanye kazi nyingine ili kutunza heshima yangu kama Mtanzania, ili kutunza heshima yangu kama msomi na ili kujenga *carrier* yangu ya kisasa. Katika hilo mimi ningekuwa ndiyo yeze vilio vya wananchi kwenye migodi, vilio vya wananchi kuhusu mikataba mibovu, vilio vya wananchi katika mikataba ya gesi, ukosefu wa umeme na matatizo chungu mzima, yote haya kwa hakika ningekuwa mimi yangeweza kupelekeea kusema pengine hii kazi imenishinda nijitoe. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo katika Wizara ya Nishati na Madini yamekuwa mengi na yamedumu kwa muda mrefu. Tumeyasikia, tumeyaona na tumeyasoma. Watanzania wamechoka hata kusikia matatizo na kero katika Wizara hii. Lakini sijawahi kuona *bold action, bold measures* zikichukuliwa na uongozi wa Wizara hii, nashindwa kuelewa kuna ubia, kati ya hawa na wale wengine au pengine viongozi wa Wizara hii wanafanya ukuadi wa kutuletea mabeberu kutoka Magharibi ili waje wavune rasilimali katika nchi yetu na mwisho wa siku nchi hii ikose rasilimali na iendelee kuwa maskini. Nayaongea haya kwa uchungu sana mpaka *point* zinaruka kichwani kwa sababu ni mambo yanayoniumiza moyo, yanayotaka kunitoa machozi. Sitaki kutumia kauli ya Mheshimiwa Mangungu ya kusema kwamba angeweza kulia mpaka dakika zake zikaisha. (*Makof*)

Mimi haya yamenisikitisha sana na ninaomba sana tusiwe na haraka katika kujadili suala hili ili tuweze kupata mustakabali mwema ambaa utatupelekea kuleta mafanikio yenyi tija katika uchumi wa nchi yetu. Bila ya hivyo tutakuwa tunacheza makida makida. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali ilivyo nikuombe sana tuweke *deadline* katika kufanya maamuzi haya na hawa wezi walipe pesa zetu walizoiba lakini pia wapelekwe Mahakamani kwa makosa ya jinai waliyoyafanya ya kughushi, ya kusema uongo na ya kuleta nyaraka ambazo zina uongo ndani yake. Kwa hayo machache naomba kuunga mkono hoja. (*Makof*)

MHE. JOHN S. MAGALLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nilikuletea ujumbe wa kwamba nilikuwa na upendo sana kuchangia ajenda ya kesho lakini kwa sababu umenishauri nizungumze nitaongea. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza kabisa napenda kuipongeza Kamati hii kwa kazi nzuri iliyofanya. Watanzania wanazungumzia maliasili gesi, lakini mimi naomba vilevile kuliomba Bunge hili Tukufu na Mheshimiwa Waziri Mkuu huko aliko anisikie na Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete unisikie; nina masikitiko makubwa sana kwa niaba ya wananchi wanaolima zao la pamba.

Mheshimiwa Rais Kikwete, ninaomba utambue ya kwamba mijini hakuna ajira. Wakulima vijijini tunataka kuwanyima ajira. Napenda kusema kwamba wananchi hawana mbegu za kulima pamba hadi leo. Huo ndiyo mgodi wa dhahabu, hiyo ndiyo gesi. Mnazungumza juu ya *Pan Africa* na wako watumishi *Pan Africa*. Nina masikitiko makubwa sana na ninawaomba Waheshimiwa Wabunge muelewe kwamba pamba inategemewa na watu wasiopungua watu milioni 14. Sasa usipokuwa na mbegu maana yake maisha bora yatapatikana wapi? (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti je, Chama cha Mapinduzi kinajithaminisha vipi kama hakijichongei na umauti? Thamani ya Mheshimiwa rafiki yangu, ndugu yangu Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete. *Legacy* yako, urithi wako kwa awamu ya nne unachongwa. CCM unachongwa, Serikali inachongwa, heshima ya Rais wangu inachongwa. Kwa hiyo, ninawaomba ndugu zangu kesho nikiomba kwamba tuahirishe Bunge tujadili suala la mbegu ya pamba naomba mniunge mkono. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno yangu yana bima ya subira katika ajenda tuliyonayo. Jambo la kwanza ambalo nawaomba Waheshimiwa Wabunge tunaweza tukawa tuna maamuzi ya kufunika uchafu, ya kufunika uvundo; mimi sijawahi kuona ya kwamba kifuniko cha kwenye uchafu huondoa uchafu. Kuna kitu tunasema uwajibikaji wa kisasa. Mimi nasema hicho ni kifuniko cha uvundo. Haya Mheshimiwa Ngeleja anaweza akajiuzulu hata kesho, lakini kama hakuna

mazalia ya mbu hakuna malaria. Sasa mazalia ya mbu hatuzungumzii, tunasema tukanunue vyandarua. Watu dhurumati ni watumishi. Hawa watumishi lazima tutafute dawa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi Tanzania inayoongozwa na Baraza la Mawaziri au linaongozwa na Makatibu Wakuu? Hivi ni Mbunge gani katika Bunge hili anathaminika na kusadikika akitoa shauri kwamba huku kuna dhuruma kwamba *DED* hafai akipigwiwa *DC* anasema hayo mambo ya wanasiasa, akapuuzwa Mbunge. Wabunge tunapuuzwa sana. Hivi maana ya mihimili mitatu ni nini? Leo tunaletewa ajenda hapa tuijadili; ndugu zangu papara papara haizai mapacha. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba hilo mlifahamu. Bunge hili linathaminika, linaongozwa na uongozi wa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi. Baraza la Mawaziri ni la Chama cha Mapinduzi. Watanzania wamechoka kukaririshwa kauli ambazo hazina tija. Serikali sikivu, kumbe imegandishwa na uhondo wa madaraka. Naomba niwaulize ndugu zangu wana CCM, waharibifu na ubadhilifu uliotajwa hapa umefanya na nani? Sheikh akishikwa ugoni wanaathirika waumini, Askofu akishikwa ugoni wanaathirika waumini. Chama cha Mapinduzi mnaathirika na ugoni wa watumishi wa Serikali. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa hifadhi ya watumishi wa kulaumu wanasiasa. Kila likitokea jambo wanasema achana na wanasiasa. Lakini malighafi ya dhuruma kwa maslahi ya Watanzania ni wataalam. Wanasheria na watalaan ndio malighafi ndio mawakala; natumia lugha ya Afisi ya *TANU* makuadi. *It's an embracement*, ni aibu. Mafuniko ya dhuruma na mikataba mibovu ni ya wataalam. Toka lini mwaniasiwa akafanya mikataba mibovu. Toka lini Waziri akafanya hivyo. Watanzania wanamini, bima ya maisha bora ni Bunge. Bima ya haki sawa ni Bunge na bima kwa maslahi ya Taifa ni Bunge. Leo tunaambiwa tuongee kwa papara papara hapa. Kejeli, kejeli, kejeli hii!

Naomba Mheshimiwa Spika atambue na aimarishe na athaminishe Bunge. Kama Mheshimiwa Spika hataki kuthaminisha Bunge, kama tumemwonea kumpa dhamana hii ajiuzulu; ajiuzulu. Haiwezekani mambo ya maslahi ya Taifa yakajadiliwa kwa dakika kumi na tano. Baba wa Taifa angekuwepo hapa leo angeitisha Kamati Kuu kumvua Uspika. Mnachezea chezea nchi hapa. Tunaacha *legacy* gani? Tunaacha urithi gani kwa hawa vijana akina Kafulila?

Hivi ninyi mnaokaa kwenye Kamati ya Uongozi hamyaoni haya? Hivi mpaka mkapanga saa kumi na moja wachangie watu wachache tumalize tuondoke. Hivi ninyi Kamati ya Uongozi mnatufaa? Makamishna wa Bunge mnatufaa nini? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka uwajibikaji. Tunapozungumza ujisadi wa watumishi wa Serikali na matendo yote yenyen upofu na utupu ni lazima yapate ujazo. Kauli za kujaza ujingga Watanzania wamechoka wamesema ya kwamba hatutaki kuambiwa kwamba haya ni maamuzi ya Serikali. Hivi Serikali ni mzimu? Serikali ni watu, kama kuna watu hatarishi amba tabia zao hazifai waondoke. Hammthaminishi Rais Kikwete, hamuithaminishi CCM, nawaambieni. Niliwhi kutamka kwamba sitaki CCM ife mnaitia kihaja nyie wenyewe, mnajitia kitanzi nyle wenyewe. Sasa kama mmechoka kama watoto si riziki harusi haiwezi kujibu. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima watu waondoke, kuni zikikosekana moto huzima, kama hakuna maudhi mtu hukasiriki, Watanzania kule Maswa hawana mbegu wamekasirika, wamenuna. *DC* yupo, Waziri wa Kilimo yupo, mbegu hazitoshi, mnataka tufanye nini? Nitaanzisha *harambee* ya kukusanya kadi za CCM. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhuruma haiitikiwi *amen!* Hakuna dini yoyote inayohubiri dhuruma iitikiwe *amen!* Lakini hapa tunataka tuambiwe tuitikiwe *amen* kwa dhuruma. Ninaomba sana, maamuzi ya Bunge ni kikolezo kwa ustawi na maendeleo ya jamii na uwajibikaji wa Serikali. Ninawaombeni sana ndugu zangu, tumekuja hapa na dini yetu ni Katiba ya nchi. Dini yetu ni Katiba ya nchi, tunaiheshimu, tunaienzi na leo mimi naomba nitoe ufanuzi na ufahamisho.

Mwaka 1977 wakati CCM inazaliwa, Katiba ya CCM na Katiba ya nchi ilikuwa itekeleze siasa na itikadi ya Chama cha Mapinduzi na ndio maana Katiba ya CCM inashabihiana na

Katiba ya nchi. Sasa ukikuta mtu hatekelezi matakwa ya Katiba ya CCM kule ni msaliti, bado mniamwita CCM huyo? Afukuzwe. Hamtekelezi ahadi za mwana CCM, shabaha na malengo ya CCM, shabaha za Katiba ya nchi hamtekelezi, tuna wananchi raia au tuna watu ambao wamekuja hapa nchini wanajiita Watanzania kama kondoo aliyeaa suti ya chui kumbe ni chui kweli kweli. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuombeni ndugu zangu. Maneno haya sina raha nayo, nimefuatilia sana, pametokea mtarafuru hapa kwa sababu hatuna bima ya subira. Lakini nakuombeni kila aliye na subira kuna Mwenyezi Mungu, kukosea njia sio kupotea njia.

Kwa hiyo, napenda kusema mjanganie. Malalamiko na mateso haya ya Watanzania, uongozi bora, utawala bora, japo TAMISEMI kwa ndugu yangu. Kada mwenzangu wa *Youth League* ambaye akifa kesho anangojea mbinguni akapigwe bakora na Baba wa Taifa, Mheshimiwa George Mkuchika. Wala si uongo, wapo watu wakifa hapa Mzee Kawawa ametangulia anamwambia Mwalimu, "Mwalimu niachie wakija tuwatandike." George Mkuchuka si wa kwanza hapa na wengine nitawataja. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusisitiza, Bunge tupewe haki yetu ya kutekeleza matakwa ya Katiba ya Ibara 63 ya kuishauri na kuisimamia Serikali, tuwe na muda wa kutosha wa kujadili taarifa hii. Tuweze kutekeleza matakwa ya Ibara ya 8, 18, 21 na Ibara ya 26. Ninaomba hayo tuyatekeleze, tusipofanya hivyo tutakuwa hatuna utiifu kwa kiapo chetu tulichokula kwa kuilinda na kuitumikia na kuidumisha Katiba ya nchi. Watanzania wapo katika fikra za kutangatanga, wapo katika uchovu wa fikra kwa nini kila siku kuna mikataba mibovu. Eeh Mwenyezi Mungu hakuna kuwasamehe peleka jehanamu... (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Shibuda, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kama tulivyoomba kwamba tuiachie Kamati ya Uongozi ya Bunge kushauriana na kuona namna gani tutaendelea na mjadala huu na kwa vile kesho tunapaswa kupokea pia taarifa ya Kamati Teule ya Bunge sasa naomba nimwite Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu atoe hoja ya kutengua Kanuni.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hotuba ya Mheshimiwa Shibuda *original* sio wa kuchongwa naomba kutoa maelezo ya hoja ya kutengua Kanuni za Bunge chini ya Kanuni ya 150(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2007. (*Makof*)

Kwa kuwa Mkutano wa Tano wa Bunge unaoendelea umepangwa kumalizika kesho tarehe 19 Novemba, 2011 ambayo ni siku ya Jumamosi;

Na kwa kuwa, kwa mujibu wa Kanuni ya 28(15), si utaratibu wa Kibunge kukutana siku ya Jumamosi, Jumapili au siku za mapumziko. Ili kuliwezesha Bunge kukamilisha shughuli zake zote zilizopangwa kikamilifu kwa kutumia Kanuni ya 150(2) Bunge litengue Kanuni ya 28(15) ili Kikao cha Bunge kiendelee kesho siku ya Jumamosi kwa kukamilisha shughuli zilizopo kwenye ratiba.

Hivyo basi, Bunge linaazia kwamba kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa shughuli za Bunge katika Mkutano huu wa Tano, Kanuni ya 28(15) itenguliwe kama ifuatavyo:-

Kanuni ya 28(15) ambayo kwa ujumla wake inaelekeza kwamba Bunge haliwezi kukutana siku ya Jumamosi, Jumapili au siku ya mapumziko itenguliwe na badala yake Bunge likutane kesho tarehe 19 Novemba, 2011 siku ya Jumamosi kuanzia saa tatu asubuhi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makof*)

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. (*Makof*)

(*Hoja Ilitolewa iamuliwe*)

(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Bunge liliafiki hoja ya kutengua Kanuni iliyotajwa)

MWENYEKITI: Kwa vile kesho tutaendelea na vikao vyetu, kabla ya kuahirisha, nina matangazo yafuatayo:-

Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mwenyekiti wa TAPAC anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kwamba leo kutakuwa na *dinner party* kwa ajili ya kuadhimisha miaka kumi ya TAPAC. Kwa hiyo, mnaombwa wote mhudhuri na Makamu wa Rais Dokta Gharib Bilal atakuwepo kwenye *dinner* hii. Lakini pia Mheshimiwa Margaret Sitta, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Huduma za Jamii anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hii kwamba kutakuwa na kikao cha dharura baada ya kuahirisha kikao hiki kwenye ukumbi wa Pius Msekwa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana naomba kuwashukuru na ninaahirisha hadi kesho saa tatu asubuhi. (*Makofi*)

*(Saa 1.45 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumamosi,
Tarehe 19 Novemba, 2011 saa tatu asubuhi)*